

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA NNE

Kikao Cha Thelathini Na Tano – Tarehe 2 Agosti, 2006

D U A

(Mkutano Ulianiza Saa Tatu Asubuhi)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaanza napenda nitoe shukrani zangu za dhati sana kwa Wenyeviti Mheshimiwa Jenista Mhagama na Mheshimiwa Job Ndugai kwa kazi nzuri sana waliyoifanya wakati sipo katika kiti hiki. Nawashukuru sana na ni faraja kubwa kwamba hamkukosea katika kuwachagua. Ahsante sana. (*Makofi*)

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Bodi ya Pamba kwa Mwaka Ulivoishia tarehe 30 Juni, 2005 (*The Annual Report and Accounts of the Tanzania Cotton Board for the year ended 30th June, 2005*).

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE. JOEL N. BENDER):

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007.

MHE. AMEIR A. AMEIR - (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII):

Maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kwa Kwa Mwaka wa Fedha Uliopita, Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2006/2007

MHE. GRACE S. KIWELU - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI:

Maoni ya Kambi ya Upinzani Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kwa Mwaka wa Fedha Uliopita, Pamoja na Maoni Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2006/2007.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 326

Kanuni za Utendaji za Madiwani

MHE. MUSSA AZAN ZUNGU aliuliza:-

Kwa kuwa, Kanuni za sasa haziwapi Madiwani fursa kubwa katika kuendesha Halmashauri zao, badala yake zimewapa watendaji uwezo mkubwa kuliko wawakilishi wa Wananchi na pale panapotokea tatizo Madiwani huwajibishwa bila sababu:-

(a) Je, Serikali haioni kwamba sasa ni wakati muafaka wa kuzipitia upya kanuni hizo?

(b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kubadilisha Bodi ya Tenda na kurudishia Kamati ya Fedha na Utawala?

(c) Je, Serikali haioni kuwa sasa ni vema kuzipa Halmashauri zipange mishahara ya Madiwani. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwadhibiti Watendaji wanaopuuza mipango ya Madiwani.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Azan Zungu, Mbunge wa Ilala, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa *program* ya maboresho, Halmashari zimepelekewa madaraka na majukumu ya kusimamia utekelezaji wa shughuli za uendeshaji wa Halmashauri. Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali vimerekebishwa ili kuendana na upelekaji wa madaraka hayo, pamoja majukumu na raslimali kwa wananchi kupitia kwa Waheshimiwa Madiwani. Kazi ya watendaji iliyobaki ni kutoa ushauri wa kitaalam na Waheshimiwa Madiwani, ndiyo wenye kutoa maamuzi kwa kuzingatia ushauri wanaopata.

Hata hivyo, Serikali itaendelea kuzipitia upya Kanuni na Miongozo mbali mbali na kufanya marekebisho inapobidi ili kuwezesha utendaji mzuri katika Halmashauri zote hapa nchini.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Manunuzi ya 2004, Wajumbe wa Bodi ya Zabuni katika Halmashauri ni pamoja na Mkurugenzi wa Halmashauri ambaye ndiyo Mwenyekiti, Afisa Ugavi ambaye ndiyo Katibu, Mweka Hazina (Mjumbe), Mkuu wa Idara husika, (Mjumbe) na Katibu Tawala wa Wilaya ambaye naye (Mjumbe).

Hivyo tofauti na iliyokuwa miaka ya nyuma, Bodi ya Zabuni za Halmashauri kwa sasa hazina wawakilishi toka Baraza la Madiwani. Aidha, ni kweli Serikali imepokea malalamiko mbalimbali kutoka kwa wadau kuhusiana na utoaji wa Zabuni mbovu kwa baadhi ya watendaji. Kutokana na malalamiko hayo ambayo kwa kiasi kikubwa yanatokana na muundo wa Bodi uliopo, Serikali inayafanya kazi malalamiko hayo ikiwa ni pamoja na kuangalia upya muundo wa Bodi ya Zabuni.

(c) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa ya 1982, Madiwani ni waajiri wa watumishi walio kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa husika ambao wanazo kazi zao zinazowapatia riziki ya kila siku wakiwa kama wafanyakazi, wakulima, au wafanyabiashara. Hivyo, Waheshimiwa Madiwani wanalipwa posho tu kama wawakilishi wa wananchi badala ya kulipwa mshahara.

Mheshimiwa Spika, mipango ya Halmashauri huanzia ngazi za chini (Vijiji/Mitaa) kwa kuwashirikisha wananchi kuibua mipango na baadaye kuidhinishwa na Halmashauri husika. Mchakato mzima wa kuibua mipango hadi kuitishwa ni karibu miezi sita, hivyo hakuna uwezekano wa kuwa na mipango ya aina mbili ya Waheshimiwa Madiwani na mipango ya Watendaji. Aidha, Madiwani kama waajiri wamepewa Mamlaka ya kuwadhitii watendaji wanaopuuza mipango iliyopitishwa na Baraza la Madiwani baada ya kuandaliwa na Watendaji.

MHE. MUSSA AZAN ZUNGU: Mheshimiwa Spika, Serikali kuitia mfuko wake maalum wa (*CDG*) *Capital Development Grand* ilitoa fedha nyingi kwa Halmashauri lakini ilikuwa lazima vigezo fulani vitimizwe. Je, Serikali itachukua hatua zipe kudhibiti au kuwaadhibu watendaji wasiofikia vigezo hivyo na kuzikosesha Halmashauri fedha kama ilivyotokea sasa hivi kuwa kuna Halmashauri nyingi sana zimekuwa *penalty* baada ya watendaji kushindwa kutimiza vigezo na wananchi kuumia katika mipango ya kusuma maendeleo yao? (*Makofî*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, Halmashauri zetu zote hapa nchini hivi majuzi tulijaribu kuwapelekea maelekezo mbalimbali yanayoonyesha namna walivyo na mamlaka na madaraka makubwa juu ya watendaji wao. Tumefanya hivi baada ya kubaini kwamba sehemu nyingi za Halmashauri hawasomi vizuri sheria zinazotawala majukumu yao. Kwa hiyo, sehemu kubwa inakuwa ni malalamiko lakini ukizipitia zile taratibu zilizopo na kama wangezizingatia hakuna mtendaji hata mmoja

atakayeweza kuponyoka mkono wa mamlaka ya Halmashauri. Kwa hiyo, naomba nitoe wito wa jumla kwamba tunayo nafasi kubwa sana ya kuweza kuwadhibiti watendaji wote pamoja na hawa ambao Mheshimiwa Zungu anawaeleza. Ilimradi katika kutengeneza mashtaka yawe ni mashtaka ambayo yako wazi bayana ambayo yanaweza yakamfikisha mtendaji yeote katika hatia kutoka na utovu huu atakaokuwa ameufanya.

MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH: Kwa kuwa imebainika katika Halmashauri nyingi watendaji katika idara zao wanakaimu nafasi zao na hivyo kupunguza ufanisi wa kazi katika idara hizo za Halmashauri. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba idara zote zinapata watu wenye sifa ili wawze kushika nafasi zao na kuleta ufanisi katika mambo ya maendeleo katika Halmashauri zetu? (*Makofi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kawaida wa kuimarisha Halmashauri zetu kiutumishi bado ni ule wa kuomba vibali kutoka Idara Kuu ya Utumishi na baada ya kupata zinatangazwa wanashindana na kisha atakayeshinda ndiye anayepewa nafasi ili kuweza kulinda ubora wa watumishi hawa.

Lakini kama ambavyo tumekwishalieleza hapa tumeshatoa maelekezo ili kurahisisha na kuharakisha zoezi hilo kwamba Halmashauri zote ambapo kuna makaimu, makaimu ambao wana sifa za kuweza kuhodhi ile *substantive post* wote wameelekezwa wawathibitishe makaimu hao mara moja tena bila kucheleva. Lakini nashangaa bado nakutana na baadhi ya Wenyeviti inaelekea kama vile mwongozo tuliusuo bado hawajaupata. Kwa hiyo, tutajitahidi tena kuwakumbusha ili hilo analolisema Mheshimiwa Rished ambayo bado iko katika sehemu nyingi basi tuweze kujaza nafasi zile ilimradi watu hao wana sifa wakati walipokuwa wanakaimu. (*Makofi*)

Na. 327

Posho ya Madiwani

MHE. ELIZABETH N. BATENGA aliuliza:-

Kwa kuwa, Madiwani wana majukumu makubwa ya kuhamasisha na kusimamia shughuli za maendeleo katika maeneo yao:-

Je, ni lini Serikali itatambua jukumu hilo la Madiwani na kuongeza kiwango cha posho kutoka 30,000/= za sasa hadi angalau 200,000/= kwa mwezi badala ya kuziachia Halmashauri za Wilaya/ Miji?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Batenga, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua nafasi, majukumu na umuhimu wa Waheshimiwa Madiwani. Mwaka 2005 Serikali iliunda Kamati (*Reference Group*) ya kuratibu zoezi la kuangalia maslahi ya Madiwani. Mtaalam Mshauri (*Consultant*) alifanya utafiti kwenye baadhi ya Halmashauri na kupata maoni ya Wadau mbalimbali hata walio nje ya Halmashauri, mionganini mwao ni Madiwani wenyewe. Kamati hiyo, ambayo iliongozwa na Mheshimiwa George Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, imekwishachambua na kuwasilisha katika ofisi yangu maoni na mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, Ofisi yangu imelitafakari suala hili na imekwisha kutayarisha Waraka wa Baraza la Mawaziri unaolenga kuinua viwango vya Posho wanayopata Madiwani pasipo kuongeza mzigo kwa Halmashauri zenyewe. (*Makofî*)

MHE. ELIZABETH N. BATENGA: Mheshimiwa Spika, namshukuru Waziri kwa majibu yake mazuri. Kwa niaba ya Madiwani wote na sisi wote Wabunge, kuipongeza Serikali kwa hatua hiyo. Lakini pia niombe hatua za haraka zifanyike ili wahusika waweze kufaidi matunda hayo. ahsante. (*Makofî*)

SPIKA: Ebu rudia tena, ilikuwa ni shukrani?

MHE ANNE K. MALECELA: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kazi ya Diwani na kazi ya Mbunge ni sawa tunachopishana zaidi ni maeneo ya kazi na kwa kuwa sisi Wabunge, ni kweli tunawategemea sana hawa wenzetu Madiwani watusaidie ili tuweze kutekeleza kazi zetu vizuri. Je, Serikali haioni kwamba zaidi ya kuwapa posho pia wangeweza kupewa mshahara japo kiasi kwa mwezi? (*Makofî*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, kwa muundo na mfumo wa kisheria tulionao sasa, Diwani hayumo katika kundi la waajiriwa wa Kiserikali kama tulivyo sisi. Sasa jambo hili linabishaniwa sehemu nyingi tumejitahidi kwenda nchi mbalimbali. Namibia, Uganda na hata nje ya nchi katika kujaribu kuona uzoefu wa nchi nyingine wanafanyaje katika eneo hili.

Lakini bado kwa sehemu hata Uingereza Madiwani wameendelea kubakia ni *civic leaders* na ambao wanategemea posho kwa kuwa *assumption* iliyopo kwamba viongozi ni watu ambao wako katika mazingira ya Kata ya Vijijini, maisha yao kwa sehemu kubwa ni yale ya kawaida katika vijiji na hawakutegemewa kwamba wangekuwa tena ni watawala kwa namna moja au nyingine.

Kwa hiyo, nadhani ni dhana nzuri na pengine tutaendelea kuilinda ili wasije wakageuka nao badala ya kuwa wawakilishi katika ngazi za chini wakaanza ku-*behave* kama watawala. Lakini mimi nadhani rai ya msingi ni kuendelea kuangalia posho pamoja

na marupurupu mengine yanayowawezesha kutimiza wajibu wao vizuri. Hili ndiyo zoezi ambalo tumelazimika kulipeleka kwenye *cabinet inshallah* tukipata matokeo mazuri basi tuna hakika Madiwani kwa kiasi fulani wataridhika. (*Makofi*)

Na. 328

Jumuiya ya Afrika Mashariki

MHE. JOB Y. NDUGAI aliliuza:-

Kwa kuwa, Jumuiya ya Afrika Mashariki imeanza kazi zake kwa miaka kadhaa sasa na kwa kuwa moja ya madhumuni ya ushirikiano huo ni kukuza biashara kati ya Kenya, Uganda na Tanzania:-

- (a) Je, tangu kuanzishwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Tanzania imeuza bidhaa zenyе thamani gani Kenya na Uganda?
- (b) Je, Kenya na Uganda wameingiza Tanzania bidhaa zenyе thamani gani?

NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalı la Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Mbunge wa Kongwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swalı la Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Mbunge wa Kongwa, lenye sehemu (a) na (b) ningependa kutoa maelezo yafuatayo:-

Mkataba wa uanzishaji Jumuiya ya Afrika Mashariki uliwekwa saini na Marais wa Tanzania, Kenya na Uganda tarehe 30 Novemba 1999. Baada ya Mkataba huo kuridhiwa na Mabunge yote ya nchi, wanachama, ulianza kutumika rasmi tarehe 7 Julai, 2000. Ili kuweza kukuza biashara kati ya nchi wanachama, Itifaki ya kuanzisha Umoja wa Forodha iliwekwa saini na wakuu wa nchi wanachama tarehe 2 Machi, 2004 na Umoja wa Forodha ulianza kutekelezwa tarehe 1 Januari, 2005.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba sasa kujibu swalı la Mheshimiwa Job Ndugai Ndugai, Mbunge wa Kongwa kama ifuatavyo:-

(a) Kati ya mwaka 1997 hadi 2005, Tanzania imeuza bidhaa zenyе thamani ya takribani Dola za Kimarekani milioni 488.10 Kenya na Uganda. Kati ya hizo bidhaa zenyе thamani ya Dola za Kimarekani milioni 403.7 ziliuzwa nchini Kenya na bidhaa zenyе thamani ya Dola za Kimarekani milioni 84.4 ziliuzwa nchini Uganda. Kwa hiyo, Tanzania inauza bidhaa nyingi nchini Kenya kuliko Uganda.

(b) Katika kipindi hicho, Kenya na Uganda ziliingiza nchini bidhaa zenyet thamani ya jumla ya takribani Dola za Kimarekani milioni 1,033.4. Kati ya hizo bidhaa zenyet thamani ya Dola za Kimarekani, milioni 982.6 ziliagizwa kutoka Kenya na bidhaa zenyet thamani ya Dola za Kimarekani milioni 50.8 ziliagizwa kutoka Uganda. Kwa hiyo, Tanzania inaagiza bidhaa nyingi zaidi kutoka Kenya kuliko Uganda.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ukweli kwamba Tanzania inaagiza bidhaa nyingi zaidi kutoka Kenya ni kweli vile vile kwamba kumekuwepo na ongezeko kubwa la mauzo ya bidhaa kutoka Tanzania kwenda Kenya na Uganda. Mauzo ya bidhaa kutoka Tanzania kwenda Kenya na Uganda yameongezeka kutoka Dola za Kimarekani milioni 24.4 mwaka 1997 hadi Dola za Kimarekani milioni 96.4. Mwaka 2005 ikiwa ni ongezeko la asilimia 300 ambalo ni ongezeko kubwa ukilinganisha na bidhaa zilizoagizwa kutoka Kenya na Uganda ambazo ziliongezeka kutoka Dola za Kimarekani milioni 97.6 mwaka 1997 hadi dola za kimarekani milioni 160.4 mwaka 2005 sawa na ongezeko la asilimia 64.

Aidha, Serikali inatoa wito kwa Watanzania kutumia fursa ya soko la Afrika Mashariki kwa kuuza zaidi bidhaa za kilimo na viwanda katika soko kubwa la Afrika Mashariki. Bidhaa zinazolishwa Tanzania hazitozwi ushuru wowote zinapouzwa Kenya na Uganda. (*Makofii*)

MHE. JOB Y. NDUGAI: Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri na shukrani zaidi kwa kuwa wiki mbili zilizopita alifika Kibaigwa Kongwa kutoa maelezo kwa upande zaidi kuhusiana na masuala ya Afrika Mashariki. Nina maswali mawili kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa katika majibu yake amesema kwamba ushuru wa forodha wa pamoja umeanza tarehe 1 Januari, 2005 ningependa kujua tangu kuanza kwa zoezi hilo la ushuru wa pamoja Tanzania tumekuwa tukinufaika vipi?

(b) Lakini la pili, kwa kuwa katika kuuza bidhaa katika nchi za Afrika Mashariki lazima mfanyakishara awe na (*Certificate of Original*) cheti cha uasili wa bidhaa anayotaka kuiuza katika nchi jirani. Hivi cheti hicho kinapatikana wapi? Je, inawezekana sehemu kama Kibaigwa kwenye soko la Kimataifa pakawepo ofisi ya kutoa cheti kama hicho? (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Spika, tangu kuanza kwa umoja wa forodha Tanzania tumenufaika kwa mambo mengi lakini uniruhusu nitaje machache. Moja, mapato ya Tanzania kati ya biashara ya ndani ya Afrika Mashariki yameongezeka kwa asilimia 8. Lakini vile vile mauzo ya bidhaa kutoka Tanzania kwenda Kenya na Uganda yameongezeka kwa asilimia 30. Lakini pamoja na ukweli kwamba mauzo yetu yameongezeka kwa asilimia 30 manunuzi kutoka Kenya kuja Tanzania yameongezeka lakini kwa asilimia 24 wakati ya kwetu yameongezeka kwa asilimia 30.

Mheshimiwa Spika, vile vile kama mlivyoona katika Bajeti ya Wizara ya Fedha iliyosomwa hapa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ni kwamba mapato yanayotokana na ushuru wa forodha ya Tanzania kwa kipindi cha kati Julai 2005 hadi Machi 2006 yameongezeka kwa asilimia 52 na huu ni ushahidi kwamba tulikuwa makini katika majadiliano ya kuanzisha ushuru wa forodha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, faida nyingine tulioipata ukiangalia mwaka 1997 urari wa biashara kati Tanzania na Nchi za Afrika Mashariki ulikuwa na upungufu wa milioni 74 lakini hivi sasa upungufu umeshuka hadi shilingi 64 na tunatarajia utaendelea kushuka kadri tunavyojipanga.

Mheshimiwa Spika, swal la pili, Mheshimiwa Job Ndugai, alitaka kujua kwamba Kibaigwa vile vile wanaweza kupata *Certificate of Origin* nasema wanaweza kupata kwa sababu utaratibu uliopo ni kwamba bidhaa zinazozalishwa Afrika Mashariki utaratibu uliopo ni kwamba bidhaa zinazozalishwa ndani ya Afrika Mashariki inabidi zipate *Certificate of Origin* ili kuondoa hatari ya bidhaa kutoka nje ya Afrika Mashariki na zikauzwa ndani ya Afrika Mashariki. Kinachotakiwa ni mambo mawili moja bidhaa hiyo ioneerane imezalishwa ndani ya Afrika Mashariki kwa asilimia 100, lakini pili, hata kama mali ghafi ya kuzalisha bidhaa hiyo, imetoka nje ya nchi iwe na sifa tatu. Moja, walau bidhaa hiyo (*CIF*) *cost insurance and flight* isiwe zaidi ya 60 iliyotumika kuzalisha bidhaa hiyo lakini bidhaa hiyo iliyozalishwa walau iwe na ongezeko la thamani la asilimia 35 lakini vile vile iwe imeandikishwa katika *rules of origin* ni kwamba imezalishwa hapa Afrika Mashariki. (*Makofi*)

MHE. ALOYCE B. KIMARO: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba swal moja kama ifuatavyo:-

Mimi nina habari kwamba kuna kampuni inayotaka kuuza bia Kenya, lakini Tanzania Breweries pamoja *East African Breweries* waliwekeana mikataba ambayo inakataza bia kutoka Tanzania kwenda Kenya. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anasema nini kuhusu hilo? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Spika, labda niseme tu Watanzania anayetakiwa kutoa *Certificate of Origin* au hati ya bidhaa asilia ni *Tanzania Tembo of Commercial, Industry and Agriculture* na hawa wanaweza wakatoa ngazi ya Taifa, wakatoa ngazi ya Mkoa wakatoa hata ngazi ya Wilaya. Kwa hiyo, kampuni yejote ile kabla ya kusema kwamba imenyimwa ruhusa ya kuuza bidhaa nchini Kenya lazima kwanza ionyeshe kwamba kwa barua hii iliomba *Certificate of Origin* ikakataliwa. Kwa sababu hiyo, nitamwomba Mheshimiwa Mbunge, tuwasiliane baadaye ili kupata maombi ya hiyo kampuni iliomba kuuza bidhaa zake Kenya na ikakataliwa. Tukianzia hapo tutaweza kujua ni kwa nini walikataliwa.

Lakini ningependa nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba masuala ya biashara huwa kuna mikataba, lakini mikataba siyo Biblia inaweza ikarekebishwa. Kama yalitokea matatizo wakakosea kwenye huo mkataba na sasa unaleta matatizo tatalitazama na Serikali ipo kuondoa matatizo ili biashara iweze kuendelea ndani ya Afrika Mashariki. (*Makofi*)

Walimu kwa Jamii ya Wafugaji

MHE. KAIKA S. TELELE (K.n.y. MHE. MICHAEL LEKULE LAIZER)
aliuliza:-

Kwa kuwa viongozi wakuu wa nchi (Marais) waliotangulia kila mmoja kwa wakati wake waliweka wazi kuwa ni muhimu kuwapa wafugaji kipaumbele kwenye suala la elimu ili kuifanya nchi yetu isiwe na matabaka ya watu wenye elimu na wasio na elimu na kwa kuwa, walisisitiza kujengwa kwa shule za bweni katika maeneo ya wafugaji:-

- (a) Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya kujenga shule za bweni pamoja na sekondari ili kuwasaidia wafugaji?
- (b) Je, Serikali ya Awamu ya Nne itatekeleza ahadi yake ya kutoa kipaumbele kwa wafugaji?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWAMTUMU BAKARI MAHIZA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Michael Lukule Laizer, Mbunge wa Longido, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, Serikali inautambua umuhimu wa elimu kwa watoto wa maeneo ya jamii wa wafugaji. Katika jitihada za kuwasaidia watoto hao Serikali imekuwa ikichangia ujenzi wa hosteli na kusaidia kuziendesha. Kwa mfano mwaka 2005/2006 Serikali imechangia ujenzi wa hosteli katika shule za Kitumbanne, Engutoto katika Mkoa wa Arusha na Oltukai katika Mkoa wa Manyara. Serikali itaendelea kujenga *Hostel* katika maeneo hayo kwa kadri fedha zitakavyopatikana.
- (b) Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutekeleza ahadi yake ya kutoa kipaumbele kwa jamii ya wafugaji kwa kusaidiana na wananchi wa maeneo hayo, ili kuhakikisha kuwa *hostel* zinajenga na zinahudumiwa. Katika mwaka huu wa fedha 2006/2007 *hostel* tano (5) zimepangwa kujengwa katika maeneo ya wafugaji. (*Makofii*)

MHE. KAIKA S. TELELE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona na kunipa nafasi. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Nataka niulize kwamba kwa kuwa hii ni ahadi na kwa kuwa Mheshimiwa Rais wakati anafanya kampeni ya kugombea nafasi hii aliyoipata aliahidi mambo mbalimbali katika sehemu mbalimbali nchini. Je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba sasa ni wakati muafaka ahadi hii nayo iwekwe katika orodha ya Mheshimiwa Rais ili iweze kutekelezwa katika Awamu hii ya Serikali ya Awamu ya Nne?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA): Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali ya Awamu ya Nne ina nia madhubuti ya kutimiza ahadi zilizotolewa na Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni na kwa kuzingatia hivyo ndiyo maana Wizara yangu imetenga fedha kwa ajili ya mabweni matano, kwa ajili ya maeneo ya wafugaji. Hata hivyo, tupo tayari kushirikiana nao endapo wananchi wenyewe wataanza kwa juhudhi zao nasi tutahakikisha kwamba tunasaidia. Ahadi zote zilizotolewa na Rais upande wa Elimu tutazitekeleza kwa awamu kwa kadri fedha itakavyopatikana. (*Makofii*)

Na. 330

Shule ya Sekondari ya Milambo

MHE. SIRAJU J. KABOYONGA aliuliza:-

Kwa kuwa Shule ya sekondari ya Milambo ya Mjini Tabora ina historia ndefu sana, ambapo zamani ilijulikana kwa jina la *St. Mary's* na ni shule ambayo Baba wa Taifa, Mwalimu J.K. Nyerere alipata kusoma na baadaye kufundisha katika shule hiyo na hivi sasa ni mionganoni mwa shule teule za Tanzania kwa wanafunzi wenye vipaji maalum.

Kwa kuwa mazingira ya shule hii ni mabaya sana kwa sababu ya majengo yake kukosa matengenezo ya mara kwa mara, vyoo vyake ni vibovu, mabati ni mabovu, jiko la shule, mabweni na samani za shule zina hali mbaya sana, pia kuna uhaba mkubwa wa maji, hali ambayo inahatarisha afya za wanafunzi, walimu na wafanyakazi wa shule hiyo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kurekebisha hali hii inayotishia afya za wanafunzi pamoja na kushughulikia mapungufu makubwa ya samani za wanafunzi ili kukidhi mahitaji muhimu yanayotakiwa kuwepo hapo shulenii?

NAIBU WAZIRI ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, Mbunge wa Tabora Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kuititia Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES) 2004-2009, imepanga kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika shule 100 za sekondari za kitaifa kwa kufanya ukarabati wa majengo yake kwa awamu ikiwemo shule ya Sekondari ya Milambo. Pamoja na kwamba mwaka 2004/2005 shule hiyo ilipelekewa shilingi milioni 55 kwa ajili ya ukarabati, katika mwaka huu wa 2006/2007 Wizara yangu itawatuma Wataalam ili kubaini hali halisi kabla ya kupeleka fedha za ukarabati pamoja na upatikanaji wa maji katika shule hiyo.

MHE. SIRAJU J. KABOYONGA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali au maswali ya nyongeza. Kwanza nashukuru kwa jibu la jumla, nasema nasisitiza jibu la jumla. Swali langu lilikuwa *specific* kwa ajili ya Milambo *Secondary School* Tabora jibu lililotolewa linazungumzia kwenda kupitia shule nyingine 100 nchi nzima. Jibu hilo lingekuwa la kujumlisha tu kwamba pamoja Milambo tunakwenda kwenye shule nyingine 100. Maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, shule hii ina historia ya kipekee hapa nchini kama nilivyoeleza kwenye swali langu. Kwa hiyo, kwa kumuenzi Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, ningombwa jibu *specific* kwa swali *specific*. (*Makofi*).

Wizara ilikuwa na swali hili kwa takriban miezi miwili na nusu. Huyo mtaalam wa kutathmini kwa nini asingekuwa amepelekwa ili leo tupate jibu, Serikali inafanya nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na Shule ya Milambo kupewa nafasi yake katika historia ya nchi hii. Kuna shule za *Tabora Girls* na *Tabora Boys* nazo zinahitaji nafasi maalum kwenye historia ya nchi hii. Na zenyewe ziko hoi bin taaban. Kwa hiyo, nataka nisisitize watakapotumwa hao wataalam kwenda kutazama hali ya mashule, shule za Tabora kwa sababu ya umuhimu wake kihistoria, ki-inchi zipewe uzito unaostahili? Nakushukuru. (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA): Mheshimiwa Spika, mwaka 2004/2005 ilionekana shule nyingi hazipati fedha za kutosha kwa ajili ya ukarabati na ndiyo maana shule zile za kitaifa zikiwemo shule hizi za Tabora zilipewa fedha na ndiyo maana katika jibu langu la msingi limesema hivi, shule ya Milambo katika shule zile 100 za kitaifa ilipewa shilingi milioni 55 kwa ajili ya ukarabati.

Kati ya fedha hizo shilingi milioni 49,695,273 zilinunulia samani zikiwepo vitanda 115, mabenchi 94 na meza 47 kwa ajili ya bwalo na madawati 143 na viti 243 kwa shilingi milioni 2,300,000. Fedha hizi zilitumika kukarabati madarasa matatu. Sh.2,999,700/= kwa ajili ya ujenzi wa choo cha shule hii ya sekondari ya Milambo.

Mwaka huu zimetengwa shilingi bilioni 1, kwa ajili ya ukarabati wa shule 30 tu za sekondari ambazo ni za kitaifa na fedha hizi zitapelekwa pia katika shule ya Milambo ili kuangalia kama haikukamilika iweze kukamilishwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inazingatia sana kuangalia shule hizi za kitaifa na zenye historia zisiendelee kuharibika ili ziweze kutengenezwa zifiki katika kiwango ambacho ni cha kuridhisha. (*Makofii*)

Na. 331

**Wanawake wajane kufuutilia malipo ya
Urithi Bila Mafanikio**

MHE. FAIDA MOHAMED BAKARI aliuliza:-

Kwa kuwa wanawake wengi wajane pale wanapokwenda kudai mafao ya urithi katika sehemu husika wanapata tabu kwa kucheleweshwa au kukosa kabisa malipo hayo:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kurahisisha upatikanaji wa urithi kwa wajane?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Faida Mohamed Bakari, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa wajane wamekuwa wanapata tabu kupata malipo ya mirathi. Ili malipo ya mirathi yasiendelee kuchelewa Serikali imechukua hatua mbalimbali kama ifuatavyo:-

- (i) Kuwaandikia barua waajiri wote wanaohusika na uletaji Hazina nyaraka pungufu kuwataka kuleta nyaraka kamilifu.
- (ii) Kutoa Waraka unaowaelekeza Waajiri wote juu ya nyaraka zinazotakiwa ziambatane na majalada ya Marehemu/Wastaafu yanapoletwa Wizara ya Fedha.
- (iii) Wizara yangu imewaelekeza wawakilishi wake kwenye vikao vya pensheni, kutoa elimu kwa waajiri hao wakati wa vikao na kuwataka kutoa elimu hiyo kwa watumishi wao na hasa wajane.

Mheshimiwa Spika, jitihada hizo zimeweza kupunguza baadhi ya kero na zimeweza wananchi wengi kuelewa taratibu za mirathi hasa kwa upande wa Jeshi la Wananchi ambako ndiko kulikuwa na matatizo mengi ya wajane kutolipwa kwa wakati. Nasema hivyo kwa sababu sasa hivi Wizara yangu inapata madai mengi sana ya mirathi na mengine ni ya nyuma sana kama miaka 10 iliyopita, hii inaonyesha kuwa wahusika walikuwa hawajui au hawakuwa wanaelewa taratibu za mirathi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, hatua zinaandaliwa kuwapeleka Wahasibu wa Pensheni Mikoani na Wilayani ili kufuatilia nyaraka hizo muhimu na kutoa elimu kwa Waajiri husika juu ya kuandaa na kutuma nyaraka kamilifu Hazina. Aidha, inakusudiwa kuweka masharti ya makusudi kwa Waajiri husika kuhakikisha majalada ya mirathi na ya wastaafu watarajiwa hayaletwi Hazina kabla ya kuhakikisha yana nyaraka kamili zinazohitajika kuandaa malipo. Wizara yangu inatarajia kuwa hatua hizi zitapunguza kwa kiasi kikubwa matatizo ya wajane na warithi kucheleweshewa malipo ya mirathi. (*Makofi*)

MHE. FAIDA MOHAMED BAKARI: Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa kunipatia nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kumwuliza maswali haya yafuatayo:-

Kwa kuwa ufuutiliaji huu wa urithi hasa wa fedha una urasimu mkubwa kama alivyosema ye ye mwenyewe. Je, endapo mrithi naye anafariki kabla ya kurithi naye hana mrithi fedha hizo zinapelekwa wapi? (*Makofi*)

Swali la pili, kwa kuwa kuna baadhi ya watu kabla ya kufa huandika wosia wa urithi. Je, Serikali hulichukulia umuhimu gani urithi huu wa wosia?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO): Mheshimiwa Spika, kuna utaratibu wa Mahakama na tuna Kabidhi Wasii Mkuu ambaye anashughulikia masuala kama hayo na tuna Kabidhi Wasii Mkuu ambaye anashughulikia masuala kama hayo endapo mrithi kafariki lazima kutakuwa na watu wengine ambao wanaelewa familia ile. Wanachotakiwa ni kwenda kwa Kabidhi Wasii Mkuu ambaye atawasaidia kuhakikisha kwamba wale ndugu zake wengine watapa urithi. (*Makofi*)

MHE. JOHN S. MALECELA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza namshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini kwa kuwa swali hili limeulizwa mara nyingi sana na majibu yanayotoka Serikalini yanakuwa mazuri lakini kwa uhakika hayalingani na vitendo vinavyotendeka kwenye Ofisi inayohusika. (*Makofi*)

Kwamba kuna wafanyakazi wa Serikali amba wamekuwa wakidai, ndugu zao wakidai mafao yao wengine zaidi ya miaka 6 na kama ilivyosemekana wengine baadhi yao wamefariki sasa wajane wao wanadai, inachukua muda mrefu. Je, Waziri yuko tayari kuturuhusu sisi Wabunge kwenye majimbo yetu kama tunao watu wenye matatizo ya namna hiyo, tumworodheshee aende akayashughulikie na halafu atuarifu? Je, Serikali iko tayari kufanya hivyo? (*Makofi*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, kwanza nakubaliana naye kwamba tatizo hili limekuwa ni kero nchini na linahitaji hatua za haraka. Tunakubaliana na pendekemo lake kwamba Wabunge walete majina ya watu walio na matatizo hayo na Serikali itachukua hatua mara moja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, ndiyo maana wote tunakupenda. (*Kicheko/Makofi*)

**Kuvitambua Vitambulisho vya Kupigia Kura
Kwa Matumizi mbalimbali**

MHE. SAID J. NKUMBA (K.n.y. MHE. MGANA I. MSINDAI) aliuliza:-

(a) Je, Serikali inaweza ikaeleza kwa nini inakataa kuvitambua vitambulisho vya wananchi walivyopewa na Tume ya Uchaguzi, kwa ajili ya kupigia kura wanapokwenda Posta, *TTCL* na kadhalika, kuchukua fedha zao, Regista na kadhalika?

(b) Je, Serikali haioni kwamba, hivi ndivyo vitambulisho halali kabisa kuliko mtindo wa zamani wa kutumia stakabadhi za kulipia kodi au kadi za vyama mbalimbali?

(c) Kama Serikali imeelewa mantiki ya sehemu (a) na (b) ya swali hilo. Je, ipo tayari kutoa agizo kuanzia sasa kwenye Ofisi zote zikiwemo Posta, *TTCL* na kadhalika, waanze kutambua vitambulisho hivyo?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Mgana Izumbe Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utambulisho wa wananchi katika nchi yoyote ni suala lenye umuhimu mkubwa. Hapa nchini Serikali na Taasisi zake inatambua aina mbalimbali za utambulisho, kwa mfano vitambulisho vya kazi, utambulisho wa hati za kusafiria (pasipoti) na kadhalika.

Katika uchaguzi uliopita, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilitoa vitambulisho kwa waliojiandikisha kupiga kura. Vitambulisho hivi vilitolewa chini ya Sheria ya Uchaguzi ya mwaka 1985, hivyo vina uhalali wa kisheria. Japokuwa madhumuni ya vitambulisho hivyo yalikuwa kuwatambua wapiga kura, lakini baada ya uchaguzi watu wengi hasa wakulima vijijini wapo wanavitumia kama utambulisho vyao.

Hoja ya Mheshimiwa Mbunge kwamba baadhi ya Taasisi zinakataa kutambua utambulisho huu, iwapo ni ya kweli, basi wanaoukataa utambulisho huu wanafanya makosa. Kauli ya Serikali ni kwamba hadi hapo Serikali itakapotoa vitambulisho vya uraia, vitambulisho vya aina zinazotambuliwa na sheria za nchi, kama vitambulisho vya kazi, pasipoti, pamoja na vitambulisho vya mpiga kura ni ruhusa kutumika. Ruhusa hii itakoma pale Serikali itakapoanza kutoa vitambulisho vya uraia.

Kwa hiyo, Taasisi zote zinazotoa huduma mbalimbali kwa mfano Posta, *TTCL*, na kadhalika zinaagizwa kukubali vitambulisho vya kupigia kura kama moja ya utambulisho halali hadi hapo vitambulisho vya uraia vitakapotolewa Wizara ya Mambo ya Ndani.

MHE. JUMA H. KILLIMBAH: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Lakini nina swali dogo la nyongeza. Kutokana na swali alilouliza hivi vitambulisho vya kupigia kura ni kweli vimeenea mahala pote kwa sababu ndiyo ilikuwa utaratibu kwa nchi nzima. Lakini namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kueleza kwamba mashirika ya Posta na *TTCL* na mengine yapokee vitambulisho hivyo.

Je, sasa Serikali inaweza inasemaje kuhusiana na vitambulisho hivi kutumika kama kwa kwenda kuwadhamini watu wanapokuwa na kesi katika Mahakama au wanapokuwa Polisi kwa sababu wananchi walio wengi vijijini wanapata tabu sana kuhusiana na suala la dhamana?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kwa kuwa vitambulisho hivi vinatambulika kisheria ni ruksa kwa wananchi kuvitumia wanapokwenda kutoa dhamana kwa wananchi wenzao. (*Makofi*)

Na. 333

Kuhamishwa Askari Polisi

MHE. SALIM HEMED KHAMIS aliuliza:-

Kwa kuwa Ibara ya 147 (3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inazuia majeshi ya ulinzi ukiwemo Jeshi kujiingiza katika masuala ya kisiasa, na kwa kuwa baada ya uchaguzi mkuu wa tarehe 14 Desemba 2005, askari Polisi walibadilishwa dhamana zao za kazi na kupewa uhamisho katika baadhi ya vituo vya Wilaya ya Pemba jambo ambalo liliibua hisia nyingi za kisiasa:-

- (a) Je, ni kitu gani hasa kilicholeta mabadiliko hayo?
- (b) Kwa nini mabadiliko haya yalihu vito maalum tu ambavyo viongozi wake walikwisha lalamikiwa mapema na askari wenywewe?
- (c) Ikitainika kuwa Wakuu wa vito husika waliendesha zoezi hilo kisiasa.
Je, Serikali italitolea kauli gani zoezi hilo?

WAZIRI WA USALAMA WA RAIA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mbunge, wa Chambani, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, uhamisho uliotolewa kwa baadhi ya askari Polisi waliokuwa Pemba mara baada ya Uchaguzi Mkuu, ulikuwa ni uhamisho wa kawaida wenye lengo la kuboresha utendaji wa kazi za Polisi.

(b) Mheshimiwa Spika, mabadiliko yaliyofanyika yalihusu askari kutoka vituo vingi nchi nzima na siyo Vituo vya Pemba tu. Zoezi hilo linaendelea kwa nchi nzima hadi sasa ambapo askari wa vyeo mbalimbali, wakiwemo Makamanda wa Polisi wa Mikoa, wamekuwa wakibadilishwa vituo vya kazi kwa kadri haja ya kufanya hivyo inapotokea.

(c) Mheshimiwa Spika, kifungu cha 60 cha *Police General Orders (PGO)* kinaeleza utaratibu wa uhamisho wa Askari na Maafisa. Katika zoezi la kuhamisha askari, wakuu wa vituo hawana mamlaka ya kumhamisha askari. Uhamisho wa askari hutolewa na Makao Makuu ya Polisi kwa vigezo maalum vya utendaji na mahitaji na siyo vigezo vya kisiasa.

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Ahsante Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo:- Kutokana na mabadiliko ya uongozi na utendaji wa Jeshi la Polisi Watanzania walio wengi sasa hivi wamejenga imani na jeshi lao. Je, mabadiliko haya yatafika lini kule Pemba ambako baadhi ya Wakuu wa Vituo tayari wamelalamikiwa wanafanya kazi kinyume na Katiba ya nchi? Ahsante.

SPIKA: Anaomba Mheshimiwa Waziri urudie swali. Halikusikika vizuri.

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Mheshimiwa Spika, kutokana na mabadiliko ya uongozi na ya utendaji katika Jeshi la Polisi Watanzania walio wengi sasa hivi wamejenga imani na jeshi lao. Je, mabadiliko haya yatafika lini kule Pemba ambako tayari baadhi ya Wakuu wa Vituo wamelalamikiwa kuwa wanafanya kazi kinyume na Katiba ya nchi? Ahsante. (*Makofi*)

WAZIRI WA USALAMA WA RAIA: Mheshimiwa Spika, zoezi hili limekuwa likifanyika, hata Pemba na tumeanza kule kwanza majina ya Maofisa ambao walihamishwa na vituo vyao ni kama ifuatavyo:-

ASP Saleh Mohamed Saleh, kutoka Mkuu wa Upelezei Wilaya ya Chake Chake kwenda kuwa Mkuu wa Polisi Wilaya ya Micheweni. *ASP* Aziz Juma Mohamed, kutoka kuwa Mkuu wa Upelezei Wilaya ya Wete, kuwa Mkuu wa Upelezei Wilaya ya Chake Chake.

ASP Rajab Khamis Hafidh, kutoka *OCD* Wilaya Micheweni kwenda *FFU* Mkao Mjini Magharibi Mjini Unguja. Inspeksa Hamad Nassor Mselem kutoka Upelezei kituo cha Konde kwa *OCD, OCCID* Wilaya ya Wete.

Inspeka Said Khamis Ali kutoka *OCCID*, Wilaya ya Micheweni kwenda Upelelezi, Makao Makuu ya Polisi Zanzibar. Kwa hiyo, zoezi hili tumekuwa tunalifanya na tutaendelea kulifanya. (*Makofi*)

MHE. FATMA MUSSA MAGHIMBI: Ahsante Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swalii la nyongeza. Kwa mujibu wa orodha aliyotoa Mheshimiwa Waziri ya uhamisho. Je, haoni kwamba ni sawa sawa na kuhamisha tatizo puanii akalipeleka mdomoni? (*Kicheko/Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri majibu. Anasema kumtoa mtu Wete na kumpeleka Chake Chake.

WAZIRI WA USALAMA WA RAIA: Mheshimiwa Spika, sababu ziko nyingi za kufanya hivyo, wakati mwingine watu wamekaa kwa muda mrefu, wamekuwa na mazoea na raia wa mahali pale. Kwa hiyo, unawapeleka katika mazingira mengine na wanakuwa na utendaji ambao ni mzuri zaidi.

SPIKA: Ingawa si kawaida Spika, kutoa maoni, nadhani swalii hili bado halijajibiwa. Kwa hiyo, tunaendelea Wizara hiyo hiyo. (*Kicheko*)

Na. 334

**Uchakavu wa Majengo wanaoishi askari
Ndani ya Boma la Ziwani**

MHE. FATMA OTHMAN ALLY aliuliza:-

Kwa kuwa majengo mengi yaliyokuwemo ndani ya Boma la Ziwani yamebomolewa, hasa mabanda wanayoishi askari na mengi yamechakaa. Je, Serikali ina mpango gani wa kuyajenga majengo yaliyobomoka na kuyakarabati yaliyochakaa?

WAZIRI WA USALAMA WA RAIA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Fatma Othman Ali, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tatizo la kubomoka au kuchakaa kwa majengo ndani ya makambi ya Jeshi la Polisi si la Kambi ya Ziwani pekee. Kama Mheshimiwa Mbunge amewahi kutembelea sehemu mbalimbali nchini, atakubaliana nami kuwa tatizo hili ni la nchi nzima. Ujenzi au ukarabati wa nyumba za kuishi askari umekuwa ukisusua kwa sababu ya uwezo wetu mdogo kiuchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Wizara yangu ina mpango wa miaka kumi kuanzia mwaka wa fedha 2003 hadi 2013 wa kupunguza tatizo hilo, ambapo katika kipindi hicho, tunatarajia kujenga nyumba 37,000 za kuishi askari. Kukamilika kwa ujenzi wa kambi ya *FFU Mfikiwa – Chake Chake Pemba* ni moja ya utekelezaji wa mpango huo. Kwa kuwa ujenzi unakwenda kwa awamu kwa nchi nzima, kipaumbele kinalekezwa kwenye maeneo yaliyoathirika zaidi. Kwa upande wa Zanzibar, maeneo yatakayoshughulikiwa ni pamoja na Ziwanî, Finya, Tunguu, Uguju, Ukuu, Chuo cha Polisi Zanzibar na nyumba za kuishi Makamanda wa Polisi Mkoa wa Kaskazini Uguju. Kwa kutambua ufinyu wa Bajeti na ukubwa wa tatizo la nyumba za kuishi askari, Wizara yangu inaendelea kuwasiliana na Taasisi, Mashirika na Makampuni yatakayokuwa tayari kujenga nyumba nyingi kwa kipindi kifupi kwa mkopo, utakaokuwa ukilipwa kwa awamu na kwa riba nafuu kulingana na makubaliano yatakayofikiwa. Mpaka sasa yapo makampuni na taasisi kadha ambazo zimeonyesha nia ya kushirikiana nasi, ikiwemo *PPF, NSSF* na Kampuni ya ujenzi ya Kichina inayojenga Uwanja wa Taifa iitwayo *Beijing Construction Engineering Group Co.Ltd. (T). (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, endapo mpango huu utafanikiwa, utarahisisha usambazaji wa huduma za ujenzi haraka sehemu mbalimbali nchini, ikiwemo kambi ya Ziwanî. Nia ya Serikali ni kuyavunjavunja mabanda hayo anayoyazungumzia Mheshimiwa Fatma na kujenga majengo ya ghorofa. Hatua hii pia itainenzi kambi hiyo kuhusu umaarufu wake wakati wa harakati za Mapinduzi ya Zanzibar.

Na. 335

Utoaji wa Huduma ya Posta na Benki

MHE. EPHRAIM N. MADEJE aliuliza:-

Kwa kuwa nchi nyingi duniani, mashirika na kampuni za Posta ndogo hutoa huduma za benki na posta na walengwa ni wananchi wa kawaida hasa vijijini:-

- (a) Je, ni kwa kiwango gani kutenganishwa kwa Shirika la Posta na Benki ya Posta mwaka 1992 kumeathiri utoaji wa huduma hizo muhimu kwa wakazi wa vijijini?
- (b) Je, Serikali haioni kwamba, huu ni wakati muafaka wa kuziunganisha huduma hizo muhimu ili kukidhi kiu ya wananchi hasa wa vijijini ya kuhudumiwa na mtandao mzuri wa Posta na Benki yake?

WAZIRI WA MIUNDOMBINU alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ephraim Nehemia Madeje, Mbunge wa Dodoma Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kutenganishwa kwa Shirika la Posta na Benki ya Posta mwaka 1991/1992 kulifanyika kwa nia nzuri ya kuimarisha sekta ya Benki kulingana na uboreshaji na uimarishaji uliotakiwa kufanyika kwa mujibu wa Sheria ya Taasisi za Fedha na Mabenki ya mwaka 1991 na vile vile kuingiza taaluma ya kibenki kwa kiwango kizuri katika uendeshaji na usimamizi wa masuala ya fedha na kibenki katika uliokuwa uwakala wa Benki kupitia Shirika la Posta Tanzania.

Mheshimiwa Spika, takriban vituo zaidi ya themanini (80) vya Shirika la Posta Tanzania vilisitisha utoaji wa Huduma za Benki ya Akiba ya Posta wakati wa zoezi la urekebiushaji wa Shirika hilo baada ya kutenganisha kisheria Huduma za Posta na Huduma za simu za lililokuwa Shirika la Posta na Simu Tanzania. Hatua zilizochukuliwa za kupunguza għarama za utoaji wa huduma za msingi za posta katika mtandao kwa kuteua wakala wa Posta (*Postal Agents*) kuendesha vituo hivyo kuliviondolea uwezo wa kisheria kuendesha huduma za uwakala wa kibenki. Wananchi waliokuwa wamezoea kupata huduma hiyo kupitia vituo hivyo iliwabidi kufuata huduma za uwakala wa Benki katika Ofisi za Posta za Wilaya au zile zilizobakia katika uendeshaji wa wafanyakazi wa kudumu wa Shirika la Posta Tanzania. Hivi sasa ni Posta moja tu wakala (*Franchised Post Office*) ya Peramiho yenze kibali cha Benki Kuu ya Tanzania (*BoT*) kuendesha uwakala wa Benki ya Posta Tanzania. (*Makofi*)

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inakubaliana na maoni ya Mheshimiwa Mbunge kuwa ni wakati muafaka wa kutafakari namna ya kuzidi kuboresha utaratibu wa utoaji wa huduma za Posta na Benki ya Posta ili ziwfikie wananchi walio wengi nchini, hususan wale waishio vijjjini. Mkakati unakamilishwa wa kuanzisha mfumo utakaoziwezesha Taasisi hizi mbili (Posta na Benki ya Posta) kutoa huduma kwa kushirikiana na siyo kwa kuunganishwa pamoja. Aidha, hatua zinazochukuliwa ni pamoja na kukamilishwa kwa zoezi la kuzifanyia marekebisho ya taasisi hizi kwanza, kuziweka katika hali ya kukopesheka ili zizidi kupata mtaji wa kutosha kuwekeza katika miradi ya maendeleo. Serikali inafanya juhudzi za kukamilisha mchakato wa kuzirekebisha Taasisi za Posta na Benki yake kisha, baadaye Mshauri Mtaalam (*Consultant*) anatafutwa ili kufanya uchambuzi na kuwasilisha ushauri na mapendekezo Serikali kuhusu namna bora na muafaka ya muundo wa taasisi na mfumo wa utaratibu wa utoaji huduma kwa wananchi kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Mbunge avute subira wakati huu hatua zinapochukuliwa. (*Makofi*)

MHESHIMIWA ANNA M. KOMU: Mheshimiwa Spika, nimeridhika kabisa na majibu aliyotoa Mheshimiwa Waziri, lakini nina swalí moja dogo tu naomba nimwulize. Naomba anihakikishie kwamba Je, nyumba hiso mpya zinazojengwa, ni za vyumba viwili au vitatu? Maana kujenga chumba kimoja na kiukumbi ni yale yale tunayozungumza ya kupoteza maadili ya watoto wetu. Kwa hiyo, naomba anihakikishie ramani ya ujenzi wa nyumba hiso, ahsante. (*Makofi*)

WAZIRI WA USALAMA WA RAIA: Mheshimiwa Spika, nakubaliana na ye ye kabisa kama sisi wenywewi Wabunge tusingependa tukaa nyumba moja tunashea vyumba

karibu karibu, askari na wenyewe ni binadamu kwa hiyo katika mpango wa nyumba hizi mpya, tutahakikisha kwamba nyumba hizi zina vyumba vyaa kutosha, ili kukidhi na kuonyesha ubinadamu kufanyika. (*Makofî*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umekwisha, na sasa nina matangazo, zaidi yanahu wageni, kwa sababu imekuwa sio rahisi utamaduni huu kuukwepa, mgeni wa kwanza ni Ndugu Hamid Suleiman Said, mgeni wa Mheshimiwa Lawrence Masha, Mbunge wa Nyamagana ambaye pia ni Naibu Waziri wa Nishati. Huyu ni Mwenyekiti wa Mtaa wa *Nyerere Road Mwanza*. (*Makofî*)

Mheshimiwa Dr. Lucas Siyame, na Mheshimwia Godfrey Zambi, Wabunge hawa wawili wa Wilaya ya Mbozi wana wageni wao Madiwani 34, kutoka Halmashauri ya Mbozi wakiongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo anaitwa Aden Mwakyombe, karibuni sana Waheshimiwa Madiwani. (*Makofî*)

Mheshimiwa Alyoce Kimaro, aliomba nimirambulish, Meja Jesse Makundi, nadhani huyu ndiye aliye kuwa Mbunge miaka ya nyuma, yule pale. Huyu ni Mbunge mstaa fu, karibu sana. Mheshimiwa Naibu Waziri Dr. David Mathayo David, Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, anaugen i wataalam watatu, kutoka mkoa wa Kilimanjaro, ambao wamekuja kujifunza namna Bunge linavyoendesa kazi zake kidemokrasia, hao ni Regnald Kombania, Rogathe Bene na Bilivia Riwa, wale pale karibuni sana. (*Makofî*)

Pia tunao upande wangu wa kushoto, kwenye *Public Gallery*, wanafunzi wengine 100 wa shule ya sekondari ya wasichana ya Msalato, pamoja na walimu wao, karibuni sana, karibuni sana vijana wetu. Shule ya Msalato ni shule ya vipaji maalum. Kwa hiyo, mnao waona hapo baadhi yao ndio ma-scientist wa baadaye, Wabunge, Mawaziri na kadhalika. (*Makofî*)

Pia kutoka Kibaha ni wageni maalum kweli kweli hawa kwa sababu ya hali zao kuna wageni hawa Bi. Happiness Shaban kutoka Kibaha, ni wafanyakishara ndogo ndogo lakini ni wale mavu, Bi. Happiness Shaban yeye haoni, ni mlema vu ambaye haoni yule pale. Bi. Tatu Kondo, yeye hasikii, ni mlema vu ambaye aasikii, Bi. Prisca Joshuwa Mwakasendile, yeye ni mkalimani, anayawenza yote hayo, anaweza kutafsiri. (*Makofî*)

Bwana Idrisa Ngulungu, ni mtoto kiongozi wa mlema vu wa macho haoni na ni mfugaji kuku, yaani haoni lakini ni mfugaji wa kuku, na bwanan Ramadhan Lubata ni kiongozi wao, yule amesimama pale anapunga mkono, karibu sana tunawashukuru sana kwa kuja kushuhudia au kusikia jinsi Bunge linavyoendesa kazi zake, na mwisho lakini si mwisho kwa umuhimu, sasa ni wageni wa Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, kama ifuatavyo:

Kwanza ni mwalimu wa viungo wa timu ya Taifa ya Tanzania ambaye anatoka Brazil, Bwana Haimo Hamoro, halafu, mgeni wetu mpya na kwa wale wanaopenda mpira wa miguu, huyu ndiye ameletwa kujaribu kukomboa mpira wa Miguu wa Tanzania. Kocha Mkuu wa timu ya taifa, Bwana Marco Maximo. Pamoja na hiyo *thanks*, sasa sijui

ki-Brazil wala Kireno, kwa hiyo namshukuru tu *thank you*. Pia wako viongozi wa shirikisho la mchezo wa mpira wa miguu *TFF* wakiongozwa na Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Michezo Ndugu Iddi Omar Kipingu, pia yupo Mtangazaji wa vipi vyta Michezo kutoka Zanzibar *FM Redio*, Bi Mwanaidi Abdul, yule pale. (*Makofit*)

Waheshimiwa Wabunge, sasa ni taarifa ya Kikao, Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi, Mheshimiwa Gideon Cheyo, anawatangazia Wajumbe kwamba kutakuwa na kikao cha Kamati leo tarehe 2 Agosti, 2006 saa tano asubuhi hii katika ukumbi Namba 428, kikao ni kifupi. Mnaombwa kuhudhuria, ni kikao kifupi lakini ni muhimu sana kupata maamuzi. Kwa hiyo, saa tano asubuhi hii, Kamati ya Kilimo na Ardhi Chumba Namba 428. (*Makofit*)

Waheshimiwa Wabunge, mwisho wa matangazo, Katibu endelea na *Order Paper*. (*Makofit*)

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2006/2007 Wizara ya Habari Utamaduni na Michezo.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa likubali kujadili na kuitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo na taasisi zake kwa mwaka wa fedha wa 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Awamu ya Nne ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Napenda pia kumpongeza sana Rais wa Zanzibara Mheshimiwa Amani Abeid Karume. Napenda pia Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais na kuitishwa na Bunge lako tukufu kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, napenda nikupongeze wewe Mheshimiwa Samuel John Sitta, kwa kuchaguliwa na Bunge hili kuwa Spika wake na Mheshimiwa Anne Semamba Makinda, kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika. Pia napenda kuwapongeza Mawaziri na Naibu Mawaziri wote kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuongoza Wizara mbali mbali. Vile vile nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuchaguliwa na wengine kuteuliwa kuwa Wabunge wa Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowasa, Mbunge wa Monduli, Waziri wa Mipango Uchumi na Uwezeshaji, Mheshimiwa Dr. Juma Alifa Ngasongwa, Mbunge wa Ulanga Magharibi na Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Zakia Hamdani Meghji, Mbunge wa Kuteuliwa, kwa hotuba zao nzuri zilizoweka wazi utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi, hali ya uchumi wetu, malengo na mikakati ya utekelezaji wa mipango ya Serikali katika kipindi cha mwaka wa 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuchukua fursa hii kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, inayoongozwa na Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Mbunge wa Peramiho, iliyojadili na kutoa ushauri kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara yangu tarehe 5 Juni, 2006. Ushauri na maelekezo yaliyotolewa na Kamati hii tumejitahidi kuyaingiza katika bajeti hii na tutaendelea kuyafanya kazi maelekezo ya Kamati yaliyobakia na yale yatakayotolewa na Bunge lako Tukufu wakati wa kujadili Bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, Kuundwa Kwa Wizara, Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo iliundwa mapema mwaka huu kwa Tangazo la Serikali Na. 1 la mwaka 2006 na kukabidhiwa majukumu ya kuongoza, kusimamia na kuratibu shughuli za Habari, Utamaduni na Michezo nchini. Dira ya Wizara ni kuhakikisha tunakuwa na Taifa lenye raia wenye ufahamu, Taifa linalothamini Utamaduni wake na Taifa lenye wananchi mahiri na hodari katika michezo.

Mheshimiwa Spika, dhamira ya Wizara katika Sekta ya Habari ni kuwa na Taifa lenye vyombo vya habari vingi na vinavyozingatia sheria, maadili ya taaluma na ya jamii na vinavyoshiriki kikamilifu katika juhudzi za maendeleo ya nchi yetu na kudumisha umoja na mshikamano wa Kitaifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika Sekta ya Utamaduni, Wizara inakusudia kupanua fursa kwa Watanzania kujenga na kudumisha maadili mema, kupata burudani, na kutumia fami mbalimbali za utamaduni, hususan sanaa, katika kujiletea maendeleo ya kiuchumi na kijamii na kuwajenga Watanzania wajivunie Utanzania wao.

Mheshimiwa Spika, Kupitia sekta ya Michezo, Wizara inadhamiria kujenga jamii yenye kuthamini mazoezi ya viungo vya mwili na michezo kwa ajili ya maendeleo, afya, amani, uchumi, kupunguza umaskini, kuongeza umri wa kuishi, na kuleta ushindi na furaha kwa jamii.

Mheshimiwa Spika, Dhima ya Wizara, dhima ya Wizara ni kukuza utaifa kwa kupanua haki ya raia kupata na kutoa habari, kujenga na kudumisha maadili ya Taifa na kukuza na kuendeleza michezo.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza dhima hii, Wizara inakusudia kuweka mazingira yanayoruhusu ukuaji wa sekta ya Habari iliyo imara na adilifu, inayowezesha wananchi kufaidi haki yao ya kupata na kutoa habari.

Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara inadhamiria kuimarisha uendeshaji, usimamizi na miundombinu ya Utamaduni kwa kutoa huduma kwa usawa na kwa haki kwa Watanzania ili kuwaletaa maendeleo na burudani.

Mheshimiwa Spika, pia, Wizara inanuia kuendeleza Michezo kwa kuwezesha utoaji wa ufundi na utaalamu wa kujifunza kucheza kwa ustadi na kwa ufundi, na kuwa

na mazingira bora ya kuchezea kwa ajili ya afya, burudani, ushindani na maendeleo ya Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, Majukumu ya Wizara, Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo ina majukumu yafuatayo:-

- § Kuandaa Sera za Sekta ya Habari, Utamaduni na Michezo.
- § Kusimamia utekelezaji wa Sera za Habari, Utamaduni na Michezo.
- § Kuandaa mipango ya ukuzaji wa sekta ya habari, utamaduni na michezo.
- § Kuhamasisha uanzishaji wa vyombo vya Habari katika maeneo ambayo hayavutii sekta binafsi.
- § Kukuza na kuimarisha fani mbalimbali za sanaa nchini hususan sanaa za maonyesho, ufundi na muziki kama kielelezo cha utaifa na chanzo cha ajira.
- § Kuimarisha na kukuza Kiswahili ambacho ni lugha ya Taifa letu. Aidha, kuhimiza lugha za kiasili ambazo ni vijenzi vya lugha ya Taifa na kuhimiza mafunzo ya lugha za kigeni kwa ajili ya mawasiliano ya kimataifa.
- § Kuimarisha utawala bora katika michezo nchini.
- § Kuimarisha mafunzo yanayohusu fani za Wizara kwa watumishi wa Wizara.
- § Kuongeza na kuimarisha miundombinu inayotakiwa kwa Wizara.
- § Kuratibu shughuli za asasi zilizo chini ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo.
- § Kuandaa na kusimamia Viwango vya Ubora wa kazi za Habari, Utamaduni na Michezo.
- § Kukuza na kuimarisha ushiriki wa wananchi katika fani mbalimbali, mazoezi, michezo na michezo ya jadi.
- § Kusimamia Maendeleo ya Watumishi katika fani ya Habari, Utamaduni na Michezo.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya 2005/2006, katika Sekta ya Habari, Wizara ilikuwa na malengo yafuatayo:-

- § Kutoa mafunzo kwa wanahabari wenye vipaji katika taaluma maalumu, pamoja na taaluma yenyewe ya habari, ili waweze kuyasanifu na kuyachambua masuala

ya fani mahususi kama vile utamaduni, michezo, kilimo, uchumi, siasa, sheria na ulinzi katika vyombo mbali mbali.

- § Kuinua ubora wa taaluma ya habari pamoja na viwango vya elimu vya wanahabari; kulinda maadili na uhuru wa vyombo vya habari almradi uhuru huo hauvuki mipaka ya sheria, mila, desturi na silka za Taifa letu.
- § Kuhakikisha kwamba Watanzania wanamiliki angalau asilimia 51 ya hisa za vyombo vya habari vinavyoanzishwa na wawekezaji kutoka nje.
- § Kuhakikisha kuwa uendeshaji wa vyombo vya habari unakuwa mikononi mwa Watanzania, na kwamba wageni wanaajiriwa tu kama utaalamu unaohitajika haupatikani nchini.
- § Kuhakikisha Vyuo vya Habari vilivyopo nchini vinatoa taaluma ya fani hii kwa viwango vinavyokubalika kitaifa na kimataifa.

Mheshimiwa Spika, katika Sekta ya Utamaduni, Wizara ilikuwa na malengo yafuatayo:-

- § Kuweka mipango madhubuti itakayokiwezesha Kiswahili kuwa chanzo kimojawapo cha ajira, hasa ya walimu wa lugha ya Kiswahili nchi za nje kama vile Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo, Rwanda, Burundi, Uganda, Libya na kadhalika.
- § Kuanzisha na kusimamia mafunzo ya wakalimani na wafasiri kwa kushirikiana na Chuo kikuu cha Dar es Salaam kutokana na kuwepo upungufu mkubwa wa wataalamu wa fani hizi humu nchini.
- § Kuhimiza matumizi ya lugha za asili za Tanzania zikiwa ni vijenzi vya lugha ya Taifa, yaani Kiswahili, na kudumisha utamaduni wetu.
- § Kuwezesha sanaa za uchongaji, ufinyanzi, uchoraji, muziki, ngoma na tamthiliya kuwa vyanzo vya ajira kwa kuwapatia wasanii mafunzo ya kuboresha sanaa zao, stadi za masoko, hakimiliki na hakishiriki.
- § Kuelekeza na kuzihimiza fani za utamaduni kama vile sanaa za maonyesho, ufundi na muziki ili kukuza uzalendo, amani, upendo, umoja na mshikamano wa Taifa letu.
- § Kuhimiza matumizi ya sanaa katika kuhamasisha na kuelimisha jamii kuhusu masuala ya kisiasa, kiuchumi na kijamii.
- § Kuweka misingi imara ya matumizi ya maarifa yaliyopo juu ya mila na desturi kwa kushirikiana na vikundi vingine vya utafiti kama vile Chuo Kikuu, mambo ya kale na nyaraka za Taifa.

Mheshimiwa Spika, katika Sekta ya Michezo, Wizara ilikuwa na mipango ifuatayo:-

- § Kutatua migogoro ya michezo nchini ambayo inaviza na kudidimiza maendeleo yake, kwa kuhakikisha kuwa vilabu vya michezo vinakuwa na katiba bora zinazofuatwa kikamilifu. Aidha na viongozi wake kuwa wanachaguliwa kwa wakati.
- § Kuhakikisha timu za Tanzania zinashiriki vema katika mashindano ya kimataifa, na kupata ushindi ili kuwaletea wananchi furaha michezoni. Azma hii itatekelezeka kwa kuandaa programu maalumu za mafunzo kwa wachezaji wa michezo mbalimbali hasa vijana na kurejesha mashindano ya michezo kikanda na kitaifa yatakayowezesha kupata wachezaji wazuri kuanzia ngazi za vijiji, wilaya na mikoa.
- § Kukamilisha ujenzi wa Uwanja wa kisasa jijini Dar es Salaam. Pia, kuongeza na kuimarisha miundombinu ya michezo nchini, ikiwemo viwanja na vifaa vya michezo ili kuinua kiwango cha mazingira ya kufundishia, kujifunzia na kuchezea michezo.
- § Kuimarisha Chuo cha Maendeleo ya Michezo cha Malya kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa walimu wengi zaidi wa michezo, hivyo kukabiliana na upungufu mkubwa wa walimu wa michezo nchini.
- § Kuweka mipango ya kupata makocha wa kimataifa wa michezo mbalimbali maarufu nchini, ukiwemo mpira wa miguu.
- § Kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu kufufua na kuimarisha michezo shulen kwa kuhakikisha kila shule ina mwalimu wa michezo, somo la michezo linafundishwa na kutahiniwa, na shule za sekondari zenye mchepuo wa Michezo zinaanzishwa.
- § Kuandaa na kurati^{ib}u mjadala wa kitaifa kuhusu mustakabali wa michezo nchini.
- § Kushirikiana na vyombo vinavyohusika ili kurejesha maeneo yaliyovamiwa na watu ili nayo yatumike kuendeleza michezo na burudani.
- § Kushirikiana na vyombo vinavyohusika kuimarisha mapambano dhidi ya UKIMWI kwa wanamichezo na wafanyakazi wa wizara.

Mheshimiwa Spika, sasa napenda kutoa maelezo ya Utekelezaji wa Malengo ya Wizara katika mwaka wa fedha wa 2005/2006 na kazi zitakazotekelzeza katika mwaka 2006/2007. Wizara yangu imezingatia ILANI ya Uchaguzi ya CCM 2005 (Ibara Na. 96 – 97 na 118), Dira ya Maendeleo 2025 pamoja na sera za uchumi za ujumla na za kisekta katika kuandaa malengo na mpango wa bajeti 2006/2007. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Taarifa kwa Kila Idara, Idara ya Habari, Habari ni moja ya Sekta za huduma za jamii nchini. Sekta hii inatoa huduma ambayo ni haki ya msingi ya raia kama inavyotamkwa kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Ibara ya 18, ambayo inasema:-

- § Anao uhuru wa kuwa na maoni na kueleza fikra zake;
- § Anayo haki ya kutafuta, kupokea na kutoa habari bila kujali mipaka ya nchi;
- § Anao uhuru wa kufanya mawasiliano na haki ya kutoingiliwa katika mawasiliano yake; na
- § Anayo haki ya kupewa taarifa wakati wote kuhusu matukio mbalimbali muhimu kwa maisha na shughuli za wananchi na pia kuhusu masuala muhimu kwa jamii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, malengo ya Wizara kuhusu Idara ya Habari yalitekelezwa kama ifuatavyo:-

- § Serikali ilipeleka Bungeni muswada wa Sheria wa kurekebisha Ibara ya 18 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ili kuondoa masharti ya haki na uhuru huo kuzingatia matakwa ya sheria nyingine. Haki hiyo sasa haiingiliwi na sheria nje ya Katiba.
- § Wadau wa Sekta ya Habari wameanza mchakato wa kuandaa mapendekezo ya rasimu ya muswada wa Sheria itakayotawala vyombo vyote vya habari hapa nchini. Pamoja na mambo mengine, mapendekezo hayo yatajumuisha haki ya raia kupata taarifa zenye manufaa kutoka taasisi za utumishi wa umma na uanzishwaji wa chombo cha kuratibu viwango vya elimu na taaluma ya uandishi wa habari. (*Makofi*)
- § Wizara na Idara zinazojitegemea zimeanzisha Vitengo vya Habari ambavyo vitashirikiana na Idara ya Habari katika kuwapatia wananchi, kupitia vyombo vya habari, taarifa muhimu zenye manufaa kwa umma. Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatarajiwu kuanzisha vitengo vya habari kuanzia mwaka wa 2006/2007.
- § Idadi ya vyombo vya Habari imeendelea kukua. Idadi ya magazeti ya kila siku imeongezeka kutoka mawili mwaka 1992 hadi kufikia magazeti 15 mwezi Januari, 2006. Aidha, idadi ya magazeti ya kila wiki imeongezeka kutoka matano mwaka 1992 hadi kufikia magazeti 40 mwezi Januari, 2006. Kadhalika idadi ya vituo vya redio katika Tanzania Bara imeongezeka kutoka kituo kimoja mwaka 1992 hadi kufikia vituo 33 mwezi Januari, 2006. Tanzania Bara hivi sasa ina vituo vya televisheni 32 ikiwemo Televisheni ya Taifa (TVT) iliyoanzishwa mwaka 2000.

Wakati Sera ya Habari inatolewa mwaka 1993, kulikuwa hakuna hata kituo kimoja cha TV Tanzania Bara. Baadhi ya vituo hivyo vya TV ni mali ya Serikali za Mitaa na Halmshauri za Wilaya na Miji.

- § Aidha, idadi ya Vyuo vya Uandishi wa habari imeongezeka kutoka viwili mwaka 1992 hadi tisa mwaka wa 2006, ambapo vitatu kati ya vyuo hivyo ni Vyuo Vikuu. Vile vile, Tume ya Utangazaji Tanzania, ilioanzishwa mwaka 1993 kusimamia Sekta ya Utangazaji, iliunganishwa na Tume ya Mawasiliano kuanzisha Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*TCRA*). Ni dhahiri kuna ongezeko kubwa la Vyombo vya Habari na Vyuo vya Uandishi wa Habari kimkoa.
- § Hadi Desemba, 2005, kulikuwa na kampuni za huduma za intaneti 25. Idara za Serikali, Mashirika na Asasi zimeanzisha tovuti zao ili wananchi wapate habari kupitia mtandao huo wa kompyuta.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Utangazaji Tanzania, Taasisi ya Utangazaji Tanzania (TUT), ilianzishwa mwaka 2003 kwa Tangazo namba 239. Majukumu makuu ya TUT ni kutoa huduma za utangazaji wa Radio na Televisheni na kumiliki na kuendeleza rasilimali za Radio Tanzania Dar es Salaam na Televisheni ya Taifa. Kwa sasa TUT inamiliki Radio Tanzania Dar es Salaam (*RTD*) na Televisheni ya Taifa (TVT). Katika mwaka 2005/2006, TUT imetekeleza kazi zifuatazo:-

- Kuifanyia matengenezo ya kawaida mitambo ya kurushia matangazo ya *RTD* katika vituo vya Arusha, Mbeya, Mwanza, Kigoma, Nachingwea, Songea na Dodoma.
- § Kuimarisha mitambo yake ya utangazaji kwa njia ya satelaiti.
- § Kujenga vituo vya *FM Radio* katika mikoa ya Arusha, Dodoma, Mwanza na Tabora ili kuongeza usikivu.
- Ujenzi wa vituo vya kurushia matangazo ya TVT katika mikoa minane ya Mbeya, Tanga, Mara, Kagera, Kigoma, Lindi, Mtwara na Tabora. Kukamilika kwa vituo hivyo kumeongeza idadi ya vituo vya kurushia matangazo ya TVT kufikia 12. Mikoa mingine yenye vituo vya kurushia matangazo ni Dar es Salaam, Pwani, Arusha, Dodoma na Mwanza.
- TUT imeongeza muda wa kurusha matangazo ya TUT kufikia saa 24. Hivyo, TVT hivi sasa inapatikana kwa saa 24 katika mikoa yote yenye mitambo ya kurushia matangazo ya TVT.
- TUT imeongeza pia muda wa kurusha matangazo ya *FM Radio* yake iitwayo *PRT* kufikia saa 24.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Magazeti ya Serikali, Kampuni ya Magazeti ya Serikali ilianzishwa mwaka 1970 kwa Sheria ya Makampuni Namba 212 ya mwaka

1968. Kazi ya Kampuni hiyo ni kuchapisha magazeti ya *Daily News* na *Sunday News*. Kama ilivyoelezwa katika Bunge la Bajeti la 2005/2006, Serikali iliipatia Kampuni jengo la ofisi pale Dar es Salaam. Aidha Kampuni imeagiza mtambo mpya wa kuchapa magazeti. Mtambo huu unatarajiwa kuwasili hapa nchini mwezi Septemba, 2006. Mtambo utakapofungwa utaongeza sana ufanisi wa utendaji kazi wa Kampuni hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninafurahi kutangaza kwamba kampuni hiyo ya magazeti ya Serikali inatarajia kuanzisha gazeti la Kiswahili la kila siku katika mwaka wa fedha wa 2006/2007, ili kuiongezea Serikali nyenzo za mawasiliano na wananchi.

- § Mheshimiwa Spika, kuhusu Mafunzo ya Taaluma ya Habari. Mwaka 2003, Chuo cha zamani cha Uandishi wa Habari (*TSJ*) kiliunganishwa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ili kiweze kutoa Shahada za Habari na Mawasiliano. Chuo hicho, ambacho sasa kinajulikana kwa jina la *Institute of Journalism and Mass Communications (IJMC)* ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kilikuwa na zaidi ya wanafunzi 180 hadi Aprili, 2006. Wanafunzi wa kwanza wa shahada za uandishi wa habari na mawasiliano watahitimu mwaka 2006/2007.
- § Vyuo Vikuu binafsi vya *St. Augustine* cha Mwanza, na Tumaini cha Iringa tayari vinatoa mafunzo ya fani za Habari na Mawasiliano. Madhumuni ya hatua hizi za Serikali ni kupata wahitimu wengi wenye kiwango cha juu cha elimu ya mawasiliano ya umma na uandishi wa habari.
- § Vyuo vya Uandishi wa Habari hivi sasa vinapaswa kujisajili na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundji (*NACTE*) ili kuhakikisha kuwa vinatoa mafunzo ya kiwango kinachotakiwa. Idadi ya vyuo vya Uandishi wa Habari ambavyo vipo katika hatua mbali mbali za usajili ni tisa. Pamoja na mambo mengine Usajili huzingatia taratibu zilizowekwa na Serikali za miundombinu na rasilimali za kutosha kuendesha mafunzo.

Mheshimiwa Spika, Vyombo vya Utangazaji, Wizara yangu ina jukumu kuu la kufuatilia vipindi vyote vinavyorushwa na vituo mbalimbali vya utangazaji na kuhakikisha kwamba yanaendana na maadili ya nchi. Katika kuzingatia hilo, sheria iliyounda Mamlaka ya Mawasiliano imejumuisha uundwaji wa Kamati ya Maudhui ili kuhakikisha kwamba maudhui ya vipindi vinavyorushwa na vituo mbalimbali vya utangazaji vinakidhi mahitaji ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, Malengo ya mwaka 2006/2007, katika mwaka wa 2006/2007 Idara ya Habari imepanga kutekeleza mipango ifuatayo:-

- § Kuanzisha Tovuti ya Habari kwa umma itakayotumiwa na wananchi kuelezea kero zao za maisha na kutoa maoni mbalimbali yatakayoisaidia Serikali katika utekelezaji wa mipango yake;
- § Kupendekeza Serikalini muswada wa Sheria kuhusu upatikanaji wa haki ya wananchi ya kupata na kutoa habari;
- § Kupendekeza Serikalini uanzishwaji wa chombo kitakachoratibu na kusimamia kisheria viwango vya elimu na taaluma ya HABARI;
- § Kuanzisha mtandao kati ya Idara ya Habari na Vitengo vya Habari vya Serikali;
- § Kufungua ofisi za habari katika Mikoa ya Kigoma, Mbeya, Mtwara, Mwanza na Rukwa na kuimarisha zilizopo kwa vifaa na mafunzo;
- § Kuchapisha kila mwezi magazeti yenye kuhamasisha maendeleo ya wananchi na kutoa taarifa za utekelezaji wa shughuli za Serikali;
- § Kuimarisha Vitengo vya Habari katika Wizara na Idara zinazojitegemea na kuanza mchakato wa kuanzisha vitengo hivyo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi nyingine za utumishi wa umma;
- § Kuendelea kusajili magazeti na vituo vya redio na televisheni;
- § Kueneza usikivu na kuonekana kwa vipindi vya *RTD* na *TVT* nchi nzima;
- § Kuongeza muda wa kurusha matangazo ya *RTD* na *TVT* kufikia saa 24;
- § Kuendelea kuinua ubora wa taaluma ya Habari;
- § Kuanzisha gazeti la Kiswahili la Serikali;
- § Kuendelea kuimarisha Idara ya Habari ambayo ni Msemaji Mkuu wa Serikali, kuongeza wafanyakazi, kutoa mafunzo na kununua vifaa vya kisasa vya kutenda kazi;
- § Kukarabati maktaba ya Taifa ya Kumbukumbu ya Picha iliyopo Dar es Salaam; na
- § Kuimarisha Kitengo cha Serekali cha kufutilia maudhui ya Redio, Magazeti na Televisheni.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Maendeleo ya Utamaduni katika mwaka wa 2005/2006 Idara ya Maendeleo ya Utamaduni imetekeliza malengo yafuatavyo:-

- § Kuandaa na kuendesha Mkutano Mkuu wa tatu wa mwaka wa Sekta ya Utamaduni tarehe 23-27, Januari, 2006, mjini Morogoro, mkutano ambao ulihudhuriwa na washiriki 157;
- § Kuendesha Tamasha Maalumu la Utamaduni lenye lengo la kuimarisha umoja, amani, mshikamano na upendo mionganoni mwa Watanzania kuanzia Oktoba 13 hadi Oktoba 16, 2005, hapa Dodoma;
- § Kuendesha mafunzo ya mbinu za utawala na uendeshaji wa shughuli za utamaduni kwa Maafisa Utamaduni na wadau wa utamaduni 120 wa wilaya manispaa na majiji;
- § Kufanya utafiti katika Mikoa mitano (Kagera, Lindi, Mbeya, Mwanza na Manyara) ili kubaini mila na desturi nzuri zinazoweza kuimarisha ufanisi katika vita dhidi ya Virusi vya UKIMWI (VVU), umaskini, rushwa na ubaguzi wa kijinsia na kubainisha mila na desturi ambazo ni kikwazo katika vita hii na kushauri wananchi kuachana nazo;
- § Kuimarisha ukuzaji wa Kiswahili sanifu kwa wizara, idara na mashirika, kwa kuendesha warsha ya kukuza matumizi ya Kiswahili sanifu na fasaha kwa vyombo vya habari iliyofanyika tarehe 13 Februari, 2006, jijini Dar es Salaam, ambapo jumla ya wanahabari 70 kutoka vyombo mbali mbali vya habari walishiriki;
- § Warsha ya wadau wa filamu na sanaa za Jukwaani ilifanyika jijini Dar es Salaam tarehe 27-29 Julai, 2005, kukiwa na jumla ya washiriki 60; na
- § Mfuko wa Utamaduni umeendesha mafunzo kwa vikundi katika nyanja mbalimbali za Utamaduni na kuwaenzi wasanii mahiri katika wiki ya Mfuko kuanzia tarehe 1 – 8 Desemba 2005. Miradi 77 imefadhiliwa mwaka 2004/2005, ambapo mwaka 2005/2006 Mfuko wa Utamaduni ulifadhili miradi 54.

Mheshimiwa Spika, Malengo ya mwaka 2006/2007, katika mwaka 2006/2007 Idara ya Maendeleo ya Utamaduni itaendelea kukuza, kuendeleza na kueneza Utamaduni kwa kutekeleza yafuatayo:-

- § Kuendesha mafunzo ya mbinu za utawala na uendeshaji wa shughuli za utamaduni kwa Maofisa Utamaduni wa Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji.
- § Kutathmini mradi wa “Tuseme” kwa wasichana wa shule za Sekondari na za Msingi.
- § Kufanya utafiti wa lugha za asili kwa makabila ya nchi yetu ili kukuza msamati wa Lugha ya Kiswahili.

- § Kuendesha warsha 2, semina 1 na mukutano 1 ili kuimarisha matumizi ya Kiswahili sanifu na fasaha kwa Wizara, Idara za Serikali na Mashirika na Umma.
- § Kuandaa na kuendesha Mkutano Mkuu wa Nne wa Sekta ya Utamaduni; utakaofanyika Novemba, 2006.
- § Kuratibu na kusimamia uendeshaji wa Tamasha la Utamaduni kitaifa litakalofanyika mwezi Mei, 2007.
- § Kuendelea na tafiti katika mikoa ili kubaini mila na desturi nzuri katika maendeleo ya taifa.
- § Kuendelea kuendesha mafunzo kwa wafanyakazi wa sekta ya Utamaduni kwa ajili ya kuwapatia mbinu sahihi za kujikinga dhidi ya VVU na UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, Kujenga Jumba la Utamaduni, katika mwaka wa 2006/2007, Wizara itaanza mchakato wa kujenga Jumba la Utamaduni la Taifa hapa Jijini Dar es Salaam. Jumba hili litajumuisha sehemu ya maonyesho ya sanaa, maigizo, kituo cha habari za utamaduni, utunzaji wa kumbukumbu za utamaduni wa historia ya nchi yetu. Malengo ya mwaka 2006/2007 ni kumpata Mshauri Mwelekezaji na kuandaa michoro ya jengo.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Ukaguzi wa Filamu, Bodi ya Filamu iliundwa kwa Sheria ya Bunge namba 4 ya mwaka 1976. Majukumu makuu ya Bodi ya Ukaguzi wa Filamu ni:-

- § Kuhakikisha filamu na michezo ya kuigiza zinawajibika na zinawiana na kawaida, mila, desturi na maadili mema ya Tanzania.
- § Kuhakikisha filamu na michezo ya kuigiza zinawapa Watanzania burudani yenyelimu na mafunzo mema, safi na stahili.
- § Kuhakikisha filamu na michezo ya kuigiza nchini Tanzania zinakuwa zenye viwango stahili vya usanii na ujumi (*aesthetics*).
- § Kuhakikisha usanii na uhuru wa ubunifu wa sanaa hauzuiliwi na kuwekewa vipingamizi bila sababu za msingi.
- § Kuhakikisha ukuaji wa maendeleo ya fani za michezo ya kuigiza na filamu unawiana na unalingana na mabadiliko halisi ya msimamo na mtazamo wa jamii ya Watanzania kuhusu maadili mema.

Katika mwaka 2005/2006 Bodi ya Ukaguzi na Filamu na Michezo ya Kuigiza ilitekeleza kazi zifuatazo:-

- § Kukagua, kutoa ushauri wa kitaalamu na kupanga filamu 2,000 katika madaraja, mikanda ya video 5,000 na programu mbalimbali za televisheni 1,000 kabla ya kuonyeshwa kwa watazamaji.

- § Kuendesha warsha kwa waratibu 21 wa Mikoa kuhusu mbinu na ujuzi wa kisasa wa kutoa huduma kwenye ofisi za Bodi ya Ukaguzi wa Filamu na Michezo ya Kuigiza katika Mikoa na Wilaya kwa kuzingatia maadili mema ya utamaduni wa Taifa letu.
- § Kuendesha warsha ya kuandaa mapendekezo ya kurekebisha Sheria Na. 4 ya mwaka 1976 ya Bodi ya Filamu na Michezo ya Kuigiza.

Malengo kwa mwaka 2006/2007. Katika mwaka 2006/07 Bodi ya Ukaguzi wa Filamu na Michezo ya Kuigiza itatekeleza kazi zifuatazo:-

- § Kuendesha warsha ya wadau wa filamu na sanaa za jukwaani.
- § Kulinda maadili ya Taifa kwa kukagua filamu, kanda za video, sanaa za jukwaani, majumba ya sinema na vipindi vya televisheni.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Sanaa Bagamoyo, Chuo cha Sanaa Bagamoyo kilianzishwa mwaka wa 1981. Chuo cha Sanaa Bagamoyo kilikusudiwa mahususi kuwafunza wahamasishaji na mameneja wa sanaa kwa ajili ya maendeleo ya sanaa nchini. Majukumu makuu ya Chuo ni:-

- § Kutoa mafunzo na ushauri wa kitaalamu kwa wasanii ili kukuza uzalendo na upenzi wa kufanya sanaa asilia za Tanzania.
- § Kukuza matumizi ya teknolojia ya kisasa katika michezo ya kuigiza na sarakasi.
- § Kutembelea maeneo yote nchini kuhamasisha na kutoa elimu kwa kutumia sanaa kwa maendeleo ya jamii.

Katika mwaka 2005/2006 Chuo cha Sanaa Bagamoyo kilitekeleza kazi zifuatazo:-

- § Kuendesha mafunzo ya Stashahada kwa washiriki 90 na mafunzo ya muda mfupi kwa wasanii 120 walio kazini katika Chuo cha Sanaa Bagamoyo.
- § Kuendesha Tamasha la Sanaa la 24 la Kimataifa Chuo cha Sanaa Bagamoyo tarehe 11 Septemba hadi 16 Septemba, 2006.

Katika mwaka 2006/2007 Chuo cha Sanaa Bagamoyo kitatekeleza kazi zifuatazo:-

- § Kuendesha mafunzo ya Stashahada kwa Washiriki 100 na mafunzo ya muda mfupi kwa wasanii 120 walio kazini katika Chuo cha Sanaa Bagamoyo.
- § Kuendesha Tamasha la 25 la Kimataifa la Chuo cha Sanaa Bagamoyo litakalofanyika mwezi Septemba, 2006.
- § Kukarabati Jengo la Maonyesho ya Sanaa.
- § Kujenga hosteli ya wanafunzi.

Chuo cha Sanaa Bagamoyo kiko katika mchakato wa kuwa Wakala wa Serikali.
(*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Utamaduni ulianzishwa mwaka 1998. Mfuko ulianzishwa kwa ajili ya kugharamia uhifadhi na uendelezaji wa Utamaduni. Katika kipindi cha 2005/2006 Mfuko wa Utamaduni ulitekeleza majukumu yafuatayo:-

- § Mfuko ulifadhili jumla ya miradi 71 kwa kutoa misaada ya jumla ya Sh. 416,906,707/=.
- § Mfuko wa Utamaduni umeendesha mafunzo katika nyanja mbali mbali za Utamaduni na kuwaenzi wasanii mahiri sita katika Wiki ya Mfuko kuanzia tarehe 1 – 8 Desemba, 2005.

Katika mwaka 2006/2007 Mfuko wa Utamaduni utatekeleza kazi zifuatazo:-

- § Utaendelea kutambua, kuenzi na kufadhili shughuli za utamaduni ili zichangie maendeleo ya sekta.
- § Kutambua, kuenzi na kutunuku watu na asasi zinazojitokeza kwa kufanya kazi zilizo bora na za kutukuka, ili kuhamasisha umma kujihusisha na shughuli za utamaduni.
- § Kujenga ushirikiano kwa kuwakutanisha watu wa hali na fani mbalimbali ili wajadili na kupeana mawazo na ujuzi wa kuboresha shughuli na mipango ya sekta. Kiambatisho 2 kilichoko ukurasa wa 62 kinaonyesha mchanganuo wa miradi iliyofadhiliwa na mfuko huu.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), Baraza la Sanaa la Taifa limeundwa kwa Sheria ya Bunge Na. 23 ya mwaka 1984. Majukumu makuu ya Baraza hili ni pamoja na:-

- § Kusimamia maendeleo ya sanaa zifuatazo:- Sanaa za Maonyesho, Sanaa za Muziki na Sanaa za Ufundu.
- § Kufanya utafiti wa maendeleo ya uundaji na ubunifu wa kazi za sanaa na utafutaji wa masoko ya kazi hizo ikiwa ni pamoja na kufanya utafiti wa viwango na thamani ya kazi za sanaa zinazofanywa Tanzania.
- § Kutoa huduma za ushauri na misaada ya kiufundi ambayo ni ya lazima au ya nyongeza katika kuendeleza shughuli za sanaa kwa mashirika ya umma na kwa watu mbalimbali wanaojishughulisha na kazi hizi.
- § Kuandaa mipango na kuratibu shughuli za sanaa zinazofanywa na watu mbali mbali Tanzania.

- § Kuishauri Serikali juu ya mambo yahusuyo maendeleo ya ubunifu wa kazi za sanaa nchini.
- § Kuhimiza maendeleo ya kazi za sanaa kwa kuandaa na kufanya maonyesho, kucheza ngoma, kuendesha warsha, semina na mashindano baina ya wasanii mbalimbali.
- § Kuandaa sheria ndogo ndogo na kuzisambaza kwa wadau.
- § Kuweka mfumo wa usajili wa watu wanaojipatia kipato kutokana na kucheza muziki, kutengeneza zana za muziki, kurekodi kwenye santuri au kanda kwa ajili ya matumizi au wanaojishughulisha na kazi inayohusiana na muziki.

Katika mwaka 2005/2006 Baraza la Sanaa la Taifa lilitekeleza mambo yafuatayo:-

- § Baraza lilitoa elimu ya hakimiliki na hakishiriki katika Mikoa ya Mtwara, Lindi, Singida, Rukwa na Pwani, na mafunzo ya uboreshaji wa sanaa za Muziki kwa wasanii Vijijini katika Wilaya ya Mtwara, Lindi Vijijini, manispaa ya Singida, Iramba, Sumbawanga Mjini na Vijijini na Wilaya ya Bagamoyo. Jumla ya wasanii 1,101 walipata mafunzo hayo.
- § Baraza lilitoa mafunzo ya uboreshaji sanaa za maonyesho, sanaa ya muziki na ufundu katika Mikoa ya Morogoro, Tanga, Arusha, Kilimanjaro, Pwani na Dar es salaam kwa wasanii 250. Aidha, mafunzo ya uongozi na utawala wa vikundi yalitolewa.
- § Baraza liliratibu programu ya utoaji tuzo za wanamuziki kuanzia ngazi ya mikoa, ambapo wasanii chipukizi 1,100 kutoka Mikoa ya Arusha, Mbeya, Mwanza na Dodoma walijitokeza. Wasanii 25 walipata tuzo za kitaifa za wanamuziki bora nchini tarehe 3/6/2006.

Mheshimiwa Spika, Malengo ya Mwaka 2006/2007, katika mwaka 2006/2007 Baraza la Sanaa la Taifa litatekeleza mambo yafuatayo:-

- § Kutoa mafunzo ya uboreshaji sanaa ya muziki, ufundu wa mikono, ngoma, sarakasi, tamthiliya kwa wasanii binafsi. Aidha, mafunzo ya uongozi bora kwa vikundi na vyama vyaa Sanaa yatatolewa;
- § Kuhimiza uundwaji, usajili, ufufuaji vyama vyaa wasanii na uchaguzi wa viongozi wa vyama vinavyoendesha shughuli za sanaa nchini;
- § Kufanya utafiti katika baadhi ya mikoa na kuelewa maeneo yenye malighafi kwa ajili ya ufinyanzi na kazi nyingine za sanaa;
- § Kutoa elimu kwa kutumia sanaa na vipeperushi katika sehemu mbalimbali za burudani nchini kuhusu namna ya kupunguza maambukizi mapya ya VVU/UKIMWI;
- § Kuendelea na kazi ya ujenzi wa ukumbi wa wazi kwa maonyesho ya sanaa awamu ya pili;

- § Kuendelea kutoa elimu ya Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki kwa wasanii malimbali; na
- § Kusimamia utoaji wa tuzo kwa wasanii bora wa mwaka 2006 katika tuzo za *Tanzania Music Awards*, na kwa wanamuziki chipukizi.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA), Baraza la Kiswahili la Taifa liliundwa kwa Sheria ya Bunge Na.27 ya mwaka 1967 na kufanyiwa marekebisho kwa Sheria Na.7 ya mwaka 1983. Kama chombo cha Serikali, lina dhamana ya kusimamia na kufutilia utekelezaji wa Sera ya Lughya ya Kiswahili nchini. Majukumu makuu ya Baraza la Kiswahili la Taifa ni:-

- § Kustawisha maendeleo ya utumiaji wa Kiswahili katika Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.
- § Kushirikiana na vikundi vingine ili kukiwezesha Kiswahili kutumika katika nyanja mbali mbali za utoaji wa elimu (kusanifu istilahi za taaluma mbali mbali).
- § Kutoa ithibati ya vitabu vya kiada vitakavyotungwa au kufasiriwa kwa Kiswahili kwa mahitaji na matumizi ya shule na kwa watu binafsi.
- § Kusimamia na kufutilia Kiswahili fasaha katika vyombo vya habari (magazeti, *TV, radio* na kadhalika.).

Katika mwaka wa fedha wa 2005/2006, Baraza la Kiswahili la Taifa lilitekeleza mambo yafuatayo:-

- § Kuandaa warsha ya Lughya kwa Wataalamu 10 wa BAKITA na wa Baraza la Kiswahili Zanzibar (BAKIZA) ili kuwianisha matumizi ya maneno ya Kiswahili. Jumla ya maneno 66 yalijadiliwa na kufikiwa muafaka.
- § Kukusanya istilahi 1300 katika uwanja wa uhusiano wa Kimataifa kwa kushirikiana na Chuo cha Diplomasia ili kuimarisha uwezo wa lughya ya Kiswahili katika uwanja huo.
- § Kuandaa semina kwa wahariri wa Vyombo vya Habari ili kudhibiti matumizi yasiyokuwa fasaha na kuleta uwiano wa matumizi ya maneno. Wahariri 50 walihudhuria semina hiyo.
- § Kuandaa na kurusha vipindi 52 vya ‘Lughya ya Taifa’, vipindi 50 vya ‘Kumepambazuka’ katika Redio, na vipindi 52 vya ‘Ulimwengu wa Kiswahili’ katika televisheni ambavyo vilijadili pia makosa yanayotokea mara kwa mara.
- § Kusoma miswada 48 na kuipa ithibati ya Kiswahili ambapo 40 ni ya elimu na 8 ni ya kawaida ikiwemo miswada miwili ya Rais Mstaafu, Benjamin William Mkapa, Ukweli na Uwazi namba 2 na namba 3.
- § Kuratibu na kutoa huduma ya ukalimani katika mkutano mmoja wa Umoja wa Afrika uliofanyika Khartoum, Sudan, na mikutano miwili ya Bunge la Afrika iliyofanyika Johannesburg, Afrika Kusini.

- § Kuchunguza makosa 110 ya Lugha yanayofanywa na Vyombo vyta Habari na watumiaji wengine wa Kiswahili na kuyasahihisha.
- § Kushiriki katika maandalizi ya matayarisho ya kuundwa kwa Baraza la Kiswahili la Afrika Mashariki (BAKAMA) ili kuongeza kasi ya matumizi ya Kiswahili katika Jumuia ya Afrika Mashariki.
- § Kuwasiliana na Shirika la Viwango Tanzania na Mamlaka ya Kudhibiti Ubora wa Dawa na Vyakula, kuwahamasisha umuhimu wa kutumia Kiswahili katika maelekezo ya namna ya kutumia bidhaa wanazodhibiti.
- § Kuchapisha nakala 3,000 za Kitabu cha Istilahi za Kiswahili za fani mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Malengo ya Mwaka 2006/2007, katika mwaka 2006/2007 Baraza la Kiswahili la Taifa litatekeleza yafuatayo:-

- § Kuandaa warsha ya wataalamu wa lugha wa BAKITA na wa Baraza la Kiswahili Zanzibar (BAKIZA) ili kuainisha matumizi fasaha ya maneno ya Kiswahili.
- § Kuchapisha kitabu cha kufundishia Kiswahili kwa wageni nchini.
- § Kuandaa warsha ya kusanifisha istilahi za kidiplomasia, za mchanganyiko na kuandaa Mwongozo wa Usanifishaji.
- § Kuchapisha kitabu cha makosa katika matumizi ya Kiswahili sanifu.
- § Kuandaa semina kwa vyombo vyta habari ili kudhibiti matumizi ya lugha ya Kiswahili yasiyokuwa sahihi.
- § Kuandaa warsha kwa wafasiri na wakalimani.
- § Kuandaa mwongozo wa waandishi wa vitabu vyta Kiswahili.
- § Kusimamia Maadhimisho ya Tisa ya Siku ya Kiswahili kwa kushirikiana na wadau mbali mbali wa Kiswahili.
- § Kuandaa na kurusha vipindi 52 vyta ‘Lugha ya Taifa’, 52 vyta ‘Kumepambazuka’ na 52 vyta ‘Ulimwengu wa Kiswahili’ katika redio na televisheni.
- § Kukarabati banda la maonyesho la Baraza katika Uwanja wa Maonyesho ya Kimataifa ya Biashara wa Mwalimu J.K. Nyerere, Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Maendeleo ya Michezo, katika mwaka 2005/2006 Wizara yangu iliedelea na jukumu la kuendeleza michezo kwa mujibu wa Sera ya Maendeleo ya Michezo ya mwaka 1995 kwa kutekeleza majukumu yafuatayo:-

- § Kuendelea kusimamia ujenzi wa Uwanja wa Michezo wa kisasa na ukarabati wa Uwanja wa Taifa wa zamani. Jiwe la msingi la Uwanja wa Kisasa liliwekwa na Rais Mstaafu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, tarehe 18/1/2005. Ujenzi wa uwanja huu unatarajiwu kukamilika mwezi Januari, 2007, na kukabidhiwa kwa Serikali mwezi Februari, 2007.

- § Kufanikisha ushiriki wa timu ya Taifa yenye wachezaji 21 na viongozi 8 katika mashindano ya Jumuiya ya Madola yaliyofanyika Melbourne, Australia. Katika mashindano hayo Tanzania ilipata medali moja ya dhahabu kupitia kwa mchezaji Samson Ramadhani aliyekimbia mbio za marathon, na medali moja ya shaba kupitia mchezaji Francis Naali aliyekimbia mbio za km 10,000. Nachukua nafasi hii kuwashukuru wananchi wa mkoa wa Dar es Salaam kwa kujitokeza kwa wingi kuwapokea mashujaa wetu hawa, na Bunge lako tukufu kwa kuwapa heshima ya kuwapongeza hapa Bungeni.
- § Kuendesha mafunzo kwa wataalamu 380 wa michezo mbali mbali, yaliyotolewa katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo cha Malya, vituo vya Kanda vya Arusha na Songea na miji mingine ya nchi yetu. Mafunzo hayo yalihusu ukocha na uamuza wa mchezo wa mpira wa mikono kwa ngazi ya stashahada, matunzo na matumizi bora ya viwanja vya michezo, tiba kwa wanamichezo na mapambano dhidi ya UKIMWI.
- § Kutoa ushauri kuhusu marekebisho ya Katiba za Vyama na Vilabu ili kupunguza migogoro. Jumla ya vyama na vilabu 162 vya michezo vilirekebisha Katiba zao. Kiambatisho Na. 3 kilichoko ukurasa wa 63 kinaonyesha idadi ya vyama na vilabu vya michezo vilivyosajiliwa hadi Desemba 2005.
- § Kukutana na uongozi wa vyama vyote vya michezo vya Taifa, ili kufahamu mipango, mafanikio na matatizo yao. Katika mazungumzo hayo imegundulika kuwa vyama vingi vina katiba zisizoteklezeka, havina mipango ya maendeleo, vimejaa migogoro na viongozi wake ni wang'ang'anizi wasiopenda kufanya chaguzi za kidemokrasia kwa wakati.

Ili kuondoa kasoro hizo Wizara yangu imekwishaanza kuchukua hatua ya kutoa mafunzo ya namna ya kuhuisha katiba, kuandika mpango wa maendeleo kwa viongozi wa juu wa vyama hivyo na kulazimisha chaguzi halali zifanyike.

Mheshimiwa Spika, katika kuhuisha uwezo wa Chuo cha Maendeleo ya Michezo cha Malya, Wizara imesambaza mabomba ya maji safi katika mabweni na jiko la Chuo hicho. Hivi sasa Chuo kinapata maji kidogo kwa matumizi mbalimbali kutoka katika bomba kuu. Aidha, fedha sh. milioni 26 zilitengwa kwa ajili ya kujenga darasa moja zaidi, uchimbaji wa kisima cha chuo, na upimaji wa eneo la Chuo kwa upande wa Wilaya ya Maswa, Mkoa wa Shinyanga, kazi ambazo hivi sasa zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, katika kuwawezesha watu wenye ulemavu kushiriki michezo na mashindano ya kitaifa na kimataifa, Wizara iliwezesha kufanyika mashindano kwa jumla ya watu 500 wenye ulemavu wa akili, jijini Mbeya kuanzia tarehe 25 Machi hadi 30 Machi 2006. Katika mashindano hayo, jumla ya wachezaji 24 watakaouna timu ya Taifa itakayoshiriki mashindano ya Dunia huko Shanghai China mwaka 2007 ilichaguiwa. Timu hiyo ina wachezaji wa mpira wa miguu na wachezaji wa riadha.

Katika kukuza ushirikiano wa kimataifa katika michezo, Wizara iliendelea kutekeleza mikataba na nchi za Cuba, Japan, Korea ya Kaskazini na Rwanda.

Wizara yangu iliendelea na mpango wake wa kupima afya za wanamichezo na kutoa ushauri na matibabu kwa wenyewe matatizo. Jumla ya wanamichezo 1428 katika mikoa ya Dar es Salaam, Tanga na Iringa walipimwa na kupewa ushauri.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Michezo iliendelea kupambana na maambukizi ya UKIMWI kwa kuendeleza programu za mafunzo kwa wanamichezo na watumishi wa Idara. Jumla ya walengwa 412 walipata mafunzo katika miji ya Morogoro, Moshi, Songea na Arusha. Aidha mafunzo kwa vijana nje ya shule yajulikanayo kama "Muongoarika la Wanamichezo" yalifanyika katika miji ya Singida, Mafia na Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya. Mafunzo hayo yalihudhuriwa na jumla ya vijana 124. Kwa upande mwingine kitabu cha kufundishia michezo kupambana na UKIMWI kimechapishwa. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, Umoja wa Mataifa mwaka 2005 ulizingatia kuwa ni mwaka wa Michezo na Elimu ya Mazoezi ya Viungo, ikihimiza kutumia michezo kuwezesha maendeleo na amani. Tanzania tuliadhimisha mwaka huo tarehe 21 Septemba 2005, jijini Dar es Salaam, kwa mashindano ya michezo na shughuli za maonyesho. Katika uwanja wa maadhisho hayo Wizara yangu iliweka banda ambalo watu walihimizwa kupima UKIMWI kwa hiyari (*VCT*) ambapo jumla ya watu 150 walijitokeza kupima. Aidha, kuanzia mwaka 2005, Serikali iliamua kuwa kila Jumamosi ya mwisho ya mwezi Septemba kila mwaka itakuwa siku ya michezo kwa Tanzania ambapo Watanzania wote watahamasishwa kushiriki. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, Shirikisho la Mpira wa Miguu la Dunia *FIFA* liliiteua Tanzania kuwa mionganoni mwa nchi za Afrika za kutembelewa na kombe la Dunia mwaka 2006. Ujio wa kombe hilo Tanzania umeamsha ari ya wadau wa michezo wa mpira wa miguu, kushiriki katika mikakati ya kuendeleza michezo huo, ili hatimaye tuweze kushiriki katika mashindano ya mataifa ya Afrika mwaka 2008 na hata mashindano ya Kombe la Dunia mwaka 2010.

Kwa niaba ya Wizara yangu kupitia Bunge lako Tukufu naomba nimshukuru kwa dhati Mheshimiwa Rais Kikwete kwa kukubali kulipokea Kombe hilo, na kutoa ahadi ya kumlipa kocha wa kigeni wa mpira wa miguu, ili aweze kuifundisha timu ya Taifa. Aidha, naishukuru Kampuni ya Coca cola tawi la Tanzania na Kampuni ya Bia Tanzania kwa kudhamini ziara ya Kombe hilo. (*Makofit*)

Wizara yangu kwa kushirikiana na Shirikisho la Mpira wa Miguu la Tanzania pamoja na wadau wa michezo huo, linaandaa mikakati ya utekelezaji wa mpango wa muda mrefu ili kuweza kutimiza azma yetu ya kuifikisha Tanzania kwenye mashindano hayo.

Mheshimiwa Spika, Malengo ya Mwaka 2006/2007, kuhusu Maendeleo ya Michezo, katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu itatekeleza majukumu yafuatayo:-

- § Kuendelea kusimamia ukamilishaji wa Uwanja wa Kisasa unaojengwa jijini Dar es Salaam hadi hapo utakapokabidhiwa kwa Serikali mwezi Februari, 2007; na kukamilisha awamu ya pili ya ukarabati wa Uwanja wa zamani wa Taifa.
- § Kuandaa na kusimamia mjadala wa kitaifa utakaowashirikisha Watanzania wote, hasa wadau wa michezo, ili kupata mawazo yao kuhusu hatma ya michezo nchini mwetu. Mategemeo ni kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano awe mgeni rasmi katika kilele cha majadiliano haya.
- § Kuandaa na kusimamia shughuli za Siku ya Michezo Tanzania itakayoadhimishwa katika nchi nzima na kilele chake kuwa Jumamosi ya mwisho ya mwezi Septemba, 2006.
- § Kuiandaa Timu ya Taifa inayojumuisha michezo mbali mbali Kwa ajili michezo ya Mataifa ya Afrika yatakayofanyika Algiers - Algeria, mwaka 2007.
- § Kuendelea kutoa mafunzo ya utaalamu wa ualimu, uamuzi, uongozi bora na huduma ya kinga na tiba, ili kuinua viwango vya fani hizo katika vyama na vilabu vya michezo.
- § Kudurusu Katiba mpya za vyama na vilabu na kuvisajili.
- § Kutoa ushauri kwa vyama na vilabu, utakaowawezesha kuhuisha Katiba zao na kuzitekeleza ili kuleta amani na utulivu michezoni. Kuendelea kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu kuboresha miundombinu ya michezo ili kuinua viwango vya ufundishaji, uamuzi na uchezaji.
- § Kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya na vituo vya Kanda vya Arusha na Songea.
- § Kuwawezesha watu wenye ulemavu kushiriki mashindano ya kitaifa na kimataifa, kwa kuiandaa timu ya Olimpiki Maalumu itakayoshiriki michezo ya Dunia itakayofanyika China mwaka 2007.
- § Kupima afya za wanamichezo, kutoa matibabu na ushauri kuhusu uboreshaji wa afya zao.
- § Kuwahamasisha wanawake kugombea nafasi za juu za uongozi katika vyama na vilabu ili kuongeza ushiriki wao michezoni.
- § Wizara yangu itashirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu kuimarisha somo la Elimu kwa Michezo shulenii kwa kutoa mafunzo ya ualimu wa michezo.
- § Kutekeleza programu za mapambano dhidi ya UKIMWI kwa wanamichezo, watumishi wa Wizara yangu na vijana nje ya shule chini ya mpango wa mafunzo

ya MUONGOARIKA LA WANAMICHEZO kwa wilaya zile ambazo hazijapata mafunzo kama njia ya kukuza uchumi na kupambana na umaskini. Aidha, kuandaa mpango wa kuwahudumia waathirika na yatima.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Baraza la Michezo la Taifa liliundwa kwa Sheria Na. 12 ya mwaka 1967 na marekebisho yake, katika Sheria Na. 6 ya mwaka 1971. Kwa mujibu wa Sheria hiyo, majukumu ya Baraza la Michezo ni pamoja na yafuatayo:-

- § Kuendeleza, kustawisha na kudhibiti aina zote za michezo ya ridhaa kwa kushirikiana na vyama vya michezo.
- § Kuhimiza na kutoa fursa za ushirikiano mionganoni mwa vyama vya michezo mbalimbali.
- § Kuidhinisha mashindano ya kitaifa na ya kimataifa katika michezo na matamasha yanayoandaliwa na vyama vya michezo.
- § Kuandaa, baada ya kushauriana na vyama vya michezo vinavyohusika, mashindano, matamasha ya kitaifa na kimataifa kwa nia ya kubadilishana uzoefu na kukuza uhusiano ya kirafiki na mataifa mengine.
- § Kuamsha ari ya kupenda aina zote za michezo kwa ngazi zote.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2005/2006 Baraza la Michezo la Taifa limetekeleza yafuatayo:-

- § Rasimu ya kwanza ya mkakati wa michezo kwa Vijana imeandaliwa na imeanza kujadiliwa na wadau mbali mbali.
- § Baraza la Michezo la Taifa limekamilisha rasimu ya marekebisho ya Sheria ya Baraza la Michezo la Taifa na hivi sasa inaendelea kujadiliwa na wadau katika ngazi mbalimbali.
- § Baraza limeanzisha ushirikiano na Baraza la Michezo la Uingereza (*UK Sports*) ambapo limewezesha taasisi mbili za Michezo, “*Tanzania Paralympic Committee*” na Elimu, Michezo na Mazoezi (EMIMA) kuingia mikataba ya kupata msaada wa fedha za kuendeshea mafunzo kwa watu wenye ulemavu na jamii kuhusu kujikinga dhidi ya maambukizi ya UKIMWI, na kupunguza umasikini kuititia shughuli za michezo.

- § Baraza limeendelea kusimamia na kuendesha chaguzi za vyama saba ambavyo ni vya mieleka, walemavu, mpira wa wavu, kuogelea, golf, mpira wa kikapu na ngumi za ridhaa.
- § Baraza la Michezo la Taifa, likishirikiana na Chama cha Kimataifa cha Watu wenyе Ulemavu (*IPC*) na “*UK Sports*” liliandaa kongamano la kwanza la kimataifa la Michezo kwa Wanawake wenyе ulemavu barani Afrika, lililolenga kuhamasisha wanawake kushiriki katika michezo na kugombea nafasi za uongozi katika sekta mbali mbali.
- § Kongamano hilo lilihusisha nchi kumi na moja ambazo ni Tanzania, Afrika Kusini, Zambia, Kenya, Uganda, Msumbiji, Nigeria, Rwanda, Burundi, Mauritius na Ethiopia.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007 Baraza la Michezo la Taifa limepanga kutekeleza yafuatayo:-

- § Kuandaa na kuendesha mafunzo kwa viongozi wa vyama vya michezo vya taifa kuhusu namna ya kuandaa Mpango Mkakati (*Strategic Plan*), uanzishaji na uendelezaji wa timu za vijana wa rika mbali mbali na jinsia zote kwa kila chama cha michezo.
- § Kuhamasisha jamii kushiriki katika michezo kwa kutoa mafunzo kwa walimu wa michezo na wataalamu wengine , viongozi wa Serikali za Mitaa na wazazi ili kujenga uwezo endelevu na kuongeza ushiriki wa kutumia michezo kuleta maendeleo ya jamii.
- § Kuandaa na kuendesha kongamano kwa vyama vya michezo na watu mbali mbali kuhusu uanzishaji wa michezo ya kulipwa na kukusanya maoni kuhusu maendeleo ya michezo kwa jumla.
- § Kuendesha mafunzo na matamasha kwa vikundi mbali mbali vya michezo, mijini na vijijini kuhusu mbinu za kuanzisha miradi mbali mbali kwa ajili ya kuongeza kipato na kupata uwezo wa kuijendesha.
- § Kuendelea kutoa elimu ya kujikinga na maambukizi ya virusi vya UKIMWI kwa njia ya matamasha na mashindano ya michezo kwa kushirikiana na asasi mbali mbali zinazojishughulisha na michezo.

- § Kuendeleza mazungumzo na “*UK Sports*” na wadau wengine kuhusu uanzishaji na uendeshaji wa miradi endelevu ya michezo; na upatikanaji wa wataalamu wa kufundisha michezo mbali mbali.
- § Kuhamasisha kwa njia ya mikutano, semina na makongamano ili kuongeza ushiriki na uundaji wa vikundi zaidi vya michezo kwa wanawake na watu wenye ulemavu.

- § Kuendelea kuratibu maandalizi na ushiriki wa timu za taifa katika mashindano ya kimataifa na kusimamia chaguzi za vyama vya michezo vya taifa na mashirikisho ya michezo.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Utawala na Maendeleo ya Utumishi, katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu, kuititia Idara ya Utawala na Maendeleo ya Utumishi, inakusudia kutekeleza majukumu yafuatayo:-

- § Kuwaandalia watumishi mazingira bora ya kufanya kazi, ikiwa ni pamoja na ofisi na vitendea kazi.
- § Kuendelea kukamilisha upatikanaji wa wafanyakazi wa taaluma mbalimbali ili kujaza nafasi wazi kwa mujibu wa ikama iliyoidhinishwa.
- § Kuwajengea uwezo watumishi kwa kuwaandalia mafunzo ya muda mfupi na mrefu.
- § Kusimamia utekelezaji wa mfumo wa kupima utendaji kazi kwa matokeo.
- § Kuhamasisha na kuelimisha watumishi juu ya ugonjwa wa UKIMWI na namna ya kupambana nao.
- § Kuwawezesha watumishi kuunda ushirika wa kuweka na kukopa.
- § Kusimamia utendaji kazi wa watumishi kwa kuzingatia misingi ya utawala bora na mapambano dhidi ya rushwa.
- § Kuendesha mafunzo kuhusu utawala bora.

§ Kuendesha mikutano ya Baraza la Wafanyakazi na ya wafanyakazi wote ili kujadili na kuushauri uongozi wa Wizara juu ya mambo mbalimbali yanayoihusu Wizara na maslahi yao.

Mheshimiwa Spika, Hitimisho, Wizara yangu katika miaka mitano ijayo itaweka msisitizo mkubwa katika maeneo yafutayo:-

- Utambuzi na Uendelezaji wa Vipaji vya Wanamichezo. Tukishirikiana na Taasisi za watu binafsi, Wizara yangu itaanzisha vituo vya mafunzo na kugawa nchi kwa kuzingatia Kanda zenyе chimbuko la vipaji vya Michezo mbalimbali kwa lengo la kutambua vipaji vya wanamichezo nchini, kufundisha waalimu watakaoibua vipaji vya wachezaji tarajiwa kuwa wanamichezo mahiri na kuandaa mashindano ya kuimarisha vipaji hivyo ili wachezaji hao waweze kupata ajira.
- Kuimarisha Ushirikiano na Wadau. Kama nilivyosema hapo awali, shughuli za Wizara yangu zinagusa maeneo mengine mbalimbali. Wizara yangu itashirikiana na Wizara zote ikiwemo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundı, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Ardhi, Nyumba na Makazi, Makampuni na vikosi vya Jeshi kuendeleza michezo katika ngazi zote – Shule, Vijiji, Kata, Tarafa, Wilaya, Mikoa na Kitaifa.
- Mafunzo: Chuo cha Maendeleo ya Michezo cha Malya kitaimarishwa ili kupata wataalamu wa fani mbalimbali. Hali kadhalika, kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundı tutaandaa walimu wa kufundisha michezo mashulenı.
- Ujenzi wa Awamu ya Pili ya Uwanja wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki Wizara yangu itasimamia ujenzi wa awamu ya pili ya Uwanja wa Ndani wa Taifa, Kijiji na Chuo cha Michezo. Kituo hiki kitasaidia pamoja na mambo mengine kujenga tabia ya Watanzania ya kupenda, kuchangia na kuzishangilia timu zao. Aidha, kituo kitasaidia kuandaa mapema na kwa ufanisi timu zetu za Taifa kabla ya mashindano mbalimbali.

· Wizara yangu ikishirikiana na Wizara ya Elimu na Ufundı na Wizara ya Ulinzi, itaanzisha vituo na shule maalum ya michepo ya michezo. Aidha, watu binafsi watahamasishwa kuanzisha na kusaidia “Sports Academies na Soccer Academies”.

Rais anasisitiza juu ya umuhimu wa kushiriki kwa vijana shulenı katika michezo kwa kusema: “Tutahimiza maendeleo ya michezo shulenı na pale inapowezekana katika sehemu za kazi. Shule ziwe mahali pa kubaini vipaji vya sanaa na michezo.” Mheshimiwa Rais Jakaya Kiwete. Tarehe 30.12.2005.

· Kuhimiza na kuhakikisha Vilabu na Vyama vya Michezo nchini vinakuwa na timu za vijana kwa kuzingatia umri. Aidha pia kuhakikisha mashindano ya ngazi za umri yanafanyika nchi nzima kuanzia vijijini, kata, Wilaya, Mikoa hadi Taifa.

- Kuhuisha Sera ya Michezo na Kuandaa Sheria ya Maendeleo ya Michezo. Wizara yangu itahuisha Sera ya Michezo ya mwaka 1995 na kuandaa Sheria ya maendeleo ya michezo ili kuhakikisha michezo inaendelezwa kwa mujibu wa sera taratibu, kanuni na sheria.
- Mheshimiwa Spika, Kuhusu Maendeleo ya Vyama vya Michezo. Wizara yangu itahakikisha kila Chama cha Michezo kina Mpango wa Maendeleo wa muda mfupi na muda mrefu na kinaandaa Ratiba ya Utekelezaji wa mpango huo. Wizara itahakikisha matumizi ya fedha zote zinazotoka nje ya nchi zikiwa ruzuku kwa vyama vya michezo zinajulikana kwa Serikali na kwa Wananchi.
- *Mini Olympic*. Ili kuimarisha ushiriki wa Tanzania katika michezo ya Kimataifa, Wizara yangu itakuwa inandaa angalau kila baada ya miaka miwili michezo ya *mini Olympic*.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Maendeleo ya Utamaduni, kwa upande wa Sekta ya Maendeleo ya Utamaduni, Wizara yangu itasimamia matumizi ya lugha ya Kiswahili katika nchi za nje.

Katika kutekeleza azma hii Wizara yangu itaboresha mafunzo ya Kiswahili kama Lugha ya Kigeni kwa kushirikiana na nchi za Afrika Mashariki na Kati. Hatua hizi zitakifanya Kiswahili kuwa chanzo kimojawapo muhimu cha ajira kwa Watanzania. Rais wetu anasisitiza umuhimu wa Kiswahili kuwa lugha ya kimataifa kwa kusema:

“Serikali ya Awamu ya Nne itahakikisha kuwa lugha ya Kiswahili inakua nje ya mipaka ya Afrika”. Mheshimiwa Jakaya M. Kikwete. Tarehe 30/12/2005. Aidha Wizara itaandaa na kuendesha kongamano la Idhaa zote za Kiswahili duniani ili kujadili matumizi sahihi ya Kiswahili na kubadilishana uzoefu.

Mheshimiwa Spika, Kuendeleza Sanaa, kwa kushirikiana na Wizara mbalimbali kama Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundji na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Wizara yangu itaanzisha vituo vya kujifunza taaluma ya sanaa ili kuinua viwango vyetu Kitaifa na Kimataifa, kuongeza ajira na uwezekano wa kuwa na Kikundi cha Taifa cha Utamaduni.

Aidha watu binafsi watakaribishwa na kusaidiwa kuanzisha shule na vituo vyenye mchepuo wa sanaa na muziki. Rais anahimiza juu ya kuwapa haki ya mapato kwa wasanii wetu:

“Tutaendeleza sekta ya Utamaduni na burdani kwa jumla. Miongoni mwa mambo ambayo tutayaangalia kwa karibu ni haki na maslahi ya wasanii ili kazi kubwa waifanyayo iwe na tija kwao”. Rais Jakaya Kikwete, Tarehe 30 Desemba, 2005.

Aidha, wizara yangu itashirikiana na TAMISEMI kufufua majumba ya Maendeleo Wilayani na kujenga mapya, ili yaweze kutumika kwa maendeleo ya sanaa.

Na mwisho, Wizara yangu itaendelea kuwasidia wasanii kupata mapato yao kwa kutumia hatimili na hatishiriki zao kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko.

Mheshimiwa Spika, Kuhusu Sekta ya Habari, katika jitihada za kuongeza usikivu wa *Radio Tanzania* Wizara itajenga vituo vya FM katika miji ya mikoa tisa.

Aidha Serikali itaanzisha baraza, “*Accreditation Council*”, kwa ajili ya waandishi wa habari ili kuweka viwango vizuri kwa ajili ya vyuo na vyuo vikuu vinavyofundisha waandishi. Vile vile Serikali itadhibiti utoaji *Press Cards* kiholela ili kuzuia waandishi (makanjanja) wasiosomea taluma hiyo kufanya kazi.

Pia Serikali inakusudia kuweka viwango vya elimu kwa wale watakaotaka kuingia katika taaluma hii ya uandishi. Katika kuimarisha taaluma ya uandishi na habari Serikali inakusudia kuanzisha utaratibu wa kipindi cha majaribio *internship* kwa waandishi wote wanaomaliza kozi zao kama ilivyo wale wasomao masomo ya sheria na utibabu.

Aidha, Serikali kwa kushirikiana na wahariri na wamiliki wa vyombo vya habari, watajenga utamaduni wa kizalendo wa kuandika mafanikio mazuri yote ili kujenga taswira nzuri ya nchi yetu. Hili litasaidia kuvutia watalii na wawekezaji. (*Makofi*)

Mwisho. Huduma zinazotolewa na Wizara yangu zinawagusa Watanzania wote kwa namna mbali mbali.

Aidha, zinazigusa Wizara nyingine zote kwani shughuli za Wizara yangu ni za mtambuka. Napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa michango yao ya mawazo na ushauri walijonipa ndani na nje ya Bunge kwa nia ya kuendeleza huduma tunazotoa.

Wizara iko tayari kuyapokea na kuyafanya kazi mapendekezo, ushauri na maoni watakayoendelea kuyatoa Waheshimiwa Wabunge ili tuendelee kutoa huduma bora.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa majukumu na malengo ya Wizara yangu umewezekana kwa ushirikiano kuwa mzuri mionganini mwa viongozi na wafanyakazi wa Wizara.

Kwa hiyo, ninapenda kuwashukuru viongozi na wafanyakazi wote wa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo pamoja na Mabaraza, Mashirika na Taasisi zote kwa jitihada zao za kutekeleza majukumu walijopewa na Taifa letu.

Ninapenda kutoa shukrani za pekee kwa Mheshimiwa Joel Nkaya Bendera, Mbunge wa Korogwe Mashariki ambaye ni Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo na Mheshimiwa Dr. Emmanuel John Nchimbi, Mbunge wa Songea Mjini,

ambaye ni Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo; kwa msaada na ushauri wao wa karibu kwangu. (*Makofi*)

Aidha, natoa shukrani zangu za dhati kwa Katibu Mkuu wa Wizara yangu, Mwanamama Bibi Kijakazi Rajabu Mtengwa, Wakuu wa Idara, Watendaji Wakuu wa Mabaraza, Mashirika na Taasisi zilizo chini ya Wizara, na Bodi zao ambazo zimeshirikiana na Wizara yangu katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nitumie nafasi hii kuwashukuru washirika wetu wote ambao wametuunga mkono katika kutekeleza majukumu ya Wizara yangu.

Vile vile, napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru wahisani wote ambao walitusaidia na nina imani wataendelea kutusaidia. Siyo rahisi kuwataja wote lakini angalau nitaje wachache ambao ni Serikali ya China, Sweden, Norway, Denmark na Finland; mashirika ya kimataifa ya *UNICEF*, *UNESCO* na *Right to Play*.

Pia, ninayashukuru mashirika na makampuni ya hapa nyumbani ambayo ni *VODACOM*, Kampuni ya Bia Tanzania (*TBL*), Kampuni ya Simu Tanzania (*TTCL*) na *Bonite Bottlers* kwa juhudhi zao mbali mbali za kufanikisha shughuli za Wizara yangu. (*Makofi*)

Makadirio ya Bajeti ya Mwaka wa 2006/2007. Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, inatarajia kukusanya jumla ya Shilingi 98,403,000/= kutokana na vyanzo vyake mbali mbali. Idara zinazokusanya mapato ni Idara ya Maendeleo ya Utamaduni, Idara ya Maendeleo ya Michezo na Idara ya Habari.

Mheshimiwa Spika, Matumizi ya Kawaida. Katika mwaka wa fedha 2006/2007 Wizara yangu imetengewa jumla ya shilingi 12,950,587,000/= zote zikiwa fedha za hapa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Fedha hizi zinajumuisha:

- § Mishahara ya Wizara Shilingi 1,048,059,000/=;
- § Mishahara ya Taasisi zilizo chini ya Wizara Shilingi 1,902,528,000/=;
- § Matumizi Mengineyo kwa Wizara Shilingi 3,012,355,000/=; na
- § Matumizi Mengineyo kwa Taasisi zilizo chini ya Wizara Shilingi 6,987,645,000/=.

Mheshimiwa Spika Bajeti ya Maendeleo. Katika mwaka wa fedha 2006/2007 Wizara imetengewa jumla ya shilingi 40,004,064,000/= kwa ajili ya miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi 10,313,064,000/= ni fedha za ndani na shilingi 29,691,000,000/= ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, ili Wizara yangu iweze kutekeleza majukumu na malengo yake ya mwaka wa 2006/2007, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe Bajeti ya jumla ya Shilingi 52,954,651,000/= ambapo kati ya hizo, shilingi 23,263,651,000/= ni fedha za ndani na shilingi 29,691,000,000/= ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofî*)

WAZIRI WA USALAMA WA RAIA: Mheshimiwa Spika, naafiki!

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

SPIKA: Ahsante sana na sasa namwita Mwenyekiti au Mwakilishi wake wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Haroub Said Masoud, huyu ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo. (*Makofî*)

MHE. HAROUB SAID MASOUD – MAKAMU MWENYEKITI KAMATI YA MAENDELEOA YA JAMII:

Mheshimiwa Spika, Utangulizi. Kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni Na.81(1) Toleo la 2005, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, kuhusu makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida na Mpango wa Maendeleo wa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kwa mwaka wa Fedha 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kutumia fursa hii, kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuwasilisha Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kwa Mwaka 2006/07.

Mheshimiwa Spika, Kwa kuwa hii ni taarifa ya kwanza ya Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii katika awamu hii, kwa niaba ya kamati napenda kwanza kabisa kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania kwa kuchaguliwa kwake kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na pia kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuwa Mwenyekiti wa Taifa wa Chama Tawala.

Aidha naungana na wasemaji waliotangulia kuwapongeza wale wote walioteuliwa na kuchaguliwa kushika nyadhifa mbalimbali katika sekretarieti ya Halmashauri kuu ya Taifa ya Chama Cha Mapinduzi wakiongozwa na Mwenyekiti wao Mheshimiwa Luteni Mstaaful Yusuph Makamba.

Napenda pia nichukue fursa hii kukupongeza kwa dhati wewe Mheshimiwa Spika (Bwana Viwango) kwa kuchaguliwa kwako na kuanza kuendesha Bunge hili kwa Kasi na Viwango vya hali ya juu. Aidha, nampongeza sana Naibu Spika na Wenyeviti wetu kwa umakini wao katika kuliongoza Bunge letu kupitia Kamati zao.

Naomba nimpongeze pia Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, kwa kuteuliwa na kuthibitishwa kwake kuwa Waziri Mkuu wa Ari Mpya, Kasi Mpya na Nguvu Mpya, nawapongeza Mawaziri na Manaibu Mawaziri kwa kazi zao nzuri.

Niwapongeze sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushindi wao na jinsi walivyoanza kazi zao vizuri. Nimshukuru sana Mwenyekiti wangu wa kamati, Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, kwa kushirikiana vizuri kuongoza kamati kwa kipindi hiki chote.

Mheshimiwa Spika, na sasa kwa namna ya pekee naishukuru sana familia yangu kwa jinsi inavyonipa moyo katika kazi zangu. Nawashukuru Wajumbe wa Kamati yangu kwa imani kubwa na ushirikiano wanaonipa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii tena kuwashukuru kwa dhati kabisa wapiga kura wangu wa Jimbo la Koani kwa kunichagua kuwa Mbunge wao kwa kipindi cha tatu mfululizo na kwa ushirikiano wanaonipa katika kazi hii ya siasa.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kupitia bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo Kamati ilizingatia mambo yafuatayo:

1. Dira na malengo ya Wizara.
2. Dhima ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo.
3. Majukumu ya Wizara.
4. Sera ya Wizara.
5. Mpango wa muda wa kati na Bajeti ya Upeo 2006.2007-2008/2009 (*MTEF*).
6. Malengo ya Bajeti ya mwaka 2006/2007 (kazi zilizopangwa kufanywa).

Mheshimiwa Spika, Dira ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo. Wakati wa kuchambua bajeti ya Wizara hii, Waziri alieleza dira ya Wizara ni kuwa na Mtanzania

mwenye haki ya kupata na kutoa habari kwa uhuru, uadilifu na anayefurahia maisha kutohana na kushiriki katika michezo.

Mheshimiwa Spika, Dhima ya Wizara. Kamati ilielezwa dhima ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kuwa ni kukuza utambulisho wa Taifa kwa kuwezesha upatikanaji na usambazaji huru wa habari, kuendeleza maadili ya Utamaduni wa Mtanzania na kukuza michezo na riadha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Sera ya Wizara ya Habari, Utamaduni, na Michezo. Wakati wa kupitia na kuchambua bajeti ya Wizara, Waziri alieleza kwa kina kuhusu Sera zinazoteklezwa na Wizara yake, sera hizo ni pamoja na:-

Mheshimiwa Spika, Sera ya Utamaduni. Kamati ilielezwa majukumu yanayoteklezwa na sera hii kuwa ni pamoja na:-

- (1) Kushirikisha shughuli za utamaduni wa Taifa kuanzia shule za awali, msingi Sekondari na Elimu ya Juu na kuhakikisha kwamba mafunzo ya Utamaduni yanaingizwa katika mitaala na mihtasari na kufundishwa shulenii na vyuoni.
- (2) Kuhimiza na kukuza utaifa kwa vijana wetu na wananchi kwa ujumla.
- (3) Kuhimiza utu katika maendeleo ya Taifa.
- (4) Kuimarisha uchangiaji wa gharama, ukuzaji, utunzaji na uimarishaji wa Taasisi za Utamaduni kwa watumiaji wa huduma hizo.
- (5) Kuelimisha jamii juu ya mambo mbalimbali na kupambana na UKIMWI kwa kutumia sanaa.

Mheshimiwa Spika, Sera ya Habari na Utangazaji. Kamati ilielezwa kuwa Sera hii ina majukumu yafuatayo:-

- (1) Kuweka mazingira yatakayowezesha Sekta ya habari kukua.
- (2) Kuhamasisha vyombo vyya habari kutoa huduma kwa kuzingatia maadili ya taaluma.
- (3) Kuhamasisha Wanahabari kuendeleza chombo cha kujisimamia kitaaluma.
- (4) Kuweka utaratibu wa kujenga uwezo endelevu katika sekta.
- (5) Kuwawezesha wananchi kutoa habari na kupata habari kwa uhuru ili zichangie kuwaletaa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Sera ya Michezo. Katika Sera ya Michezo Waziri aliwaeleza Wajumbe kuwa ina majukumu yafuatayo:-

- (1) Uhamasishaji wa Wananchi kushiriki katika Michezo na kuimarisha viungo.
- (2) Upatikanaji wa Viwanja na vifaa bora kwa ajili ya kuimarisha Maendeleo ya Michezo.
- (3) Uandaaji na utayarishaji wa Wataalamu katika fani na taaluma mbalimbali za Michezo.
- (4) Kuhakikisha tunahimiza Wachezaji wetu kushiriki kikamilifu katika mashindano na michezo ya Kimataifa.
- (5) Utafiti katika Michezo ya Jadi kwa lengo la kuifufua na kuiendeleza.
- (6) Ushirikiano na Mataifa mengine katika utoaji elimu kwa Michezo na Wanamichezo.
- (7) Kusimamia Ujenzi wa Uwanja wa Michezo wa Kisasa.
- (8) Kuimarisha Utawala bora katika michezo.
- (9) Kutoa mafunzo ya Wataalam wa Michezo.
- (10) Kupambana na janga la Ukimwi katika Michezo.
- (11) Uendelezaji, Utambuzi wa vipaji vyta vijana katika michezo kuanzia Umri mdogo.
- (12) Kuhamasisha Jamii kushiriki Michezo katika Maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, Maombi ya Fedha kwa Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007. Kamati ilipitia na kuchambua Maombi ya Makadirio ya Fedha kwa mwaka wa Fedha 2006/2007; ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, kiasi cha Sh.52,954,651,000/= kiliombwa ili kutekeleza majukumu yaliyopangwa kutekelezwa kama ifuatavyo:-

Matumizi ya Kawaida Tsh.12,950,587,000/= na Miradi ya Maendeleo Tsh.40,004,064,000/=.

Mheshimiwa Spika, Maoni, Ushauri Na Mapendekezo Ya Kamati. Baada ya Kamati kupitia na kupata maelezo ya kina kuhusu Makadirio ya Mapato na matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, Kamati inatoa Ushauri ufuataao.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kukua kwa Teknolojia, na Uhuru wa Habari kumekuwepo na mmong'onyoko wa Maadili ya Utamaduni wetu, mfano Magazeti ya Udaku yanaandika na kuchora picha za Ajabu sana na ambazo ni hatari kwa Maadili ya Watoto wetu, Luninga nazo zinaonesha picha na filamu mbaya, chafu sana na zenye madhara kwa maadili ya Watoto, Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kutoa tamko kuhusu mmong'onyoko huu na kutoa mwongozo kwa wahusika ili kukinusuru kizazi hiki.

1. Serikali ilipe kipaumbele suala la Utamaduni wetu na hasa katika matumizi ya Lugha ya Kiswahili, na kuweka wazi vazi halisi la kitaifa kwa Mwanamke na Mwanaume.

2 .Kutokana na Sheria nyingi za sanaa kuwa za zamani sana na hivyo kupitwa na wakati tulio nao. Kamati inaishauri Serikali kuzifanyia marekebisho sheria hizo.

3. Kamati inashauri Wizara kuweka mkakati wa Makusudi kwa lengo la kukuza Utamaduni na kuanzisha Vikundi vya Utamaduni vitakavyotambulika Kitaifa.

4. Kumekuwepo na Utamaduni/tibia ya vyombo/Kampuni binafsi kuandaa maonesho bila kupata kibali au kuishirikisha Wizara husika. Kamati inatoa ushauri kuwa vyombo hivi vinapoandaa maonyesho ni lazima vipate kibali kwa Wizara husika na pia Kamati inaiagiza Wizara kusisitiza matumizi ya Lugha ya Kiswahili katika Maonyesho yanayofanyika ili Wananchi waweze kupata ujumbe kamili wa maonyesho husika.

5. Kumekuwepo na kuibuka kwa Wasanii katika Mashindano mbalimbali ambao wengi wao hawana utaalamu wa kutosha. Kamati inaishauri Wizara kuboresha viwango vya Wasanii wanaoshiriki katika mashindano hayo ikiwa ni pamoja na kuwahamasisha kutunga nyimbo mpya na zenye maadili kwa jamii.

6. Kamati inashauri Serikali kuzingatia Viwangovya Kimataifa wakati wa kujenga Ukumbi wa Sanaa za Maonesho wa Taifa.

7. Mfuko wa Utamaduni Wengi wa wananchi hawafahamu kuwa mfuko huo unapokea maombi na kutoa mikopo kwa Watanzania kwa ajili ya kuendeleza michezo.

Kamati inaishauri Serikali Kuhamasisha wananchi jinsi ya njia bora ya kutumia Mfuko wa Utamaduni.

Muziki na haki Miliki ya Wasanii. Muziki una nafasi kubwa sana katika maisha ya kila siku ya mwanadamu ,muziki unatumika kama burudani, kwenye Harusi,kampeni,vilioni,kanisani,kwenye elimu, na kadhalika. Hivi sasa muziki umekuwa ni mojawapo ya Ajira kwa vijana wengi. Hivyo ni vyema tuuchukulie Muziki kuwa ni ajira inayochangia katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika,hivi sasa mitaani kuna vijana kadha wa kadha katika mitaa mbalimbali nchini wanaouza kanda za muziki na wanategemea biashara hiyo kuendesha maisha yao. Lakini imegundulika kuwa kanda nyingi zinazouzwa mitaani zinatengenezwa pasipo mikataba maalum kati ya mtunzi wa muziki huo,hivyo faida kubwa huenda kwa watengenezaji na wauzaji kuliko mwanamuziki mwenyewe.Mwaka 1997 Serikali ililetta sera ya utamaduni na mwaka 1979 ililetwa sheria ya haki miliki,Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko nayo iliandaa kanuni na kupitishwa mwaka 2003 ili zitumike katika kulinda haki za utunzi.Mheshimiwa Spika,halii iliyopo sasa ni kuwa ajira katika Muziki inakatisha tamaa kwa kuwa watengenezaji wa muziki wanaendelea kuneemeka bila kulipa kodi yoyote,Kamati inaishari serikali iangalie upya sheria ya haki miliki ya muziki ili hatimaye muziki uweze kuwa ajira nzuri kwa vijana wetu,na pia uchangie katika pato la Taifa

Mheshimiwa Spika, Michezo. Ili kuwa na Wachezaji wazuri wenye kuleta ushindani ni lazima waanze kujifunza tangu wakiwa wadogo Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundis kuongeza somo la Michezo katika

Mitaala yake katika Shule za awali, msingi na Sekondari, ikiwa ni pamoja na kuandaa wataalam.

Kamati inashauri Serikali kuitia Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kuweka mkakati maalum wa kukuza vipaji katika Michezo. Ili kukuza vipaji vya michezo kwa watu wenye ulemavu. Kamati inashauri kuwepo na wataalam maalum wak ushughulikia michezo kwa watu wenye ulemavu. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua nzuri iliyofikia katika ujenzi wa Uwanja wa Michezo wa kisasa wa Taifa.

Hata hivyo Kamati inashauri Serikali kuwa ili Uwanja huo ufikie ubora wake uliokusudiwa ni vema kuwe na maandalizi ya kukamilisha hatua ya 2 na 3, na pia Serikali iandae utaratibu mzuri wa utunzaji wa uwanja huo.

Kamati pia inampongeza Mheshimiwa Rais kwa kutekeleza ahadi yake mapema kuipatia timu ya Taifa ya mpira wa miguu kocha wa kigeni, kwani kocha huyo kutoka nchini Brazil ameshawasili nchini.

Mheshimiwa Spika, Habari na Utangazaji. Kwa kuwa kumekuwepo na Matangazo yenyeye Picha mbaya ndani ya Luninga, ambayo kimsingi yanaleta mmong'onyoko wa maadili katika jamii. Kamati inashauri kuwepo na chombo cha kuyafanya upembuzi wa kina matangazo yote yanayoletwa na kutangazwa kwenye Luninga, Chombo hiki kifanye kazi za kuhakiki kila tangazo kabla ya kupelekwa kutangazwa, na ikitokea chombo cha habari kutangaza mambo yasiyofaa, basi Serikali ichukue hatua za kisheria dhidi ya Tangazo husika.

Mheshimiwa Spika, Hitimisho. Baada ya kusema hayo naomba nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Mohamed Seif Khatib, Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo kwa hotuba na maeleo yake mazuri aliyoyatoa wakati Kamati inapitia Bajeti hii, Naibu Waziri, Mheshimiwa Joel Bendera, Mheshimiwa Emmanuel Nchimbi, Katibu Mkuu Mwanamama Bibi Mlegwa na Maafisa wote wa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kwa ushirikiano waliota kwa Kamati wakati wa kuchambua Bajeti ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza vijana wawili walioshinda katika michezo ya *Olympic* huko Melbourne Australia na kuipa Tanzania Heshima kubwa, naomba niwatambue na kuwataja kwa majina:- Koplo Samson Ramadhan Nyoni na Ndugu Phabian Josep Naasi. (*Makofi*)

Pia naomba nimpongeze Mrembo wa Tanzania Ms Nancy Sumari, kwa kutwaa Taji la *Miss World Africa*. Nawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee napenda niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, kwa ushirikiano na michango yao wakati wakuchambua bajeti hii, naomba niwatambue kwa kuwataja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati na Mheshimiwa Haroub S. Masoud, ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati. Wajumbe wengine ni Mheshimiwa Dr. Binilith S. Mahenge, Mheshimiwa Maulidah A. Komu, Mheshimiwa Ameir A. Ameir, Mheshimiwa Zuleikha Y. Haji, Mheshimiwa Issa K. Issa, Mheshimiwa Anna R. Lupembe, Mheshimiwa Capt. John Komba, na Mheshimiwa Mwanawetu S. Zarafi.

Mheshimiwa Spika, wajumbe wengine ni Mheshimiwa Mohamed A. Said, Mheshimiwa Fatma O. Ali, Mheshimiwa Mwinchoum A. Msomi, Mheshimiwa Bernadetha K. Mushashu, Mheshimiwa Kiumbwa M. Mbaraka, Mheshimiwa Dorah H. Mushi, Mheshimiwa Bujiku P. Sakila, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mheshimiwa Amina C. Mpakanjia, Mheshimiwa Ezekiel Maige, Mheshimiwa Salimu A. Khalifan na Mheshimiwa Elietta N. Switi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kukushukuru wewe binafsi na Naibu Spika, Mheshimiwa Anne S. Makinda, Mb, kwa uongozi wenu makini katika kuliendesha Bunge letu tukufu. Ninawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, napenda pia nimshukuru sana Katibu wa Bunge Ndugu Damian Foka, kwa kuiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake kama ilivyopanga. Aidha nawashukuru Makatibu Kamati wa Kamati hii Ndugu Angelina L. Sanga na Joshua Chamwella, kwa kuihudumia Kamati na kuanda Taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, Kamati yangu inaunga mkono Mapendekezo ya Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007 ambayo ni kiasi cha Tsh.52,954,651,000/= (Billioni Hamsini na Mbili, Milioni Mia Tisa Hamsini na Nne, Laki Sita na Hamsini na moja Elfu).

Naomba Bunge lako tukufu likubali kuijadili na hatimaye kuipitisha Bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

MHE. GRACE S. KIWELU – MSEMAJI WA UPINZANI WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:

Mheshimiwa Spika, Nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Bajeti hii ya Wizara ya Habari, Michezo na Utamaduni mwaka wa fedha 2006/2007 kwa mujibu wa kanuni za Bunge kifungu 43(5)(b)(c) na 81(1) toleo la 2004.

Natoa shukrani zangu kwa viongozi wangu na wanachama wa chama changu cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kwa kunteua kukiwakilisha hapa Bungeni kwa mara ya pili katika nafasi ya Ubunge Viti Maalum, ninaahidi kuwa nitafanya kazi kwa

uwezo wangu wote kwa maslahi ya chama na watanzania wote. Naomba Mwenyezi Mungu anisaidie!! Aidha, nina toa shukrani na pongezi kwa Viongozi wetu wa Kambi ya Upinzani chini ya Mhe. Hamad Rashid na Mheshimiwa Dr. Slaa kwa kazi kubwa wanayoifanya kuhakikisha tunatoa changamoto hapa Bungeni. Pia napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake aliyoiwasilisha hapa Bungeni na ninamshukuru kwa ushirikiano alionipa katika kuandaa hotuba hii. Ninatoa shukrani zangu za pekee kwa Naibu wangu Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga kwa ushirikiano wake mkubwa katika kuandaa hotuba hii. Sekta ya habari ni sekta muhimu sana katika maendeleo ya nchi. Sekta hii hutumika kama kiungo muhimu kati ya jamii na Serikali popote duniani. Jamii kupitia njia mbalimbali za mawasiliano imekuwa ikipata maelekezo ya Serikali kuhusu masuala ambayo Serikali inataka kuwajulisha wananchi wake, vivyo hivyo Serikali imekuwa ikipata maoni na matokeo ya mapokeo ya wananchi juu ya maelekezo iyatoayo mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, Sera, mipango na mikakati mbalimbali ya Serikali hufanikiwa tu katika utekelezaji wake kama habari sahihi zitawafikia wale ambao wanahusika kwa namna moja au nyingine katika utekelezaji wa mikakati hiyo. Hivyo, kutokana na umuhimu wao katika jamii, napenda kuwapongeza wadau wa sekta ya habari- nikimaanisha vyombo vy a habari na waandishi wa habari kwa kuweza kutumia uhuru wao waliopewa kikatiba na kuweza kuwafikishia Watanzania habari muhimu kwa wakati muafaka bila ya kujali maslahi ya watu wachache ambao habari hizo zinawahusu. Kwa kutambua umuhimu wa sekta ya habari ambayo katika ulimwengu wa leo,inachukuliwa kama MUHIMILI wa Nne katika mfumo wa Dola ina mchango mkubwa katika suala zima la utawala bora. Hivyo, kazi yao sio tu kuripoti matukio bali hata kuhakikisha uwajibikaji wa viongozi wetu na uwazi katika utendaji wao. Kambi ya Upinzani inasisitiza kuwa viongozi wa Serikali wasivione vyombo vy a habari na waandishi wa habari kama maadui, bali wawe karibu nao, wawape habari ambazo zinatakiwa kuwafikia wananchi hata kama haziipendezi Serikali ilioko madarakani.

Mheshimiwa Spika, Ninasema hayo kwa sababu kumekuwa na malalamiko kutoka kwa baadhi ya waandishi wa habari kuwa, viongozi wengi wa Serikali wapo mbali nao pamoja na Rais kuagiza kuwa viongozi wa Serikali wawe karibu navyo. Lakini wakati huohuo, tumewasikia mara nyingi viongozi wa Serikali wakilalamika kuwa vyombo vy a habari havikutoa kwa usahihi taarifa fulani kutoka katika mamlaka zao. Kwa kukaa mbali na vyombo vy a habari, unategemea waandishi waandike kwa usahihi upi suala ambalo wewe mwenyewe hukutaka kulizungumzia? Tunatambua kwamba Wizara hii ni mpya, na mpongeza Rais wa awamu ya nne wa Jamhuri ya Muungano kwa kutambua kuwa sekta ya habari inashabihiana sana Sekta za utamaduni na michezo. Katika harakati za kukuza michezo na kuuenzi utamaduni wetu vyombo vy a habari ni muhimu sana. Hivyo, ni wajibu wa vyombo vy a habari kuhakikisha vinazitangaza hizi sekta nyingine ili zifahamike nchini na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Imewahi kutokea mara kadhaa, vyombo vy a habari vy a serikali kushindwa kujiepusha na upendeleo hasa kipindi cha uchaguzi na kufanya kazi zao kwa upendeleo wa chama fulani dhidi ya vyama vingine kama inavyoonyeshwa na vyombo mbalimbali vilivyofanya tathmini ya vyombo vy a habari kipindi cha Uchaguzi.

Kambi ya Upinzani inasisitiza kuwa, taaluma ya uandishi wa habari kama ilivyo kwa taaluma nyingine kama madaktari na wanasheria inabidi izingatie maadili ya taaluma hiyo. Hivyo basi tunatoa wito kwa vyombo vya habari vya serikali na vya sekta binafsi kuzingatia maadili ya uandishi wa habari katika utendaji wa kazi zao ili wananchi wasikose imani na habari wanazozitoa.

Moja kati ya majukumu ya wizara ni kuandaa mipango ya ukuzaji wa sekta ya habari. Ushauri wa Kambi ya Upinzani Bungeni juu ya maendeleo ya sekta ya habari ni Ni vyema serikali ikavijenga vyombo vya habari kama taasisi iliyo huru ambayo itachangia maendeleo ya nchi yetu kwa kukosoa, kulaumu, na kutoa maoni yatakayosaidia kuirejesha serikali au chombo chochote katika mstari ulio sahihi. Taarifa inayotolewa na vyombo vya habari zifanyiwe kazi badala ya kutumia muda mwingu katika kuvilaumu au kuvifunga bila uchunguzi wa kina. (*Makofi*)

(b) Kujenga na kuimarisha utamaduni wa kuwajibika kwa kila kiongozi katika ngazi zote za Serikali na Sekta Binafsi, bila kuwa na mashaka au uwoga.

(c) Serikali ijenge tabia ya uwazi kwa kuhakikisha kuwa, Idara zake zote zinatoa habari ambazo Watanzania na waandishi wa habari, wana wajibu wa kuzifahamu ili waweze kuujulisha umma. Pasiwe na tabia ya baadhi ya viongozi, kuwakimbia waandishi wa habari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika kuzungumzia mazingira ambayo Vyombo vya Habari vinaendeshwa na mazingira ya kazi ya uandishi wa habari, Kambi ya Upinzani inashauri maboresho yafuatayo yazingatiwe:-

- Kwa kuzingatia umuhimu wa kazi zao katika jamii, mazingira magumu na ya hatari ambayo waandishi wa habari wanafanya kazi zao ili waweze kuufikishia umma habari, Kambi ya Upinzani inashauri Serikali na vyombo binafsi vya habari kuboresha mishahara ya waandishi wa habari, wapiga picha na watangazaji.
- Vyombo vya dola viache kuwabughudhi wafanyakazi wa vyombo vya habari bila sababu za msingi na za kisheria, hususan wanapokuwa kazini. Panapokuwa na ulazima wa hatua hizo mathalan kwa usalama wa Taifa, utaratibu wa kisheria tu utumike.
- Pawepo na mikakati ya kuboresha taaluma za wafanyakazi katika sekta ya habari kwa Serikali kuwfadhili wale wanaosomea taaluma hizo, ili wapatikane wataalamu waliofuzu vyema na watakaozingatia maadili ya taaluma hizo.
- Serikali iangalie uwezekano wa kuondoa kabisa ushuru katika vifaa vinavyotumika katika kuandaa habari kama vile makaratsi, ili waandishi wa habari waweze kupata nyenzo za kufanyia kazi na pia wananchi wapate nafuu katika kununua kazi za waandishi, kwani ni ukweli usiofichika kuwa, Watanzania wa kipato cha chini zaidi, wanashindwa kununua magazeti kwa sababu ya bei kupanda mara kwa mara.

- Mheshimiwa Spika, tunamtaka Waziri alieleze Bunge hili, ule mkataba ambao haukutayarishwa na Mwanasheria Mkuu, wa kujenga vituo vya TvT, ambapo mzabuni hadi leo hajakabidhiwa rasmi kazi zake baada ya kulipwa Dola za Kimarekani milioni nne na zaidi kwamba, kampuni hiyo haikuwa na *account* hapa, hivyo hata kodi haikulipa, taarifa zake zikoje? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya sheria zinazoongoza Sekta ya Habari, ambazo zimepigwi kelele sana tangu Serikali ya Awamu ya Pili, lakini hakuna hatua zozote zilizo chukuliwa aidha, kuzifanya marekebisho sheria hizi au kutunga sheria mpya kwa ajili ya kulinda uhuru wa vyombo vya habari. Baadhi ya sheria hizo ni Sheria ya Magazeti ya mwaka 1976; Sheria ya Magereza ya mwaka 1967; Sheria ya Usalama wa Taifa ya mwaka 1970; *Film and Stage Plays Act, 1976*; na Sheria ya Mamlaka ya Mapato ya mwaka 1995.

Mheshimiwa Spika, chini ya Sheria ya Magazeti ya mwaka 1976, Waziri anayehusika na Habari na Msajili wa Vyombo vya Habari (magazeti), wamepewa mamlaka ya juu sana kudhibiti vyombo vya habari kila anapohisi kwamba, maslahi ya umma yako hatarini. Lakini pamoja na uzuri wa neno hilo, (maslahi ya umma), jamii ya Watanzania imekuwa ikishuhudia watawala wakiyafungia magazeti kwa hofu ya kuhatarisha maslahi ya umma, ambayo hayakutafsiriwa. Hivi nani anayetoa tafsiri ya maslahi ya umma, anaweza kuachiwa tu mtu mmoja kazi hiyo, bila hata kushauriwa na chombo chochote? Maamuzi mengine yanatia mashaka makubwa kama kweli ni maslahi ya umma au kwa vile hakuna vigezo vilivyowekwa na wala vilivyo wazi. Ni dhahiri kuwa, sheria hii hailindi maslahi ya umma bali kuficha uovu, huku Serikali mara kwa mara ikivitisha vyombo vya habari kuwa vitafungiwa. Lakini Serikali inasahau kuwa imeshikilia mpini, wakati vyombo vya habari vimeshikilia makali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Magereza ya mwaka 1967, inamzuia mtu yejote kupiga picha maeneo ya magereza au mfungwa, pia kukaribiana nao mahali walipo. Kibaya zaidi, sheria hii imetafsiri magereza kuwa ni popote alipo mfungwa. Kwa hiyo, hata mfungwa akitoroka akavamia maeneo ya watu, kwa mujibu wa sheria hii, hakuna anayeruhusiwa kujihusisha naye kumpiga picha wala kumhoji. Je, askari akikutwa akimdhailisha mfungwa hata mbele ya wapiga picha, wasichukuliwe picha? Hii ni kuifanya Serikali, ishiriki katika udhalilishaji na uovu. Sheria hii ni mbaya na inahitaji kufanyiwa marekebisho haraka sana.

Mheshimiwa Spika, ni kwa mujibu wa sheria hii, baadhi ya wanahabari walishambuliwa na kuumizwa vibaya na askari magereza, waliotumia wafungwa kuwapiga mwaka 2005. Katika hali iliyoonesha utovu wa nidhamu na ukatili wa hali ya juu, aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani, aliwakebehi wanahabari kwa kipigo walichopata. Je, habari na manyanyaso ya mfungwa, hayapaswi kujulikana kwa umma wa Watanzania? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuonesha kuwa sheria hizi hazifai, ipo sheria ambayo sasa inavunjwa kila kukicha na imepoteza maana yake. Sheria hii inasisitiza kuwa, kupiga picha za aina yoyote, kuhusu tukio lolote ni lazima mpiga picha, apate kibali cha

maandishi cha Waziri anayehusika. Hakuna anayeruhusiwa kupiga picha za kumbukumbu yoyote ya kifamilia au tukio lolote la jamii bila kibali hiki. Hii ni kwa mujibu wa Sheria ya Filamu na Michezo ya Kuigiza ya mwaka 1976.

Mheshimiwa Spika, ni wangapi mionganoni mwetu, tumepiga picha hizo katika sherehe za kipaimara cha watoto, ubatizo au ndoa? Ni wangapi tumekuwa tunapiga picha kuweka kumbukumbu hata ya ushindi baada ya uchaguzi? Ni nani kati ya hao walifanya hivyo, kwa kibali cha Waziri anayehusika kama sheria inavyosema?

Mheshimiwa Spika, sheria hii ipo na hata kwa utambuzi wa kawaida tu, inaonesha kuwa sheria hii haina maana kuendelea kuwepo. Kambi ya Upinzani inapenda Waziri alieleze Bunge hili, ni lini ataleta Bungeni marekebisho ya sheria hii na zote zinazofanana na hii ambayo haina mantiki, hazitekelezwi lakini zipo kwenye vitabu vy'a Sheria? (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, zipo baadhi ya sheria zinazowazuia maofisa katika Serikali kutoa habari; sheria ya Usalama wa Taifa, Sheria ya Utumishi wa Umma na Sheria ya Mamlaka ya Mapato, ni baadhi tu ya sheria zinazowanyima haki watendaji kutoa habari. Wanahabari wamefungwa midomo, ndiyo maana nao sasa, kwa kuogopa sheria hizo dhidi yao, wamekuwa wakiandika sifa za wakubwa badala ya kuandika habari. Taarifa zetu nyingi ni za fulani kasema tu, bila uchambuzi halisi wa kilichosemwa kama kina manufaa, mantiki yoyote au kinatekelezeka au ni maneno tu ya kisiasa. *Investigative Journalism* hufanyika na vyombo vichache na hivyo navyo hufungwa mikono kwa kupelekwa mahakamani, hata kama yaliyoelezwa ni ya kweli. Serikali inayaona yote haya na imekaa kimya. Magazeti ya aina hiyo ni kama *This Day*, Kulikoni, Tanzania Daima, Mwana Halisi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, sheria hizi zote zinakiuka kwa namna moja au nyingine, Katiba ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania hasa Ibara ya 18(d) inayosema kuwa: "Kila mtu anayo haki ya kupewa taarifa wakati wote, kuhusu matukio mbalimbali muhimu kwa maisha na shughuli za wananchi na pia kuhusu masuala muhimu ya jamii."

Suala la uhuru wa vyombo vy'a habari kama lilivyo ainishwa katika Muswada wa Haki za Binadamu wa Kimataifa, ambao Bunge lako Tukufu liliupokea, liliuridhia na kuufanya sheria.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyaainisha mambo haya, Kambi ya Upinzani inataka Wizara, itoe maelezo kuhusu mambo yafuatayo:-

- Je Wizara hii inatambua kuwepo kwa sheria hizi zinazokiuka kanuni za uhuru wa kutoa na kupokea habari na uhuru wa vyombo vy'a habari? Kama inatambua kuwepo kwa sheria hizi ni hatua gani imechukua au inachukua au itachukua ili kuzibadilisha au kuzifuta sheria hizi ili kuruhusu demokrasia ya kweli ishamiri nchini?

- Kwa nini Gazeti la Serikali ambalo ndilo gazeti linalochapisha taarifa muhimu za Serikali, haliwafikii wananchi wa ngazi zote na katika Mikoa yote na Wilaya zote za nchi? Pia kwa nini Hotuba za Kambi ya Upinzani hazichapishwi katika Gazeti la Serikali? (*Makofsi*)
- Ni lugha gani inatumika katika gazeti hili na wakala gani hulisambaza hili gazeti na ni watu gani wanapatiwa gazeti kila chapisho linapotoka?
- Utendaji wa Idara ya Habari Maelezo, kwa kuzingatia sheria zinazoongoza Sekta ya Habari na kanuni na taratibu ambao Idara hii imejiwekea, unanufaishaje au unazingatia vipi uhuru wa vyombo vya habari kama ilivyoelezwa kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania?
- Taratibu gani zilizotumika kumpata mkandarasi wa kununua na kujenga mitambo ya TvT, wakati zabuni haikutangazwa?
- Ni kampuni gani ilikuwa mshauri katika awamu ya kwanza ya mradi wa ujenzi wa vituo vya Televisheni ya TvT?
- Utaratibu gani uliotumika katika kumlipa mkandarasi, kwani inaonesha *invoice* hazikuonesha mchanganuo wa kazi alizozifanya. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni moja ya nchi ambazo ina vipaji vingi vya wanamichezo katika nyanja mbalimbali. Historia inatueleza kuwa, katika miaka ya sabini na themanini, nchi yetu ni moja kati ya nchi zilizokuwa zinashiriki na kufanya vyema katika mashindano mbalimbali, yakiwemo ya olympiki na michezo ya Jumuiya ya Madola.

Mheshimiwa Spika, lakini ukweli ni kwamba, hali ya sasa ya Tanzania katika Sekta ya Michezo, inakatisha tamaa sana. Ingawa nchi yetu ina amani na utulivu na watu wenye vipaji vya kila aina, inashangaza jinsi sekta yetu ya michezo, inavyozidi kudidimia siku hadi siku, tofauti na ilivyo kwa nchi za jirani. Ni miaka mingapi sasa, Tanzania hajashikika nafasi ya kwanza katika Kombe la Mataifa ya Afrika? Je tutapata lini nafasi ya kushiriki hata kwenye kombe la Dunia tu, ukiondolea mbali ndoto ya kushinda?

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa Watanzania wanapenda sana mafanikio ya timu zao katika medani za Kimataifa. Mfano mzuri ni mwaka 2004, timu ya soka ya Simba ilipomtoa bingwa mtetezi timu ya Zamaleki ya Misri na kufanikiwa kuingia katika hatua ya makundi, ambapo Watanzania walishangilia sana. *Miss Tanzania 2005*, Nancy Sumari, alipotwaa *Miss World Africa* na Samson Ramadhani alipotwaa medali ya dhahabu wakati wa michezo ya jumuiya ya madola, walileta faraja sana kwa nchi yetu. Kambi ya Upinzani inatoa pongezi kwa wanamichezo hao na kuwatia nguvu wawakilishi wetu wengine katika medani za Kimataifa. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Spika, mafanikio hayo na kutokufanikiwa kwa namna nyingine ni changamoto kwa Wizara na Watanzania kwa ujumla ili tuweze kuinua Sekta ya Michezo

nchini. Kambi ya Upinzani ina maoni yafuatayo katika suala zima la kuinua michezo nchini:-

Mheshimiwa Spika, mpira wa miguu (soka) ni kati ya michezo maarufu sana duniani. Mchezo huu umeweza kuzijengea heshima na kuziongezea pato la kiuchumi nchi nyingi duniani, kama vile Brazil, Argentina kutoka Amerika ya Kusini na hata hapa kwetu Afrika nchi kama Nigeria, Cameroon na Afrika Kusini. Mchezo huu pia umeweza kuwaajiri vijana wengi sana nje na ndani ya nchi hizo na kuwafanya waweze kuboresha maisha yao.

Mheshimiwa Spika, kati ya matatizo makubwa yanayokwamisha maendeleo ya soka Tanzania ni pamoja na wachezaji na wadau mbalimbali, kutouchukulia mchezo huu kama kazi, kama vile zilivyo taaluma nyingine. Vijana wenyе vipaji vya soka, hushindwa kuweka malengo yao katika soka kutohana na kutokuona matunda ya mchezo huo kwa waliowatangulia. Ni wakati muafaka sasa wa kufahamu ukweli kuwa, wachezaji wa mpira wa miguu ni kati ya watu wanaolipwa zaidi na kuongoza kwa kipato katika nchi zilizoendelea kama Ujeruman, Uingereza, Ufaransa na kadhalika. Wachezaji wa nchi ya Nigeria wanaocheza nje, huchangia kwa kiasi kikubwa mno pato la nchi yao. Kambi ya Upinzani ina imani kuwa, kama mikakati endelevu itawekwa katika mchezo huu, Watanzania watanufaika kama nchi nyingine za hapa hapa Afrika zinavyonufaika.

Mheshimiwa Spika, katika mpango wa kukuza vipaji vya soka, kulikuwa na shule zinazotoa elimu pamoja na kuendeleza michezo kama Shule ya Sekondari Makongo na Jitegemee. Mpango huu uliwekwa wakati sekta ya michezo ikiwa chini ya Wizara ya Elimu na Utamaduni, ingawa mpango huu haukuwa na mafanikio yanayoonekana lakini inaleta maana zaidi kama utambuzi wa vipaji vya vijana katika michezo kuanzia umri mdogo kama utafanyika mashulen.

Mheshimiwa Spika, vijana wenyе kipaji cha soka waliweza kutambuliwa vyema zaidi katika michezo ya UMISHUMTA na UMISETA. Sasa hivi mashindano hayo yamefutwa mashulen, bila sababu zinazoelewaka. Lakini tunadhani ni ule utamaduni wa kufanya majoribio kwa kila sera inayoletwa. Hivyo basi, kwa kutambua kuwa sekta hii sasa ipo katika Wizara mpya tofauti na Wizara ya Elimu, Kambi ya Upinzani inataka Waziri atoe maelezo ni kwa namna gani, ataweka mikakati ya kufanikisha azma ya kutambua na kuendeleza vipaji kwa hawa vijana wetu? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, katika kuinua na kuipa heshima Tanzania katika ulimwengu wa soka, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ifanye mambo yafuatayo:-

- Wizara ianzishe shule na makambi ya soka kwa vijana wadogo sehemu mbalimbali nchini. Kambi ya Upinzani inaamini kuwa, shule na makambi hayo, yanaweza kuwasaidia vijana kutambua vipaji vyao na kuviboresha zaidi ili taaluma hiyo iwe ajira zao baadaye kama ilivyo kwa madaktari na wanasheria. Kukosekana kwa shule kama hizo, kumesababisha vijana wengi kujiingiza katika vitendo viovu hasa pale ambapo hawapati nafasi ya kujiendeleza kielimu. Vijana hao watakuwa pia mabalozi wazuri wa kutangaza jina la nchi yetu Kimataifa bila gharama kubwa.

- Serikali iweke utaratibu wa kuwahimiza watu binafsi, kuanzisha timu za kukuza vipaji na kuziorodhesha timu hizo ili zipewe ruzuku, kuwawezesha wamiliki hao binafsi wanaoendesha timu za wachezaji chipukizi hata katika ligi daraja la pili au daraja la tatu. Kwa mfano, Timu ya Palsons ya Arusha, iliyokuwa ikimilikiwa na mtu binafsi, ilishindwa kuendelea na ratiba ya michuano baada ya mmiliki kuyumba kifedha. Hivyo, watu kama hao Serikali inapaswa kuwasaidia ili kukuza mchezo wa soka nchini. (*Makofi*)

- Vianzishwe vyuo vya kuwafundisha makocha mbinu za kisasa katika ufundishaji wa soka ili waweze kutumia ujuzi huo katika kukuza vipaji sehemu mbalimbali nchini.
- Vyombo vya habari virushe matangazo ya mchezo huu moja kwa moja (*live*) ili kuwajengea Watanzania tabia ya kuzipenda timu zao, badala ya kuhamishia upenzi wao katika ligi za Ulaya. Inakatisha tamaa kuona vijana wetu wanathamini zaidi timu za Uingereza au Ulaya kuliko timu zetu za hapa nyumbani.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inapongeza jitihada zilizofanywa na Rais wa Tatu katika kujenga uwanja wa kisasa zaidi nchini na jitihada za Rais wa Awamu ya Nne, kuwaleta makocha wa kigeni kuja kuifundisha Timu ya Taifa. Lakini juhudhi hizi zitazaa matunda tu pale ambapo walimu hao wenye ujuzi wa juu kutoka nje, watakapo chukuliwa nchini kuandaa mpango wa muda mrefu wa kukuza soka nchini kwa kuzingatia yafuatayo:-

- Kutoa ujuzi wa soka kwa walimu Watanzania katika chuo maalumu cha ukocha kama tulivyoshauri hapo juu.
- Kutengeneza mitaala ya soka itakayotumika katika shule za kukuza vipaji vya vijana wadogo katika shule maalumu za soka.
- Serikali itenye fedha za kutosha kutekeleza mipango na mikakati itakayowekwa. Vinginevyo ni wimbo ule ule wa kawaida. Mathalan, hata tungelikuwa na walimu bora kabisa, bila fedha za maandalizi ya timu, michezo mingi ya kirafiki ndani na nje ya nchi kama sehemu ya maandalizi, motisha kwa wanamichezo wenyewe na uhakika wa maisha kwa familia zao, jitihada za kuwaleta makocha tu hazitakuwa na manufaa yoyote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vilabu vya soka nchini vimejaa migogoro mingi sana. Migogoro hiyo inatokana hasa na vilabu kukosa njia mbadala ya kujipatia mapato na kutegemea mapato ya mlangoni. Mgogoro huu umeonekana kati ya vilabu na shirikisho la mpira wa miguu na kwa namna moja kuathiri maendeleo ya soka nchini. Inasadikika kuwa hiyo ni moja ya sababu za kushindwa kuoneshwa kwa mechili hizo moja kwa moja, kwa kuogopa kukosa mapato ya mlangoni. Serikali na vyombo husika, havitambui ni jinsi gani wasivyowatendea haki wananchi wa Mikoa ambayo mechili hizo hazichezwi.

Mheshimiwa Spika, kama viwanja vya mchezo huu vitaboresha, sehemu ya kuegesha magari zikawepo na watazamaji watacaa kwa starehe, hata mechii zikioneshwa moja kwa moja kwenye luninga, haitawafanya watu washindwe kwenda kushabikia timu zao. Changamoto ni kuandaa miundombinu, itakayowavuta watu kwenda kuangalia mechii hiso, kwani kwa kushindwa kuonesha mechii hiso, kunafanya hata wale vijana wachache wenyewe vipaji, wasionekane wakapata soko nje.

Mheshimiwa Spika, ushauri wa Kambi ya Upinzani kwa timu ni kuhakikisha zinakuwa na njia mbadala za kujipatia mapato, kama mauzo ya jezi kwa wapenzi, kuboresha miradi waliyokuwa nayo kama magazeti na kalenda zenye picha na matukio mazuri, ili waweze kujipatia mapato zaidi na si kutegemea mapato ya mlangoni. Uboreshaji wa miradi yao, unawezekana tu kama watawatumia wataalamu (*consultants*) wenyewe ujuzi na kazi hiso. Pia vilabu viendeshwe kwa mbinu za kisasa na kisayansi zaidi.

Mheshimiwa Spika, vijana wa Kitanzania wanavyo vipaji katika michezo na kama watawezesha kukuza na kuendeleza vipaji hivi, basi wataweza kupata ajira katika vilabu vingi vya nje na ndani ya nchi na kuweza kujipatia kipato kutokana na fani hiso na hivyo kuongeza Pato la Taifa. Kambi ya Upinzani pia inashauri jitihada zifanyike katika kukuza michezo ya jadi.

Mheshimiwa Spika, wakati mashindano ya Kombe la Dunia yalipofanyika Ujerumani mwaka huu, nchi za jirani kama Poland, Switzerland na Australia, zilinufaika sana kiutalii, kutokana na wageni walitembelea nchi hiso. Kwa kuwa mashindano haya yatafanyika nchini Afrika Kusini mwaka 2010 na kwa kuzingatia kwamba, Tanzania na Afrika ya Kusini ni karibu, hivyo basi nchi yetu inaweza kunufaika kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, tukiboresha viwanja vyetu, tunaweza kupata timu zitakazopumzika na kufanya mazoezi hapa nchini, kwani nchi yetu inaaminika sana kwa hali ya usalama Duniani. Timu na hata maelfu ya mashabiki, wanaweza kuvutiwa kutembelea maeneo yetu ya utalii kama tukiweka mikakati imara na ya uhakika ya kujitangaza. Tuna miaka minne ya kuijandaa, tunaweza tukiamua.

Mheshimiwa Spika, tunaweza kutumia fursa hiyo pia kutangaza vivutio vyetu vya kitalii kama vile Mlima Kilimanjaro na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro na Serengeti, kwa kuwa sehemu ya wadhamini wa mashindano hayo. Yawezekana fedha nyingi zitahitajika lakini ni lazima ujasiriamali utumike. Hii ni nafasi ya pekee, ambapo macho ya Dunia nzima yataelekezwa Afrika. Hivyo, sidhani kama nchi yetu itashindwa kutumia nafasi hii ya pekee, ubunifu ndio unaotakiwa.

Mheshimiwa Spika, utamaduni unaitambulisha nchi katika anga za Kimataifa na kila nchi zilizoendelea zinazingatia kudumisha utamaduni wake. Ni ukweli usiofichika kuwa, utamaduni unaitangaza nchi na hata kuijengea heshima. Lakini kadiri siku na miaka inavyokwenda, utamaduni wa Mtanzania unazidi kupotea. Vielelezo vya utamaduni ni vingi lakini katika hotuba hii, ningependa kutilia mkazo suala la lugha, mila, mavazi na sanaa za maonesho.

Mheshimiwa Spika, lugha, Mataifa makubwa duniani kama China, Japani, Ujerumani, yanajitahidi kila kukicha kuhakikisha kuwa lugha zao zinapata nafasi ya kufahamika katika anga za Kimataifa. Lakini lugha yetu ya Kiswahili, ingawa ipo katika orodha ya lugha za Kimataifa, bado haijafanyika mikakati ya makusudi ya ndani na nje ya nchi, kuikuza lugha hii. La ajabu hata Katiba yetu, haitamki kwamba, Kiswahili ni lugha ya Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sanjari na jitihada za kuendeleza lugha ya Taifa, Kambi ya Upinzani inataka msisitizo pia uwekwe katika kukuza na kuziendeleza lugha za asili. Kambi ya Upinzani inashauri mambo yafuatayo yazingatiwe katika kukuza lugha ya Kiswahili Tanzania:-

- Kwa vile Katiba yetu, iko kimya kuhusu Kiswahili kuwa lugha ya Taifa letu, hatua za haraka sana zichukuliwe ili Kiswahili kitajwe katika Katiba na Sheria yetu kuwa Lugha ya Taifa. Hakuna pahali pazuri pa kukienzi kama kukiweka kwenye Katiba ya nchi.
- Wizara iandae mpango wa kudumu wa kutengeneza mitaala ya kufundishia lugha ya Kiswahili pamoja na walimu wajuzi katika mitaala hiyo ili watumike kufundisha lugha hiyo nje ya nchi kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.
- Baraza la Taifa la Kiswahili lichukue hatua za makusudi, kubuni na kusanifu maneno mbadala ya Kiswahili yatakayochukua nafasi ya lugha za kigeni katika nyanja za sayansi na technolojia. Kwa kuwa sekta hii ipo pamoja na sekta ya habari, basi pawepo namna ambayo maneno haya yatawafikia Watanzania kwa haraka zaidi ili yapate kuzoleka.
- Baraza la Kiswahili lipanue wigo wa utendaji wake zaidi kwa kuanzisha na kuboresha Mabaraza ya Kiswahili katika Wilaya na hata Tarafa.

Mheshimiwa Spika, mwezi Aprili, 2004 kulikuwa na harakati za Kitaifa za kutafuta vazi la Mtanzania. Tunatambua kwamba, fedha nydingi zilitumika katika harakati hizo lakini mpaka sasa bado haijafahamika wazi ni vazi gani linamtambulisha Mtanzania. Kambi ya Upinzani, inamtaka Waziri atoe maelezo ni vazi gani linamtambulisha Mtanzania? Ni nini matokeo ya Mashindano na mchakato ule umeishia wapi?

Mheshimiwa Spika, tunatambua ya kuwa kuna mila na desturi zilizopitwa na wakati au zenye athari kwa jamii. Lakini kuna mila na desturi nyingine ambazo hazina budi kuenziwa kwani ni muhimu sana katika kuwajenga Watanzania wenye heshima, maadili mema na moyo wa uzalendo. Utandawazi umekuwa kikwazo kikubwa katika kuziendeleza mila na desturi hizi hasa mijini. Vyombo vyta viwe mstari wa mbele katika kulinda, kukuza na kuenzi mila zetu nzuri na kupiga vita mila mbovu.

Mheshimiwa Spika, Tanzania tuna ngoma za jadi na muziki wa asili wa kuvutia kama nchi za kigeni. Kikwazo ni kuwa Serikali haijafanya jitihada za makusudi, kuienzi

na kuikuza sekta hii ya sanaa za maonesho na hivyo, kuwafanya wasanii wetu kuiga zaidi sanaa za kigeni. Kwa kuwa sekta hii iko pamoja na sekta ya habari, wakati umefika wa kutangaza sanaa za asili ili zipate nafasi katika ulimwengu wa sasa wa utandawazi. Kuna sanaa nyingine kama mazingaombwe na iwapo zitaboreshw na wahusika kuwezesewa, tungeweza kuwavutia watalii wengi nchini huku tukinufaika kwa fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge ahsante sana. Kabla hatujaendelea, napenda niwatambue wageni walioko *Speaker's Gallery*, upande wa kushoto ambaao ni Viongozi wa Kampuni inayoitwa *Sub Sahara Resources* ya Australia na tayari wamekutana na Kamati ya Uwekezaji na Biashara, Kamati ya Miundombinu na Kamati ya Fedha na Uchumi. Wanataka kuona jinsi gani wanaweza kushiriki katika Sekta ya Madini. Wameonesha shauku ya kufanya utafiti juu ya Mkaa wa Mchuchuma na Chuma cha Liganga. *Welcome to the House. We are very pleased that you could have come all the way from Australia to visit us. I hope our cooperation will be mutually beneficial. Thanks very much.* (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, orodha niliyonayo ni ndefu, lakini Wizara hii ina Waziri na Naibu Mawaziri wawili, kwa hiyo, haitawezekana kutoa nafasi ya kuchangia kwa jioni. Kwa hiyo, nitamwita Naibu Waziri wa kwanza saa 11.00 jioni na Naibu Waziri wa pili saa 11.15, baada ya hapo mtoa hoja saa 11.30 hadi saa 12.30 ili tuingie kwenye Kamati ya Matumizi. Sasa kwa uzoefu wetu basi inapokuwa ni asubuhi tu ndipo uchangiaji unakuwa hadi saa 7.00, kuna uwezekano wa wachangiaji sita, kama mmoja atakubali kuchangia kwa dakika kumi. Hivi ndivyo tulivyochambua tukaona. Sasa kwa mchanganyiko ule ule unaozingatia waliochangia kidogo zaidi, yaani ambaao hawajachangia kabisa au ambaao wamechangia mara moja wanapewa kipaumbele. Kwa mchanganyiko wa Waheshimiwa Wabunge kutoka Bara na Zanzibar. Orodha yangu sasa inayojitokeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mbunge, ambaye hajachangia hata mara moja ni Mheshimiwa Ali Haroon Suleiman, Waziri wa Elimu Zanzibar. Waheshimiwa Wabunge, waliochangia mara moja tu ni Mheshimiwa Zanaib M. Vulu, Mheshimiwa Nuru A. Bafadhili, Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir na Mheshimiwa Thomas A. Mwang'onda. Sasa hapo tayari Waheshimiwa Wabunge watano. Waheshimiwa Wabunge ambaao wamechangia mara mbili na ambaao itabidi nimteue mmoja na nimekwishafanya hivyo, sidhani kama niwataje wote, lakini kwa jinsi namna ilivyokaa orodha yenyewe, nimeona nimirambue Mheshimiwa Capt. John D. Komba. Kama zitabaki dakika 10, nitampa Mheshimiwa Amina C. Mpakanjia. Hiyo ndiyo orodha. Kwa hiyo, sasa namwita Mheshimiwa Ali Haroon Suleiman.

MHE. ALI HAROON SULEIMAN: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa asubuhi ya leo, kutujalia afya njema sote na pia nakushukuru wewe Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kwanza kuchangia katika Bunge hili Tukufu.

Nachukua nafasi hii kwa vile ninasema kwa mara ya kwanza, basi nampongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa ushindi mkubwa alioupata. Nampongeza Mheshimiwa Amani Abeid Karume, Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa ushindi alioupata. Nawapongeza vilevile Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nakupongeza wewe Mheshimiwa Spika, kwa dhati kabisa kwa kuchaguliwa kwako kuwa Spika wa Bunge letu hili Tukufu, pamoja na Naibu Spika na Wenyeviti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba pia nichukue nafasi hii, kuwashukuru Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, kwa heshima hii walijonipa, kunichagua mionganoni mwa Wajumbe watano kuwakilisha Baraza katika Bunge hili Tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii, kumpongeza sana Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib na Manaibu wake, kwa hotuba nzuri iliyowasilishwa hapa. Kwa kweli Wizara hii inamgusa kila mmoja wetu katika nchi yetu hii Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lakini sitotenda haki kwa sababu mimi nilikuwa na jukumu wakati wa Awamu iliyopita Zanzibar, nikiwa Waziri wa Elimu, Utamaduni na Michezo, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mawaziri waliotangulia, ambao walikuwa na majukumu ya Utamaduni na Michezo. Nilishirikiana sana na Mheshimiwa Prof. Juma A. Kapuya na Naibu Waziri, Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir na kwa kweli walisaidia sana maendeleo ya michezo katika Jamhuri yetu ya Muungano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii vilevile kulishukuru Baraza la Michezo (*TFF*), chini ya uongozi wa Leodgard Tenga, kwa ushirikiano mkubwa waliotupa. Nakumbuka wazi tukiwa tunakaribia Uchaguzi Mkuu 2005, tukiwa wanachama tuliokuwa na *status ya observer* katika Shirikisho la Mpira wa Miguu la Afrika (*CAF*), michezo basi tukapewa hadhi kwamba, tuwe *observers* katika Shirikisho la Mpira Miguu la Afrika. Tukapata mtihani mkubwa, tulipokaribia kwenye Uchaguzi Mkuu wa 2005, tukaambiya kwamba, Zanzibar imefutwa kwenye Uanachama ule. Kwa kweli ulikuwa ni mtihani mkubwa wakati uchaguzi ulishaingia na mimi nikiwa Waziri wa Michezo, nikasema sasa unga wangu unaanza kuharibika haribika.

Mheshimiwa Spika, lakini namshukuru Mwenyezi Mungu, chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Prof. Juma A. Kapuya na Baraza la Michezo na *President* wa *TFF* walikuja Zanzibar, ikafanyika juhudi kubwa sana. Hatimaye tukapeleka ujumbe Cairo na nazishukuru Wizara zote mbili ya Zanzibar na ile ya Jamhuri ya Muungano, zimeendeleza ushirikiano huo na hatimaye Zanzibar imepata tena Uanachama wake ule. Hizi ni juhudi kubwa, ambazo zinastahili kupongezwa na ninaomba ziendelee sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii, kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kauli zake za vitendo za kuahidi kwamba, ataendeleza sana mchezo huu wa soka na kwa kweli watu huwa wanasema nyota njema huonekana alfajiri.

Leo hii tumeshuhudia kocha aliyeahidi Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, yupo hapa Dodoma. Nachukua nafasi hii kumpongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini naomba nitoe tahadhari kidogo, tusiwe na haraka ya kutoa maamuzi ya kuamua kocha huyu mapema. Mara nyingi sana tunakuwa na jazba, tukicheza mechili za majaribio mara mbili, mara tatu, tukifungwa tunaanza kusema kocha huyu hafai. Kila kocha mpya anapokuja basi tunampungeza, safari hii tumepata kocha mzuri na tunaanza kumsifia, lakini wakifungwa tu basi inakuwa ni matatizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, maadamu tumeshaamini kwamba, Brazil ndiyo ardhi ambayo mpira umeumbwa, basi naamini kabisa kwamba, uwezo tunao Watanzania kufanya vizuri na hatimaye kushiriki katika Kombe la Dunia litakalofanyika kule Afrika Kusini. Tusije tukafanya ile hadithi fulani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba uniruhusu nitoe hadithi ndogo tu ya mzee wetu mmoja, wakati niko pale Shule ya Sekondari ya Haile Selassie, nikiwa Mwalimu Mkuu. Kuna mzee wetu mmoja alikuwa anasema ana matatizo ya macho, sasa walikuwa wanakuja kututembelea watu wa *Lions Club* pale katika shule yetu na kupima macho wanafunzi, walimu na wananchi. Yule mzee alikuwa *messenger* pale shulenii, akaniambaa Mwalimu Mkuu nimekuja kwako na mimi unipeleke kwa wale Madaktari wanipime macho. Nikamwuliza una matatizo ya macho, akaniambia ninayo matatizo ya macho. Nikamwambia twende, akawekewa *lens* zile sijui namba ngapi, akasema ni nzuri, akawekewa *lens* nyingine, akasema hii ni nzuri zaidi. Alipowekewa *lens* namba nyingine akasema tena hii niachie niondoke nayo, nikamwambia yule daktari hebu mpeni miwani ambayo haina *lens* yoyote, yaani miwani ambayo haina kioo. Alipopewa ile akasema hii ndiyo nzuri kabisa kupidia zote. Sasa hii ni kuonesha kwamba, alichokuwa anahitaji ni kupata *status* kwamba na yeche na anavaa miwani. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, sasa makocha wetu, kila aliyejua mwanzo anaanza kazi tunamsifia ni mzuri, yanapoharibika tena tusije tukamlau. Kocha huyu tusianze kumsifia kwamba ni mzuri, naomba tuwe wastahimilivu na tuendelee kumtunza kocha huyu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tuna nafasi nzuri sana kwa kulitumia Kombe la Dunia litakalofanyika Afrika ya Kusini, sisi Tanzania kuijendeleza kiuchumi na kiutalii vilevile. Wakati nikiwa Afrika Kusini hivi karibuni katika Ujumbe wa Rais, wafanyabiashara hata Ubalozi wetu pale Afrika Kusini walitushauri kwamba, Tanzania tuna nafasi nzuri sana ya kutumia Kombe la Dunia litakalofanyika Afrika Kusini katika kuendeleza uchumi wa nchi yetu na kukuza utalii. Mungu ametujalia Rais wa Awamu ya Tatu, aliahidi kujenga kiwanja na kiwanja kinajengwa na kitamalizika hivi karibuni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunaweza tukatumia nafasi hii kwa kutumia kiwanja chetu kizuri cha kisasa, hizo timu zitakazotoka huko nje hasa huko Mashariki ya Mbali, pengine na *Europe*, wakaamua pengine kuweka *station* yao kwa muda hapa Tanzania na wakafanya mazoezi hapa wakati huo na hiyo itakuwa ni faraja kubwa. Wakati huo huo, kwa imani niliyokuwa nayo kwa kocha aliyejukwepo chini ya Uongozi wa *TFF*, nina

imani kubwa sana kwamba, vijana wetu watakuza vipaji vyao na tutakuwa na wachezaji wazuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika hili naomba nishauri kwamba, tutembee Tanzania mpaka Vijijini, tukuze vipaji vyaa watoto wenye umri chini ya miaka 23. Mimi nina imani kubwa kwamba, wachezaji wazuri tunao, kocha mzuri tunaye, tunachohitaji ni wachezaji wazuri vilevile, kwa hiyo, tujitahidi kuandaa vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba uniruhusu nizungumzie kidogo suala la utamaduni, hasa kwenye sehemu ya lugha. Napata mtihani mkubwa mimi nikiwa ni Waziri wa Elimu kwa upande wa Zanzibar na lugha ya sehemu zote mbili ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na inayokubalika ni lugha ya Taifa tunayotumia katika Taasisi zetu mbalimbali. Sasa kuna maneno mapya, ambayo yanaingizwa katika lugha yetu. Kwa bahati mbaya sana, baadhi ya maneno ambayo yapo kwenye Kamusi ya Kiswahili Zanzibar, kuna baadhi ambayo yanatumika sasa hivi hapa Tanzania, lakini hayako katika Kamusi ile ya Zanzibar.

Wasiwasi niliokuwa nao kwenye Baraza la Mitihani, kuna baadhi ya maneno yatatumika kwa sababu yanakubalika upande mmoja, lakini yanaweza yasikubalike upande mwingine kwa mujibu wa utaratibu wa Kiswahili kilivyo.

Kuna maneno kwa mfano hili neno kuboresha. Hapa nilikuwa nahesabu toka nimeingia Bungeni, maneno kuboresha sijui elfu ngapi, milioni ngapi yameshatumika. Kiswahili kinakua, mimi nakubali na mimi napongeza sana juhudzi za Wizara kwamba, Baraza la Kiswahili la Tanzania na Baraza la Kiswahili la Zanzibar, wamekaa, wamekubaliana na wamefikia muafaka kwamba, kuna maneno 66 wameshakubaliana kwamba, yatumike sehemu zote mbili. Lakini wataalamu wa lugha za Kiswahili wanasema kweli Kiswahili kinakua, lakini pia kuna neno kwa mfano la sifa wanasema kuongeza neno mbele ni kosa.

Kwa mfano, huwezi kusema zuri halafu ukasema zurisha, baya, ukasema baisha. Sasa na hili neno bora ni sifa sasa unasema boresha. Sasa haya maneno yaangaliwe vizuri katika matumizi yake. Mimi nakubali kwamba, yanaweza yakatumika pindi pande zote mbili zikikaa na Mabaraza yetu ya Kiswahili yakakubalika.

Kwa mfano, televisheni tunatumia neno luninga na baisedeli tunaendelea kutumia neno baisedeli, kwani kuna haja gani kutumia luninga tusiendelee kutumia televisheni.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi kwa heshima kubwa kabisa, naomba Mabaraza haya mawili yakae, yakutane, yakubaliane ili yasije yakaleta matatizo katika mitihani yetu. Kwa sababu watoto wataendelea kutumia na haya ni maneno ambayo wanafundishwa na walimu wao.

Mheshimiwa Spika, kwa kuheshimu muda wako na kwa kuwa ni mara yangu ya mwanzo, ili kuja kupata nafasi hii mara nyingine, naomba kuunga mkono hoja hii. Ahsante sana.

MHE. ZAYNAB M. VULU: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumuunga mkono Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri, yenye matumaini kwa wananchi wa Tanzania, ambao wanapenda kuhabarishwa na kupata burudani kuitipia vyombo vya habari. Kila Mtanzania kama hotuba yake inavyoelezea, ana haki ya kupata habari, kutafuta na kuzitumia kwenye vyombo vya habari. Ni hatua kubwa tumepiga Watanzania, napenda niipongeze Wizara kwa kuruhusu kuwa na vyombo vya habari vingi. Tulianza na magazeti mawili, bila shaka lilanza moja yakafika mawili, hadi sasa hivi magazeti ya kila siku tunayo 15. Tulianza na redio moja ikaenda zikawa tano, sasa hivi tunazo redio stesheni 40. Tulianza na televisheni stesheni moja, hatimaye sasa hivi tunazo stesheni 32. Sasa haya ni matumaini makubwa sana. Lakini mimi hoja yangu kuitipia hivi vyombo vya habari ni moja tu hasa kwenye redio na televisheni.

Televisheni na redio utakuta wamiliki wa hivyo vyombo vya habari, sehemu kubwa wanayoitumia ni habari zinazotoka Magharibi. Sisi Katiba yetu tunasema kwamba, Watanzania ndio wafaidike zaidi na habari za ndani ya nchi yao na Wizara ikiwa na jukumu la kuhakikisha kwamba, wananaufaika na kupata hizo habari. Lakini unakuta hata sasa hivi ukienda kufungua stesheni kule watoto wangu wa Kisukuma, sijui hata kama wanaelewa kile kinachozungumzwa mle ndani. Wakifungua *Sky News*, BBC na *CNN*. Sasa sijui mlengwa mkuu ni nani. Wizara katika hili inatuambia nini? Ikiwa sisi Tanzania ni nchi kubwa sana, tuna mambo mengi sana katika maendeleo ya jamii, kilimo na uchumi, ambayo kila mkoaa au kila mwananchi, ana haki aelezwe kitu gani ambacho kinapatikana kwa wenziwe ili naye aweze kujifunza. Lakini badala yake, tumeruhusu vyombo hivi sehemu kubwa ya matangazo yanatumika matangazo ya Magharibi, ambayo mimi naona kweli tuna haki ya kuyapata matangazo ya Magharibi, lakini bado hatujafikia kiasi hicho, kuna asilimia bila shaka 65 kama sio 75 ya matangazo ya televisheni zetu zinatumia matangazo ya Magharibi.

Naiomba Wizara inipatie ufanuzi kwa nini suala hili wameliweka hivyo na kuwapa nafasi hawa wamiliki wa vyombo vya habari. Kwa sababu mimi nina hakika, wamiliki wa vyombo vya habari wana uwezo wa kutoa matangazo mengi kwa sababu wenyewe taaluma ya Uandishi wa Habari ni wengi lakini badala yake, wanawatumia kuwafanya Waandishi wa Habari wa Kujitegemea. Wananyanyasika Waandishi wa Habari hawa, kama tulivyokuwa tunazungumzia Madaktari, Askari na hawa Waandishi wa Habari inabidi na wao watazamwe maslahi yao yakoje.

Vyombo vya habari vilivyokuwepo, nina hakika vikakidhi kabisa. Mtu mmoja unaweza ukakuta anamiliki zaidi ya vyombo vine au vitano; iwe redio au televisheni. Lakini anaowatumia ni hao Waandishi wa Habari wa Kujitegemea. Mwandishi wa Habari wa Kujitegemea, tuchukulie mathalani anatoka Kisarawe apeleke habari alizozikusanya Dar es Salaam, anatumia nauli, lakini yeye analipwa shilingi 2,000/= na hiyo shilingi 2,000/= halipwi siku hiyo hiyo anayopeleka hiyo habari. Sasa sijui katika hili Mheshimiwa Waziri, watu hawa tunaowategemea sisi Wabunge wote humu ndani, watumie habari zetu kutuletea maendeleo na kutuhabarisha kwa watu wengine, wajue tumefanya nini. Mimi nashangaa sioni kwa nini Wizara mpaka sasa hivi, hajjaweza kusema kwamba kuna maslahi gani ambayo yameweza yakawasaidia au kuvidhibiti

hivyo vyombo au hao wamiliki wa vyombo hivyo walivyokuwa wamevichukua vyombo vingi sana.

Mheshimiwa Spika, ushindani uko kila mahali, kuna televisheni za watu binafsi nyingi na tunashukuru Mwenyezi Mungu amejalia na Serikali ina televisheni yake au chombo chake (TUT). Chombo hiki kama tunataka kifanikiwe, basi mimi nashauri kiendeshwe katika misingi ya kibashara na kiingizwe katika ushindani ili viweze kukidhi na kuleta maslahi kwa Taifa letu. Waandishi wa Habari wapatiwe mafunzo ya kutosha, waangaliwe na wao, vyuo vilivyokuwepo vihakikiwe kwamba kweli vinatoa mafunzo sawa sawa ili navyo vipelekewe watu waweze kupata elimu ya kutosha. Wamiliki wa vyombo vyaa habari wengine wapo, wenye nia njema kabisa ya kutoa habari zao zisizokuwa na upendeleo wa aina yoyote ile. Lakini unakuta wengine wanakwazwa kwa kutokuweza kununua vifaa mbalimbali, kutokana na kodi inayowekwa kuwa kubwa sana. Kodi katika *News Print* ni kubwa, katika wino, vifaa mbalimbali vya redio na televisheni.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara husika, iliangular suala la kodi katika umiliki wa vyombo vyaa habari ili wanaomiliki vyombo vyaa habari na wao waweze kupata unafuu wa aina yake. Nilikuwa naomba kuundwe chombo cha kusimamia masuala ya urushwaji na utoaji wa habari ili kusiwe na upotofu wowote katika utoaji wa habari katika vyombo hivyo vinavyohusika.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wengi wameomba kuchangia, nisiwe mchoyo naomba niishie hapo niwape nafasi wengine.

MHE. NURU A. BAFADHILI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia. Kwanza, napenda kuipongeza Serikali kwa kuweza kutujengea uwanja mpya wa kisasa. Ni imani yangu kwamba, uwanja huo utatumika ipasavyo kuwapa wanamichezo wetu hususan wa soka, mazoezi na kuweza kushiriki vizuri katika Mashindano ya *Olympic* yanayotegemewa kufanyika mwaka 2010 Afrika ya Kusini.

Mheshimiwa Spika, naanza na mchezo wa soka. Kwa kweli soka ni mchezo ambao ni burudani na pia ni ajira. Nchi nyingi wananchi wake wanapata ajira kutokana na kushiriki katika soka. Hata sisi tuna baadhi ya wananchi wetu, wako nchi za nje wanacheza mpira wa kulipwa. Lakini cha kushangaza ni kwamba, soka kwa sasa hivi imefanywa kama ni mchezo ambao wa kupoteza wakati tu tofauti na miaka ya nyuma, miaka ya 1960 na 1970. Mchezo wa Mpira uliitangaza nchi yetu katika sehemu mbalimbali. Tulikuwa na wachezaji waliosifika kipindi hicho, kama kina Marehemu Sembuli, Kajole, Mweri Simba, Omar Zimbwe, Saleh Zimbwe, Hemed Seif, Abdallah Kibadeni na wengine wengi tu, ambao waliweza kuleta sifa katika nchi yetu. Lakini leo mpira umesahaulika na miaka ya nyuma hiyo, watoto walikuwa wakijinasibu kwa majina hayo ,mwingine alikuwa akijiita Abdallah Kibadeni, mwingine akijiita Mweri, Hemed Seif na kadhalika au Sunday Manara.

Leo watoto wanajinasibu kwa majina ya wachezaji kutoka nje. Kuna akina David Beckham, Ronaldino Gaucho, Samwel Ericho, Zinedine Zidane, sijui na wengineo wengi tu. Mpaka ukiangalia kwenye mabasi yetu tunayosafiria, utakuta nyuma kumechorwa

nembo labda za timu ya Manchester, Arsenal, Liverpool, Real Madrid na timu nyinginezo. Ambapo tungetegemea sisi mabasi yetu yangechorwa kwa nembo za timu za Taifa letu la Tanzania. Tuna *Simba Sports*, *Yanga Sports*, *Serengeti Boys*, *Moro United*, *Kagera Sugar* na timu nyinginezo nyingi, tuna *African Sports* na *Coastal Union*. Kwa hiyo, utakuta mchezo wa mpira umekuwa ni kama umedharauliwa, kiasi ambacho Taifa linadidimia. Tunaiomba Serikali isisitizie zaidi mchezo huu wa mpira, hususan Halmashauri zetu za Majiji, Miji, Wilaya, zihamasishwe kuona kuwa huu ni mchezo ambao unastahili kupewa kipaumbele ambao utalitangaza Taifa popote katika ulimwengu huu.

Pia kuhusu hivyo viwanja vya kuchzeza, kwa kweli viwanja vingine viko katika hali mbaya sana. Utakuta viwanja vya mpira vimekuwa ni barabara za kupitia magari. Magari yanapita katikati ya viwanja, baiskeli zinapita katikati ya viwanja, hatuvienzi viwanja vyetu kwa nini tusivienzi? Kwa hiyo, ni wakati muafaka sasa hivi Serikali kutilia mkazo katika kuvienzi viwanja vyetu vya michezo ili michezo yetu iweze kuwa bora zaidi au kuimarika zaidi.

Nikizungumzia pia kuhusu hawa wachezaji wa zamani kama akina Hemed Seif, Omar Zimbwe, Abdallah Kibadeni; Taifa linawaenzi vipi wachezaji hawa ambao walililetea Taifa sifa? Leo mfano hai nina kaka yangu mmoja, Mbwana Bushiri, alichezea mpira ya nyuma miaka ya 1960 au 1970 kwenye *Gossage Cup* wakaleta faida nchini, leo ukimkuta huko Tanga, huwezi kujua kama alikuwa ni mchezaji mpira. Lakini tofauti na wenzetu, tuchukue mfano katika mchezo wa ndondi, Cassias Clay au sasa hivi Mohamed Ali, alikuwa mpiganaji mzuri wa ngumi lakini ngumi zilezile amezirithirisha kwa binti yake, sasa hivi anashiriki katika mchezo wa ngumi. Sasa ilikuwa na sisi wachezaji wetu hawa pia tuwahamasithe kiasi hata yeye kama atakuwa amestaafu kucheza mpira, mtoto wake aweze kurithi uchezaji ule wa baba yake. Lakini matokeo yake, watoto wengi wa wachezaji mpira ni wala unga maarufu, badala ya kushiriki katika mchezo. Kwa sababu mpira umeonekana kama sio mchezo mzuri.

Nikija kwenye masuala ya utamaduni, sanaa za muziki, tuna wanamuziki wazuri, wanamuziki wa taarab na bendi za muziki. Sasa utakuta katika taarab zamani tulikuwa na waimbaji wa wazuri, tulikuwa na akina Shakila Said, Issa Matona na wengineo. Kwa kweli nyimbo zao zilikuwa zina maadili mazuri, japokuwa zilikuwa za mipasho lakini mipasho ile haikuwa ni mipasho ya matusi kiasi ambacho inapoteza maadili. Leo tuna nyimbo nyingine utakuta tena zinaoneshwa kwenye hizo TV, napenda kunukuu, kuna bendi fulani nanukuu aya tu za maneno hayo. Wimbo huo huoneshwa kwenye TV unasema: "Wasela wa vijiweni nafuu wajipatia, uroda kwa foleni kwako wajipendelea." Vitu kama hivyo. Ukiangalia kwenye luninga kama umekaa na mtu ambaye unamwonea haya, huwezi kuangalia ule wimbo kwa sababu yule mwanamama anaonekana ameshika kandiri, anaingia ndani na baba yuko nyuma anashusha suruali yake. Je, yule mtoto anayeangalia luninga akitaka kujifunza pale, atajifunza nini? Ndiyo matokeo yake, watoto wetu wanaingia kwenye maadili mabaya kutokana na nyimbo ambazo hazihakikiwi. Naiomba Wizara ihakikishe kabla nyimbo hazijatolewa rasmi, ziwe zinahakikiwa.

Napenda kuvipongeza sana vyombo vya habari. Tuna vyombo vya habari vingi TVT, Redio Tanzania, *Radio One*, *Channel Ten*, *Star TV* na magazeti, vyote hivyo ni vyombo vyetu vinavyotupa habari. Lakini ninachoomba katika vyombo vya habari, inapofika kipindi cha kampeni tunajua tuna chombo chetu cha Taifa, Redio Tanzania na TVT. Lakini utakuta wakati wa kipindi cha kampeni, vyombo hivyo vya habari, haviruhusu vyama vingine kuonesha kampeni zao katika hizo redio. Tunaomba pia Wizara ihakikishe kusiwe na ubaguzi wa vyama, Kila chama kinachoona kinafaa kushiriki katika redio au katika TV, kishiriki kihalali.

Mwisho, napenda kuwapongeza Waandishi wetu wa habari, wanatuandikia habari nzuri lakini pia napenda kuwalamu kitu kimoja. Mimi nimeshajionea kwenye magazeti mara mbili katika kuchangia kuuliza maswali. Gazeti la Mwananchi na Majira, utakuta limeandikwa jina langu chini, Nuru Awadhi Bafadhili katika mabano (CCM). Tunaomba mtuainishe sisi sote hapa sio CCM, wako watu wa vyama tofauti. Kwa hiyo, mtuainishe kwa vyama vyetu, msituite tu CCM, maana yake huko majimboni kwetu tunaulizw je, mmeshabadi? Kwa hiyo, tunaomba Waandishi wa Habari muwe mnaandika vitu ambavyo ni sahihi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba nikae ili niwape nafasi wenzangu.

MHE. KHERI KHATIB AMEIR: Mheshimiwa Spika, naomba kuungana na wale walioipongeza Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, kwa hotuba nzuri. Nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri na Katibu Mkuu wa Wizara hii, kwa hotuba nzuri ambayo wametuletea. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kitabu hiki kinajieleza chenyewe nini Awamu ya Nne inakoelekea. Juu kwenye *cover*, kuna picha ya Rais kuonesha kwamba, anatilia mkazo suala la michezo. Lakini nyuma kwenye *back cover* unakuta kuna picha amayo ni ya Waziri Mkuu amefuatana na wale ambao wameshatuletea tuze nchini mwetu. Ukifungua nyuma kidogo, kuna kitu kimekaa kama kome, sisi kwetu kule tunaita kome, huu unasemekana ni uwanja ambao unataka kujengwa, hongereni sana. Mnakotuelekeza nadhani ni sawa sawa.

Mheshimiwa Spika, kama mara zote unavyozungumza kwamba, Waandishi wa Habari ni watu muhimu sana katika nchi yetu na kwa kweli sio katika nchi yetu tu, katika nchi zote duniani. Inazungumzwa kwamba, tuna mafiga matatu, lakini kwa mtazamo wa haraka haraka Waandishi wa Habari ni moja katika figa la nne. Kama binadamu tunakula basi tunahitaji habari, tunahitaji kusikia, kusoma, kuona na ni ndugu zetu hawa Waandishi wa Habari kazi hiyo wanaifanya, tunawapongeza sana. Ni kazi nzito na ni kazi nzuri na ni kazi ambayo haiwezekani kukosekana. Hapa tulipo sisi tukitoka hapa ili uweze kupata habari za Kitaifa au za Kimataifa, unakuta sisi tunafukuzia magazeti kuweza kusoma nini kinachoendelea. Dada yangu pale Mheshimiwa Nuru A. Bafadhili, hata naye amesema kwamba, akipigwa picha mle katika magazeti anaonekana kwamba, anapewa sura ambayo siyo, badala ya *CUF* anapewa sura ya CCM. Nayo hiyo ilikuwa ni taadhari kwamba, kuna habari huku zinapelekwa ndivyo sivyo.

Lakini tunazungumza ndugu zetu Waandishi wa Habari kwa vile tunawategemeeni, tunawaombeni tupeni habari zilizokuwepo za kweli, msitupe habari ambazo sio za kweli. Wakati mkitupa habari za kweli sisi tunafarijika kwa sababu tunasoma na tunafuatilia. Mkitupa habari ambazo si za kweli na tukisoma tukifuatilia zikiwa sivyo ndivyo, mnatunyanya. Kuna wakati Fulani, Gazeti la Mwananchi walizungumza kwamba, Waziri Kiongozi wa Serikali ya Zanzibar, amekana ama hakubaliani na mazungumzo waliyokuwa wamefanya na Waziri Mkuu kuhusu suala la mafuta la Zanzibar. Bahati nzuri Waziri Kiongozi wakati anafungua Bunge la Bajeti la Baraza la Wawakilishi, akalizungumza suala hilo kinaganaga kwamba, Zanzibar haikani mazungumzo waliyokuwa wamefanya na Waziri Mkuu, yaani baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Muungano wa Tanzania.

Sasa sisi tunaposoma habari hizi, ninasema mnatunyanya kwa sababu wanatupa habari ambazo si za kweli. Kuna wakati mwingine unajikuta kana kwamba, unababaishwa na kwa sababu unaamini au unaviamini vyombo vya habari, unaona na yale unayoelezwa vile vile ni ya kweli. Tunawaombeni ndugu zetu Waandishi wa Habari, nafikiri taaluma ya habari mimi si mtaalamu, lakini ninavyosikia, wataalamu wanavyosema pale *inputs* yako hutii katika unayoandika, unaandika mambo kuonesha katika sehemu zote mbili. Usijitafutie ukapita katikati ukasema lako, sema mambo yalivyo na usiseme mambo kwa mujibu wa utashi, utatupoteza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuna suala lingine nataka kulizungumzia la vyombo vya habari vya Tanzania. Nadhani hili limezungumzwa na Msemaji aliyepita, lakini maadam nilikuwa nalo, nataka kulizungumza. Tumefika wakati unakuta *ITV* kwa mfano au hata *TvT*, wana *coverage* kubwa sana ya stesheni za Kichina ama za *BBC* au za *CNN*. Tunazungumza waandishi wa habari ni watu wenye nguvu, wenzetu Mataifa hasa ya Magharibi wanazungumza yao zaidi kuliko wanavyo yazungumzia yetu. Sasa hebu tuangalie kwa nini hatuingii katika nchi za Kiafrika. Kuna wakati fulani nikiangalia Televisheni ya Afrika ya Kusini, Mama Getrude I. Mongella pale, ambaye ye ye ni Mtanzania na ni Rais wa Bunge la Afrika alikuwa anahojiwa na alikuwa anaeleza mambo mbalimbali, viongozi mbalimbali wa Afrika hata Rais alipokuwa amekwenda Afrika ya Kusini hivi karibuni, hatukuona katika vyombo vya *CNN* wala hatukuona katika *BBC*.

Lakini vyombo vya Afrika ya Kusini walikuwa wanaoneshwa kwa nini ndugu zetu hawa, stesheni hizi za *ITV*, *TvT* na *Channel Ten* hawaelekei kuona kwamba, wanaelekea kujipeleka zaidi katika nchi za Kiafrika na tukawa tunapata taarifa zaidi za Kiafrika kuliko habari za Kimagharibi. Magharibi wanachokieleza wao ni zile *interests* zao, wanatueleza watu wanakwenda uchi. Hata juzi Mheshimiwa Rais alipokuwa Mwanza, amezungumzia suala la filamu ile iliyokuwa imeoneshwa kuona kwamba, tunakula mabichwa yale ya samaki na watu wanakwenda uchi. Hawa hawatutakii mema sasa, kwa nini sisi hatujielekezi zaidi katika vyombo vya wenzetu vya Kiafrika. Siku zote *CNN* na hivi vyombo vingine, hawaelezi mambo mazuri ya Afrika, wanachoeleza yote mabaya na kwa sababu ya *interests* zao. Nawaomba Wazee wetu, akina Mengi na wengine, hebu basi waelekee zaidi upande wa Afrika kuona kwamba tunaishaisha sisi wenywewe.

Mheshimiwa Spika, kuna suala lingine ambalo vile vile limezungumzwa hapa la vipindi vinavyo tayarishwa katika TV. Vipi wakati tunavyokaa katika televisheni na watoto wetu na jamii zetu, familia zetu zinatukimbiza. Huwezi kukaa na mwanao anakuja mtu anakata manyanga sisi tunasema manyanga kule, anakata manyanga pale umekaa na mtoto wako unakuta kwamba, hujui suruali iko chini au juu ili mradi kila kitu unashindwa kabisa. Sasa tunaomba jamani kama kulikuwa kuna wale ambaao wana sensa masuala haya, basi watusaidie kusensa kuona kwamba, hivi vipindi vingine haviendi moja kwa moja katika familia.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, naunga mkono hoja mia kwa mia. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. THOMAS A. MWANG'ONDA: Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi adimu ya kuweza kuchangia hoja ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo.

Awali ya yote, naomba kwanza kupeleka shukrani zangu maalum kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Chama chetu cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Shukrani nyingine maalum naomba nipeleke kwa Serikali Kuu mpya, iliyoteuliwa hivi karibuni ikiwemo na Wajumbe kina Mheshimiwa Rajab Yusuf Makamba, Katibu Mkuu, Mheshimiwa Aggrey D. J. Mwanri, Katibu Mwenezi, Kapteni Jaka Mwambi, Katibu Mkuu mpya upande wa Bara, Mheshimiwa Dr. Asha-Rose M. Migiro, Katibu wa Ushirikiano wa Kimataifa na Mambo ya Nje, Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe na vile vile kurudi kwa Mheshimiwa Feruzi.

Pongezi maalum pia nizitoa kwa Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, Mheshimiwa Muhammad Seif Khatib, kwa hotuba yake nzuri, imejaa umakini na inayoendana na dira ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Lakini nisiwe mwizi wa fadhila kwa kumuacha Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, Mheshimiwa Dr. Emmanuel J. Nchimbi, ambaye anafanya kazi kubwa sana katika kuhakikisha kwamba, kiwango cha utamaduni hapa nchini kinapanda zaidi.

Mfano mzuri ni mchango wake mkubwa, akishirikiana bila ya kumsahau Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Anthony M. Diallo alipohakikisha kwamba, kwa mara ya kwanza, Tanzania tunakuwa na mashindano ya Utalii ya Dunia, ambayo tutakuwa nayo kwa miaka mingine miwili, mwaka huu ulikuwa wa kwanza. Vile vile bila ya kumsahau Naibu Waziri mwengine, Mheshijiwa Joel N. Bendera. Kila unapokutana nao, kilio changu kimoja kwake unamwambia bwana wewe Angola wamecheza Kombe la Dunia wewe ulikuwa kocha wa Taifa sasa tumekupa lile rungu la Uwaziri, nina hakika 2010 haiko mbali na Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba niipongeze Wizara kiujumla, machache ambayo nataka kuchangia Wizara haikuniacha mbali. Wizara hasa katika Sekta ya Michezo kwa

kweli nitakachofanya ni kuongezea tu. Mengi waliyoyaweka yanaonekana yanaenda na yale ambayo nilikuwa na mawazo nayo kichwani na ambayo nina hakika, yanaweza kutuboresha na kutunyanya kimichezo.

Mheshimiwa Spika, si dharau, lakini naomba tu kwenda kwa zaidi na kwa ufupi zaidi na kuwapa nafasi kwa Wabunge wengine, nielekeze mchango wangu kwenye suala la soka au kandanda na michezo kwa ujumla. Habari na utamaduni, nadhani wengi wameligusa naomba niliache kwa muda. Suala langu la kwanza linalolinikera na limetajwa katika hotuba hii ni umuhimu wa kuwepo na vyuo vyta michezo, kwa lugha ya kigeni *Sports Academy*. Mafanikio ya wenzetu katika *Olympics* na kadhalika, si uchawi, si miujiza, wala si mazingaombwe.

Mheshimiwa Spika, mafanikio haya yanatokana na maandalizi ya dhati tangu enzi za udogo za wale wanariadha au wanamchizo wanaoshiriki. Wenzetu wana vyuo vyta michezo vyta watoto wadogo, tangu wakiwa na miaka mitano kwenda juu, sisi hatuna. *Sports Academy* ni njia mojawapo kubwa sana inayoweza kutuweka katika ukombozi mzito wa kuhakikisha tunapata maendeleo ya kweli.

Tumeona medali za ajabu sana wanapata Wachina, Waingereza, Wamarekani katika *Olympic*. Uingeleza pale wanakuwa wakifika robo finali na kadhalika, Italy juzi wamechukua Kombe la Dunia, narudia tena si uchawi, wenzetu wanavyuo vyta watoto wadogo. (*Makofit*)

Mfano mzuri pale *South Africa*, kuna ndugu yangu mmoja anasomesha mtoto wake pale *Pretoria Sports Academy*, watoto wanaosoma katika chuo cha michezo nadhani wengi wanafahamu, kuna timu kama *Barcelona* au *Juventus*, ambazo ni kubwa sana duniani. Watoto wale wanachukuliwa moja kwa moja katika umri mdogo wa miaka 14 au 15 wanaenda kuandikishwa katika shule za watoto wadogo za *Juventus* na *Barcelona*. Maana yake ni nini?

Maana yake watoto wale wanapata ajira kubwa. Kama mnafahamu wachezaji duniani wanalipwa hata dola 200,000 kwa wiki. *This is a dream* kwa mchezaji wa Kitanzania kupata mshahara mkubwa kama huu kwa wiki. Sasa wenzetu tutasema labda *South Africa* wao ni nchi iliyoendelea zaidi, lakini Tanzania inaweza na nina imani hiyo, ndiyo maana katika hotuba ya Waziri naona hili limewekwa.

Tuna uwezo mkubwa na mfano mzuri ni mchezaji mmoja anajulikana na watu wengi, huyu David Beckham. David Beckham Uingereza hakusoma sekondari, ameishia darasa la saba la Uingereza, angenisikia nadhani angenirarua lakini ndiyo ukweli wenye. Amepelekwa katika Chuo cha Michezo cha *Manchester United*, kocha wa pale Alex Ferguson akamchukua akamwendeleza taratibu, leo hii *Real Madrid* wanamlipa hela nyingi, anagombewa duniani. Yote ni matunda ya kuwa na vyuo vyta watoto wadogo vyta michezo. (*Makofit*)

Hatuwezi kuendeleza bila hili, lakini pamoja na yote haya, bado kuna mapungufu, mimi nina marafiki zangu nilikuwa nikicheza nao nilikuwa namba saba enzi zangu na

sibahatishi, naongea kwa *experience* kabisa. Lakini wengine timesoma soma tukaingia kwenye siasa, tukaonekana leo hii tumo Bungeni, wenzangu wanafanya kazi za kawaida. Lakini unajua kabisa, mtu huyu ukimpeleka kwenye ndondi anatandika makonde kweli kweli na ukimpeleka uwanjani anacheza mpira mzuri lakini maisha yao ni duni sana. Sasa huwa nakaa nafikiria, labda leo nitoe siri wakati nina ndoto za kisiasa, nikiwa kijana mdogo tu nilisema ipo siku nitapata nafasi ya kuchangia Wizara ya Michezo. Kwa kweli leo hii, nashukuru sana nimepata nafasi hii. Vijana wale wako hoi, lakini unajua kabisa kipaji wanacho cha kucheza mpira wa miguu. Ninachosema tumekuwa na michezo ya UMISETA na ile ya msingi na kadhalika, lakini wale wenye vipaji walioishia darasa la saba na wengine hawakufika la saba, tunawaacha nje.

Mheshimiwa Spika, mfano mzuri ni Marekani, Marekani kukigundulika kuna mtoto mdogo, ana uwezo mzuri katika mchezo wowote ule, anapata udhamini kwenye shule au Chuo Kikuu anasomeshwa. Kwa namna hiyo, anapata fursa ya kuweza kushiriki katika michezo kwenye nganzi za vyuo au mashulen na ndiyo maana Marekani leo hii unakuta timu yao ya mpira ya wanawake ni hatari, wanashindana na Wachina. Leo hii Marekani kwa *Basketball* hatuwapatii.

Mpira wa miguu walikuwa hawaujui lakini cha ajabu sasa hivi kila mwaka wanacheza Kombe la Dunia ni maandalizi *not only money*, ni *focus* ya Serikali kwamba lazima watukuze mchezo. Kwa hotuba hii ya leo naona hili lipo, lakini pia michezo tuingalie kama ni sehemu ya ajira, kwa hiyo, unapokuwa na watu wanaoratibiwa vizuri, wanafunzwa vizuri, ninao uhakika zile ajira milioni moja tulizoahidi, tutapata nafasi nzuri sana ya kuzifanyia maandalizi mazuri ya kuweza kutimiza ahadi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, najua muda unanikimbia lakini naomba niongelee kuhusu michezo, vilabu na makampuni. Watakaochukia humu ndani, wachukie lakini mimi ni mshabiki wa Simba. (*Makofii*)

Kama alivyo Mheshimiwa Prof. Phillemon M. Sarungi pale, lakini utaifa kwangu mbele, narudia tena utaifa kwangu mbele. Migogoro tunayoipata kwenye Simba na Yanga pale ndiyo kichocheo cha kuweza kukua kimchezo. Migogoro ipo kwa sababu watu wanaendekeza njaa zao kwenye vilabu. Naiomba Serikali tuletewe Miswaada iwe lazima vilabu viendeshwe kwa mtindo wa makampuni. Kwa njia hii tutaweza kudhibiti mapato na matumizi kwa kisayansi zaidi, tutaweza kuongeza ajira mle mle ndani ya makampuni. Juzi wametangaza hisa za Twiga, kila mtu amezikimbilia, wananchi wanapata hisa tutakuwa tunaingia kwenye MKUKUTA kwa kutumia michezo. Watanunua hisa kwenye hivi vilabu, mwininge atanunua kwa upenzi tu, bila hata kuangalia *business sense* lakini itatusaidia zaidi.

Ninaomba kazi inayofanywa pamoja na kuwa Simba, lakini nawapongeza Rais wa Yanga, Ndugu Francis Kifukwe na Ndugu Reginald Mengi, kwa juhudzi zao za kuwa na kampuni. Kwa hiyo, si vichaa ni namna pekee ya kuendesha michezo kisayansi. Mfano mzuri pale *Chelsea*, wana *Chelsea village* au *Manchester United*. *Manchester United* ndiyo klabu tajiri kuliko zote duniani, wanaendesha kwa kampuni. Huwezi kuendesha kimitaani taani mkaendelea. Tunapoongelea hivi vyuo vya michezo lazima uwekeze, njia bora ya kumwita mwekezaji lazima uwe na vitabu vyako vya ukaguzi au kuwe na

mkurugenzi, mhasibu na kadhalika. Siyo unaona wale watu wanakaa kugangaganga tu milangoni, haitoshi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nasema wananchi waliunge mkono hili, mabadiliko yana uzuri wake. Kuna wakati inabidi tufanye maamuzi magumu sana lakini kwa faida ya baadaye. Tanzania tunataka kucheza Kombe la Dunia 2010, lakini vilevile tunataka tung'ale kwenye *Olympics*. Kwa hiyo, naomba hilo la makampuni, mtuletee Muswada tulifanyie kazi na tutalipitisha.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Rais, akishirikiana na Mawaziri wote wa Wizara hii iliyotoa hoja leo, kwa kuweza kutupatia kocha ambaye yuko hapa Bungeni pomoja na nasi. Ilikuwa ni ahadi, tuliona ndoto lakini leo kocha wa Brazil yupo. Mimi nasema suala la wataalam wa kigeni ni la muhimu sana, tunao makocha wamesoma, akina Kibadeni, Mkwasa na kadhalika. Lakini haitoshi, *we need experience*, sasa wenzetu uzoefu wanao, Brazil hao wamechukua kombe mara nyingi ndiyo wanaongoza. Marekani inaongoza kila siku kwenye *Olympics*. Makocha wao wana uzoefu, ujuzi pekee wa darasani hautoshi. Kwa hiyo, hili suala la makocha wa kigeni, nimeliona kwenye hotuba lipo, mimi naliunga mkono mia kwa mia, naomba tuendelee kuwatumia hawa watu.

Lakini vile vile, ni muhimu sana tukawa na mashindano ama ligi za watoto wadogo, Mheshimiwa Dr. Omari M. Nibuka, ye ye ameanza hilo, mimi mwenyewe nimeanza hilo Mbeya. Naomba nimpongeze Mheshimiwa Joel N. Bendera, kwa kazi kubwa aliyoifanya, tumepata udhamini wa *Coca Cola*, wafanyabiashara wako tayari kutusaidia kwa shilingi nadhani milioni 400. Sasa tutakuwa na wadhamini, tutaweza kuwa na ligi ya watoto wadogo wa miaka 16 au 17, hili tunalihitaji. Vipaji vyetu tunavikuza tangu utotoni, hatuwezi tukaanzia huku juu kwa juu. Hawa walimu tunaowaleta, tutaweza kuona pesa zetu zinapotea kama maandalizi ya msingi ya utotoni hayajafanyika. Ni muhimu sana tukayaweka vizuri.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, ninataka niongelee kwa ufupi sana juu ya kandanda la ridhaa kwenda kwenye kandanda la kulipwa. Wachezaji wetu wanalipwa lakini kienyeji enyeji, ni kama vibarua tu.

Mheshimiwa Spika naomba kuunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza kabisa, nachukua nafasi hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Kikwete, kwa kutuundia Wizara hii ya Habari, Utamaduni na Michezo. (*Makofi*)

Wizara hii wakati ikiwa ni Wizara ya Utamaduni peke yake miaka ya 1970 na 1980, ndipo ambapo nchi yetu iliweza kuandikwa vizuri sana katika ulimwengu huu wa michezo na utamaduni. Ndiyo kipindi ambacho akina Filbert Bayi, Ikangaa na Shehangaa, wakapatikana. Ni kipindi hicho hicho ambacho Timu yetu ya Taifa, ilitinga fainali za mashindano ya Afrika kule *Lagos Nigeria*, ni kipindi ambacho Yanga na Simba ndizo

ziliwa Yanga na Simba kweli siyo za sasa. Kwa hiyo, kwa kipindi hiki ambacho Rais ameama kuifufua Wizara hii na kwa kutupatia hawa Mawaziri watatu, ambao wote ni fani yao, nina hakika tutavuka kuliko pale tulipovuka wakati ule. Sasa mchango wangu uende moja kwa moja kwenye sehemu nne.

Kwanza, lugha yetu ya Kiswahili. Kiswahili hakiwezi kukamilika kwa ukamilifu wake, kama hatutamtaja mtu ambaye alihimiza Kiswahili kuwa lugha ya Taifa na lugha ya Afrika Mashariki na hatimaye Afrika nzima, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Mtu ambaye ameweza kuunganisha nchi yetu, makabila zaidi ya 100 kuwa kitu kimoja, kuzunguza lugha moja, haijawahi kutokea duniani. Kwa hiyo, kwa kweli Mwalimu Nyerere ndiyo anayestahili kabisa kukibeba Kiswahili katika dunia hii. (Makofi)

Sasa Kiswahili hiki kiko chini ya Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA). Kwa bahati nzuri sasa Viongozi wa Afrika wameanza kukiona Kiswahili kama kweli ni lugha ya Taifa. Rais Chissano mwaka 2005, Rais wetu mwaka huu wa 2006 na jana nimesikia pia Rais Mseveni wa Uganda, akisema Kiswahili kiwe ni lugha ya Uganda na Afrika na Marais kadhaa na sasa nimesikia tumetaka kujenga Taasisi ya Kiswahili kule Ethiopia kwenye Makao Makuu ya nchi za Afrika, lakini BAKITA sijui kama Waheshimiwa Wabunge wanafahamu, Makao Makuu ya Baraza hili? Waende wakaone Makao Makuu ya Baraza hili, wajue liko mtaa gani, ofisi ya namna gani, lakini mimi ninapopajua pana buibui, mende na kila aina ya uchafu. Kitu ambacho kwa kweli sisi wenyewe hatuoni kwamba, BAKITA wanastahili kupewa heshima kubwa ya Kitaifa. Mtu akitoka Uingereza, Marekani, akisema sasa hiki Kiswahili ni lugha ya Afrika, ngoja nikaone Makao Makuu yao yalipo, tutapata aibu sana na tutadunishwa sana. (Makofi)

Kwa hiyo, naomba Waziri na Naibu Waziri, mlitupie macho sana Makao Makuu ya BAKITA yawe *attractive* ili watu wapende kukizungumza Kiswahili kwa sababu hata mahali penye ni pa zuri. Makao Makuu ya Chama cha Mapinduzi Dodoma pazuri, si unaona nyumba zinapendeza Chimwaga, sijui ya CUF; nadhani nayo ni mazuri pia. Lakini BAKITA Makao Makuu yanahuzunisha sana. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Spika, la pili ni matumizi yenye ya Kiswahili, kwa vile mahali ambapo BAKITA ipo, hali ni duni, kwa vyovyote vile inaathari watendaji. Lazima na mawazo fulani fulani yatakuwa duni pia, kwa sababu mazingira ya kazi si mazuri. Lugha yetu ya Kiswahili sasa hivi inapanuka lakini kuna jambo ambalo linaniudhi, matumizi ya lugha yenye. Kwa mfano, neno msanii, neno hili mimi nafahamu msanii ni yule ambaye anaumba vyungu vizuri, anaweka nakshi, huyo ndiyo msanii, anaimba vizuri, anatunga nyimbo anaweka kwenye maandishi, anacheza ngoma vizuri, anadumisha utamaduni wa Kiafrika huyo ni msanii, anazungumza lugha ya Kiswahili vizuri kwa ufasaha. (Makofi)

Lakini leo msanii ni tofauti akikamatwa mvuta bangi, akasukumwa huko nje akafika mahali akaanza kujieleza tu kwamba, wewe umevuta bangi? Anasema hapana mimi nilikuwa nimeshika sigara tu, utasikia msanii huyo. Akikamatwa mwizi ameshika pochi kaiba kule *Airport*, fukuza fukuza, ulizwa pochi ya nani? Mimi nimeokota na nini,

nilikuwa nampelekea mwenyewe, msaanii huyo bwana. Sasa unaona neno usanii, tayari limeleta maana nyine kabisa kwamba ni watu matapeli, wahuni, inadhalilisha fani za watu hata sisi tunaosema wasanii ambao tumesoma. Kwa hiyo, naomba Wizara yetu iwe makini sana katika neno hili maana yake kuitia BAKITA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), hili kazi yake ni kuongoza, kuhifadhi na kuwasaidia wasanii kulinda haki zao. Kuna Mabaraza mengi lakini Uongozi wa BASATA, tangu nilipoajiriwa Jeshini huko zamani, naona viongozi ni wale wale, watendaji ni wale wale na wengi waliteuliwa kutokana na kikundi kile cha Taifa cha kucheza ngoma. Hawa leo ndiyo Maofisa wa BASATA, ili wafundishe wasanii, usanii mzuri, wakisasa na wakiteknolojia mpya, wengine hata shule hawakwenda, wengine tuliwapeleka China kujifunza sarakasi. Leo ndiyo wako pale Maofisa ya BASATA, wanatoa semina kila wakati, lakini wao wenyewe hawafanyiwi semina, mawazo mapya wanayatoa wapi? Kwa hiyo, naomba tulichunguze Baraza hili, liendane na kipindi hiki cha sayansi na teknolojia.

Jambo lingine ni suala la Chama cha Kutetea Hakimiliki za wasanii *COSOTA*, ni muhimu sana kwa wasanii. Mahali ilipoweka maana wasanii wako chini ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, lakini *COSOTA* ipo Wizara ya Biashara na Masoko. Sasa mtoto anazaliwa na Komba, unavyomwambia mimi nimekuzaa tu atakulea Yusuf Seleman. Hivi kweli atatoa malezi gani ambayo ni mazuri; ana mapenzi gani? Kwa hiyo, naomba *COSOTA* irudi kwenye Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, kwa mzazi wake. Hapo ndipo tunaweza kuwatetea vizuri zaidi wasanii wetu na haki zao.

Mheshimiwa Spika, mwisho michezo, zamani michezo ilikuwa inafanyika tangu vijijini, Wilayani, Mikoani anapatikana mshindi, ngoma nyimbo ndiko sisi wengine tulibuliwa huko. Majeshi yalikuwa yanafanya mashindano, tangu chini huko kwenye ngazi ya kikosi mpaka ngazi ya Taifa, unapata wanamichezo wazuri, wasanii wazuri, siku hizi hakuna. Kwa hiyo naomba Wizara ishirikiane na majeshi yetu, Wizara nyininge, Mikoa na Wilaya ili tupate wanamichezo na wasanii wazuri, maana baada ya si muda mrefu, wanamuziki wa nchi hii hawatakuwepo, watakuwepo hawa hawa wasanii mnaowasema, kwa sababu mziki ni kwenda shule kuandika, ni *identity*. Lakini leo mtu akienda *studio*, akipata *beats* akitoa nyimbo yake, kuku wanatembea, nyani anasaga kiuno, basi msanii. (*Kicheko*)

Sasa wanaoandika muziki hawapo, wanaopiga magitaa hawapo. Kwa hiyo, naomba Wizara irudi ianzishe vyuo, ianzishe mashindano ili tupate wanamuziki ambao watarithi na kuendeleza utamaduni wetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofî*)

MHE. AMINA C. MPAKANJIA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika hoja hii ya Bajeti ya Wizara ya Habari Utamaduni na Michezo. Kwanza kabisa, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia uzima, afya na kutuwezesha kukutana hapa Bungeni na kujadili masuala mbalimbali, yanayohusiana na nchi yetu na Watanzania wote kwa ujumla. Baada ya

hapo naomba niwapongeze wahuksika wa Wizara hii ya Habari, Utamaduni na Michezo, nikianza na Waziri, Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, nawapongeza Naibu Mawaziri wake; Mheshimiwa Joel N. Bendera na Mheshimiwa Dr. Emmanuel J. Nchimbi. (*Makofî*)

Hapo hapo pia napenda kuchukua nafasi hii, kumpongeza Katibu Mkuu wa Wizara hii ya Habari na haswa ikiwa inaongozwa na mwanamke, Bibi Kijakazi Rajab Mtengwa. Nakupa hongera sana, kwa kazi nzuri unayoifanya na unatuwakilisha vyema wanawake na inaonesha ni jinsi gani kweli wanawake wakipewa majukumu, wanaweza kuyatimiza.

Nawapongeza pia Watendji wengine wote wa Wizara hii, lakini pia nachukua nafasi hii kuwapongeza waandishi wa habari, vyombo mbalimbali vyakaribishwa na radio, televisheni, magazeti na vitu vingine vyote, ambavyo vinahusika katika kutupatia habari, ukizingatia hii ni siku yao rasmi. Lakini pia nachukua nafasi hii kuwapongeza wanamichezo mbalimbali nchini kote Tanzania, katika fani zote, fani ya urembo, muziki na sanaa nyingine mbalimbali. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, naomba nianze na upande wa habari. Naanza kwa kuwapongeza waandishi wetu wa habari, kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuhabarisha wananchi na hasa Watanzania. Lakini katika upande huu wa habari, naomba itungwe sheria ambayo itakuwa inawalinda waandishi wa habari wanapokuwa kazini ili waweze kufanya kazi zao vizuri na waepukane na matatizo mbalimbali, ambayo yamekuwa yakiwapata wandishi wa habari. Hapa nataka kuzungumzia tukio lililotokea siku za nyuma, waandishi wa habari baadhi yao walipigwa na wafuasi wa chama kimoja cha siasa, wakati walipokuwa wakifanya kazi zao. Lakini pia waandishi hawa wa habari, walishawahi kupigwa na askari magereza na matukio mengine mengi tu, ambayo yamekuwa yaktokoa yakiwadhalilisha waandishi wa habari.

Mheshimiwa Spika, naomba itungwe sheria nzuri kabisa, ambayo itakuwa inawalinda waandishi wa habari watakopokuwa kazini na kama itatokea tukio lolote baya dhidi yao la kumdhuru mwandishi wa habari anapokuwa kazini, basi sheria iweze kuchukua mkondo wake na huyo muhusika aweze kuchukuliwa hatua za kisheria. Najua sasa hivi wapo waandishi wa habari wengine ambao tayari wamekwishaenda mahakamani kutokana na matukio haya yalijyotokea. Lakini kama itakuwa hakuna sheria iliyo rasmi, ambayo inamlinda mwandishi, anaweza akazungushwa mpaka mwisho wa siku kisipatikane chochote.

Mheshimiwa Spika, waandishi wa habari ni watu mhimu sana, tunawahitaji katika matukio karibu yote ambayo yanakuwa yakifanyika nchini kwetu, katika kila shughuli tunawahitaji waandishi wa habari ili waweze kuripoti na kuweza kuyawasilisha yale matukio, kwa sababu si rahisi kwa Watanzania wote kuwepo katika tukio hilo. Kwa wale ambao wako vijiini au mijini, wanahitaji kupata hizo taarifa. Kwa hiyo, basi naomba waandishi wa habari, wachukuliwe kama watu muhimu na yanapotokea matukio labda kama ya moto, waandishi wanahitaji kwenda sehemu kama hizo, viwepo vifaa maalum

kabisa nya kuwapa, kujikinga ili wasiweze kudhurika na moto, wafike mpaka katika maeneo hayo na kuweza kuripoti habari zao vizuri. (*Makofî*)

Baada ya kuwatetea waandishi kwa upande huo, pia napenda kurudi kwa wenzangu waandishi wa habari na kuwaambia kwamba, watumie kalamu zao vizuri. Waandishi wanaaminiwa kwamba ni watu ambao watakuwa wanatoa taarifa nzuri na kuwaelimisha wananchi hata kama ni mbaya lakini ni ya kweli wanaruhusiwa kuitoa. Lakini baadhi ya waandishi, wamekuwa wakitumia kalamu zao kwa ajili ya visasi, kama wanakisasi na mtu basi ni kumwandika. Wamekuwa wakiripoti habari nyingine ambazo hazina ukweli kwa maslahi yao binafsi. Kwa hiyo, naomba waandishi wenzangu wa habari, muweke utaifa wa Tanzania mbele, mripoti matukio ambayo ni kweli yametokea na kweli Watanzania wanatakiwa kuyajua na tusiende kunyume, tukazitumia kalamu zetu vibaya. Natumaini hapo nitakuwa nimeeleweka na waandishi mtakuwa mmenielewa.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo sasa naomba niingie upande wa utamaduni na michezo. Nachukua nafasi hii kumpongeza kwa dhati kabisa, Rais wa Awamu ya Nne, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, sambamba na mkewe mama Salma Kikwete, kwa jinsi ambavyo wameonekana kuipa kipaumbele sekta hii ya michezo na wamekuwa wakijitoa kabisa. Mheshimiwa Rais wetu, wakati alipokuwa akizindua Bunge katika ule Ukumbi wa Zamani, mtakumbuka alionesa nia yake ya dhati kabisa ya Serikali kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya, jinsi ambavyo itaendeleza michezo kutoka Serikali ya Awamu ya Tatu. Mheshimiwa Rais, amekuwa akishiriki katika michezo mbalimbali na nadhani mtakumbuka na mlimwona hata wakati wa ile mechii ambayo ilifanyika Uwanja wa Taifa, alikwenda kuiangalia timu yetu japokuwa tulifungwa. Kwa hiyo, naomba nimpongeze Rais kwa kuweza kujitoa na pia alionesa nia yake ya dhati wakati wa mashindano ya *Miss Tourism*, nilimwona katika televisheni na vyombo vingine nya habari, jinsi ambavyo alikuwa akiwasaidia wale waandaaji wa mashindano hayo.

Mama Salma Kikwete naye amekuwa bega kwa bega katika upande huu wa michezo. Kama mtakumbuka, alimpokea Mrembo wetu wa Tanzania, ambaye alifanya vizuri, Nancy Sumari katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Nyerere pale Dar es Salaam na baada ya hapo, aliweza kumwalika mrembo yule Ikulu kwa kumpongeza na mimi nilikuwa mmoja wa kati ya watu ambao tulikuwepo pale. Kwa hiyo, naomba nampongeza sana. Lakini Mama Salma Kikwete pia alikuwa Mgeni Rasmi katika shindano la kumtafuta mrembo wa utalii kwa dunia nzima, ambapo warembo wengi tu kutoka nchi mbalimbali, walikuja hapa nchini kwetu Tanzania. Kwa dhati kabisa, nampongeza Mheshimiwa Rais, pamoja na mkewe, kwa jitihada zao ambazo wameonesha na kwa kwenda hivi. Naamini kabisa, Serikali ya Awamu ya Nne, itafanya vizuri sana katika upande wa michezo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini katika upande huu wa michezo kwanza, naomba nianze kuwapongeza Kamati ya *Miss Tanzania*, ambayo inaandaa mashindano ya *Miss Tanzania* kwa kipindi cha miaka 12 mfululizo toka mwaka 1994 mpaka leo 2006. Mimi nawapongeza kwa sababu naamini kabisa, mashindano haya ya urembo ni moja kati ya sehemu kubwa kabisa ambazo zitatoa ajira kwa vijana na kwa wingi sana. Kama mtakumbuka mwaka 2005, Mrembo Nancy Sumari, aliweza kushinda na akawenza kupata

zawadi ya gari na nyumba. Hii si kama ajira, tena ajira ya nguvu kabisa ni kitu gani; Watanzania mnataka mkipate? Ni ajira kubwa kabisa kwa mtoto mdogo kama Nancy, mwenye umri wa miaka 20, leo anamiliki gari na nyumba. Wakati wapo wafanyakazi wanaofanya kazi kwa muda wa miaka 20 hadi 40, wanastaafu hawana nyumba wala hawana uwezo wa kumiliki magari. Kwa hiyo, nawapongeza Kamati ya *Miss Tanzania*, kwa kitu kizuri ambacho wanakifanya na mimi binafsi naona ni ajira tena ajira kubwa kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, hapa ninachokiomba na kuwasihhi Watanzania, wawaruhusu vijana hasa warembo, washiriki katika mashindano haya ili waweze kujiajiri. Kwa mfano, mwaka huu katika Shindano hili la Urembo, mbali ya mrembo kupatiwa gari na fedha taslimu shilingi milioni saba, lakini pia warembo kumi kuanzia nafasi ya pili mpaka ya kumi, watapata ajira za kudumu (ajira za moja kwa moja), kutoka Kampuni ya *Vodacom*. Hiki ni kitu kizuri sana, sisi kama Watanzania, tunatakiwa tujivunie.

Mheshimiwa Spika, lakini ombi langu kwa wandaaji wa mashindano haya, naomba watumie vigezo vizuri kuwapata wasichana, lakini katika upande wa mavazi ambayo yamekuwa yakilalamikiwa, wawe makini, wawe na mavazi ambayo yatakuwa yanaudumisha utamaduni wetu wa Tanzania ili tuweze kwenda vizuri na taratibu zetu za maadili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu wasichana wamekuwa wakilalamikiwa kwamba, urembo ni uhuni, basi naomba wanapopata heshima kubwa kama hii, wajitunze na wawaoneshe Watanzania kwamba, urembo si uhuni, walinde heshima zao na isiwe tofauti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika hili, Serikali imekuwa ikitoa Bendera kwa mwakilishi ambaye anaenda kuiwakilisha Tanzania nje ya nchi, kwenye upande wa urembo, mpira wa miguu, michezo mingine na sanaa tofauti tofauti. Lakini, mimi binafsi naona kuwapa tu Bendera haitoshi, kwa sababu msanii anapokwenda nje, anaibeba Bendera ya Tanzania, amebeba Utaifa wa Tanzania, haendi kule kama Nancy, haendi kama Hoyce, anaenda kama Mtanzania kuwakilisha katika Mataifa mbali mbali.

Serikali sasa iangalie, itengeneze utaratibu wa kuwalipia gharama za usafiri hawa wanamichezo ambao wanakwenda kuiwakilisha nje ya nchi. Kama ni posho za kujikimu wanapokuwa kule nje ya nchi, pamoja na vitu vingine vingi tu, ambavyo vitakuwa na vinahusiana na safari yao ili kweli tuseme tumetoa Mtanzania tumempa Bendera, lakini pia tumempa na pesa za kujikimu, si Bendera tu wakati hana hela ya usafiri, hana hela ya kujikimu na vitu kama hivyo. Kwa hiyo, naomba Serikali iangalie kwa makini na nitaomba Mheshimiwa Waziri, anipe majibu wakati atakapokuwa anajibu hoja hizi za Wabunge, kuelezea kama hilo atakuwa amelielewa na nitahitaji majibu ya dhati.

Mheshimiwa Spika, muziki nchini Marekani ni sekta ya tatu ambayo inakubalika na imeipeleka Marekani mpaka kuwa juu kiuchumi. Nchini Tanzania, tunakadiririwa kuwa Watanzania milioni 35. Nimejaribu kupiga hesabu ndogo tu, kama asilimia kumi ya Watanzania watanunua kanda za muziki tano kwa mwaka, ina maana zitapatikana

shilingi bilioni 17 kwa mwaka kutoka kwa wanamuziki watano, yaani kama asilimia kumi ya Watanzania, wataamua kununua kanda tano za muziki basi zitapatikana shilingi bilioni 17.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali imeshafikiria jinsi ya kupata kodi kuitia katika sekta hii ya muziki? Kama Serikali itaamua kukusanya kodi kuitia muziki, naamini wanamuziki sasa watafaidika, kazi zao hazitaibiwa tena kwa sababu kutakuwa kuna usimamizi kutoka Serikalini. Baada ya kupata zile kodi kutoka kwa wanamuziki, basi watakuwa wanaziangalia kwa umakini kabisa kazi zao, tofauti na hivi sasa, ambapo wanamuziki wanalamika, wanafanya kazi katika mazingira magumu, lakini wanakuwa wanaabiwa kazi zao.

Kwa hiyo, naiomba basi Serikali ya Awamu ya Nne, iangalie ni jinsi gani inaweza ikaanza kutoza kodi kwa muziki ili waweze kuwasaidia wasanii wetu.

Mheshimiwa Spika, lakini hapa pia, ningeomba vyombo vya muziki viletwe bure bila ushuru, yaani bila kulipiwa kodi. Kama mtajua muziki ni kitu ambacho kimekuwa kikisaidia sana katika jamii yetu, umekuwa unatumika katika kampeni, umewawezesha Wabunge mbali mbali na Mheshimiwa Spika hapo mbele kufika humu ndani. Muziki unatumika kwenye harusi, muziki unatumika kwenye msiba, muziki unatumika kila mahali kutangaza sera za Taifa letu pamoja na mambo mengine.

Mheshimiwa Spika, wasanii hawa ambao wameamua kujiajiri wenyewe, wanapata tabu sana. Kwanza ni vijana tu ambao hawana uwezo, leo anataka kuimba anahitaji gitaa, anahitaji kinanda, anahitaji ngoma, anahitaji vyombo vingi ili aweze kuendeleza muziki wake. Kwa hiyo, kama kweli Wizara hii itaamua kuwasaidia wasanii wetu, basi mimi ningeomba vyombo hivi viingie bila ushuru, ili vijana wengi waweze kujiajiri na tumsaidie Mheshimiwa Rais katika fani hii ya muziki, kuweza kupata ajira nyingi na kutimiza lile lengo lake ambalo aliahidi ajira zaidi ya milioni moja zitapatikana. Naomba hilo lizingatiwe.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu sina uhakika na muda ambao umebaki, nadhani umebaki muda mfupi sana, basi naomba kuchukua nafasi hii kusema, naunga mkono hoja mia kwa mia na mengine yaliyobaki nitayachangia kwa maandishi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. HAROUB SAID MASOUD: Mheshimiwa Spika, kwanza, nakushukuru wewe binafsi, kwa kunipatia nafasi na mimi nichangie maoni yangu binafsi, baada ya kuchangia kwa niaba ya Kamati yangu.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, mimi naipongeza hotuba hii mia kwa mia na ninaiunga mkono kabisa kwa sababu nachelea nisije nikapungukiwa na wakati, nikaja nikasahau kutamka hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naanza kwa kutamka haya yafuatayo: Jana nilikuwa nikifuatilia vipindi vya TvT na RTD. Kama kuchangia, basi RTD na TvT jana walichangia hotuba hii mia kwa mia. Katika RTD walikuwa wakiwahoji baadhi ya wasanii, zikipigwa nyimbo za zamani na ile ni ushahidi tosha kwamba, RTD wanasisitiza kwamba, tusizitupe nyimbo zetu za kale. Lakini kasheshe ikawa kwenye TvT, ambayo iliniweka niwe macho mpaka saa sita za usiku. TvT, ukweli nyimbo walizozionesha pale na wanazozitoa katika luninga ni nyimbo za zamni sana ikiwemo nyimbo ya Bi. Kidude. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hapa kati Bi. Kidude alikuwa akisemwa sana kwamba waambiwe wanawe kama anao, aache kuimba, nasema hao ni wachoyo. Bi. Kidude nyimbo ambayo imeonekana kwenye TvT jana, ameiimba Dubai. Hao wanaomchukia, wenyе uchu wa kumwona hayuko kwenye luninga, jana waliona haya. Nafikiria mimi, nyimbo ile aliimba Dubai, alishangiliwa sana, alitunzwa sana na ukweli aliwaweka hoi watu wote pale. Sasa na nyimbo aliyoimba Bi. Kidude jana ilikuwa “*Yalaiti*” Walibusu sana Waarabu wote pale na walimshangilia sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa ninasema wasanii kama wale watunzwe. Katika hotuba ya Waziri Mkuu, nilimwambia Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, kwa nini hatuanzishi aidha maktaba maalum au *museum* ya kuzihifadhi nyimbo za zamani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakutajia nyimbo moja tu ambayo nataka Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib atakapokuja kutoa majumuisho, yeye mwenyewe, nina hakika hanayo na umati huu wa Bunge na wengineo wa nje, wanaitamani nyimbo hiyo. Nyimbo hiyo inaitwa “Paka Shume.” (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, maneno yaliyomo katika beti moja tu ya wimbo huo inasema hivi:-

“Paka mtaka vya watu,
Itakufika ajali
Watamba kama Chatu
Nyumbani kwa Bwana Ali
Kwako hutapata kitu
Kwani mwenyewe mkali.”

Mheshimiwa Spika, utashangaa nyimbo hii ameitunga nani? Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo wakati huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa nina nyimbo kadha wa kadha, lakini nasema nyimbo moja hii tu. Waziri wa Habari yule pale mbele yangu, Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib. Sasa kama nyimbo ile moja na nyinginezo nitakazozitaja hapa chache, kama ingekuwa zimekekwa, nina hakika Wabunge hawa wangelitoka hapa, wangelikwenda kuzinunua kanda zote za Paka Shume, ina maneno mazuri.

Mheshimiwa Spika, hatukatai nyimbo za kizazi kipyä, ni nzuri, lakini tusitupe tunakotoka. Yaani tukitupa hayo, ina maana hata wewe mzee wako utamtupa. Tuseme kuna wimbo wa Bi. Kidude vile vile, Jimboni kwa Mheshimiwa Muhammed Seif Khatibu anasema, "Mhogo wa Jang'ombe, Usiulambe mwiko." Nyimbo nzuri kama hiyo. Lakini vile vile kuna nyimbo ya Marehemu Seif Salum, "Mpenzi nipepee, nina usingizi nataka kulala." (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, lakini nataja nyimbo nyingine ya mwisho, ambayo aliimba Bakari Abeid, ni mtunzi na mwimbaji bora katika Bara la Afrika nyimbo za Kiswahili. Amesema, katika nyimbo yake, beti moja tu:-

"Nyama zetu za ulimi
Ambazo tukipeana
Na mengineyo sisemi
Mengi tukifanyiana
Ni mageni kwangu mimi
Sijapata kuyaona." (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, chonde chonde, namwomba Mheshimiwa Waziri kwa niaba ya Watanzania, ambao wanataka kuzielewa nyimbo za zamani. Wanataka kuzielewa nyimbo za Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, chungu nzima alizozimba. Tunaomba zitafutwe nyimbo hizo, zihifadhiwe na kanda zake ziuzwe.

Mheshimiwa Spika, nasema baada ya maelezo hayo, sasa ninakwenda moja kwa moja katika suala la hati miliki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sheria ya hati miliki kama nilivyoeleza katika hotuba kwa niaba ya Kamati, ipo lakini haina maslahi kwa waimbaji.

Mheshimiwa Spika, nina picha hapa inaonesha watu watatu na nitampatia baadaye Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib. Inaonesha mtunzi wa nyimbo jinsi alivyokonda, alivyodhoofika umbo lake, maskini kama mimi au Mheshimiwa Said J. Nkumba. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, lakini picha ya pili, amebeba kibegi chake, ni *promoter* huyo, kidogo ametonomonoka, umbo lake kama Mheshimiwa Capt. John D. Komba. Lakini wa tatu, ambaye amevimba viti viwili au vitatu havimtoshi, kama Mheshimiwa Mgana I. Msindai, huyo ni msambazaji wa muziki. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwa nini ikawa hivyo? Akishaimba mtu nyimbo yake, eti anakwenda kwa *promoter*, anaambiwa nitakutolea mimi, zinatolewa kiasi kanda 1,000 anauziwa, yameshamkuta Mheshimiwa Capt. John D. Komba, amepata shilingi milioni mbili. Kanda zile zile, *promoter* au yejote mwengine, lakini zaidi ni *promoter*, anaanza kuzitoa upya yeye, *it means* kwamba, anapata *a lot of money* kuliko hata yule aliyetunga nyimbo na kuimba. Lakini wa tatu, ambaye anavimba mpaka tumbo linataka kupasuka

njiani, ni yule ambaye anazi-*dub*, anazirekodi upya nyimbo zote zile, anaziuza, Serikali hailewei, mwenye nyimbo hatambui, walishakufa wenyewe, nyimbo zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, lakini sababu kuu ni ipi? Napenda nimsaidie Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, ashirikiane na Wizara zinazohusika. Serikali ya Tanzania, tumekuwa wapole, hatusikii wala hatuoni. Kisa ni kimoja, unaporuhusu kanda tupu (*empty cassettes*) za *Video* na *Audio* kutoka nje kuletwa hapa, ina maana kuwaambia wasanii wetu waibiwe nyimbo zao, ziwe *recorded* mle. Sababu zipi zinaletwa kanda tupu hapa? Kanda waache wasanii wenyewe, waende kwa *promoter* wao, warekodi na *promoter* iwe *very strictly*, akatazwe kutoa hata kanda moja.

Mheshimiwa Spika, kuna kesi mbili au tatu zimejitokeza Tanzania; limekamatwa gari zima lina kanda kwa mamilioni. Kutokana na sheria yetu kuwa bado ni butu, kesi imekwenda mahakamani, aliyechukua kanda zile kwa sababu amezirekodi yeye bila ridhaa ya mwenye mwanamuziki, amekuwa *convicted*. Cha kushangaza, hatusemi kwamba mahakama imekosea, kwa sababu ni sheria iliyokuwepo. Ametozwa shilingi laki mbili, kanda zote amerejeshewa mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, tuwaonee huruma hawa. Ninamwomba Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib katika kazi ya mwanzo ya Awamu hii, atakayoifanya yeye, ahakikishe na Wizara yake inawasimamia wasanii wetu.

Mheshimiwa Spika, wasanii hasa waimbaji wa Misri wote wana *degree* na katika matajiri ambao wanaongoza katika nchi ile ni waimbaji. Marehemu Umm Kurouthm, alihojiwa na *BBC* wakati wa uhai wake, “Mbona kila tukija katika hafla zako, tunakuona ushakuwa kizee, huachi kuimba, lini utaacha kuimba?” Aliuambia umati wa Ulimwengu “Nitaacha kuimba ile siku ambayo nitaona kiti kimoja tu katika hafla yoyote ambayo naiandaa mimi mwenyewe, nitayokuta kiti kimoja kitupu. Mpaka amefariki, hapana hata siku moja Umm Kurouthm ameimba kuna kiti kitupu kilitokezea. Kwa nini ikawa hivyo? Nyimbo zake nzuri, lakini na mwenyewe alikuwa na mapato makubwa, aliweza kuwashawishi watu wakaja katika hafla zile.

Mheshimiwa Spika, Mungu ametujalia, Tanzania ni mionganii mwa nchi nyingi sana ambazo zina waimbaji wazuri, wamezagaa wanakwenda. Nimekwenda Arabuni mimi mwaka 2004, nilizikuta bendi zetu zinapiga kule. Lakini tuijilize, wanapata nini? Matokeo yake Issa Matona, kagongwa na gari pale Dar es Salaam, amefariki. Sasa, angalau tunashukuru jana TvT, angalau wamemwonesha Issa Matona. Nilihisi kama yuko hai, amerejea duniani kuja kutuambia.

Mheshimiwa Spika, haya ni mambo ambayo lazima tuyaangalie.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, ni suala la UKIMWI. Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, ina mchango wake mkubwa sana katika suala la UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, aliuliza swali hapa kuhusu wanenguaji wetu wanaovaa nguo mbaya. Mheshimiwa Waziri, alijibu. Lakini

bado tuijilize, kweli ni silika yetu, kweli ni tabia yetu, kweli tuyaruhusu hayo, anakuja mtu ananengua, unaviona vya ndani vimetokeza juu, halali hiyo? (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, mimi nasema sikatai, wewe Mheshimiwa Waziri, Manaibu wako na sisi Wabunge tunapotaka yale, tutafute mahali pa stara tuyaone. Tunakwenda mahali kama Dodoma Hoteli, tunakaa na Waziri Mkuu wetu pale, wanenguaji wanakuja pale wanavaa nguo, ukweli mimi siku moja nilimkimbia Mheshimiwa Dr. Mary M. Nagu pale. Namwonea haya. Mheshimiwa Dr. Mary M. Nagu kaa, niko nyuma yake, ilinibidi niondoke mimi, namwonea haya, naona mambo ambayo tangu nilipozaliwa sijafundishwa yale wala sijayaona hata siku moja. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nasema kwa uchungu kabisa. Tujaribu kurekebisha vyombo vyetu vya habari hasa luninga zetu, baadhi ya mambo tusioneshwe jamani. Tunakaa na watu tunawastahi. Kama mimi nikikaa na Mheshimiwa Anna M. Komu, sistahili kuyaona yale. Mheshimiwa Fatma Mussa Maghimbi nikikaa naye, sistahili kuyaona yale. Wapo watu wanaostahili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya haya, naunga mkono hotuba hii mia kwa mia. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

MHE. IDD M. AZZAN: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Natumia nafasi hii pamoja na kwamba nilishawashukuru wananchi wangu wa Kinondoni, lakini naendelea kuwashukuru tena. Ninawashukuru kwa mara ya kwanza kabisa, wanamichezo wote wa Wilaya ya Kinondoni na Mkoa wa Dar es Salaam, kwa jitihada zao walizofanya na kuhakikisha ninakuwa Mbunge wa Jimbo la Kinondoni.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii tena, kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuanzisha au kuunda Wizara hii muhimu sana ya Habari, Utamaduni na Michezo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitatoa shukrani ama kumpongeza Rais wetu wa Awamu ya Tatu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa na uongozi wote wa Awamu ya Tatu, kwa kitendo cha kuamua kujenga Uwanja Mkubwa na wa Kisasa Tanzania na ninafikiri katika Afrika, pale Dar es Salaam. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii pia, kumpongeza tena Rais wetu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa uamuzi wake wa kutuletea Makocha kwa ajili ya kuifundisha Timu yetu ya Taifa ya Mpira wa Miguu, tena wametoka katika nchi ambayo imeendelea sana katika mchezo wa mpira wa miguu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hii inaonesha ni jinsi gani Serikali ya Awamu ya Nne, inavyopenda maendeleo ya michezo. Nina hakika ile azma ya Rais wetu kwamba, ifikapo mwaka 2008, basi angalau tucheze Fainali za Mataifa ya Afrika ambazo zitafanyika Ghana. Kitendo cha kumleta Kocha huyu, nina hakika kabisa, kitasaidia na kitaiwezesha Tanzania kucheza Fainali hizo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na azma hiyo nzuri ya Serikali yetu, pamoja na azma nzuri ya Rais wetu, lakini mchezo wa mpira umekumbwa na migogoro mingi sana na kama Wizara hii haitakuwa makini, nina hakika azma ya Rais, haiwezi kufikiwa. Migogoro katika vyama vya michezo, migogoro katika vilabu imekuwa ni mikubwa sana.

Mheshimiwa Spika, chanzo kikubwa cha migogoro hiyo, watendaji wa Wizara yetu wanahusika sana. Nampongeza sana Waziri wa Wizara hiyo aliyepita, Mheshimiwa Prof. Juma A. Kapuya na Naibu wake, Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir, kwa kazi nzuri waliyoifanya kipindi kile, lakini walikwamishwa sana na watendaji katika Wizara ile.

Mheshimiwa Spika, mahali ambapo kuna migogoro, hapawezi kuwa na maendeleo. Hiyo migogoro ndiyo ilitufikisha hapa tulipo hivi sasa. Mheshimiwa Capt. John D. Komba, alizungumzia miaka ya 1970 na alionesa jinsi gani Tanzania tulipiga hatua katika michezo, mchezo wa mpira wa miguu lakini hata michezo mingine. Lakini kuanzia miaka ya 1990 – 1995 mpaka hivi sasa, kwa kweli tumerudi nyuma sana katika michezo, lakini kubwa ni migogoro. Migogoro hii, watendaji wetu wamekuwa wakihusika kwa namna moja ama nyingine, kuisababisha itokee ama kuifanya iendelee kuwepo.

Mheshimiwa Spika, huwezi kuzungumza maendeleo ya michezo wa mpira wa miguu Tanzania, ukakosa kuitaja Simba ama ukakosa kuitaja Yanga. Panapotokea matatizo ama migogoro katika vyama hivyo viwili, basi ujue hata Timu ya Taifa, haitafanya vizuri kwa sababu asilimia kubwa ya wachezaji ambao tunawatumia wanatoka katika vilabu hivyo.

Mheshimiwa Spika, lakini migogoro imeendelea kuwepo na naomba ninukuu baadhi ya Kanuni zilizounda Baraza la Michezo la Taifa na nina hakika kama kweli watendaji wetu wangekuwa wanazifuata, sidhani kama tungefika hapa tulipo. Tunataka maendeleo, tunataka mabadiliko, lakini mabadiliko ni lazima yaendane na sheria, taratibu na kanuni zilizopo. Leo katika Klabu ya Yanga, kuna mvutano mkubwa sana kati ya pande mbili na bahati nzuri na tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwamba, Watanzania wote tunaongea Kiswahili. Lakini kama tungekuwa tunaongea lugha tofauti tofauti, basi sasa hivi nafikiri tungekuwa tunasema mengine katika Vilabu hivyo, tungeuwana au kutwa tungekuwa tunapigana.

Mheshimiwa Spika, Yanga wana mgogoro katika kuboresha *Young African Sports Club*, lipo kundi liliamua kwamba, hapana twende kibiashara kwa maana ya kuanzisha Kampuni. Sasa *Young Sports Club* iwe Kampuni. Lakini kwa mujibu wa Kanuni zetu za Baraza, zinapingana na hilo.

Mheshimiwa Spika, ninukuu Kanuni za Baraza la Michezo, Sheria ya Baraza la Michezo ya mwaka 1967, ikafanyiwa marekebisho mwaka 1971. Utaratibu wa kusajili vyama vya michezo, kipengele cha sita. Naomba kunukuu “Chama cha Michezo wowote, hakitaruhusiwa kuendesha shughuli za michezo bila kusajiliwa na Msajili wa Vyama vya

Michezo. Aidha, chama kilichosajiliwa, hakiruhusiwi kuwa na ushirikiano wa kimechezo na chama chochote, ambacho hakijasajiliwa.”

Mheshimiwa Spika, juzi niliuliza swalii kati ya Yanga mbili hizi, Yanga Kampuni na *Young African Sports Club*, Naibu Waziri alinijibu kwamba, Yanga Kampuni imesajiliwa chini ya Sheria Na. 212 ya Msajili wa Makampuni. Yanga *Sports Club* imesajiliwa chini ya Sheria ya Msajili wa Vyama vya Michezo. Kwa mujibu wa kanini hizi za Baraza ni kwamba, ndiyo ambayo inatambulika. Lakini kwa sababu ni mpango mzuri wa kuiondona Yanga pale ilipo, kuipeleka sasa kwenye mahali ambapo watajipatia kipato kizuri, kuifanya iwe kampuni, kuiendesha kisasa. Hapa tunakingana sasa na kanuni ya Baraza. Nawaomba viongozi wa Baraza, wazipitie na kuzitafsiri vizuri hizi kanuni kabla ya kuanza kuingia kwenye mambo mengine ya maendeleo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tunao mpango hivi sasa labda tunataka soka la kulipwa, tunao mpango wa kuvinfanya vilabu vyetu viwe kampuni lakini tunapingana na sheria na ndiyo maana wakati wa kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais, aliyoitoa tarehe 30 Desemba, nilisema Serikali iangalie uvezekano wa kuzirekebisha kama si kufuta kabisa Sheria hizi za Baraza la Michezo.

Mheshimiwa Spika, lakini kanuni hizo hizo tena kwenye marekebisho ya Katiba, kwa sababu huwezi kusajili chama cha mchezo wa miguu pale, msajili ni lazima uwe na Katiba. Marekebisho ya Katiba unapotaka kuyafanya, kanuni inaelekeza, naomba kunukuu: “Chama chochote kitakachofanya mabadiliko ya jina, anuani, madhumuni au kifungu chochote cha Katiba yake, kitatakiwa kupata idhini kwa kuipeleka maombi kwa msajili kuitia msajili msaidizi kwa kujaza fomu za maombi.” Zimetajwa hizo fomu. Sasa kuifanya Yanga iwe kampuni na itambulike, ni lazima hizi sheria tuzifuate. Lakini tukitaka kwenda tunavyokwenda hivi sasa, ndio maana tunazaa migogoro hii. Wizara imeshindwa kuwa wazi tangu mapema, kuelekeza ama kushauri kuhusu suala hili la Yanga, ndio tumefika hapa tulipo.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara sasa, bahati nzuri nimeandika, wanieleze jitihada ambazo watazifanya kwa makusudi, kuhakikisha mgogoro huu wa Yanga Asili na Yanga Kampuni unakwisha.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, upo mgogoro katika *Club* ya Simba, ambaao nao pia umechangiwa kwa kiasi kikubwa na Watendaji wa Wizara. Mara baada ya Msajili kwenda kufanya uhakiki wa wachama wa Simba, kuanzia pale ndipo zogo lilipotokea. Sasa ili tuendane na kauli ya Mheshimiwa Rais ya kuhakikisha Tanzania inacheza Fainali za Afrika mwaka 2008, ili maendeleo yapatikane, ni lazima tuhakikishe migogoro hii, tunaiondoa.

Mheshimiwa Spika, nina hakika kabisa Mheshimiwa Waziri ni mtunzi mzuri wa nyimbo, lakini nina hakika pia ni mchezaji mzuri sana, alikuwa zamani akichezea Timu ya Kikwajuni. *Centre Forward* mzuri sana. Mheshimiwa Joel N. Bendera, amechezea Korogwe Nyota, anaujua mpira vizuri sana. Nina hakika mgogoro huu katika kipindi kifupi wataumaliza ili tuweze kwendana na ahadi ya Rais.

Mheshimiwa Spika, sambamba na kurudisha michezo shulenii, ningeiomba Wizara ihakikishe tunawapa angalau mafunzo ya awali, walimu wa shule za msingi na walimu wa shule za sekondari, angalau wajue kuwafundisha wale watoto wetu pale shulenii michezo huu wa mpira wa miguu. Kuwe na kozi fupi fupi kwa walimu ili ziweze kuwasaidia.

Mheshimiwa Spika, nazungumzia vyombo vyaa habari. Nimekuwa nikisoma magazeti na kwa kweli sasa inabidi hata nisiyasome, yapo baadhi ya magazeti yamekuwa yakihoji na kueleza mgogoro wa suala la *NSSF* na *Quality Group*, juu ya mikataba ya ununuzi wa yale majengo. Hilo limezungumzwa sana kwenye vyombo vyaa habari na baadhi ya vyombo ndivyo ambavyo wamebebea bango suala hilo, yaani ndivyo ambavyo vinaandika habari hizo.

Magazeti yote ya *IPP*, huwa yanaandika habari hizo kila kukicha. Sasa ningependa katika majumuisho, mnifahamishe yanayoandikwa na magazeti yale, yako sawa sawa? Kama yako sawa sawa, Serikali inachukua hatua gani na kama yanayoandikwa siyo sawa sawa, basi pia nitaomba tamko la Wizara, ni hatua gani mnachukua kwa sababu kama yatakuwa siyo sahihi, ina maana wanatupotosha? Nitaomba maelezo hayo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kuwapongeza wandaaji wa Mashindano ya *Miss Tanzania*, pamoja na wandaaji wa Mashindano ya *Miss Utalii*. Niwapongeze hasa wa Utalii na nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kuhakikisha kwamba, mashindano yale ya Utalii Duniani yalifanyika hapa Tanzania na yalifanyika kwa ufanisi mkubwa sana, baada ya Serikali kuamua kuingilia na kusimamia Mashindano yale. Naipongeza sana Serikali kwa sababu kinyume cha hivyo, Tanzania tungeweza kupata aibu.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la makocha, tayari tunao makocha wa Kigeni ambaa watafundisha Timu yetu ya Taifa, lakini bado tunataka makocha kwa ajili ya timu zetu za mitaani. Naiomba Wizara iandae utaratibu wa makusudi kabisa wa kuhakikisha vijana wetu wanapata mafunzo ya ukocha hapa nyumbani au kwa kupelekwa nje.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofî*)

SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, sasa tumefikia mwisho wa shughuli za asubuhi kwenye kikao chetu hiki. Matangazo machache tu; jioni nimesahihisha kidogo, hisia zangu ni kwamba, Wizara haina mambo mengi sana kwenye Kamati ya Matumizi. Kwa hiyo, naruhusu mchangiaji mmoja, ambaye ameomba kwa nguvu sana, Mheshimiwa Dr. Omari Mzeru Nibuka, Mbunge wa Morogoro Mjini.

Nitampa nafasi hiyo saa 11.00 jioni na kwa maana hiyo basi, nitamwita Naibu Waziri wa Kwanza, Mheshimiwa Joel N. Bendera saa 11.15 jioni. Atafuatiwa na Naibu Waziri wa pili, ndivyo walivyopangana tu, siyo kwamba nawapanga kwa umuhimu au

vipi, ni namna ya kuongea tu kwamba, atatangulia Mheshimiwa Joel N. Bendera, atafuatiwa na Mhesimiwa Dr. Emmanuel J. Nchimbi saa 11.30.

Kwa hiyo, nitamwita mtoa hoja saa 11.45 jioni ili amalize saa 12.45 jioni ikiwa atafika huko, ituwezeshe kuwa na saa moja ya Kamati ya Matumizi. Nimehisi kwamba inatosha.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo na kwa kuwa muda umewadia wa kusitisha shughuli za Bunge kwa asubuhi hii, basi natamka kusitisha shughuli za Bunge hadi hapo saa 11.00 jioni.

(Saa 07.00 mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)

SPIKA: Kama nilivytangaza pale saa 7.00 tutakuwa na mchangiaji mmoja, Dr. Mzeru, Mbunge wa Morogoro Mjini na baada ya hapo nitawaita Manaibu wawili kwa mpangilio kwa robo saa, robo saa.

MHE. DR. OMARI M. NIBUKA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii angalau na mimi niweze kuchangia Wizara hii ya Habari, Utamaduni na Michezo.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nguvu na uwezo wa kusimama hapa Bungeni kuweza kuchangia kwenye hotuba hii ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo ili niwawakilishe wananchi wangu wa Jimbo la Morogoro Mjini. Lakini pamoja na kumshukuru Mwenyezi Mungu, ningependa kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Morogoro Mjini kwa kunipa tiketi ya kuja hapa Bungeni ili niweze kuwawakilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mwizi wa fadhila kama sitamshukuru mke wangu mpendwa Mrs. Mzeru kwa kunitunza kama hivi mnavyoniona, lakini pia naomba niwashukuru familia yangu kwa kunipa nguvu wakati ule wa kampeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kuzungumzia hasa hii Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, naomba pia nichukue nafasi hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ndugu yetu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa na Wajumbe wa Mkutano Mkuu Taifa kuwa Mwenyekiti wetu wa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Yusuf Rajab Makamba (Mbunge), kwa kuchaguliwa kuwa Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi. Lakini pia naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Capt. Jaka Mwambi, kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi. Lakini pia naomba niendelee kumpongeza Mheshimiwa Aggrey Mwanri (Mbunge), kuwa Katibu Mwenezi wa Chama cha Mapinduzi. Lakini siwezi kumsahau ndugu yetu Mheshimiwa Rostam

Azizi, kwa kuchaguliwa kuwa Mweka Hazina wa Chama cha Mapinduzi. Pamoja na hayo, naomba pia niipongeze Sekretarieti yote ya Chama cha Mapinduzi Taifa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ya Habari, Utamaduni na Michezo ni Wizara nyeti sana kuliko labda watu wengine wanavyoifikiria. Taifa lolote ili liweze kuendelea, linategemea watu wenyewe afya njema na bora kwa ajili ya kufanya kazi ili waweze kuzalisha, hatimaye nchi iweze kuwa katika hali nzuri. Lakini nchi ambayo wananchi wake watakuwa hawana afya njema, nchi hiyo kwa vyovyyote vile, itakuwa maskini kwa sababu wazalishaji mali hawana uwezo wa kuzalisha mali kutokana na afya zao kuwa mbovu. Hivyo basi, nataka kuzungumzia kuhusu michezo, ni muhimu sana kwa sababu kwanza michezo ni afya, michezo ni furaha, michezo inaleta uhusiano mwema kati ya wachezaji na wachezaji, lakini pia hata nchi na nchi. Pia, michezo huleta amani na nidhamu na michezo ni siasa.

Mheshimiwa Spika, nadhani mtakumbuka miaka michache ya nyuma ndugu zetu wa Afrika ya Kusini kabla hawajapata uhuru baadhi ya nchi zilikuwa zinagomea kucheza na timu za Afrika Kusini kwa sababu ya ukandamizaji. Hivyo basi, michezo ni sehemu ya siasa kwa maana ya kupeleka ujumbe katika sehemu husika. Michezo pia ni elimu, lakini pia ni ajira.

Mheshimiwa Spika, kama unavyofahamu ni kwamba, wako vijana wengi tu ambao huko nyuma, familia zao zilikuwa maskini, lakini michezo imeweza kuwasaidia kuwa katika hali njema kabisa pengine kutupita hata sisi Wabunge. Kwa mfano, wako vijana wa nchi mbalimbali kutoka Bara la Afrika ambao wanacheza mpira Ulaya. Lakini siyo Ulaya tu, hata hapa nchini ziko Wizara ambazo zinaajiri vijana kwa sifa ya uanamichezo. Kwa mfano, Wizara ya Ulinzi, Wizara ya Usalama wa Raia, Wizara ya Mambo ya Ndani, kwa maana ya Magereza na nyinginezo, wakati mwingine vijana huwa wanaajiriwa, lakini sifa mojawapo ni kuwa mwanamichezo wa aidha mpira wa miguu, kukimbia, ngumi na kadhalika. Kwa hiyo, michezo ni ajira.

Mheshimiwa Spika, lakini michezo pia ni *identity*, yaani kitambulisho, kwa maana ziko nchi ukitaja jina lake tu watu wanajua kabisa kwamba hii ni nchi fulani na ni mahiri kwa kitu fulani. Kwa mfano, nchi ya Brazil ukiitaja kwa namna yoyote ile utajua kwamba hawa ndiyo mahiri wanaosakata kandanda katika dunia na wala hakuna mjadala katika hilo.

Mheshimiwa Spika, nataka nizungumze jambo ambalo kama tukitaka kupata mafanikio katika michezo ni lazima tuanzie chini kwa vijana wadogo wadogo, vijana wa Mitaani, lakini siyo Mitaani tu, pia katika Shule zetu za Msingi na Shule za Sekondari ili kuwe na *program* ya michezo katika Shule hizo. Kwa mfano kuwe na *Physical Education (PE)* ambapo zamani lilikuwa ni somo mojawapo katika Shule zetu. Hata sisi wakati tukisoma tulikuwa tunafanya hivyo ili kuibua vipaji vya vijana katika sehemu hizo.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu haina budi kuandaa viwanja vya michezo katika Miji yetu, Vijiji pamoja na Kata zetu ili vijana wetu waweze kupata mahali pa kucheza na

ili tuweze kuibua vipaji vyao. Viwanja hivyo ni vizuri vikaenda pamoja na upatikanaji wa vifaa vya michezo kwa sababu kama viwanja vitakuwepo, halafu vifaa vya michezo vikiwa havipo itakuwa ni kazi ya bure, kwa sababu vifaa vya michezo ndiyo nyenzo kama viatu, mipira, jezi na vifaa vya michezo mingine. Lakini kama itawezekana, katika *program* ya hapo baadaye, ni vizuri tukaandaa angalau kujenga Shule au Vyuo *specific* kwa ajili ya michezo kwa sababu sio vizuri kumfundisha tu mtu nadharia ya juu juu kwa sababu michezo yote ina *principles* zake. Kwa hiyo, ili mtu aweze kuelewa vizuri mchezo, ni vizuri akaenda darasani ambako anaweza akafundishwa michezo mbalimbali ili aelewae namna na *principles* zake.

Mheshimiwa Spika, kwanza nimefurahi kwamba Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hakukosea alipowachagua watu hawa mahiri ambaa wanaiongoza Wizara hii ya Habari, Utamaduni na Michezo kwa sababu kwanza wenyewe ni wanamichezo. Kwa mfano, Mheshimiwa Waziri, Mohamed Seif Khatib, yeze kwanza aliupiga mpira kwa ngazi ya juu, lakini pia kama tulivyoambiwa asubuhi na mmoja wetu aliyechangia mada hapa Bungeni kwamba na yeze pia aliquwa mtunzi wa nyimbo na nyimbo nyingine mpaka leo hii zipo kwenye chati. Kwa hiyo, ni haki yake kuiongoza Wizara hii. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kama hiyo haitoshi, naomba pia nielekee kwa Naibu Waziri, ndugu yetu Joel Bendera. Yeye ni mwanamichezo mahiri na ni mtaalam kwa sababu siku za nyuma aliwahi kuwa hata Kocha wa Timu ya Taifa ya Tanzania na sio kocha tu, aliwahi pia kuwa Kocha Mkuu wa Timu ya Taifa ya Tanzania. Pia, ni kocha wa Bunge kwa kipindi hiki.

Kwa hiyo basi, kumchagua kuongoza Wizara hii, maana yake ni mahali pake. Naomba nitoe ujumbe au rai kwa Mheshimiwa Rais, nafikiri hawa watu waendelee kuwa katika Wizara hii kwa kipindi chao chote ambacho wananchi wao watakuwa wamewachagua kuingia hapa Bungeni. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe sifa kwa Naibu Waziri mwingine, ndugu yetu, Mheshimiwa Emmanuel Nchimbi, kwani yeze pia ni mwanamichezo. Lakini licha ya kuwa mwanamichezo, yeze ndiye Mwenyekiti wa Vijana hapa nchini na michezo kwa kawaida inachezwa na vijana. Kwa hiyo, kupewa Wizara hii ili aweze kuiongoza ni mahali pake na wala hakuna matatizo. Hawa niliowataja ni watu mahiri na ni makini, sina wasiwasi nao hata kidogo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, jukumu la kuendeleza michezo katika nchi yetu lipo chini ya Wizara hii muhimu kwa kusaidiana na Vyama mbalimbali vya Michezo kwa mfano Shirikisho la Chama cha Mpira wa Miguu Tanzania (*TFF*). Kwa bahati nzuri, Chama hiki kinaongozwa na kiongozi wake, ndugu yetu, Leodiger Chilla Tenga, ambaye kwa kweli yeze ni mwanamichezo kwa sababu Tenga ni mtu mwenye sifa ya ajabu.

Kwanza aliwahi kuwa mchezaji wa Timu ya Taifa kwa maana ya Mchezaji wa Kimataifa. Lakini wakati huo huo akicheza mpira katika Timu ya Taifa, aliquwa anasoma Chuo Kikuu, kitu ambacho kwa mtu mwingine isingekuwa rahisi kufanya

mambo yote mawili kwa wakati mmoja. Kwa hiyo, ni mtu mwenye kipaji cha pekee. Kwa kumpa kuwa Rais wa Shirikisho la Chama cha Mpira wa Miguu Tanzania (*TFF*) maana yake ni haki yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, viko Vyama vingine kama vya mpira wa wavu, mpira wa pete, mpira wa meza na michezo mingine, kwa mfano mchezo wa ngumi, kukimbia, *Kung Fu, caret*, muziki na kuogelea. Lakini pia katika kuendeleza michezo, tunahitaji wadau wengine waweze kusaidia kwa mfano wazazi wa watoto, Walimu na Viongozi mbalimbali, kwa mfano sisi Wabunge na Madiwani.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano mimi hapa niliyesimama na kuzungumzia suala hili nimeshaanza. Kama mtakumbuka, hivi majuzi tu mwezi Juni, 2006 kulikuwa na Kombe la Mzeru (*Mzeru Cup*) ambalo lilikuwa limejumuisha timu mbalimbali za hapa nchini. Timu hizo zilikuwa 32 kutoka Mikoa mbalimbali zikiwemo timu za Visiwani Zanzibar na mchezo huo ulikuwa ni wa vijana chini ya umri wa miaka 14 na miaka 17.

Nia yangu kubwa licha ya kudhamini michezo hii, ilikuwa ni kutafuta namna ya kuibua vipaji vya vijana katika nchi yetu na kwa bahati nzuri michezo hiyo kwa uzito wake ilifunguliwa na Mheshimiwa Balozi wa Comoro hapa nchini ndugu Islam. Katika kufungwa kwake, ilifungwa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, Mheshimiwa Nchimbi, lakini mimi nilikwenda kufunga kwa niaba yake kwa sababu yeeye alikuwa ana majukumu mengine ya kitaifa.

Mheshimiwa Spika, katika michezo hiyo, napenda niwapongeze au niwashukuru Chama cha Mpira wa Miguu Tanzania kwa jinsi walivyotuunga mkono, kwani walitusaidia sana. Kwanza walileta Viongozi wao Wakuu wakati wa ufunguzi na wakati wa kufunga, lakini kama haitoshi, walitoa pesa kwa ajili ya kununulia zawadi kwa mfano medali za dhahabu, medali za fedha na medali za shaba ambazo tuliwapa zile timu ambazo zilipata ushindi. Mimi niligharimia vikombe, jezi, mipira na vitu vingine.

Mheshimiwa Spika, kuongoza michezo au kuandaa michezo siyo jambo la lelemama kwa sababu linahitaji fedha. Kwa hiyo, naomba ndugu zangu, Wabunge wenzangu wasiogope gharama ilimradi tu wasaidie katika kuendeleza michezo ili angalau vijana wetu waweze kuonyesha vipaji vyao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kilichonipa faraja katika mashindano haya ni kwamba timu ambazo ziliingia fainali katika umri chini ya miaka 17, ilikuwa ni timu moja ya Visiwani na timu ya Dar es Salaam ambapo timu ya Visiwani ilikuwa mshindi wa pili na timu ya Dar es Salaam ilikuwa ni mshindi wa kwanza ambao walipata dhahabu na kikombe. Lakini chini ya miaka 14, timu zilizofika fainali ilikuwa ni timu moja ya Dar es Salaam na timu moja ya Morogoro. Kwa bahati mbaya timu ya Dar es Salaam ndiyo ilikuwa mshindi na timu yangu ya Morogoro ikawa mshindi wa pili.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa nichukue nafasi hii niipongeze timu yangu ya *Moro United* ambayo hivi karibuni tu ilikuwa inawakilisha nchi hii ikiwa ni timu pekee mbali ya timu nyingine zote za Tanzania. Pamoja na

kwamba tulifungwa, lakini tulionyesha kwamba sisi tulikuwa Wawakilishi wazuri ila kwa bahati mbaya timu tuliyopangwa nayo ilikuwa timu mahiri kwa sababu ndiyo timu bora katika Afrika.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, nazitakia kheri timu zangu nyingine kwa mfano timu ya Polisi Morogoro ambayo iko kwenye kiwango cha kucheza *Vodacom League* na timu nyingine ndogondogo za Morogoro ambazo kwa kweli zinakuja kwa kasi kwa mfano timu yangu ya *Atlas Sports Club, Maskani Sports Club, Jabal Hilal, Rhino* na kadhalika. Kwa hiyo, nawaombea waongeze juhudhi angalau tuweze kuwa katika hali nzuri kimichezo katika Mkoa wetu wa Morogoro.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ila tu Spika hakuungi mkono kuipongeza timu iliyofungwa magoli saba kwa moja. Nadhani ungewapa pole. (*Kicheko*)

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. YONO S. KEVELA: Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la habari, Waandishi wa Habari walipwe vizuri katika mishahara na marupurupu mengine ikiwemo mikopo na tatizo la kamera na usafiri hasa pikipiki ili kuweza kupata habari kiurahisi. Sasa hivi hata nauzi kwao ni tatizo. Hata hivyo, nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Mohammed Seif Khatib, Manaibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Emmanuel Nchimbi na Mheshimiwa Joel Bendera, kwa jinsi walivyojipanga, pamoja na watumishi wote wa Wizara yao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utamaduni, ninawaomba wajitahidi kutembelea Jimboni kwangu kule Njombe Magharibi. Kuna kikundi kizuri cha taarabu Igosi na kikundi cha ngoma za jadi cha Masaulwa, kipo jirani na Kata ya Imalinyi. Vikundi hivi ukiviona vinaweza kuwa vya Kitaifa kutoa burudani kwa Viongozi wa Kitaifa na wageni mashuhuri, kwani sasa hivi isiwe vikundi vinachukuliwa vya Mjini tu.

Naomba sana wakati mtakapokuja, basi mnipe taarifa ili tuweze kuunda vizuri kwa ajili ya kuweka majina yenu kwenye nyimbo na ikiwezekana tufanye mashindano ya kitaifa kwa vikundi vya ngoma.

Mheshimiwa Spika, kuhusu michezo, naomba vijengwe Vyuo vya Michezo kwa vijana wenyе vipaji vya michezo hasa watoto wadogo, kwa mfano vipaji kwenye mpira wa miguu, *netball, tennis* na kadhalika na hiyo isiwe kwa vijana wa kiume tu. Michezo wa miguu kwa wanawake ni burudani nzuri sana kwa akinamama na Taifa kwa ujumla. Hivyo, uboreshwe na walipwe vizuri kwa njia ya michango ya harambee kwa wadau hasa wafanyabiashara.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nawapongeza sana Serikali kwa kuleta kocha Mbwanzil.

MHE. BUJIKU P. SAKILA: Mheshimiwa Spika, naomba niitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara walioshiriki kwa njia moja au nyingine katika kuiandaa hotuba hii. Nampongeza sana na ninaunga mkono hoja hii. Aidha, napenda nichangie katika maeneo kadhaa kama ifuatavyo: -

Katika Idara ya Maendeleo ya Michezo, nampongeza Mheshimiwa Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu kwa uamuzi wake wa ujenzi wa uwanja wa kisasa. Naomba huu uwe mfano kwa Wizara na viongozi wengine ili hatimaye tuwe na viwanja kama hivyo vingi angalau kimoja kwa kila Kanda. Ni vyema Awamu ya Nne ikamalizia ujenzi wa uwanja huo na kuanza ujenzi wa kiwanja kingine hususan katika Kanda ya Ziwa.

Mheshimiwa Spika, viwanja peke yake hata hivyo havitatuifikisha mbali katika michezo, ni vichocheo tu. Cha msingi ni mabadiliko ya kifikra kwa Watanzania juu ya michezo. Watanzania wanatakiwa kutambua kifikra umuhimu wa michezo kwa afya zao na kiuchumi. Hivyo, juhudzi za makusudi ziendelee kufanywa kuwapatia wananchi elimu hiyo muafaka na ni muhimu. Ni jambo jema mafunzo ya michezo mbalimbali yakaanzishwa kwa mtu akiwa bado na umri mdogo.

Mheshimiwa Spika, tukumbuke samaki hana budi kukunjwa angali mbichi, ukimwacha akakauka juhudzi zozote za kutaka kumkunja zitamvunja. Hivyo, kama tunapenda tuwe na timu nzuri, timu zitakazoleta heshima kwa Taifa letu, timu zitakazotoa ajira kwa vijana wetu, basi hatuna budi kuanza na vijana wakiwa wadogo ili wakue na michezo ndani ya damu zao na kwa vijana wa aina hiyo tutarajie vijana wazalendo kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, napenda nitoe tahadhari na angalizo kwa timu zetu. Tumeshuhudia katika miaka iliyopita, timu kubwa kuhujumu timu ndogo ndogo. Mara kadhaa timu ya Pamba kwa mfano, imekuwa chimbuko la wachezaji wazuri wa timu kubwa hapa nchini. Nashauri kila timu kubwa iwe na timu ya watoto na vijana na kuwa uwepo utaratibu wa kuzilinda timu zinazoinukia ili zikue na ziimarike. Mtindo wa mashindano ya timu ya Simba na Yanga tu hautatuifikisha popote. Tunatakiwa kuwa na utaratibu wa kulea timu hadi tupate timu nyingi nzuri zinazoweza kupeana ushindani wa kweli. Njia mojawapo ya kulinda timu ndogo ni katika usajili, utaratibu utoe upendeleo wa makusudi kwa timu changa. Timu iruhusiwe kusajili wachezaji mara moja tu kwa kipindi cha miaka mitatu na pale inapokuwa ni lazima, ada iwe kubwa tena kwa idadi ndogo tu ya wachezaji.

Mheshimiwa Spika, tukiwa na timu nyingi nzuri, hatutahitaji sana timu za nje za majaribio ambazo gharama yake ni kubwa na mara nyingi tutashindwa kumudu. Tujijengee uwezo wetu wa ndani kwanza. Mtindo wa kumezanamezana sisi kwa sisi utatuacha kama watu wa Mwanza wanavyouangalia uwanja wa Kirumba na kusubiri timu kubwa kutoka nje ya Mkoa kuja kuutumia na wasipofika wanauangalia uwanja huo kama kaburi.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Habari ni muhimu sana kwa uhai wa mtu. Habari hutambulisha mtu alipo, alivyo na hali ya mazingira aliyomo. Habari humilinda mtu. Hivyo, kwa uhai, afya na maendeleo ya mtu, habari ni kitu cha lazima sana. Ili kupata umuhimu wa kilichomo ndani ya habari yoyote, mtu lazima asome, asikilize, aangalie au kuhadithiwa. Sasa tujiulize, ni Watanzania wangapi walio na uwezo wa kununua *television* na kuangalia? Ni wangapi walio na uwezo wa kununua redio na kuzisikiliza na ni wangapi walio na uwezo wa kununua gazeti moja tu na Sh.200/= kila siku na kulisoma? Serikali kama kweli inatambua umuhimu wa habari kwa wananchi wake, haina budi kujielekeza katika kuwawezesha wananchi wake wengi kupata habari. Uwezo wa Watanzania (zaidi ya asilimia 90) unaishia kwenye magazeti.

Mheshimiwa Spika, magazeti mengi yanauzwa Sh.200/. Kwa mnunuzi mzuri wa magazeti anahitaji Sh.6,000/= kwa mwezi, inawezekana? Tatizo kubwa wananchi wengi hawana utamaduni wa kusoma. Ninachoomba ni bei ya magazeti ipunguzwe ili yavutie wanunuzi na wasomaji wengi wa magazeti. Habari zinapowafikia watu wengi, umuhimu wa taarifa sahihi unajitokeza mara moja. Hivyo, Serikali isaidie wenye Vyombo vyta Habari kutoa taarifa hizo kwa gharama ndogo. Kwa upande mwingine, Serikali idhibiti taarifa/habari zinazotolewa kwa wananchi wachache. Wananchi wanaoweza kununua habari, wapate habari hizo kwa bei nafuu na wapate taarifa sahihi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Idara ya Utamaduni, Serikali ikamilishe suala hili. Suala la vazi la Kitanzania kwa mawazo yangu vazi, la Kimasai hasa kwa akinamama naona ni zuri sana.

MHE. FATMA A. MIKIDADI: Mheshimiwa Spika, kwanza ninachukua nafasi hii kuipongeza Wizara kwa mikakati safi hasa kuwa na uwanja mzuri wa michezo ambaa umepamba taarifa ya kitabu cha Bajeti, ukurasa wa mwisho. Hongera sana.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja nzima ya Bajeti kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 24 kuhusu suala la kujenga jumba la utamaduni: Je, Serikali inafikiriaje juu ya kujenga jengo la kumbukumbu (*museum*) ya kuweka mijusi (*dinosaurs*) wetu waliyopo kule Berlin Ujerumani? Hata ile tu kuwaza ule mchoro na wapi tatajenga. Naomba majibu, ni yule mijusi aliyetoka Mkao wa Lindi.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 15, mitambo ya redio Kusini Lindi, haisikiki kabisa. Pia, pamoja na kwamba kuna stesheni za Nachingwea na Lindi, lakini sauti za redio hazisikiki kabisa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kufungua Ofisi za Habari, nimeona sasa ni kwa nini Lindi watu hawaijui. Hii ni kwa sababu Lindi haitangazwi katika Vyombo vyta Habari hivyo, shughuli zake za jamii hazijulikani. Hii ni kwa sababu hakuna Ofisi za Habari katika Mkao mzima wa Lindi. Hatuwezi kutegemea vyombo vyta binafsi tu kwa miaka yote hii.

Tunaomba tafadhali sana, mwaka huu na sisi Mkoa wa Lindi Ofisi za Habari zifunguliwe, Lindi na Mtwara ni pacha. Ukiweka maendeleo yoyote Mtwara, basi inabidi na Lindi uweke pia kama ukurasa wa 19 unavyosema kuwa: "Zitafunguliwa Ofisi za Habari katika Mikoa kadhaa hadi Mtwara." Kwa nini na Lindi nako kusifunguliwe? Sisi sote ni maskini na ni Mikoa ya pembezoni, kwa nini sio Lindi? Rais ametangaza kusaidia Mikoa ya pembezoni, hata Ofisi ya Habari pia tunyimwe? Tusaidieni tafadhali.

Mheshimiwa Spika, Tanzania imekuwa mpenzi wa mpira wa miguu na hata wanawake wanacheza, lakini sioni kama Serikali inaupa umuhimu wake. Mchezo huu umekuwa kama hiari ya watu timu hizo kucheza. Sasa tunaiagiza Serikali iweke umuhimu kwa mchezo wa mpira wa miguu. Ili timu za Taifa ziweze kushiriki Kimataifa na kutuletea ushindi, wapewe nyenzo za kufanyia kazi na waweke Kambi ya Mafunzo ya Mazoezi na yote yanayostahili katika maandalizi ya michezo ili kujiletea ushindi. Tanzania wanapenda sana mpira wa miguu, waandalowiwananawake na wanaume.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa miaka ya nyuma michezo ilikuwa imepewa kipaumbele, sasa huu ndiyo muda muafaka wa michezo ya *netball* na mpira wa miguu.

Waliokuwa wakifanya kazi katika makampuni mbalimbali walikuwa na mashindano mbalimbali na watumishi wa Benki vile vile walikuwa wakishindana na Benki nyingine. Lakini sasa hivi michezo hiyo hakuna.

Mheshimiwa Spika, ninaomba michezo ifufuliwe kila Idara ishindane na nyingine.

MHE. SIGFRID S. NG'ITU: Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja yetu hii kwa asilimia zote, yaani asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa ni nzuri. Pili, matatizo mengi ya kule kwetu Ruangwa tayari nimeongea na Naibu Waziri, Mheshimiwa Joel Bendera, naye alinisikiliza na kuahidi kutembelea Septemba mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, naomba nimjulishe Mheshimiwa Waziri kuwa, kule Ruangwa wanamsubiri kwa hamu kubwa, lakini kwa hasira kali. Hasira hizo zimesababishwa na mambo yafuatavyo: -

- (i) Hawajawahi kuona mpira wa ngozi ya ng'ombe ambao wanatumia wenzao katika viwanja vingi vya mipira. Wao bado wanatumia mipira ya utomvu wa porini au furushi la nguo.
- (ii) Uwanja wa mpira wa Ruangwa bado ni wa mianzi na magoli ni ya miti. Mbona hivi? Wanahitaji kuchoma moto uwanja huu kwa sherehe ambazo

mgeni wake wa heshima atakuwa Mheshimiwa Bendera. Naomba Mheshimiwa Waziri amuarifu ili ajiandae.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri ajiandae vipi?

- (i) Aje pamoja na *visiting coach*, atuachie pale Ruangwa angalau kwa wiki moja tu ili atuboreshe.
- (ii) Atuletee zawadi ya mipira angalau 200 tu, jezi angalau 50 tu na hata filimbi.
- (iii) Mwisho, ni ule uwanja: Je, hawawezi kutusaidia chochote kile kama kutunyooshea vidole ili tuendelee kujitahidi tupate matofali ya kujengea uwanja wa *chap chap*? Kweli tunaomba sana.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, tunaomba tusaidiwe chochote kile katika jitihada zetu za kutaka kufungua redio yetu ili itupatие habari kama wenzetu, ituburudishe na kutuelimisha. Redio Tanzania wakati mwengine haisikiki hata kwa wiki nzima. Bado hatujapata masafa na wafanyakazi, yaani watangazaji. Tunadhani ni vyema redio hiyo ikaanza kusikika kuanzia Oktoba, 2006.

MHE. ALI KHAMIS SEIF: Mheshimiwa Spika, nchi yetu imepata makocha wa kufundisha mpira (kocha wa viungo na kocha wa mpira wenye) kutoka nje. Ni hatua nzuri ya kupongezwa. Kuwa na kocha wa kigeni pekee siyo jambo litakalotuhakikishia ushindi wa mpira wa miguu. Ninavyokiri mimi, kwanza hao wachezaji wawe wanafundishika. Kuchukua wachezaji ambao wameshachoka katika kucheza mpira, sio vizuri na hatuna njia ya mkato kwa hili. Kwa jambo hili nashauri watafundutwe vijana wapya ili wafundishwe na makocha hao. Tusitegemee kupata matokeo mazuri ya mpira wa miguu kwa mwaka mmoja.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa nane (8) wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri amesema anataka aweke mikakati au mipango ili walimu wa Kiswahili wa Tanzania wakafundishe Kiswahili nchi za nje. Wasiwasi wangu kwa hili ni kuwa, mipango hiyo inaweza ikachukua muda mrefu sana hatma yake soko hili la ajira likachukuliwa na Kenya. Ninaomba Mheshimiwa Waziri anieleze mipango hiyo itakamilika lini na ni mipango gani.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii inao wajibu wa kulinda na kuendeleza utamaduni. Kwa hilo, ipo haja vyombo vinavyohusiana na Wizara hii kwa mfano *TVT* na *RTD* vipindi vyao viende sambamba na utamaduni wetu. Pia, ipo haja ya kuwa na mkakati madhubuti wa kudhibiti vitendo vyote vinavyosababisha mmomonyoko wa maadili mema hapa nchini mfano Vituo vya *internet* juu ya ngono.

Mheshimiwa Spika, ipo haja kwa Wizara, licha ya nia yake ya kukuza mpira wa miguu, pia mkazo uwekwe kwenye michezo mingine ambayo baadhi ya michezo hiyo imetupatia heshima kubwa duniani kwa mfano riadha. Ninashauri michezo kama wa kuogelea, upewe msisitizo maalum, kwani michezo pia unaweza ukatuletea heshima.

Ninashauri pia michezo ianzishwe mashulen, hii itasababisha mabadiliko makubwa katika michezo. Ahsante.

MHE. JOYCE N. MACHIMU: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kupata fursa hii ili nami niweze kuchangia hoja ya Wizara hii ya Habari, Utamaduni na Michezo.

Mheshimiwa Spika, kwanza niwapongeze wahusika wa Wizara hii ambaao ni Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, Mheshimiwa Mohammed Seif Khatib , Naibu Mawaziri wake na wataalam wa Wizara hii kwa kazi na maandalizi mema wanayoyaboresha ili kuiweka Wizara hii katika hali bora.

Mheshimiwa Spika, binafsi, sina tatizo sana na hii Wizara ila tu kuna kitu kinachonikera na niombe Wizara na Serikali iweze kutazama upya ili kuweka suala hili sawa. Suala lenyewe ni kuhusu utangazaji wa habari mbalimbali katika Vyombo vy'a Habari kwa mfano kipindi palipojitokeza mgogoro wa Bwana Reginald Mengi, Mkurugenzi wa IPP. Vyombo hivi vilimpa nafasi kubwa ya kulielezea Taifa maelezo mengi kuhusu tuhuma zake kiasi ambacho mimi binafsi sikupenda, kwani kwa kufanya hivyo kunajenga hisia na vishawishi mbalimbali katika jamii yetu ambayo ina amani kubwa, hivyo kuleta hisia za ghasia kitu ambacho ni kibaya. Je, kwa nini Serikali inaruhusu hoja kama hizi zitumie muda mwangi kutangazwa kwa jamii tofauti na masuala mazuri ya Kitaifa yenye kujenga maadili mema? Serikali inasemaje kuhusu haya?

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni kuhusu picha za ngono. Serikali haioni kuwa kuonyeshwa picha hizi mara kwa mara hasa *channel five* na kadhalika vinajenga maadili mabovu katika vizazi vyetu na ndiyo maana kumekuwa na lugha ya vizazi vipy'a kutumika vibaya katika Taifa letu ambayo misingi ya maadili ilikuwa mizuri na sasa inapotea? Naomba hilo pia Serikali ilione na ikiwezekana iwepo sheria maalum kuhusu vyombo hivi ili kuzuia mmomonyoko wa maadili.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ALI JUMA HAJI: Mheshimiwa Spika, kwanza nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wengine wote wa Wizara hii ambaao wamewzesha kwa namna moja ama nyingine kufanikisha uandaaji wa hotuba hii. Nawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali ya Awamu ya Batu kuptia Wizara hii kwa hatua iliyochukua ya kuanzisha uwanja mpya wa kisasa kabisa wa mchezo wa mpira wa miguu ambao hivi sasa uko katika hatua nzuri sana za kumalizika. Pia, naipongeza Serikali ya Awamu ya Nne kwa kutilia mkazo mkubwa wa kuinua kiwango cha mpira wa miguu kwa kukubali kudhamini/kugharamia wakufunzi wa mchezo huo kutoka nje ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naiomba pia Serikali ya Awamu ya Nne kuptitia Wizara hii kutilia mkazo mkubwa katika michezo mingine na isiwe tu katika mpira wa miguu ili nchi yetu itokane na aibu ya kuwa wasindikizaji tu katika michezo mbingi kama sio yote.

Mheshimiwa Spika, mmomonyoko wa maadili unatokana na mambo mengi ambayo kwa kiasi fulani yanachangia sana hali hiyo. Kwa mfano, *channel* nyingine za televisheni zetu zinaonyesha vipindi vya muziki ambao kwa kweli wasanii wake hasa wale wa kigeni wanakuwa wamevaa vivazi vichafu sana vya chupi na sidiria tu, jambo ambalo hata kama mzazi anaangalia *TV* na mtoto wake, analazimika ama aondoke, abadilishe *channel* au azime kabisa televisheni.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kuhusu uuzwaji wa vitabu mbalimbali vya udaku. Vitabu hivi vinauzwa kwa wingi sana na katika sehemu mbalimbali ya Miji ya Tanzania. Vitabu vinakuwa vinaandikwa mambo ya kimpenzi matupu na hata namna za kufanya mapenzi hayo chumbani. Baya zaidi vitabu hivi siku hizi vinauzwa bayana na bila kuchagua rika za kuweza kuuziwa vitabu hivyo. Kutokana na hali hiyo ya uuzwaji holela wa vitabu hivyo, vijana na watoto wetu wanavinunua sana na kusoma yaliyomo ambayo ndiyo hayo yanapotosha maadili kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kuptitia Wizaara hii, kuliangalia sana suala hili na ikiwezekana ipige marufuku uuzwaji wa vitabu hivi kiholela.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri atueleze hivi iko Bodi inayohakiki vitabu hivi? Kama ipo; je, Bodи hiyo haiyaoni haya au inayafumbia macho?

Mheshimiwa Spika, hata uimbaji wetu siku hizi hasa wa muziki wa taarabu, baadhi ya nyimbo zao zimekuwa za matusi ya wazi sana. Baya zaidi, wakati wanapoimba huwa wanaashiria.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara hii izihakiki nyimbo zote kabla ya kuimbwa kwenye Televisheni zetu na wakiona nyimbo imejaa matusi, basi ni vyema ipigwe marufuku kabla ya kuimbwa nyimbo hiyo na kuonyeshwa kwenye Televisheni zetu.

Mheshimiwa Spika, kama haya yatazingatiwa vizuri na kudhibitiwa vya kutosha, basi nadhani kwa kiasi fulani mmomonyoko wa maadili utapungua.

Mheshimiwa Spika, yapo mambo mengi ambayo yanachangia mmomonyoko wa maadili kama vile uvaaji wa nguo zisizostahili kwa wanenguaji wa kike wanapokuwa jukwaani. Mambo haya yote yakizingatiwa na kudhibitiwa bila shaka yatasaidia sana.

Mheshimiwa Spika, sasa nazungumzia kuhusu ukuzwaji wa lugha ya Kiswahili. Kiswahili ni lugha ambayo imetoka kupendwa sana duniani, hadi kufikia baadhi ya Mataifa kutoa ajira kwa Walimu wa Lugha ya Kiswahili. Lakini sisi wenywewe Watanzania tunaonekana kana kwamba hatujaipa umuhimu lugha hii licha ya kuizungumza tu.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali sasa itilie mkazo wa dhati kupitia Wizara hii kuona Kiswahili kinatumika kwa nguvu na itakuwa ni vyema tukianzia hapa Bungeni, isiwe tunatumia Kiswahili kwa kuzungumza tu bali tutumie hata katika kuwasilisha Miswada ya Sheria na mambo mengine.

Mheshimiwa Spika, tutumie Kiswahili ili wananchi wetu wapate moyo wa kukitumia muda wote na kila mahali wakati watakapowaona viongozi wao Wabunge wanatumia Kiswahili kila wakati na kwa kila jambo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja kwa asilimia 100. Ahsante sana.

MHE. MHONGA S. RUHWANYA: Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kuona umuhimu wa Wizara hii ya Habari, Utamaduni na Michezo na kuipa Mawaziri watatu ikiongozwa na Mheshimiwa Mohammed Seif Khatib - Waziri, Mheshimiwa Joel Bendera na Mheshimiwa Dr. Emmanuel John Nchimbi kuwa Manaibu wake. Ninaamini, utamaduni, habari na michezo itakuwa bora kuliko miaka ya nyuma kwani Wizara ina Watendaji wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, michezo ni burudani na pia ni afya, kwani *hu-regulate* viungo na husaidia moyo kupidisha damu vizuri katika mishipa yetu na ndiyo maana wenye miili mikubwa hushauriwa kufanya mazoezi ya mwili ingawa wote tunashuriwa kufanya mazoezi ya mwili.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, michezo ni ajira, michezo huweza kuajiri watu wengi kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha sana kuona katika nchi yetu michezo haina tija kwa wachezaji, kwani maisha yao ni duni mno kiasi kwamba haivutii watoto kujiendeleza katika fani hiyo.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara hii ituelezee ina mikakati gani kuhakikisha kuwa michezo ni ajira kama zilivyo fani nyingine ili angalau tufanane na nchi nyingine na kama Mheshimiwa Rais alivyosema, atahakikisha ajira milioni moja zinapatikana. Naamini Sekta hii ya Michezo ikiboreshwa itaongeza kiasi kikubwa sana cha ajira kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia katika suala la vazi la Taifa. Mara nyingi kumekuwa na mashindano ya kubuni vazi la Taifa. Ninaomba Wizara hii itueleze ina mikakati gani ya kuhakikisha kuwa Tanzania tunakuwa na vazi letu ambalo ukiingia nchi yoyote inakuwa ni utambulisho wetu. Je, na hayo mashindano ya ubunifu wa vazi hilo yameishia wapi?

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia katika suala la lugha yetu ya Taifa, Kiswahili. Nachukua nafasi hii kumpongeza na kumshukuru Marehemu Baba wa Taifa kwa kusisitiza na kutangaza Kiswahili ambacho kilisaidia kurahisisha mawasiliano

ambayo yalisaidia katika kupatikana kwa uhuru kwani waliongea lugha moja ingawa Tanzania tuna lugha zaidi ya 123.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara hii ihakikishe matumizi thabiti ya lugha hii yanazingatiwa. Iweje wenzetu Wachina, Wavietnam watumie lugha zao katika nchi nyingine na katika Mikutano Mikuu ya Kimataifa lakini Watanzania wasiitumie kama wenzetu hao!

Mheshimiwa Spika, tujivunie lugha hii na Wizara hii itangaze na isisitize matumizi yake. Ikitumika duniani katika Mikutano mbalimbali, tutaitangaza vyema lugha hii. Tusione aibu kutumia wakalimani, hii haitaonyesha kuwa hatujui Kiingereza, bali itaonyesha uzalendo na utaifa wetu na jinsi tunavyoijali lugha yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara hii ihakikishe utamaduni, michezo, uigizaji pamoja na fani zote za usanii ziwe na tija kwa maisha ya wadau wa sekta hizo. Ziwe ajira ili maisha yao yabadilike ili vipaji visigeuke kama adhabu kwao.

Mheshimiwa Spika, naomba kuishia hapo nikiamini mchango wangu utaboresha kazi ya Wizara hii na panapohitajika majibu, basi nitajibiwa. Naomba kuwasilisha.

MHE. ABBAS Z. MTEMVU: Mheshimiwa Spika, nianze kutoa mchango wangu kwa kusema kuwa Waandishi wa Habari maslahi yao yatazamwe ikiwa ni pamoja na mishahara, mafunzo, usafiri na Bima.

Mheshimiwa Spika, pili nzungumzie Soka. Ninaomba Mheshimiwa Waziri tufikirie Timu hizi za Daraja la kwanza; Simba, Yanga, *Moro United*, Kagera, Twiga, na kadhalika, ziwe timu za wachezaji wa kulipwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kumwambia Mheshimiwa Waziri kwamba kiko kilio cha watoto wa Mzee Morris juu ya nyimbo za Baba yao zinazotumika katika taarifa za Habari *TVT*.

Mheshimiwa Spika, watoto wa Msanii huyo Marehemu, wanaishi Mtoni katika mazingira magumu sana ya maisha. Wamedai fidia ya nyimbo hizo wakati wa Redio Tanzania hadi leo wanazungushwa bila kulipwa na hakuna maelezo yoyote.

Mheshimiwa Spika, nzungumzie vyombo vya habari. Vyombo vya Habari na wamiliki wa vyombo hivyo wahakiki habari wanazorusha hewani kabla ya kabla ya kuzitoa hewani. Sio vyema kutoa habari za upande mmoja bila kuhakikisha upande wa pili.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Manaibu wake wawili, Katibu Mkuu na Wafanyakazi wote.

Ninaomba maelezo ya kina kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. Naunga mkono hoja.

MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA: Mheshimiwa Spika, pongezi nyingi kwa hotuba nzuri na yenye kutia matumaini.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, jamii ielimishwe na Wizara hii juu ya umuhimu wa Vyomo vya Habari. Hivyo, Serikali pamoja na Umma wanapaswa kuvilinda na kuvisaidia Vyombo vya Habari na Waandishi wa Habari.

Mheshimiwa Spika, Vyombo vya Habari vipewe uhuru zaidi wa kufichua kero mbalimbali hata kama zitakuwa zinawahusisha viongozi wenyewe dhamana kubwa (Uhuru zaidi wa Vyombo vya Habari).

Mheshimiwa Spika, Vyombo vya Habari vyenyewe vielimishwe kuwa *impartial*, sio vyema kutoa habari za upande mmoja tu. Mara nyingine haya hufanyika hata bila ya maelekezo ya Viongozi wa juu wa Wizara hii. Mfano, Taarifa ya Habari ya usiku wa jana ya *TVT*, kamwe haikusema chochote juu ya mchango wa Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mchango mzuri uliotolewa na Mhesimiwa Anna M. Komu kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, alionyeshwa Mheshimiwa Devota M. Likokola na Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar tu. Hii mimi nimeona nieleze kwani haitoi sura nzuri katika zama hizi za Awamu Mpya inayojitahidi kujenga Umoja wa Kitaifa (*National Integrity*).

Mheshimiwa Spika, jitihada kubwa ziendelee kuchukuliwa katika kuwaelimisha wanahabari juu ya namna ya kuripoti taarifa katika zama hizi za Mfumo wa Vyama Vingi.

Nawatakiwa kila la kheri. Ahsante sana.

MHE. IDDI M. AZZAN: Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi kwa Wizara hii, naomba maelezo/ufafanuzi katika yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kuhusu migogoro iliyopo katika vilabu vya Simba, Yanga na hatua zinazochukuliwa na Wizara kukomesha migogoro hiyo.

Mheshimiwa Spika, pili, ninaomba maelezo ya mapato ya mechili ya Simba na Yanga ambazo fedha za kulipa Uwanja wa Taifa zililipwa nusu na nyingine zimechukuliwa na wajanja wachache. Je, pesa zile zimepatikana na ni nani alizichukua? Hatua gani Wizara imechukua?

Mheshimiwa Spika, ninaomba maelezo kuhusu Vyombo vya Habari vinavyomilikiwa na *IPP* (*TV, Radio, Magazeti*) kuhusu madai ya vyombo hivyo juu ya Mikataba ya *NSSF* na *Quality Group* kama yana ukweli.

Mheshimiwa Spika, kama madai hayo yana ukweli, Serikali inachukua hatua gani kuhusu mikataba hiyo? Kama madai hayo hayana ukweli, kwa nini Magazeti hayo yanaendelea kuandika uongo na kuendelea kuwadanganya Watanzania?

Mheshimiwa Spika, katika haya, naomba Serikali inipatie maelezo ni lini italeta Bungeni Muswada wa Sheria utakaosimamia Vyombo vyote vya Habari na utendaji wa kazi zake.

Mheshimiwa Spika, ni lini sheria ya *BMT* ya mwaka 1967/1971 itarekebishwa?

MHE. EUSTACE O. KATAGIRA: Mheshimiwa Spika, nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Manaibu na Watendaji kwa kuandaa Bajeti nzuri. Pia, nawapongeza kwa utendaji mzuri katika Wizara.

Mheshimiwa Spika, vile vile nawapongeza kwa kuwa Sekta ya Habari imepanuka sana, magazeti, Radio na Televisheni.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Michezo inalegalega, lakini nafarijika angalau wanaona kwamba kuna tatizo na wameanza kulishughulikia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu magazeti, napendekeza uwekwe mkakati wa makusudi, baadhi ya magazeti ya Kiswahili yafike Vijijini. Nainaomba wapewe *support* wale wanaoanzisha magazeti ya Kimkooa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Radio na Televisheni, naomba uwekwe mkakati ili Televisheni ya Taifa na Radio Tanzania viwafikie wakazi wa Wilaya ya Karagwe hususan Jimbo la Kyerwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sanaa (Bendi, Uigizaji na kadhalika); watu wetu wanajitahidi katika nyanja hizi, nyimbo za bendi hasa vijana, michezo ya kuigiza na kadhalika. Serikali iwasaidie kuinua viwango na pia kuwatafutia masoko. Wenzetu wa Nigeria wamesonga mbele.

Mheshimiwa Spika, filamu na nyimbo vinaweza kuingiza pesa nyingi za kigeni, lakini pia na kukuza ajira. Yote yanahitaji sasa msukumo wa Serikali. Sekta ya filamu, uigizaji ina *potential* kubwa hasa ya vijana kujajiri, tuwape *support* kubwa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nazungumzia lugha ya Kiswahili. Ninashauri tuweke msukumo katika kusambaza Kiswahili. Tutoe *offer* za Walimu ambao wako tayari kufundisha Kiswahili nchi nyingine.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Spika, mwaka 2001- 2002, Tanzania ikiwa kama Mwanachama wa *SADC* na *AU* iliridhia mikataba kadhaa inayohusiana na habari na utangazaji:-

Mheshimiwa Spika, mwaka 2002, *The African Commission of Human and People's Rights adopted the Declaration of Principles of Freedom of Expression in Africa. Declaration* hii ina-bind wanachama wote wa Umoja wa Afrika, Tanzania ikiwa mojawapo.

Mheshimiwa Spika, Mwaka 2001 Tanzania iliridhia *The SADC Protocol on Culture, Information and Sport*.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2001 Tanzania kama mwanachama wa *SADC* iliridhia *The SACD Declaration on Information and Communications Technology (ICT)*.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri anipe ufanuzi, ni lini makubaliano haya ambayo Tanzania imeyaridhia yatafanyika kuwa sehemu ya Sheria za Tanzania (zinazohusu Vyombo vya Habari) kwa kuzingatia umuhimu wake katika kukuza na kuboresha Sekta ya Habari Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naamini Wizara hii inafahamu *Declaration* hizo kwa ufasaha, hivyo naomba kunipatia majibu yanayoridhisha. Ahsante.

MHE. AMEIR ALI AMEIR: Mheshimiwa Spika, kama ilivyo kawaida, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika katika Bunge lako Tukufu tukiwa wazima na kuendesha shughuliza Bunge.

Mheshimiwa Spika, sasa niwapongeze na kuwashukuru wapiga kura wa Jimbo la Fuoni kwa kukichagua Chama Cha Mapinduzi na kuniwezesha kuwa Mbunge wao.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Manaibu kwa kazi kubwa walijonayo ambayo kwa kipindi kifupi wanaonyesha kuimudu kazi hiyo, lakini pia nimpongeze Rais kwa kuiweka Wizara hii ikawa inajitegemea pamoja na uteuzi wa Mawaziri wanaongoza Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kazi ya Wizara hii zinaigusa jamii moja kwa moja. Kwa hiyo, kuna kazi kubwa ya kuridhisha jamii na kuridhisha ni kushinda michezo tunayoshindana pamoja na uongozi mzuri katika shughuli hizo.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ina michezo mingi sana, lakini uwakilishi wetu huwa hauridhishi kwa kushindwa mapema sana katika mashindano ya kitaifa na kimataifa na baadaye hutafuta visingizio mbalimbali vikiwemo uongozi mbovu na maandalizi mabovu.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Nne imeonyesha kukerwa na sababu hizo ambazo ukweli wake ni mfupi kwa kuamua kuweka Wizara na kuchagua viongozi

wenye sifa ya kuongoza Wizara hii kuagiza kocha wa timu ya Taifa na kujenga uwanja mpya wa kimataifa utakaohusisha michezo yote.

Mheshimiwa Spika, mategemeo makubwa ya kufanya vizuri katika michezo hasa maazimio ya Wizara kama yatatekelezwa, kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri maazimio ya Wizara yake yasiishie kwenye kitabu hiki cha hotuba yake.

Mheshimiwa Spika, lugha ya Kiswahili. Katika kuimarisha lugha ya Kiswahili itumike kuwa lugha ya Taifa, hatuna budi kuitangaza lugha hii duniani kote ili dunia iwelewe hivyo.

Pia, katika kuitangaza lugha hii hatuna budi sisi wenyewe kuitumia lugha hiyo katika Mikutano na Makongamano ya kimataifa inayofanyika katika nchi yetu au nje ya nchi yetu kama alivyofanya Rais wetu alivyokuwa anahotubia Marais wa Afrika huko Sudan. Mfano huu ni mzuri na unafaa kuigwa na Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, kuhusu sanaa ya muziki, vijana wengi siku hizi wamejikita katika sanaa hii kwa kuendesha maisha yao na wamepiga hatua kubwa sana ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, muziki hivi sasa ni ajira kubwa sana na imeajiri vijana wengi sana. Kwa kuwa muziki sasa ni ajira inayopendwa na vijana, Serikali haina budi kuwawezesha vijana hawa kwa kuwapatia ujuzi zaidi wa fani hii pia kutokana na uhalali wa bei ya vifaa vya muziki. Serikali ingetenga fedha kuvisaidia vikundi hivi. Pia, Serikali ingeondoa kodi ya vifaa hivi vinavyoingia nchini na kuchukua kodi kwa vile vinavyo toka nje ya nchi tu.

Mheshimiwa Spika, kuwaboresha vijana hawa, pamoja na kuwaelimisha namna ya sanaa zinazoleta maadili mema, vijana hawa wataneemeka kwa kupata fedha nyingi na pia Taifa litaongeza mapato yake.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante.

MHE. MANJU S. O. MSAMBYA: Awali ya yote, nachukua fursa hii kutamka rasmi kuwa naunga mkono hoja nikiwa na matarajio kuwa Wizara itatekeleza yale iliyokusudia kwa nia ya kuwaletea maendeleo Watanzania.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuunga mkono hoja hii, ninayo machache ya kueleza ambayo mionganoni mwake nitaomba nipaye ufanuzi wakati Waziri atakapokuwa anajumuisha.

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia kuhusu uhuru wa habari. Ibara ya 18 (*a - d*) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano inatoa Haki ya Uhuru wa mawazo. Hata hivyo uhuru bila mipaka ni uhuni. Naomba Wizara katika majumuisho inipe maelezo kwa hili lifuatalo: Kwa kisingizio cha habari za uchunguzi au *investigative journalism*

yapo magazeti nchini ambayo uchunguzi wao ni kumsakama mtu mmoja tangu magazeti hayo yameanza hadi sasa.

Mheshimiwa Spika, hivi Wizara imechukua hatua gani za makusudi za kufanya magazeti hayo yasiandike habari za kusakama? Nakumbuka hivi karibuni kumezuka malumbano ya wafanyabiashara maarufu nchini. Bahati mbaya mmoja wa wafanyabiashara hao amekuwa anatumia vyombo vyake vya habari kumsakama mwenzie. Hivi Wizara inachukua hatua gani za kuzuia haya malumbano au habari za kusakama?

Mheshimiwa Spika, hivi Wizara haioni kuwa kwa Waandishi wa mfanyakishashara mmoja kumsakama mwenzie ni kujenga mazingira ya uvunjifu wa amani? Serikali inasemaje kuhusu juhudhi zilizoanzishwa na Viongozi wa Dini kutaka kusuluhisha mgogoro huu? Serikali inakubali kuona mtu anatumia vyombo vyake kuelekea kuvuruga amani kwa kuelekeza vyombo vyake kuandika habari za kusakama? Naamini maelezo na ufanuzi wa namna gani Serikali inashughulikia uandishi wa habari za kusakama.

Kinadharia Kiswahili ni lugha ya Taifa. Lakini kivitendo Kiswahili sio lugha ya Taifa, kwani kama nilivyowaeleza siku ya Jumapili wakati wa Semina ya uzinduzi wa kitabu cha *The Promise*, lugha ya Kiswahili haitamkwi ndani ya Katiba. Hivi ni wapi tunabanwa ili kutumia lugha ya Kiswahili kwa mujibu wa Sheria?

Kumekuwa na kasumba ya kusema Kiingereza ni Kiswahili cha dunia. Kwanza kwa kufanikisha Kiingereza kuwa Kiswahili cha dunia, yaelekeea tunapenda Kiswahili kitawale dunia. Kiswahili kitawezaje kutawala dunia kama hakuna utaratibu wa makusudi wakukiendeleza na kukikuza? Ili Kiswahili kikue ni lazima kifundishwe mashuleni. Kiswahili kitumike kifundishwa katika masomo yote. Hili linawezekana tu kama tunaweza kuanza kwa makusudi kubadilisha vitabu vinavyotumika mashuleni. Ni vyema tuenzi Kiswahili sio kwa kauli za mdomo na maandishi, bali vitendo. Kiswahili kikitumika kuwa lugha ya kifundishia masomo yote, kitawezesha hata vijana wetu kuyaelewa masomo wafundishwayo na kwa maana hiyo, kuwawezesha kupata wataalam wa kutosha. Wizara ina mpango gani wakukifanya Kiswahili kiwe ni muhimili wa elimu Tanzania?

Mheshimiwa Spika, kuhusu mpira wa miguu, nashukuru kwa juhudzi za Mheshimiwa Rais ambazo zimetuwezesha kumpata Mwalimu wa kifundishia kikosi cha Taifa. Hata hivyo, naishauri Wizara isimruhusu Mwalimu huyo kuingiliwa katika utendaji wake wa kazi. Lakini nauliza, Wizara inao mpango gani wa kuwa na vilabu vinavyoendesa mchezo wa mpira wa kulipwa? Hivi Serikali haioni kuwa kuna haja ya kusaidia vilabu kwa njia hiyo ili kuviondoa kwenye ukata? Nitashukuru kupata maelezo ya hatua zinazochukuliwa na Serikali za kuwa na soka la kulipwa.

MHE. BALOZI SEIF ALI IDDI: Mheshimiwa Spika, napenda sana kumpongeza Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo kwa hotuba yake nzuri ambayo imetupa mwanga wapi tunakwenda katika kukuza mchezo na hasa mchezo wa mpira wa miguu nchini mwetu. Naipongeza Wizara kwa maelekezo yake mazuri ya hivi karibuni

yaliyotolewa na Naibu Waziri, Joel Bendera kwamba timu zote za mpira wa miguu ziwe na timu ndogo (*junior teams*) kwa nia ya kuvikuza vipaji vya vijana hao katika mchezo huo.

Kwa muda mrefu sasa mchezo wa mpira wa miguu umekuwa ukienda chini badala ya kuendelea mbele. Timu zetu katika mashindano ya kimataifa ziliwu zinafanya vizuri hadi kufikia nusu fainali, lakini sasa zinafungwa katika raundi ya pili na zikijikaza, zinafikia robo fainali tu. Ni vyema sasa Wizara kwa kushirikiana na vyombo vilivyoko chini yake, kama vile *TFF* ikafanya utafiti wa kina kuona ni kwa nini hasa timu zetu zimekuwa zikifanya vibaya ili hatua za marekebisho zifanyike ili mchezo huu uweze kukua tena? Maradhi hutibiwa baada ya *diagnosis* halisi kufanyika ili kujua maradhi yenye, tuyajue maradhi yanayotusibu ili tuyaponye. Tukifanya hivyo, nina hakika tutapiga hatua katika mchezo huu ili nasi tuweze kujulikana tena katika fani hii ya kandanda.

Pia, mashindano ya wachezaji wetu wa chini wa miaka 17 uendelezwe na kukuzwa. Hii ni hatua nyingine ya kukuza vipaji vya vijana wetu katika mchezo huu. Tuwe waangalifu timu yetu inapoingia katika michuano ya kitaifa tusidanganye umri kama tulivyofanya katika kipindi kilichopita ambapo tulinyimwa ushindi. Tutafute nchi nzima vijana wanaostahili kuiunda timu hii.

Naunga mkono hoja.

MHE. PAUL P. KIMITI: Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Manaibu wake na Katibu Mkuu kwa maandalizi mazuri ya hotuba iliojaa dira, maelekezo na miongozo mizuri ya jinsi ya kuendesha shughuli za Wizara katika mwaka huu wa fedha. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa uteuzi mzuri wa timu hiyo. Nina imani Wizara itavuna kama Rais mwenyewe alivyoanza kuisaidia kwa kuwapatia makocha toka Brazil. Naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, mimi ninayo maombi machache ambayo ningeishauri Wizara iyashughulikie.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima aliyoutuachia Rais Mstaafu Mheshimiwa Mkapa kwa ujenzi wa Uwanja wa Mpira huko Temeke, nashauri sasa ili uwanja usibakie kwa ajili ya timu zetu za humu humu, nashauri sasa kuwepo utaratibu maalum wa kuzialika timu mashuhuri za Afrika na baadaye za nje ya Afrika ili waje kutoa hamasa ya mchezo huu na kuutumia vizuri ili ulete mapato mazuri.

Mheshimiwa Spika, nashauri tuanze mpango wa kuwa na wachezaji wa kulipwa, wawe *full fine* wachezaji na siyo waajiriwa wa kazi nyingine. Naelewa haya yanahitaji maandalizi ya mapema kuanzia wachezaji chipukizi. Kwa msingi huo, ni vizuri tukajua vipaji vilivyomo katika Vijiji na mashulenii kwa kupeleka mipira ya miguu na *netball* kwa vijiji vyote nchini na mashulenii.

Mheshimiwa Spika, Mikoa mingi haina kumbukumbu ya rekodi ya nyimbo za makabila mbalimbali. Naomba *TVT* na *RTD* waje Sumbawanga kurekodi nyimbo zetu za utamaduni. Pamoja na hilo, pawepo ratiba ya kualika vikundi nya ngoma za asili zije hapa Dar es Salaam kwenye Kijiji cha Makumbusho ili wakazi wa Dar es Salaam waburudike na rasilimali kubwa tuliyonayo nchini. Utaratibu wa wiki maalum kwa Mkoa kuonyesha fani zao za utamaduni urejeshwe Mkoa kwa Mkoa.

Mheshimiwa Spika, Bendi za muziki zilizopo zipewe semina na mafunzo ya jinsi ya kuimarisha utamaduni wa nyimbo za asilia kama wafanyakyo wenzetu wa South Africa, Nigeria, Uganda na hata Zambia. Hatua ya bendi nydingi kuwa waiga mitindo ya nje, kunaweza kubomoa utamaduni wetu ambao tuna wajibu wa kujifunza na kuuensi. Hili ni pamoja na kuimarisha Chuo cha Sanaa Bagamoyo. Nakipongeza Chuo hiki, lakini ni budi kiboreshw na kipewe nafasi ya juu ili kitoe mafunzo kwa vijana wetu toka Mikoa yote! Wapewe mafunzo kwa ruzuku ya Serikali, maana wengi wao hawana uwezo wa kugharamia mafunzo yao. Tuwasaidie ili wajajiri wenyewe.

Mheshimiwa Spika, watumishi wa Vyombo nya Habari *RTD*, *TVT* na magazeti yote ya Serikali wapewe motisha na mishahara mizuri ili wasije wakatuhamu. Hatari iliyopo ni kuwa, sisi tusiwe tunaawaandalia wenzetu wa vyombo binafsi watumishi na tubaki hatuna watumishi. Tusishangae wakituhamu na kuchukuliwa na vyombo binafsi nya habari. Watumishi wa Vyombo nya Habari wawe wanapewa nafasi kubwa kuelezea matatizo yao na wapewe pia nafasi ya kutoa ushauri wa jinsi ya kiboresha sekta hii muhimu kwa uhai wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kumekuwepo na malalamiko na tuhuma nydingi ndani ya klabu za michezo, ndani ya vyombo nya habari *RTD*, *TVT* na mengineyo ni vizuri Serikali ikaweka utaratibu wa kudumu wa kufuatilia tuhuma hizi na kuzitafutia ufumbuzi wa kudumu. Vurugu katika Vyama, klabu na Taasisi zetu, kunaweza kudumaza jitihada za Wizara katika kufanikisha azma nzuri na dira ya maendeleo kama yalivyoainishwa na Ilani ya Uchaguzi (CCM) kuhusu michezo!

Naunga mkono hoja hii kwa asilimia moja.

MHE. FETEH SAID MGENI: Mheshimiwa Spika, baada ya kuwapongeza kwa heshima ya juu, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Makamu wa Rais - Dr. Ali Mohamed Shein na Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar - Amani Abeid Karume kwa ushindi wao mkubwa walioupata katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005, aidha, ninampongeza Waziri Mkuu - Mheshimiwa Edward Lowassa kwa kuteuliwa kwake na Mheshimiwa Rais na Bunge lako Tukufu kumpitisha kwa kishindo.

Mheshimiwa Spika, sina budi kukupongeza wewe binafsi kwa kuitishwa kwa kura za ushindi mkubwa kuwa Spika wa Bunge hili Tukufu. Kwa upendo mkubwa, ninawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushindi mkubwa katika Majimbo yao na wale wote waliobahatiwa kuwa Mawaziri.

Mheshimiwa Spika, sasa ninaomba kuchangia baadhi ya sehemu chache juu ya Wizara hii. Mchango wangu wa mwanzo unaanza kwenye Tamasha la Michezo linalofanyika kila mwaka kati ya Tanzania Bara na Zanzibar ambalo liliiasisiwa na Marehemu Mzee Abeid Amani Karume, Rais wa kwanza wa Zanzibar. Tamasha hili lengo lake kuu ni kuimarisha michezo, udugu na upendo kati ya nchi zetu mbili za Muungano. Tamasha hili hivi sasa limepoteza hadhi yake na kupungua ile ari yake, hivyo ninaiomba Serikali irejeshe hadhi na ari ile.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu kumomonyoka kwa maadili yetu. Kuna baadhi ya magazeti na vitabu vya Mitaani ambavyo vinachora picha mbaya zinazoharibu maadili yetu. Aidha, kuna baadhi ya vyombo vyetu vya *TV* ambavyo navyo vinaonyesha filamu chafu ambazo zinachangia sana kuvuruga utamaduni na silka zetu za kiafrika. Ninaishauri Serikali ni vyema kufuatilia na kuyarekebisha masuala hayo.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Sanaa Bagamoyo. Chuo hiki ninakipongeza na ninashauri kiimarishe na kikuzwe. Aidha, kiwe na uwezo wa kuelimisha vikundi vingine maadili na utamaduni wetu wa kiafrika ambaa unaendana na heshima, silka na utamaduni wetu halisi wa kiafrika.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba yangu na wananchi wa Jimbo langu la Bumbwini, tunaunga mkono hoja ya Wizara hii kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante.

MHE. KIUMBWA M. MBARAKA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuchangia Wizara hii. Namshukuru Waziri na Naibu Waziri na wafanyakazi wake wote wanaoendesha Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli habari ni kitu kikubwa sana katika nchi yetu na hivyo Wizara hii inatakiwa kupewa kipaumbele kwa sababu katika dunia ikiwa hakuna kitu hiki cha kutoa habari, nchi hiyo itakuwa ina upungufu katika maisha ya binadamu. Idara ya Habari inataka ipewe nyenzo kubwa sana na ipewe kipaumbele. Kuna wafanyakazi wengine hawajui maadili ya kazi zao kuipotosha Serikali kwa kutangaza yaliyokuwa sio na kutia matope Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba haya yanayotokea juu ya wafanyakazi yachukuliwe hatua za kisheria na wala wasifungiwe macho, ikiwa kosa linaruhusu kuonywa waonywe na ikiwa kuachishwa kazi basi waachishwe.

Mheshimiwa Spika, michezo ni tiba kwa binadam na michezo inapendwa sana na watu nchini iwe mpira au ngoma. Naomba Waziri azidi kuinua kiwango cha michezo kwa sababu vijana walio wengi wanapenda michezo sakini hawana nyenzo.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara ya Michezo iwaone watoto hawa wanaopenda michezo kwa kuwasaidia.

MHE. TATU M. NTIMIZI: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Michezo imekufa Vijijini kutokana na kutokuwa na Maafisa Michezo walioajiri Walimu

wa Michezo katika Shule hawapo pia. Sasa hivi Vijijini, Wabunge ndio wenye dhamana ya michezo. Uhamasishaji uwezeshe uanzishaji. Ikiwa Mbunge hana mwamko wa michezo, Jimbo hilo halina harakati za michezo. Je, Serikali inalionaje hilo na ni maandalizi yapi yatakayoonekana katika kuhamasisha michezo katika kipindi hiki cha Bajeti iliyowasilishwa? Naomba maelezo.

MHE. DUNSTAN D. MKAPA: Kwanza kabisa, napenda kutoa pongezi kwa Waziri mwenye dhamana ya Wizara hii kwa hotuba yake nzuri aliyoiwasilisha leo Bungeni, nami ninaiunga mkono kwa asilimia mia moja.

Pamoja na kuiunga mkono hoja hii, nina machache ya kuchangia yanayoweza kuisaidia Wizara kurekebisha baadhi ya maeneo ndani ya Wizara hii.

Uamuzi wa Serikai kurudisha michezo katika Shule za Msingi ni jambo la kupongezwa sana, kwani vipaji vingi vya watoto wetu vilikuwa vinapotea na/au kutojitekeza kutokana na kupigwa marufuku michezo mashuleni.

Hata hivyo, kuna mengi ambayo Serikali inatakiwa kufanya ili kuboresha michezo mashuleni nayo ni kuzipatia Shule vifaa vya michezo kama jezi, mipira na vifaa vya riadha, kuelekeza Shule zote ziwe na viwanja vya michezo vyenye viwango vizuri, kuwepo na Walimu wa michezo katika kila Shule, Serikali iendeleze na kuboresha michezo ya UMISHUMTA na UMISETA. Je, Wizara ina mkakati gani wa kuendeleza michezo mashuleni?

Mheshimiwa Spika, mpira wa miguu ni moja ya michezo ambayo hupendwa sana hapa nchini, lakini kiwango chake kinashuka siku hadi siku kutokana na Serikali kuacha kuweka raslimali nyingi katika mchezo huu wa mpira, migogoro ya muda mrefu na isiyokwisha ndani ya Klabu zetu na hasa Yanga na Simba. Kutokuwa na programu nzuri kuhusu mchezo huu katika ngazi zote na hata *TFF* yenye.

Hivyo, ninaiomba Wizara hii inieleze itayakabilije mambo hayo hapo juu? Vile vile, kuna vipaji vingi huko Vijijini katika mchezo huu wa mpira wa miguu. Kwa mfano, katika Jimbo langu la Uchaguzi la Nanyumbu kuna vijana wengi wenye vipaji, lakini vipaji vyao vinaishia huko huko Vijijini. Kwa kuwa Wilaya hii ni mpya: Je, Wizara hii itatusaidiaje Wana-Nanyumbu kuwaendeleza vijana hawa?

Mheshimiwa Spika, Utamaduni, hapa Tanzania tumejaliwa kuwa na makabila mengi yenye hazina ya tamaduni nyingi sana. Lakini bado kuna tamaduni nyingi katika fani ya ngoma ambazo hazijaibuliwa kutoka huko Vijijini. Ngoma tunazoziona hasa katika kumbi zetu na wakati wa mapokezi ya wageni wa Kitaifa ni chache sana ikilinganishwa na hazina tulionayo.

Ninaomba Idara ya Utamaduni na Idara ya *TUT* itembelee Vijijini ipate kuibua ngoma nyingine ambazo hazipo kwenye Maktaba yake. Kwa mfano, Jimboni kwangu Nanyumbu kuna ngoma pale Maswela, Namasogo na Mpawahia kwa mfano ambazo

napendekeza ziwekwe kwenye Maktaba. Naomba wahusika wa Idara hizi waje Wilayani Nanyumbu warekodi ngoma kutoka maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ningependa kutoa ushauri kuwa ndani ya Wizara hii kuna baadhi ya Maofisa ambao wamekaa sana katika Vituo vyao kwa muda mrefu na wamekuwa ni chanzo cha migogoro hasa hapo Dar es Salaam. Uhamisho kama Wizara inaweza, nomba ifanye *re-shuffle* ya watumishi wa Idara ya Michezo hapo Wizarani na wa Mkoa wa Dar es Salaam wapelekwe Mikoa mingine. Hii itasaidia sana kupunguza migogoro ya soka Mkoani Dar es Salaam, kwani kuna wakati wanakuwa na maamuzi yanayochochea zaidi migogoro hasa kwa Klabu za Yanga na Simba.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Spika, suala la kuimarisha mchezo na utamaduni wa Watanzania ni muhimu sana hili lihamie kwenye ngazi ya chini kabisa ya watoto wadogo. Pamoja na michezo kuhimizwa kwa kasi mashulenii, pia watoto hao wapatiwe maeneo ya kutosha kufanyia mazoezi pindi wanapokuwa nyumbani.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali itoe kauli leo kwamba inachukua hatua gani za kisheria kwa watu/kampuni walioingilia au waliovamia viwanja vya michezo vya watoto na kujenga makazi maeneo mbalimbali ya nchi hii?

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali baada ya kutoa kauli hiyo iweke sheria itakayolinda maeneo haya ya michezo kwa vijana wetu na hivyo kuenzi michezo Tanzania.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni wasanii wa muziki wanaovaa kinyume cha maadili ya Watanzania. Msanii anatakiwa kuwa kioo cha jamii na sio vikwazo kwa jamii. Wakati mwingine Wizara inatakiwa kuingilia kati pale inapoona maadili yanamomonyoka.

Mheshimiwa Spika, kitendo cha baadhi ya wasanii kuvala nusu uchi akaenda jukwaani kutumbukiza kwenye ukumbi wa watu wa rika mbalimbali vinatakiwa kupigwa vita na kila mtu. Jamii yetu inaheshimika kwa uvaaji wenye nidhamu. Suala hili lisiachwe huru kwa kusema kwamba suala la uvaaji kwa wasanii ni huria! Hatutafika. Tutajikuta tunaharibu watoto wetu badala ya kuwajenga. Serikali iweke sheria itakayodhibiti uvaaji wa wasanii wanapokuwa kwenye kumbi mbalimbali wanapokuwa wanaburudisha/wanatumbuiza.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine ni kukosekana kwa uongozi imara wenye uzalendo wa kuimarisha/kudumisha michezo hapa nchini ndani ya Shirikisho la Vyama vya Michezo Tanzania. *FIFA – TFF* mara zote viongozi wanaoingia kwenye ngazi ya juu ya Shirikisho hilo wamekuwa ni watu wa kuvuna tu kile kilichoko na bila kuendeleza chochote na hatima yake sasa wanamichezo wanakatishwa tamaa na uongozi huo na wengine kuachana na kazi ya michezo na kujishughulisha na masuala mengine. Viongozi hawa wanapelekea kuua soka hapa nchini kwa sababu ya tamaa, ulafi na ubin afsi wao.

Mheshimiwa Spika, ni wakati muafaka sasa Serikali kuliangalia hili kwa upekee. Chombo hiki ni muhimu kilete maslahi kwa Taifa hili na sio kukatisha tamaa wachezaji na mashabiki.

MHE. ALI HAJI ALI: Mheshimiwa Spika, kwanza nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Manaibu, Katibu Mkuu na Watendaji wote na wanamichezo wa aina zote Tanzania.

Pili, kuhusu utamaduni, nina furaha sana kwa kuwepo Sera ya Utamaduni na kutekelezwa na hotuba ya Waziri imejieleza kwa dhima na mipango mbalimbali. Lugha, sanaa zote, mila michezo ni maeneo ambayo yanatekelezwa kwa kiasi. Kwa maoni yangu, historia haikupewa nafasi inayostahiki. Ombi langu, historia ipewe nafasi yake ili iimarishe uzalendo, umoja na utaifa. Hivyo, *Curriculum* (mitaala) na *syllabus* (mihutasari) shulenii litazamwe ili kukidhi jambo hili.

Tatu, ni kuhusu lugha. Nashauri Mabaraza yaendeleze lugha ya asili ili kuimarishe utamaduni wetu. Ombi langu, maneno mapya ya lugha ya Kiswahili yatoholewe badala ya kubuni. Tutaepukana na kutumia maneno kama vile kifiriro, kwa maana ya kichongeo cha kalamu. Kwa vile Kiswahili kinatarajiwa kuwa lugha ya Afrika, bado sio lugha ya kufundishia hapa nchini. Kiswahili kitawezaje kuwa lugha ya Afrika? Kiingereza kinatumika duniani pamoja na sababu nyingine ni lugha inayotumika Vyoni.

Nne, kuhusu michezo, naipongeza Wizara hii kuandaa sera ya michezo. Lakini Sera ya Michezo imetilia maanani zaidi michezo ya kigeni. Michezo ya asili inafunza jamii tabia njema, ushujaa, utu, heshima na maadili kadhaa. Ombi langu ni kwamba, michezo ya asili ipewe nafasi katika sera.

MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR: Mheshimiwa Spika, kuhusu michezo, naomba Mheshimiwa Waziri katika taarifa yake ya leo anipe ufanuzi wa mambo yafuatayo kwa ajili ya kuboresha michezo. Ligi ya Muungano ni bora tuirudishe, inaleta uhusiano mzuri zaidi kama ligi ile ya Muungano Mufindi, inaleta ushirikiano mzuri. Kuhusu Pasaka, michezo ya Pasaka inaleta uhusiano mzuri.

Kuhusu ruzuku katika viwanja vya mpira ili kuvifanyia ukarabati vina hali ngumu ingawa ni vya CCM. Lakini vinatumwa na wananchi katika shughuli mbalimbali.

Kuhusu michezo ya Jeshini. Ipo haja ya michezo kuangaliwa upya uraiani tuhamasishe zaidi wananchi kufufua michezo uraiani kwa kuacha migogoro na ubadhirusi. Naipongeza sana timu ya majeshi kwa kuimarishe michezo. Kuhusu utenzi wa *Taifa Star* kuwepo na jopo la wataalamu asiwe mtu mmoja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Kiswahili, misemo, misimu, nahau na vitendawili ni viwamba jengo vya lugha na kuipa utamu lugha hiyo. Lakini maneno yaliyofanyiwa utafiti na kutumika ni 66. Ni machache, ipo haja kuongeza juhudhi na utafiti wa maneno

mengi zaidi. Kiswahili ni lugha ya Taifa na rasmi Tanzania, lakini kwa nini haipo kisheria katika matumizi wala haipo Kikatiba? Naomba tuweke msisitizo wa jambo hilo.

MHE. AGGREY D. J. MWANRI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Siha, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, kwa hotuba nzuri na yenye uchambuzi wa kina ambayo ameitoa asubuhi hii. Naamini kuwa hotuba hii itatumika kama dira ambayo itatoa changamoto kubwa kwa jamii na maendeleo kwa ujumla. Naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, kipekee ningependa kuishauri Serikali ihakikishe kuwa filamu na picha ambazo zinaonyesha masuala ya ngono katika *TV* yaonyeshwe/zionyeshwe baada ya saa nne usiku ili tusije tukawaharibu watoto wetu na utamaduni wa nje ambao ni kinyume kabisa na maadili na mwenendo wa nchi yetu ya Tanzania na Afrika kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, katika nchi zilizoendelea za Ulaya na hata Marekani, picha zenyе masuala ya ngono ni kwa ajili ya watu wazima na sio watoto wadogo ambao wanatakiwa watumie muda wao mwangi kwa ajili ya masomo ya Shuleni ili waweze kujijengea maisha yao ya baadaye. Wao wanaonyesha picha za aina hiyo baada ya watoto kulala. Sisi huku kwetu watoto wanaona picha za aina hiyo wakati wazazi wao wapo kazini. Nitashukuru kama ushauri huu utazingatiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena, natamka kwamba naunga mkono hoja.

MHE. VUAI ABDALLAH KHAMIS: Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Awamu ya Nne ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Sina budi kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib kwa kuisimamia vyema Wizara hii na kwa hotuba aliowasilisha Bungeni.

Mheshimiwa Spika, Sera ya Habari na Utangazaji ina majukumu makubwa kuweka mazingira yatakayowezesha Sekta ya Habari, kutoa huduma kwa kuzingatia maadili ya taaluma kwa nchi yetu, kwani maadili yasigeuke na tabia nzuri ya Serikali kupitia Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, Vyombo vya Habari Radio, *TV*, magazeti, Majarida na kadhalika vyote kwa pamoja vijali maadili na utamaduni wa Tanzania na Wizara iwe kama msimamizi, yasikiukwe maadili na mila zetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utamaduni wa mavazi, Tanzania kila mtu ana uhuru wake ilimradi asivunje sheria. Kwa hiyo, wananchi au watu wengi wanavaa nguo zao wanavyotaka, lakini mavazi mengine hayana utamaduni mzuri kwa Tanzania yetu. Kwa hiyo, Serikali kupitia Wizara hii iwe inatoa mafunzo kwa wale waliokuwa wanakiuka maadili na mila na utamaduni nzuri.

Mheshimiwa Spika, Waandishi wa Habari wanapokuwa wakitafuta habari, watafute habari sahihi sio habari za kufitinisha au za kutatanisha, wawe wakweli.

Mheshimiwa Spika, kuhusu michezo yetu Tanzania, bado tuko nyuma kimichezo. Naiomba Serikali itoe uwezo na pia kuhamasisha vijana kwa Semina na mafunzo washiriki michezo mbalimbali ili kupata uwezo na afya bora na Tanzania iwe mbele kimichezo.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu, nami naunga mkono hoja.

MHE. MUSSA AZAN ZUNGU: Mheshimiwa Spika, moja, naipongeza Serikali kwa kuleta kocha wa mpira wa miguu hapa nchini. Hofu yangu *TFF* pamoja na wadau wa soka kutompa fursa na ushirikiano kwa sababu ya maslahi binafsi. Tunaomba Serikali ilitazame suala hili kwa makini.

Mheshimiwa Spika, pili, kwa sasa umeibuka mtindo wa magazeti kutumika kwa uzushi na uongo dhidi ya wafanyabiashara, wanaoshindana kibiashara nchini na kupeleka hisia mbaya kwa wananchi. Serikali inachukua hatua zifi kudhibiti hali hii na kuyafanya magazeti yawe na *ethics* za uandishi?

Mheshimiwa Spika, tatu, malalamiko mengi ya wanataluma ya Uandishi kuwa wananyimwa haki ya maslahi na waajiri wao, mishahara huchelewa na wengine hunyimwa mishahara: Serikali itawalinda vipi wanataluma hawa wa Uandishi?

MHE. OMAR ALI MZEE: Mheshimiwa Spika, michezo ni afya, furaha na maelewano baina ya jamii, kikundi na kikundi na nchi na nchi. Tanzania ni nchi kubwa yenye watu wengi na wenyewe ni wapenda michezo.

Mheshimiwa Spika, viwanja vyta michezo hapa Tanzania havina hadhi ya Kitaifa, mionganoni mwake ni chakavu na majengo yake hayaridhishi. Kwa hiyo, ningeiomba Serikali kupitia Wizara hii kuviboresha viwanja vyetu kwa kukidhi haja ya kuwa na viwanja vyta Kimataifa ili viweze kutuingizia tija.

Mheshimiwa Spika, tukitaka tuendelee katika michezo, hatuna budi kuongeza ushindani katika michezo, kwani kwa kufanya hivyo kutaibua vipaji vyta wanamichezo, aina ya michezo na hata ushiriki wetu na nchi nyingine katika michezo kwa madhumuni ya kuwa washindani na sio wasindikizaji katika michezo.

Mheshimiwa Spika, kuimarisha mafunzo ya michezo ni jambo la msingi. Naipongeza Serikali kwa kumleta Mocha kwa ajili ya kufundisha timu ya Taifa. Hapa isiwe mwisho kwa kuwa tuna michezo mingi na yote inahitaji kupatiwa mafunzo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ajira katika michezo, ni jambo la msingi kwa watu watakaoonesha ufanisi mzuri, wanahitaji kupata ajira na kuwa vivutio kwa watu wengine nao waweze kuiga na kupunguza tatizo la ajira kwa watu wetu.

Mheshimiwa Spika, Timu ya Taifa ni kioo cha jamii katika nchi yetu. Kwa hiyo, inahitaji huduma bora zaidi ili kupata ufanisi ili iweze kutuletea ushindi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Tanzania kuna wasanii wengi wenye vipaji, kwa hiyo, wasanii wanahitaji kusaidiwa na kulindwa, pamoja na kutunzwa. Ahsante.

MHE. MGENI JADI KADIKA: Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuwa na afya njema na kuweza kuchangia hotuba ya Wizara hii ya Habari, Utamaduni na Michezo.

Mheshimiwa Spika, nakupongeza wewe pamoja na Naibu Spika na Wenyeviti kwa ufanisi na umahiri mkubwa. Nampongeza Waziri na Manaibu Waziri pamoja na Watendaji wake na wale wote walioshirikiana nao kwa kuandaa hotuba ya Bajeti hii. Naipongeza Kamati ya Wizara hii pamoja na Mwenyekiti wake kwa kazi nzuri ya kuweza kuikamilisha Bajeti kwa uchambuzi mzuri sana.

Mheshimiwa Spika, Sera ya Habari ni kuwa na Taifa lenye Vyombo vya Habari vingi vinavyozingatia sheria na maadili ya taaluma na ya jamii, kushirikiana kikamilifu na wananchi ili waweze kupata habari sahihi.

Mheshimiwa Spika, kuna masikitiko makubwa kuwa, kuna baadhi ya Vyombo vya Habari vinapotosha ukweli na kutoa habari za upotoshaji zisizokuwa na ukweli ndani yake na kusababisha mfarakano ndani ya jamii, kazini au nchi na nchi vyombo hivyo ni kama magazeti au *Radio, TV* na kadhalika.

Kwa hiyo, kwa kuititia Wizara hii, Serikali ikibaini vyombo hivyo vinakwenda kinyume na maadili hayo inachukua hatua gani? Kwa sababu kuna magazeti, hufungiwa na mengine hulipa fidia, lakini bado wanaendelea. Kwa hiyo, kuna kupewa adhabu zaidi ili wakome. Sheria hii iliyopo inahitaji kufanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Spika, tunaamini kuwa michezo ni afya ya binadamu, na ni burudani ya kukosha nyoyo za binadamu ili awe na furaha na uchangamfu na kuleta ukakamavu, kama mazoezi ya viungo, mpira wa miguu au mpira wa *Netball*, mpira wa vikapu na kadhalika. Kwanza, kuhusu michezo, Serikali itoe kipaumbele mashulenii ili watoto wetu wawe na afya bora na wawe wakakamavu, wafanye mashindano ndani ya Shule na nje ya Shule, kama mpira na ngoma za asili.

Vilevile, watoto wetu wapatiwe viwanja vizuri kwa kuendeleza michezo na Vijijini. Tunao watoto wengi wenye vipaji, lakini hawajulikani kwa sababu bado Wizara hii haijaipa michezo bora. Kwa hiyo, Wizara itafute wataalam wa michezo baina ya Mikoa na Mikoa au Wilaya kwa Wilaya au Kata kwa Kata, hapa watapata hao wenye vipaji hivyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utamaduni, kila nchi ina utamaduni wake na lugha yake. Kwa hiyo, Serikali ifanye kadri iwezavyo kuipa kipaumbele lugha yetu ya Kiswahili. Vilevile, ngoma zetu za asili tuziimarishe ili tuwe na ngoma maalum ya utamaduni wa nchi yetu. Mfano kama Zanzibar, Pemba kuna ngoma maalum kama ngoma ya Msewe.

Mheshimiwa Spika, naiombea kila la kheri Wizara hii.

MHE. SAID AMOUR ARFI: Mheshimiwa Spika, napenda kuchuku nafasi hii kuwapongeza Waziri, Naibu Mawaziri na Watendaji wa Wizara ambayo inasimamia utamaduni wetu.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nijielekeze katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni suala la utangazaji. Kwa masikitiko makubwa pamoja najitahada zote ambazo zimefanyika katika kuboresha matangazo ya *Radio Tanzania* kwa kujenga vituo Kigoma na Mbeya, bado matangazo ya *Radio Tanzania* hayasikiki vizuri katika maeneo mengi ya Mkao wa Rukwa na hususan Mpanda Mjini na hivyo wananchi wengi wanapata taarifa na matangazo mbalimbali kupitia vituo vingine vya *Radio* kama *RFA* ambayo inasikika vizuri karibu katika nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwashauri Watangazaji wetu katika matumizi sahihi ya lugha ya matamshi. Inakera sana inapokuwa mtangazaji hawezi kujua tofauti ya “la” na “ra” kama “Tabora” na “Tabola” au “kulala” na “kurara”, inatia kichefuchefu.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ni Baraza la Sanaa la Taifa na Bodi ya Filamu ambayo yote yapo kwa mujibu wa Sheria za nchi hii. Inakuwaje sasa wanashindwa kusimamia na kutekeleza wajibu wake na kuchukua hatua inapobidi? Wewe angalia sanaa zetu na filamu zinazoonyeshwa kwenye Luninga, ni mwendelezo wa kubomoa maadili na utamaduni wetu. Wizara inapaswa sasa kusimamia kwa karibu sana utendaji kazi wa vyombo hivi ili kunusuru vizazi vyetu kuangamia katika tamaduni ngeni kupitia sanaa na filamu.

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu ni michezo. Awali, ningependa kufahamu tunaelekewa wapi katika michezo wa mpira wa miguu? Ni michezo bado wa ridhaa au wa kulipwa? Tupo wapi na tunakwenda wapi? Ni lazima kwanza tujitambue ndipo tunaweza kutoa maelekezo sahihi kwa mustakabali wa michezo huu unaopendwa sana nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa maoni yangu kama Taifa ni lazima tujue michezo gani ni ya wanaume na ipi ya wanawake. Sio lazima kwetu kuiga kila kitu kinachofanywa na

wengine. Kwa mfano, mpira wa miguu ni mchezo wa wananume na mpira wa pete (*Netball*) ni kwa wanawake. Sasa inashangaza sama tunawekeza pesa nyingi, muda na mambo kadha wa kadha kwa ajili ya mpira wa miguu kwa wanawake badala ya *netball* ambayo sasa hata kusikika haisikiki tena kama ilivyokuwa hapo zamani. Sikatai mabadiliko, lakini kwa nini mpira wa pete hakuna jitihada za kuuendeleza? Sio *netball* tu, michezo yote ya jadi haipewi kipaumbele kama mchezo wa Bao, Mieleka na mingineyo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, kadri ya mabadiliko ya dunia yanavyotokea kama Taifa ni lazima tuwe na maadili, utamaduni na lugha ambao Wizara hii ina dhamana ya kusimamia, hatuwezi kuendelea kuona vizazi vyetu vinapotoka kwa misingi tu ya uhuru. Ni lazima iwepo mipaka katika uhuru huo. Leo mabinti wetu wanatembea nusu uchi, tunasema ni uhuru. Uhuru gani unaotuondolea heshima na haiba kama Taifa? Watanzania leo wanavaa kizungu, wanaimba kizungu, wanacheza kizaire, utamaduni wetu upo wapi? Hii ni changamoto kwa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Nichukue fursa hii kuwapongeza Waandishi wa Habari katika mchango wao wa kufichua uozo na kuelimisha Umma wa Watanzania wasichoke kuandika hata kama wachache watakasirika. Ahsate sana.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa kuandaa hotuba nzuri ya Bajeti. Hata hivyo, nina mchango mdogo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Matumizi ya Lugha ya Kiswahili. Kwanza nalipongeza Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) kwa kuendelea kuwaelimisha Watanzania juu ya matumizi ya maelekezo ya Kiswahili.

Hata hivyo, pamoja na maelekezo mazuri ya BAKITA, bado Vyombo vya Habari na wananchi kwa ujumla wanapotosha matumizi sahihi ya maneno ya lugha hii ya Kiswahili. Kwa mfano neno “kupelekeea” kwa maana ya “kusababisha”. Je, neno kupelekeea ni sawa na kusababisha? Hivi ni kwa nini Wizara maneno ambayo hayaleti maana bado inayafumbia macho? Hii ni kinyume kabisa ya matumizi sahihi ya lugha hii nzuri Barani Afrika.

MHE. ADAM K. A. MALIMA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba nimpongeze kwa dhati kabisa Ndugu yangu, Kaka yangu, Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, kwa hotuba yake nzuri ambayo kweli kabisa ina mwelekeo wa utekelezaji wa malengo ya sera za Habari, Utamaduni na Michezo.

Mheshimiwa Spika, naomba niwapongeze sana Manaibu Waziri wa Wizara hii, Mheshimiwa Joel Bendera, Mbunge na Kocha wa Timu yetu ya Wabunge na pia Mheshimiwa Dr. Emmanuel Nchimbi, ambao wote kwa pamoja wamejidhihirisha hapa katika Bunge lako na huko nje wakiwa wanatekeleza majukumu yao kuwa ni viongozi wazuri sana, tena sana.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme yafuatayo kuhusu Sekta ya Habari:-

Mheshimiwa Spika, Tanzania imepiga hatua kubwa sana katika maendeleo ya Sekta hii katika sehemu zote *TV, Radio, Magazeti* katika kipindi kifupi sana. Pia, naamini kuwa Vyombo vya Habari vinafanya kazi katika mazingira mazuri yanayowaruhusu kutekeleza majukumu yao kwa uhuru bila kubughudhiwa na Mamlaka.

Lakini pia lazima tukubali kwamba uhuru wa kutoa habari una mipaka. Una viwango! Huwezi kwa sababu ya kumiliki Vyombo vya Habari ukatumia nafasi hiyo kwa ajili ya kudhalilisha Watanzania wenzako kwa kusema maneno ya uongo, au kwa kutoa habari zinazopotosha kwa makusudi. Utoaji wa habari ni huduma ya jamii.

Naomba maelekezo ya kina, Muswada wa Sheria wa Vyombo vya Habari uliotajwa na Mheshimiwa Waziri Ibara ya 19 ya hotuba yake itakuwa tayari, itakamilika lini?

Pia, naomba maelezo. Ni chombo gani cha kitaifa kinachohusika na usimamizi wa viwango vya utangazaji na habari kwa mfano katika baadhi ya Televisheni zetu, taarifa nyeti zenye umuhimu wa kitaifa za Rais, Waziri Mkuu, Bunge zinapewa dakika mbilimbili kila moja. Habari za mmiliki wa *TV* kwenda kwa watoto wa *Madrasa Msasani* ili kuendeleza ugomvi wake na Sheikh mmoja wa Msikiti wa Kariakoo peke yake unachukua dakika 10, za kipindi cha habari za kitaifa ambazo jumla zina dakika 20. Ni nani mhusika mkuu wa kusimamia viwango vya utangazaji?

Mheshimiwa Spika, naomba katika hayo nizungumzie suala la utamaduni. Naomba sana Serikali ya Awamu ya Nne iandae rasimu ambayo itachangiwa na Wabunge kuhusu ni nini utamaduni wa Mtanzania kwa tafsiri pana ya utamaduni. Serikali iingie gharama na kwa makusudi kabisa wasimamie mikakati ya kuwafanya Watanzania wao. Napenda kutambua mchango wa Chuo cha Sanaa, Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), BAKITA. Mfuko wa utamaduni una mchango gani na mipango gani katika kuchangia mikakati hii ya utambuka wa utamaduni wa Mtanzania?

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba niongezee mchango wangu kwenye suala la michezo. Michezo iko ya aina nyingi Tanzania. Tuna vipaji vya wanamichezo katika michezo mbalimbali. Naomba tufanye utafiti wa kitaifa ili tujue ni gharama gani na kutoka maeneo gani ambayo Serikali itafanya ili katika miaka ijayo ya karibu tuone mabadiliko yatakayosimamiwa na Baraza la Michezo (*BMT*).

Migogoro ya mpira wa miguu haswa katika vilabu vikubwa vinaleta sura mbaya sana. Naomba tupate maelezo ya Serikali, ni mikakati gani inayoleweka ya kupata ufumbuzi wa haraka? Mfano, kule Hispania migogoro ya Real Madrid na Barcelona huingiliwa kati moja kwa moja na Serikali kwa kutambua umuhimu wa klabu hizi kwa jamii na utulivu ndani ya jamii.

Mheshimiwa Spika, naomba nisisitize kwamba kuwe na uwekezaji unaokusudiwa wa kunyanya viwango vya michezo, kuanzia ngazi za kijana/watoto. Hii ni namna moja ya kumsaidia Kocha mpya wa Taifa wa kandanda kutekeleza kazi yale.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MARGARET AGNES MKANGA: Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri Muhammed Seif Khatib, Manaibu Waziri wake, Mheshimiwa Joel Bendera na Mheshimiwa Dr. Emmanuel John Nchimbi, Wakurugenzi na Watendaji wote wa Wizara kwa kuandaa hotuba nzuri inayotoa matumanini kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Wizara kwa kuwezesha watu wenye ulemavu kushiriki kikamilifu katika michezo yao huko Mbeya Machi, 2006. Hata hivyo, naomba sana utafiti ufanyike ili kuongeza aina ya michezo ambayo watu wenye ulemavu wanapaswa kujifunza na kushiriki. Pia, timu ya Taifa iwekwe Kambini mapema na mazoezi yasiwe ya Zimamoto na timu ihudumiwe vizuri ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa kuongeza aina ya michezo ambayo watu wenye ulemavu wanaweza kuicheza ni kwamba wahusika wataweza kufaidika na matumizi ya uwanja mpya wa michezo wa kisasa.

Mheshimiwa Spika, naomba usafanuzi toka kwa Waziri kuwa ni kwa kiasi gani Vyama vya Michezo vya watu wenye ulemavu licha ya kile cha *Special Olympic*, vinasaidiwa na Wizara, pamoja kwamba tumewahi kupata medali za michezo kutokana na juhudi za Vyama hivyo.

Mheshimiwa Spika, pia naunga mkono hoja iliyotolewa na Kamati ya Maendeleo ya Jamii kuhusu kuwa na wataalam wa michezo kwa watu wenye ulemavu. Uwepo wao utasaidia sana kuboresha michezo hiyo na kuwezesha timu zetu kushinda vizuri kutokana na ujuzi watakaoupata.

Msisitizo ni kwamba, timu itakayoshiriki mashindano ya Walemaru huko uchina iandaliwe vizuri na wadau wote wanaohusika.

Mheshimiwa Spika, baada ya haya, naunga mkono hoja.

MHE. HEMED MOHAMMED HEMED: Mheshimiwa Spika, nimwombe Mwenyezi Mungu anipe uwezo wa kuchangia katika Wizara hii ya Habari na Michezo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu haya, sasa naomba nianze kutoa mchango wangu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuanza, naanza na *RTD*, yaani *Radio Tanzania Dar es Salaam*. Hiki ni chaombo cha Taifa chenye majukumu mazito ya kuelimisha,

kuburudisha na kutaarifu Umma kuhusu masuala muhimu ya maendeleo na hali ya maisha ya kawaida ya wananchi.

Pia *RTD* inawaeleza na kuwahamasisha wananchi kuhusu mikakati ya maendeleo. Kutokana na majukumu haya, *RTD* ina mpangilio wa vipindi vyake kama ifuatavyo: Muziki, Elimu, Habari, Matangazo ya Vifo, Mahubiri ya Dini, Biashara, Wanawake na Watoto, Michezo na vipindi vingine.

Mheshimiwa Spika, mionganoni mwa vipindi hivi ni maeneo ya biashara kwa shida za Umma. Ni vyema basi Serikali ingekuwa wazi kulijulisha Bunge ni kiasi gani kinachopatikana kutokana ma matangazo ya malipo.

Mheshimiwa Spika, kwa mtazamo wangu, *RTD* ni chombo kinachoingizia kipato nchi yetu. Je, ni kiasi gani hicho?

Mheshimiwa Spika, sasa naomba niende kwenye michezo. Ufahamu wangu, michezo imegawika katika maeneo mawili. Michezo ya kugiza na Michezo ya Mipira (Mbio na kadhalika hii ni sehemu ya pili).

Kuhusu michezo ya kuigiza. Wizara inapaswa, mchezo kabla ya kurushwa hewani Wizara ingeutazama mchezo maadili yake. Kuna baadhi ya michezo maadili yake siyo mazuri, hivyo kwenda kinyume na maadili yetu ndani ya jamii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mchezo wa Mpira wa Miguu, kwa kuwa nchi yetu ni mionganoni mwa nchi zinazoendelea na kushiriki katika mchezo wa mpira duniani, ni vyema Serikali itafute mbinu nasi tushangilie badala ya kulia pale timu yetu inapofungwa.

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwani nchi yetu hatujapata ushindi katika mashindano ya Afrika ama mengineyo. Wizara sio suluhu kuleta mtaalamu au Kocha, zipo sababu. Wizra ndiyo mhusika mkuu. Mimi naona la kufanya ni kumuanza mwanamichezo tangu angali mdogo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia kuhusu nidhamu vilabuni. Ni wazi vilabu vyetu pamoja na kuwa Katiba zao ni nzuri, lakini hazireshimiwi. Viongozi wa vilabu huzitumia katiba kwa maslahi yao. Jambo ambalo mara nyingi hupelekeea vilabu vyetu kugombana. Mpasuko wa kilabu mara nyingi hukidhofisha kilabu, kwani hupelekeea maganyiko ama kwa viongozi ama wachezaji.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kujua kuwepo kwa umuhimu wa timu za mpira hapa nchini, sasa ikae na kupanga upya timu zetu.

Mheshimiwa Spika, kwa kujua hili, Katiba za Vilabu hazireshimiwi, ni vyema Serikali ingeandaa Katiba mama kwa timu zetu zote ili Vilabu viwe na mfumo kuitia Serikali yao.

Mheshimiwa Spika, sasa niulize maswali kwa Wizara. Wizara haioni kuna baadhi ya vipindi katika *TV* zinakwenda kinyume na mila na desturi ya nchi yetu? Wizara itafanya nini nasi Watanzania tupige hatua za mchezo wa mpira wa miguu?

Mwisho natoa pole kwa kifo cha Mwanamichezo wetu, aliyefariki katika mchezo wa ngumi. Pole hii iende kwa familia ya Marehemu, Wizara, Chama cha Ngumi nchini pamoja na Watanzania wote. Ahsante.

MHE. JUMA H. KILLIMBAH: Mheshimiwa Spika, nami nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Manaibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa maandalizi mazuri ya Bajeti ya mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, nami nichangie kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utendaji wa Vyombo vya Habari, maadili ya wanahabari hayafuatwi, Vyombo vya Habari sasa vimejaa upendeleo rushwa na uongo.

Katika hatua hii, Vyombo vingi vya Habari, aidha kwa makusudi vimekuwa vikipotosha ukweli, lakini hali halisi juu ya mambo mbalimbali yaliyo muhimu na hata kupelekea kuleta tafrani kwa jamii, tumejionea migogoro mingi kati ya wamiliki wa Vyombo vya Habari na jamii juu ya uzushi na pengine kwa madai ya rushwa ili habari fulani zitokee au zisikike.

Mheshimiwa Spika, nashauri kwamba ni muhimu sana Wizara ikaweka udhibiti mpya kwa sekta hii muhimu ya habari ambayo inayo jukumu kubwa katika kuelimisha jamii juu masuala mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mpira wa miguu unapendwa sana na ni pekee wenye mashabiki wengi nchini mwetu Tanzania, kimsingi Watanzania wanahitaji kuona timu zao ama timu ya Taifa inafanya vizuri.

Mheshimiwa Spika, tunamshukuru Rais wa Awamu ya Batu kwa kutimiza azma juu ya ujenzi wa uwanja wa kisasa wa mpira wa miguu ili sasa uwanja huu wa kisasa uendane na hadhi yake, basi ni lazima soka letu nalo libadilike liwe la kisasa.

Namshukuru Rais wa Awamu ya Nne, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kutuletea Kocha wa kisasa kutoka Brazil. Kocha huyu nashauri apewe mamlaka yote na asiingiliwe kiutendaji na pengine aruhusiwe kuibua vipaji kwa rika la chini kwa vijana wetu nao wakaandaliwe kwa ajili ya baadaye. Pengine kama upo ushauri, basi uwе kwa mapendekezo kutoka kwake na katika muda utakaofaa.

Tuenzi na kuendeleza utamaduni wa makabila kwa hatua ya Wizara, kuanzisha mashindano kwa kila mwaka ili makabila mbalimbali yakaonyeshe utamaduni wao ambao kwa sasa unaelekea kupotea.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. DR. BATILDA S. BURIAN: Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, Manaibu Waziri, Mheshimiwa Joel Bendera na Mheshimiwa Dr. Emmanuel Nchimbi pamoja na Katibu Mkuu Bibi Kijakazi Mtengwa na Watalaam wote wa Wizara kwa kazi nzuri sana hata kutayarisha Bajeti nzuri na yenyewe mwelekeo wa kimapinduzi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia katika maeneo machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sekta ya Habari, nashauri Wizara iwe na utaratibu wa kutoa mafunzo na Semina kwa wanahabari ili kujenga taaluma hii. Kwa kushirikiana na Chuo cha Dipolomasia, Wizara iwashirikishe wanahabari katika kongamano na semina zenye mwelekeo wa kutoa mafunzo kuhusu madhara ya taarifa chanya (*negative publicity*) kuhusu nchi yetu (ndani na nje) na jinsi inavyoweza kuathiri uchumi na hali ya kijamii, hivyo wanahabari wetu wahimizwe kujenga uzalendo.

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la kuendeleza Sanaa. Hotuba ya Waziri imenifurahisha kuona kuwa Wizara itashirikiana na TAMISEMI kufufua majumba ya Maendeleo Wilayani. Napenda niwakumbushe tu kuwa Majumba ya Maendeleo yapo chini ya Wizara yetu ya Maendeleo ya Jamii, Jinsi na Watoto. Hivyo basi, ili tuwe na mipango mizuri, Wizara hii ya Habari, Utamaduni na Michezo ishirikiane na Wizara yetu na TAMISEMI kuboresha na kujenga majumba hayo.

Mheshimiwa Spika, Serikali hii ni Serikali ya CCM na katika Ilani na mwelekeo wa CCM 200 – 2010 inaonyesha wazi kabisa mtazamo wa CCM kuhusu mavazi ya heshima. Hivyo, Wizara hii kama Wizara chini ya Serikali ya CCM, sidhani kama inaweza ikaenda au kusema kinyume na kile kinachosemwa na Chama Cha Mapinduzi. Hivyo, tunategemea Wizara itoe kauli na msisitizo juu ya mavazi ya heshima hasa kwa akina dada. Wizara yetu ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto iko yatari kushirikiana na Wizara hii ya Habari, Utamaduni na Michezo.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Wizara kwa kasi na ari mpya na kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kupata Kocha wa Taifa.

Pia, naomba vijana wetu waangaliwe ili wawe na lishe bora na hivyo kuweza kutekeleza mazoezi yao bila matatizo. Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Wizara ya Vijana kuendelea kuibua vipaji vyaa watoto na vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mchezo wa Kubahatisha, nchi nyingi duniani asilimia fulani ya pato la mchezo wa Bahati Nasibu ya Taifa kwa shughuli za Maendeleo ya Jamii. Hivyo basi, pamoja na asilimia fulani kutengwa kwa Maendeleo ya Michezo, tunaomba tupatiwe pia asilimia fulani kwa ajili ya kusaidia watoto yatima na wale wanaoishi katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Spika, naomba kumpongeza Waziri na Manaibu Waziri wote wawili kwa kuandaa hotuba nzuri bila kumsahau Katibu Mkuu wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia *TVT*. Kwanza tunashukuru hatimaye *TVT* inarusha moja kwa moja matangazo yake toka Bungeni.

Wananchi walikuwa wanajuliza, inakuwaje Televisheni ya Taifa ilikuwa hairushi *live* Mikutano na shughuli za Bunge? Ilifika wakati mpaka wakawa wanasema hii inashangaza, chombo cha nchi kinachoghamariwa na walipa kodi hakitoi moja kwa moja jinsi ya shughuli na kazi za kuzigawa kodi zao kwenda kufanyiwa kazi inavyofanyiwa.

Mheshimiwa Spika, sasa inarusha, naomba kuishauri Serikali kuwa kazi kubwa iliyio mbele yetu ni kuiimarisha *TVT* kwa kuipa uwezo wa vifaa, magari na nyenzo nyingine zitakazowezesha kuipa uwezo *TVT* wa kushirikiana kitaalam na Vituo vingine vya watu binafsi.

Mheshimiwa Spika, mimi kwa macho yangu, nimeshuhudia gari la *TVT* limetumwa kazi ya kufanya hapa Dodoma, lakini kufika njiani hapa Dodoma likagoma kwenda mbele na kutoka pale likawa linakwenda kinyumenyume. Sababu *gear* za kuongoza mbele ziligoma. Hii inaonyesha jinsi gani walivyo na uhaba wa vyombo vya utendaji au vimechoka.

Mheshimiwa Spika, ili kuwa na utendaji mzuri wenyewe ufanisi kwa chombo hiki, *TVT* haina vifaa vya kutendea kazi. Naomba ipewe kipaumbele, mimi sidhani kama wana *camera* za kutosha ili *Crew Team* wanapotawanyika kwenda sehemu mbalimbali kufanya kazi. Kama hawana za kutosha, naishauri Serikali iwaongeze ili wafanye kazi zao kwa mapana zaidi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kukupongeza kwa hotuba yako nzuri yenye usafanuzi mzuri kuhusu sekta za habari, utamaduni na michezo. Pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100. Pamoja na kuunga mkono hoja hii, naomba kuchangia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, nawapongeza Manaibu Waziri kwa kuwa Sekta ya Habari ni muhimu kwa nchi yetu na kwa kuwa wafanyakazi wa vyombo vya habari vya *TVT*, *Radio Tanzania* Idara ya Maelezo, wamefanya kazi katika mazingira magumu sana ya ufinyu wa Bajeti, maslahi duni, ukosefu wa vitendea kazi kwa ajili ya kukusanya habari Mijini na Vijijini, ukosefu wa nyumba za kuishi na kadhalika: Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha hali hiyo?

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia vitendea kazi kama vile kuboresha hali ya usafiri kwa wafanyakazi wa *Radio Tanzania* Kanda ya Kati Dodoma, kuboresha

makazi yao na kuwekea mitambo ya kisasa ili *Radio Tanzania* Kanda ya Kati Dodoma iweze kusikika eneo kubwa la nchi yetu. Usikivu wa *Radio Tanzania* nchi nzima ni muhimu sana kwa ajili ya maendeleo na uchumi wa nchi yetu. Je, Serikali itakubaliana nami kwamba ipo haja ya kuboresha iweze kusikika vizuri nchi nzima? Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka Maafisa Habari Wilaya zote hapa nchini ili kuandika habari za maendeleo na uchumi?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Watanzania wengi wanapenda michezo na hasa mpira wa miguu, lakini mchezo huu unakabiliwa na matatizo makubwa ya uongozi kwenye vilabu vya mpira na matatizo hayo yanababisha kushuka kwa mchezo huo hapa nchini, uongozi mbovu ndani ya Vilabu ubovu wa Viwanja vya Michezo Wilayani, Mikoani vinahitaji ukarabati mkubwa, kutatua migogoro ndani ya Vyama vyote vya michezo *football, netball, handball, basket ball* na kadhalika. Viongozi wasing'ang'anie madaraka baada ya muda wao kumalizika. Hii itasaidia kuboresha hali ya michezo nchini.

Ni muhimu kutafuta makocha wazuri wenyewe uwezo wa kitaaluma kufundisha timu zetu ili ziweze kufanya vizuri mashindano ya kitaifa na hasa timu zetu kubwa za Simba na Yanga. Naipongeza timu ya Mji Mpwapwa ambayo ilishiriki ligi kuu ya *Vodacom* Tanzania Bara miaka tisa (9) mfululizo na kuamua kujitoa mwaka 2005 kutokana na matatizo ya kifedha, nashauri Serikali itenye fedha kama ruzuku kusaidia vilabu vya mpira. Hii itasaidia kuboresha hali ya michezo hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sekta ya Utamaduni, Chuo cha Sanaa cha Bagamoyo ni muhimu sana katika kuendeleza mafunzo ya sanaa mbalimbali hapa nchini. Je, ni sanaa za aina gani zinafundishwa katika Chuo hicho? Je, Serikali ina mpango gani kukiboresha Chuo hicho ili kiweze kutoa mafunzo bora zaidi ya sanaa na ya kimataifa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

MHE. RUTH B. MSAFIRI: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naunga mkono hoja. Naishauri Serikali kuendelea kuimarisha mkakati wa kuiwezesha nchi yetu kung'ara katika michezo ya kitaifa na kimataifa hasa soka, riadha, masumbwi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ili nchi yetu ing'are, maandalizi ya mapema ni lazima. Vipaji vya mwanadamu huanza kujitokeza mapema kabisa anapokuwa angali mtoto.

Vile vile, mwanadamu anaweza kuhamisishwa na akaweza kujenga kipaji/*talent* akiwa mtoto bado. Kwa msingi huo, michezo yetu ianze kupimwa tangu Shule za chekechea/awali. Hii itasaidia watoto kufahamu na kupenda vipaji vyao. Naomba utaratibu huu uendelezwe toka Shule za Awali, Msingi, Sekondari hadi Vyuoni.

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika, michezo na vipaji visiishie pale mtu anapotoka katika mazingira rasimi tu. Vipaji viendelezwe hata Vijijini na Mijini ambako

wananchi wanaishi maisha ya kawaida. Nashauri pia uchujaji wa picha zinazoonyeshwa kwenye luninga. Baadhi ya picha za luninga, zinavunja maadili ya nchi.

Mheshimiwa Spika, mabango yanayotundikwa kwa matangazo ya biashara pia yaangaliwe na yapitishwe na mamlaka husika kabla ya kutundikwa. Mathalani picha zenye tangazo la *tigo*, yenye msichana aliyefinya jicho moja na kuacha mdomo wazi kwa kutangaza *tigo* na upunguzaji wa gharama za mtandao wa *tigo*, ni la kufedhehesha jinsia ya kike na hasa wasichana wadogo. Hivi ukitaka kupunguza gharama za mtandao, kweli picha ya msichana ya namna ile ndiyo pekee inayofaa? Nashauri tangazo hilo libadilishwe mara moja na lisirudiwe.

Nashauri utaratibu wa Waheshimiwa Wabunge kushiriki katika mazoezi na mbio za kilometra tano kwa kushindanishwa na zawadi, uendelee na ikibidi uboreshwwe zaidi. Kipindi kilichopita tulishindana na Wakenya na kuweka kambi Dodoma na Arusha. Nashauri utaratibu huu uendelee, tucheze na timu za Mabunge ya Afrika Mashariki na hata Rwanda na Burundi. Inaimarisha afya, pia ni burudani. Bunge lilishindana pia na Mabalozi, ilitia changamoto, iendelezwe. Aidha, nawapongeza *Cargo Stars* kwa kuifadhibili Bunge *Sports Clubs* kwa mfululizo wa miaka sita nilipokuwa hapa Bungeni. Nawapongeza sana na wasituchoke.

Mheshimiwa Spika, nashauri pia vifaa vya michezo viwe katika maduka maalum, viwe na viwango vizuri na gharama nafuu. Naiomba Serikali iondoe ushuru katika vifaa vya michezo ili viwe na bei nafuu na vinunuliwe na wahitaji wengi.

Mheshimiwa Spika, naishauri pia Serikali iwasomeshe watalaam wa michezo ili michezo iendeshwe kiutaalam. Michezo isiendeshwe kwa kujuana/kufahamiana/upendeleo, bali kwa uwezo na vigezo vya michezo husika, kuzingatiwa. Watalaam wanatakiwa katika fani ya michezo.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha kwa heshima zote.

MHE. SAVELINA SLIVANUS MWIJAGE: Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake. Mimi naomba nichangie sehemu ya viwanja ambavyo ni vya Mikoa kwa kutokuwa na hadhi.

Mheshimiwa Spika, kama viwanja vya Mikoa, ni aibu kubwa timu kutoka Mikoa mingi na nchi za jirani kwa mfano kama viwanja viwili Huru na Kaitaba, hivi viwanja vimekuwa vikilalamikiwa muda mrefu. Angalau kimoja kama Kaitaba ni sehemu nyingi ambazo kuna viwanja wananchi wanakua na maduka yao wanaendelea kufanyia biashara.

Naomba leo njue kwa nini Kaitaba wananchi wengi walikuwa wamejenga vibanda vyao wanafanya maonyesho na kujipatia kipato chao na kipindi hicho wananchi hawa wanajipatia kipato kizuri kwa kila mwenye biashara yake.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali ina mikakati gani? Naomba nipate jibu. Je, kwa nini Serikali isiboreshe kile kiwanja cha Huru kilichoko katikati ya Mji? Kiwanja hicho

kiko katikati ya Mji, kimechakaa sana na wale wananchi waliosimamishwa waelezwe kuhusu vibanda vyao kwa kutovitumia kuwazalishia kipato.

Mheshimiwa Spika, huu ni unyanyasaji na ni kukosesha Mkoa mzima kiwanja chenye kulingana na Manispaa yake. Naomba jibu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

MHE. MASOLWA C. MASOLWA: Mheshimiwa Spika, niwapongeze Waheshimiwa wote wawili pamoja na Watendaji wao wote kwa kufanikisha matayarisho yote muhimu ya Bajeti hii. Ninaomba nichangie katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza Sekta ya Habari. Vyombo nya Habari hususan waandishi wetu na mara nyingine watangazaji wetu kwenye vyombo mbalimbali nya habari *radio, TV*, na kadhalika vinatumia vibaya lugha ya Kiswahili kwa maana ya kuwa maneno wanayoyatumia huwa siyo sahihi. Kwa mfano, “limebaki saa moja,” “watu nane” na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Kiswahili ni lugha mojawapo ambayo imekubalika kutumika kitaifa, Wizara ya Habari haina budi kusimamia matumizi ya maneno sahihi ya lugha hii ya kimataifa.

Pili, Sekta ya Michezo, pamoja na juhudzi za makusudi zinazochukuliwa na Serikali za kuinua viwango nya michezo katika nchi yetu ikiwa ni pamoja na kuleta makocha wa kigeni wa kuzifundisha timu zetu hasa zile za mpira wa miguu, lakini bado kutaendelea kuwa na matatizo ya kutopanda kwa kiwango hasa kile cha mpira wa miguu hapa nchini kwa sababu zifuatazo:-

- (a) Mishahara/posho wanazolipwa/pesa wachezaji wetu haitoshelezi au haikidhi mahitaji yao, hivyo kuwafanya wasijitume kutokana na udhaifu wa afya zao;
- (b) Wachezaji wetu, hasa wanaochaguliwa kuliwakilisha Taifa letu katika michezo wa mpira wa miguu wengi wao hawana uzalendo; na
- (c) Nidhamu kwa wachezaji wetu imeshuka sana ukilinganisha na miaka ya 1970. Mfano wachezaji huwa hawahudhurii kwenye kambi za mazoezi kwa muda uliopangwa na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ili kuinua kiwango hasa cha michezo wa mpira wa miguu, mishahara au posho la wachezaji wetu ni lazima ziangaliwe upya. Endapo wachezaji wetu watalipwa au kupewa angalau posho ya Sh. 300,000/= tu kwa kila juma, kwa kuanzia nina imani kuwa wachezaji wetu watakuwa na ari pamoja na ushindani wa kuwania nafasi ya kucheza kwenye timu ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mikakati ya Wizara na ushauri wangu nilioainisha hapo juu, endapo utatekelezwa, nina imani kuwa soko letu la Tanzania litapanda.

Tatu, sekta ya sanaa, muziki wa kizazi kipywa Tanzania umepanda chati katika Afrika ya Mashariki, vijana wengi wameunganisha vikundi vyao vya muziki kwa kujajiri wenye. Makundi hayo ya wasanii yamekuwa hayanufaiki na matunda ya usanii wao kutokana na watu wajanja kujinufaisha na sanaa zao.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Wizara iwadhibiti wale wanaojinufaisha na sanaa za wasanii wetu kwa kuwachukulia hatua kali za kisheria kama zipo na kama hazipo, Wizara itayariske Muswada wa Sheria hizo za kuwalinda wanasanaa wetu na kuziwasilisha Bungeni kwa kupidishwa.

Mheshimiwa Spika, mwisho ninaipongeza sana Serikali kwa kutafuta muhisani wa kujenga uwanja wa kisasa wa mpira wa miguu huko Dar es Saalam. Uwanja huo na uwe wa faraja kwa timu zetu na ninaunga mkono hoja hii.

MHE. FELIX N. KIJKO: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hotuba ya Waziri wa Wizara hii katika kuboresha michezo katika Mikoa pamoja na kufikisha michezo kwa vijana kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Kigoma pamoja na Wilaya zake unalo tatizo kubwa la kupata habari kwa kutumia redio Tanzania. Mtambo wa *RTD* uliopo Mohambe Kigoma, hauna uwezo wa kurusha taarifa ama habari kwa Wilaya za Kasulu Kibondo. Ni kwa mantiki hiyo, wananchi wa maeneo hayo badala ya kupata habari kwenye chombo cha Taifa, wanajikuta wanasikiliza redio ya Burundi inayotoa taarifa kwa wakimbizi makambini. Redio hiyo inaitwa Redio Kwizela.

Mheshimiwa Spika, hawa wananchi wa Kasulu na Kibondo ni raia wa Tanzania, wanayo haki ya kupata taarifa ya Taifa badala ya kuendelea kupata taarifa ya Burundi. Ninaomba Wizara yenye dhamana, ieleteze ina mkakati gani ili kufikisha huduma hiyo kwa wananchi wa Kibondo na Kasulu.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Kigoma ni mionganini mwa Mikoa inayotoa wachezaji wa mpira kwa timu ya Taifa. Lipo tatizo la Wilaya ya Mkoa huo kutokuwa na viwanja ili vijana wawewe kuijendezea kimichezo. Makao Makuu ya Mkoa yanao uwanja wa *Lake Tanganyika* na Uwanja huo unatumika vizuri kimichezo. Tatizo kubwa lipo Wilaya ya Kibondo, mahali ambapo mbali na vijana kuwa na moyo wa michezo, lakini wanakatishwa tamaa na Wilaya kutokuwa na uwanja.

Mheshimiwa Spika, wananchi wapenda michezo katika Wilaya hiyo wako tayari kuchangia ujenzi wa uwanja, lakini wanaiomba Serikali kuwaunga mkono katika ujenzi wa uwanja huo pamoja na kuwapeleka watalaamu wa kupima uwanja wa kisasa.

MHE. KABUZI RWILOMBA: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naunga mkono hoja. Nampongeza Rais kwa kuipa umuhimu Wizara hii. Naomba Watendaji nao waheshimu na kulinda jitihada za Rais. Katika kukamilisha hayo, naomba yafuatayo yaangaliwe na kuanza:-

Kuanzisha mashindano ya michezo ya mpira, yote kuanzia ngazi ya Kata, Tarafa, Wilaya, Mikoa hadi Taifa;

Kuanzisha michezo ya utamaduni, yaani fani na ngoma, ufundu na muziki ngazi ya Kata, Wilaya Mikoa hadi Taifa;

Kuwe na Shule, Vyuo maalum kwa ajili ya fani za sanaa na michezo;

Kuimarisha Chuo cha Malya na Butimba ili kuendeleza Walimu wa Michezo; na

Wizara ya Elimu ifufue michezo ya UMISETA, UMISHUMTA, UMITASHUMTA, ianze kisingizio cha vipindi kwani mipango ikiwa mizuri, masomo hayawezi kuathiriwa na michezo.

Mheshimiwa Spika, naomba wakati wa kujibu hoja, nielezwe Tanzania inajiandaa vipi kuhakikisha tunashiriki *World Cup* ijayo Afrika Kusini? Kuna mikakati gani? Ni kiasi gani cha fedha kimetengwa kwa maandalizi hayo? Tunapenda kuona wachezaji wetu wanashiriki.

Naomba pia nielezwe kama kuna Bajeti imewekwa kwa ajili ya kuwezesha mashindano ya Mikoa hadi ngazi ya Taifa. Huwezi kufanikisha kupata wachezaji bora bila maandalizi ya Taifa kuanzisha ngazi ya Kata, Tarafa, Wilaya, Mikoa hadi Taifa. Naomba nielezwe (Marudio) *World Cup* tutaingiaje mwaka 2010?

Mwisho, siyo pesa ya maendeleo kwa ajili ya kuendesha michezo ngazi ya Wilaya, Mikoa na Taifa. Wizara itasaidiaje ili kufanikisha michezo hiyo? Sioni Bajeti kwa ajili ya Chuo cha Malya. Kumbuka michezo ni afya, ajira, kujenga *body balance* (kwa watoto), elimu, hujenga mahusiano, nidhamu, uvumilivu, huongeza umri, hujenga utaifa, ishara ya Taifa, kinga ya magonjwa, kitambulisho cha jamii, huleta upendo, huondoa upweke na pia michezo ni tiba.

MHE. FATMA OTHMAN ALI: Mheshimiwa Spika, mimi nachangia kuhusu nyimbo zinazotungwa na kuimbwa ndani ya vyombo vyetu vy'a Redio na Televisheni, hazina maadili wala huwezi kukaa na mtu unayemheshimu. Lingine, wala hujui zinaelimisha nini. Je, kwa nini siku hizi hakuna vile vyombo vy'a kuchunguza haya mashairi ya nyimbo? Kama viro: Je, wanasi kia hizi nyimbo, yaani za taarab na hata za vizazi vipy'a?

La pili, michezo hii ya kuigiza, ningeshauri Wizara, kama hii michezo haijatoka ndani ya vyombo vyetu, nayo ifanyiwe uchunguzi, kwani mingine haioneshi maana yoyote wala haifai kwa maadili yetu ya kiafrika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mpira wa miguu, kuna timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu ya Wanawake na kama mnnavyofahamu, ikiwa ni timu ya Taifa, ina maana ya

kuwa Zanzibar nayo imo. La kushangaza, inapokuwa timu iko kambini huwachukua watoto wetu wa Zanzibar kufanya mazoezi ya pamoja. Siku timu inapotoka nje, vijana hao huenguliwa dakika za mwisho, aidha watateremshwa ndani ya gari na kuambiwa wao hawamo. Je, siku zote walizofanya mazoezi mpaka wakateuliwa kwamba wakashiriki Mechi, inakuwaje watolewe siku ya mwisho, tena wameshaingia ndani ya mabasi kwa kwenda kwenye mech? Matatizo hayo yametokea mara mbili kwa timu yetu ya Taifa ya Mpira wa Miguu ya Wanawake Zanzibar. Huwa wanawaita vizuri waje washiriki, lakini siku ya mwisho huwa wanawatoa. Naomba suala hili liangaliwe vizuri.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

MHE. MWANTUMU B. MAHIZA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote naunga mkono hoja.

Pili, napenda kuchangia kwa kushauri juu ya mavazi ya wanenguaji katika Bendi mbalimbali za muziki hapa nchini. Sipendezwi na siridhishwi na mavazi ya nusu uchi, hali ya kuwa wanenguaji wanaume hucaa kwa kujisitiri, nini lengo la mavazi haya? Hivi ni mwanamke tu anayepaswa kuoneshwa maungo yake? Naamini kizuri huijuza. Kila chenye sifa kitajiua tu.

Napenda kushauri kuwa, ufile wakati sasa wa Serikali yetu kutunza heshima ya mwanamke hasa majukwaani. Mavazi ya nusu uchi yatumike kwenye ngoma za ndani tu ambazo hapo kale zilichezwa kwa lengo la unyago au jando, huko ni watu wachache tu ambao hualikwa na yale yanayofanyika huko ni siri yao tu. Haipendezi kabisa aina nyingine za unenguaji hadharani. Ni fedhaha mbele ya macho ya wengi!

Nawaomba wahusika wapatiwe semina ya namna ya kuonesha ustadi wa ngoma au unenguaji wao. Yako mambo ya hadharani na yale yanayofanyika nyumbani. Huo unaofanyika sasa sio uhodari, bali ni fedhaha na matusi kwa jamii yetu.

Mheshimiwa Spika, taaribu asili yake ni uhodari wa utunzi wa mashairi, tenzi na ngonjera kwa ustadi mkubwa ambao huzingatia sana vina, mizani na kadhalika. Nyimbo nyingi za taaribu hapo kale zilikuwa zenye mafunzo, vitendawili na mafumbo yenye kuelimisha. Mfano: “Mdudu kaingiaje ndani ya kokwa ya embe?”, “Kuku na yai nani kaanza?”, “Nahodha kukaa nyuma.” Hii ni mifano michache ya ustadi wa watunzi wetu hapo kale.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa taaribu imekuwa fani ya fedheha, matusi matupu kiasi cha kudhalilishana. Mifano ni mingi. Kila nyimbo za mipasho ni kulumbana wanaume tu! Hivi hakuna suala lingine ambalo jamii ingependa kusikia/kujifunza? Nyimbo hazina mafumbo, ziko wazi mno! Mfano: “Hazipendi nyeti zako!”, “Nampa raha hadi analia” na kadhalika. Hivi anatarajia nini mwimbaji huyu? Ni ujumbe gani unatarajiwa kumfikia msikilizaji?

Mheshimiwa Spika, nashauri ufile wakati sasa, Wizara iunde Tume kukagua upya nyimbo zote zenye lugha isiyoridhisha, zifutwe au kurekebishwa. Tukumbuke kwa

kumuenzi muimbaji wa kale aliyeacha jina na sifa kubwa, Siti Binti Saad ambaye hadi leo ukisoma mashairi yake hutosikia vibaya kuimba mbele ya mwanao au wazazi hata mbele ya jamii. Hivi tunasubiri nani atueleze tatizo hili?

Mheshimiwa Spika, naomba sana tufanyie kazi suala hili, linatudhalilisha.

MHE. MWAJUMA HASSAN KHAMIS: Mheshimiwa Spika, ni vyema nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuchangia.

Mheshimiwa Spika, kwa kuanzia, napenda nianze na lugha yetu ya Kiswahili. Pamoja na nia njema ya Serikali kukifanya Kiswahili kuwa ni lugha ya kitaifa. Bado Serikali haijawa tayari katika hili; haijawa tayari kutokana na mambo mawili ya msingi. Sisi wenyewe bado tuna utafauti wa maneno yetu kati ya Zanzibar na Tanzania Bara. Kama Kiswahili kinataka kuwa lugha ya kitaifa, Watanzania tutatumia Kiswahili cha nchi gani?

Jambo la pili, kama Serikali iko wazi na hili, iweje Bajeti vitabu vyake vitungwe kwa lugha ya kigeni?

Mheshimiwa Spika, kuhusu habari; Televisheni pamoja na kutoa habari kwa jamii, lakini pia kinatoa maadili maovu katika jamii. Uhuru ni jambo kubwa, lakini linahitaji kwenda na sheria ya nchi. Hali ya baadhi ya Televisheni zetu zinatoa taaluma kinyume na utamaduni wetu. Hivyo basi, Serikali yapaswa kukemea mambo ambayo yanatoa maadili yasiyo ya kitanzania.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mpira wa miguu, ni lini nchi yetu itaonekana kushinda na hata kutoa upinzani angalau Kombe la Afrika? Tuseme nchi yetu haina wana michezo?

Mheshimiwa Spika, vilabu vyetu havina katiba zinazolingana na vilabu vyenyewe. Viongozi mara nyingi hutumia pato lao kupitia vilabu, jambo ambalo hupelekeea vilabu vyetu kukosa ushindi, kwani timu zetu kila kiongozi wa timu ana mchezaji wake katika vilabu. Ni vyema sasa Serikali ichukue hatua ili vilabu vyetu viwe na msimamizi Serikalini. Kwa leo nasita hapa.

MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Manaibu Waziri wote wawili, Mheshimiwa Joel Bendera na Mheshimiwa Emmanuel Nchimbi pamoja na Watendaji wao wote kwa kuweza kuwasilisha hotuba yao ya Bajeti katika Bunge lako hili Tukufu kwa ufasaha na umakini kwa hali ya juu hasa ukizingatia kuwa Mheshimiwa Waziri Muhammed Seif Khatib ni msanifu wa lugha ya Kiswahili, imechangia kuifanya hotuba hii iwe ya kuvutia zaidi kwa usanifu huo wa lugha.

Mheshimiwa Spika, napenda niipongeze *TFF* kwa hatua waliyoifikia kuiondoa kiu ya Watanzania na kutimiza ndoto ya Watanzania walio wengi kwa kutupatia Mwalimu wa Mpira wa Miguu kutoka Brazili, ambaye kuja kwake kuwaonesha dhahiri

kuwa sasa Tanzania tumekusudia kwa dhati kuwaendeleza wanasoka wa nchi hii, kwani mchezo huu wa mpira wa miguu kila siku ufundu na utaalamu unabadilika kutokana na maendeleo ya kasi na mbinu za mchezo huu zinavyobadilila kila mara.

Mheshimiwa Spika, kupatikana kwa Mwalimu huyu tunategemea nasi kuwemo katika nchi ambazo zimekusudia kukuza mchezo huu wa mpira wa miguu na kuleta ushindani ndani ya Afrika ili tujenge historia mpya katika kubadilisha na kuufanya mchezo huu urudiwe kupendwa zaidi, kwani Watanzania wengi wamepoteza imani hata kuitwa Kichwa cha Mwendawazimu.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo machache napenda hutamka rasmi kwamba, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

MHE. OMAR S. KWAANGW’: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri, nawapongeza Manaibu Mawaziri wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, napongeza juhudzi za Serikali za kujenga uwanja mpya wa Kisasa pamoja na kukamilisha awamu ya pili ya uwanja wa Taifa. Kwa muda wa miaka mingi sasa, Serikali haijajishughulisha na ujenzi wa viwanja na kuangalia viwango vya viwanja hasa ngazi za Wilaya na zaidi Vijijini kwenye vitovu vya vipaji vya michezo.

Viwanja vingi katika ngazi za Makao Makuu ya Mikoa mingi vimejengwa na CCM hasa katika kipindi cha mfumo wetu wa Vyama vingi na hivyo Serikali haikuwa ikijenga viwanja na kwa sababu hiyo, Sekta ya Michezo haitakuwa inatengewa Bajeti ya Maendeleo kwa ajili ya kujenga viwanja vya michezo. Nashauri sasa Serikali iwe inaweka fedha kwa ajili ya ujenzi wa viwanja vya kisasa. Hii itasaidia kupata wanamichezo wenye vipaji vinavyoiletea sifa Tanzania, kwa mfano, wanamichezo wengi wa riadha ambaa wameiletea sifa na medali za dhahabu wanatoka Mkoa wa Manyara, lakini Mkoa hauna uwanja wowote wenye kiwango chochote pale Makao Makuu ya Mkoa Mjini Babati. Wageni wengi mashuhuri kutoka nje ya nchi wanaposikia kuwa Manyara ndiyo eneo walipotoka vijana walioletea nchi hii sifa, wanashangaa sana. Ama kweli kwenye miti mingi hakuna wajenzi.

Kwa mantiki hii, naona sasa ni muda muafaka kwa Serikali ya Awamu ya Nne kujenga uwanja angalau mmoja Mjini Babati kwa ajili ya kukuza vipaji vya riadha. Awamu ya tatu iliamua kujenga uwanja wa kisasa Dar es Salaam zaidi kwa michezo ya mipira na michezo ya ndani ingawa riadha pia imo. Nashauri uwanja wa michezo hasa riadha uwe Babati kwa sababu pia Mkoa wa Manyara ni mpya na hauna uwanja wowote wa michezo licha ya eneo la wazi kubwa ambalo limetengwa kwa miaka mingi sasa.

Naomba mawazo haya yapate nafasi kwenye mipango ya kuimarisha michezo kama alivyonena Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania: “Nitaanzisha mjadala wa kitaifa wa kuendeleza michezo nchini. Wadau wote washiriki na Watanzania tukubaliane juu ya mustakabali wa michezo nchini mwetu.” “....Lazima tutoke huko na inawezekana”

Kwa sasa lipo tatizo la viwango vya viwanja kutokidhi vipimo sahihi. Viwanja vingi hasa Wilayani na Vijijini havina vipimo sahihi. Hii ni hatari sana. Unakuta vijana wanacheza kwenye viwanja Mtaani, kandokando ya barabara, mashambani na kadhalika, vingine vidogo, vingine vikubwa na kadhalika, kwa mfano goli kipa aliyezoea kukaa kwenye magoli yenye vipimo vidogo akienda kushindana kwenye magoli yenye vipimo sahihi atashindwa tu.

Mheshimiwa Spika, Babati Half Marathon ni mchezo wa ziada ambao hufanyika kila tarehe 31 Desemba kila mwaka Mjini Babati. Wanamichezo wote maarufu kitaifa hupenda kuhudhuria michezo hii kila mwaka tarehe 31 Desemba. Naomba Wizara hii itambue mchezo huu kwa viongozi, Waheshimiwa Mawaziri wa Wizara hii kuhudhuria, kuikuza na kuitangaza Babati Half Marathon kwa wafadhili mbalimbali ili ipate msukumo kwa ajili ya kupata vijana wenye vipaji. Wizara hii ichangie kwa hali mchezo huu.

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Wizara hii ya Habari, Utamaduni na Michezo kwa kasi mpya ya kukuza michezo.

Mheshimiwa Spika, michezo ni kitalu pekee cha uhakika katika kumwendeleza binadamu, ni kwa wazazi wake na Shule wanayosoma watoto hao. Hivyo, ili kuendeleza michezo na michezo hiyo kuwa kitalu cha ajira na kujenga afya, nashauri, hadi hapo Chuo kitakapokamilika, hivi sasa Wizara kwa kushirikiana na Wizara za Elimu na Vyuo, nipate orodha ya Waalimu (makocha) ili kuwe na programu ya kitaifa ya mafunzo itakayoshirikisha wanafunzi hao wa Shule na Vyuo. Aidha, Wizara ijithidi kuongeza idadi ya Waalimu na Waalimu wa michezo mbalimbali.

Vyombo vya Ulinzi vina nafasi nzuri ya kuendeleza michezo. Wizara iwe karibu na vyombo vya ulinzi kwa nia ya kuwa na kikosi ambacho kitakuwa na wachezaji bora ili vyombo hivi vinapoingia kwenye mashindano visishindwe kirahisi.

Mheshimiwa Spika, tunaipongeza Wizara kwa kuanzisha gazeti la Kiswahili, kwani wakati wote Serikali imekuwa ikilifanya gazeti la Chama cha Mapinduzi kama gazeti la Serikali. Pamoja na hatua hiyo, wakati umefika kwa vyombo vya Serikali kutoa huduma sawa kwa Serikali na Serikali kivuli Bungeni, kwani hivi sasa vyombo hivyo hasa *TVT* kwenye habari na *Daily News* hawatoi vya kutosha habari za upinzani ambao nao ni Wasemaji Wakuu wa Wananchi.

Mheshimiwa Spika, nivyema Waziri atakapo jibu hoja, aliarifu Bunge juu ya hatma ya mkandarasi aliyekabidhiwa kujenga minara na Vituo vya *TVT*. Naomba kuwasilisha.

MHE. MARIAM S. MFAKI: Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wote wawili na Watendaji wa Wizara hii kwa maandalizi mazuri na kuwasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu. Hotuba hii inatoa mwelekeo wa Wizara kwa siku zijazo kwa mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, natoa mchango wangu ili kuboresha Wizara hii. Wizara hii inaratibu suala zima la utamaduni, jambo ambalo ni muhimu kwa Taifa ambalo halina utamaduni, linapungua sifa za Taifa hilo. Inaonekana Wizara hajajihusisha kuzijua mila na desturi nzuri za makabila yote ya Tanzania ili zinazofaa ziendelezwe na zile ambazo hazifai ziwekwe kama kumbukumbu. Inasikitisha kuona imechagua Mikoa michache au Mikoa mitano tu na hii ni kwa ajili ya kudhibiti UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara ieleze kwanini haifanyi utafiti wa mila na desturi za makabila yote ya nchi hii na zile mila nzuri zitumiwe kwa maana ya kuimarisha tabia nzuri kwa vijana wetu?

Mheshimiwa Spika, naomba niunge mkono pendekezo la Kamati kwamba ni wakati muafaka sasa Serikali kuweka wazi vazi linalotunza, kulinda heshima kwa wananchi wa Tanzania kwa wanawake na wanaume. Suala hili la mavazi limekuwa kero kwa wananchi wengi na lawama zinatolewa kwa Serikali kwa kushindwa kudhibiti suala hili. Mavazi yanayovaliwa sasa na vijana wetu, nadhani sisi wote ni mashahidi kwamba sasa karibu vijana watatembea bila nguo. Imefikia hatua hiyo sasa na bado Serikali haioni ni tatizo. Naomba Serikali itamke vazi la Taifa la heshima kulinda heshima ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba nielezwe juu ya picha na Senima na zile kanda zinazouzwa kutoka nje ya nchi ambazo zinaingia. Picha hizo zinachafua maadili ya watoto na vijana. Mara nyingi Serikali inaeleza jinsi inavyojitahidi kudhibiti wakati hailingani na matendo. Naomba Wizara ieleze jinsi inavyodhibiti, ni wangapi wamekamatwa kwa kosa hilo, ni nani anayepaswa kuwakamata na kuwashitaki?

Mheshimiwa Spika, mchezo wa soka ili uwe endelevu zaidi ya kujenga vijana kupenda kucheza mpira, naishauri Serikali ianzishe mashindano haya yaanze katika ngazi za chini kwa mfano, Kata zishindane na hatimaye Wilaya, Mikoa na Taifa. Vilevile, vijana na wananchi wahamasishwe kuunda timu za mpira zitakazojenga tabia za kujitegemee ili zisitegemee misaada peke yake. Dawa yake ni tiba, zianzie chini na zinapokomaa ndipo zisajiliwe. Usajili huu uwekwe kwa viwango vya Kata, Wilaya, Mikoa na Taifa. Vilevile, viwanja vya ngazi ya Kata navyo vihamasishwe vijengwe ili viwe vya kukusanya mapato.

Mheshimiwa Spika, suala la ngoma za makabila mbalimbali ni muhimu nazo ziendelee kuthaminiwa na hata ziweze kupelekwa nchi za nje kuonyesha na kutangaza ngoma zetu ili kwa namna nyingine ni ajira kwa vikundi vyetu.

Mheshimiwa Spika, naomba kujuu kama kunauwezekano wa Serikali kuzihamasisha nchi nyingine ili vikundi vyetu viende nje ya nchi kuonyesha michezo hiyo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii asilimia mia kwa mia.

MHE. MASOUD ABDALLA SALIM: Mheshimiwa Spika, ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema zake nikiwa hai na uzima wa afya. Kwanza kabisa, nataka

nizungumze mashindano ya warembo, yanayoendeshwa katika ngazi mbalimbali Wilaya hadi Taifa, yamekuwa yakipoteza mtazamo mzuri wa kujenga maadili mazuri katika kurithisha kizazi ambapo taswira inaonesha vizazi vyetu vimekuwa vikiangalia heshima na utu wa mwanamke anavyodhalishwa kwa Serikali kutotoa utaratibu vizuri wa mavazi gani yanayostahili kuvaliwa.

Mheshimiwa Spika, nasikitisha na inasononesha sana kuona warembo hao wakiwa nusu uchi. Hivi utamaduni huu wa kuvaanu nusu uchi kwa warembo hao, Serikali haioni ni kumomonyoa maadili mazuri ya Watanzania na hatimaye kuchochea UKIMWI?

Mheshimiwa Spika, kwanini Serikali imekuwa na kigugumizi kuandaa utaratibu mzuri wa mavazi kwa mashindano ya warembo hao? Je, Serikali ina mkakati gani wa kurekebisha hili?

Mheshimiwa Spika, tunayapongeza magazeti jinsi wanavyoelimisha Umma, lakini hali inaonesha magazeti mengi bado hayaandiki habari za Vijijini ambako ndiko kwenye idadi kubwa ya Watanzania, hivyo Umma huu ungeendelea kupata elimu zaidi kuititia waandishi. Kwa hiyo, ushauri wangu, Wizara iandae utaratibu mzuri wa kuwabana waandishi kwenda Vijijini, sambamba na wale wa redio na televisheni.

Mheshimiwa Spika, pia ninaishauri Serikali na Wizara husika kuandaa utaratibu zaidi kwa kuhakikisha redio, televisheni na magazeti yote yawe yanatumia Kiswahili sanifu katika lengo la kukikuza Kiswahili na ni vyema Serikali ikaangalia namna ya kudhibiti magazeti yanaonesha mambo ya ngono katika kujipatia umaarufu, kwani yanamomonyoa maadili ya Watanzania, hatimaye kurithisha maadili potofu kwa kizazi chetu cha sasa na baadaye. Naomba kuwasilisha.

MHE. HAJI JUMA SEREWEJI: Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru wewe binafsi kwa kuniruhusu kuchangia hotuba hii.

Pili, niipongeza hotuba hii ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, pamoja na kuwapongeza wataalamu wote wa Wizara hii akiwemo Katibu Mkuu wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea na mchango huu, kwa niaba yangu na wananchi wangu wa Jimbo la Mwanakwerekwe, nainze kwa kuunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, mimi kwanza niipongeze Wizara hii hivi sasa kwa dhamira ya kuleta hali ya michezo hapa nchini kuwa na kiwango cha juu. Pia, kwa kujenga kiwanja cha kisasa ambacho kitatupa fursa Watanzania kuona michezo mbalimbali ya kimataifa ka vile kuweza kufakinisha kuleta Walimu wa michezo wenye kiwango cha kimataifa. Natumaini tutafika mbali kimichezo.

Mheshimiwa Spika, mimi nafsi yangu nasikitishwa sana na wasanii wetu. Hata bendi zetu ambazo mara nyingi wakati wa burudani basi wachezaji au wanenguaji wa ngoma hizo huwa wanacheza wakiwa nusu uchi, jambo ambalo linamong'onyoa maadili

yetu ya Tanzania na wachezaji wanawake wanaocheza nusu uchi. Hata nyimbo vile vile ni za matusi kabisa. Hivi sasa matusi imekua jambo la kawaida kwenye redio, televisheni, magazeti kutokana na vitendo, nyimbo na michezo ya wasanii wetu.

Mheshimiwa Spika, natumaini Serikali ina uwezo wa kukemea ili yasiwepo au yapungue kabisa. Natumai Serikali itachukua hatua ya kufaa kuhusu haya.

Mheshimiwa Spika, kuhusu michezo mashulen, naipongeza sana Serikali kwa kuliona hili, lakini naiomba Serikali jambo hili lisimamiwe kikamilifu. Kwa sababu humu humu mashulen, ndimo mtamopatikana wachezaji wazuri na watoto wenyе vipaji.

Mheshimiwa Spika, navipongeza vyombo vyetu vya habari kwa jinsi vinavyotoa elimu burudani na habari mbalimbali, television na redio zote, *Radio One* na Redio ya Taifa.

Lakini naiomba Wizara kuliona hili la kuwa Televisheni zetu zilinde mmomonyoko wa maadili kwa kutuletea vipindi vya heshima.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa viwanja vya michezo, hivi sasa sehemu nyingi na Mijini wakati wa kutoa viwanja vya nyumba, basi sehemu za viwanja vya michezo husahaulika. Kwa hiyo, kwenye ramani hizo viwanja vya mipira au michezo viwepo.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara hii ivilinde vile viwanja vya michezo vilivyoko Mitaani visivamiwe kwa sababu bila viwanja vya michezo hatutaendelea na michezo. Nakushukuru na naunga mkono hoja.

MHE. ATHUMAN S. M. JANGUO: Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri na Manaibu wake wawili, Katibu Mkuu wa Wizara na Wasaidizi wenu wote kwa mwanzo mzuri wa kuendesha shughuli za Wizara na kwa hotuba fupi, lakini yenye kina na malengo endelevu ya shughuli zenu. Lakini nina maoni yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwenye Ibara ya nane, pamoja na mambo mengine mnadhamiria kuongeza umri wa kuishi wa Tanzania. Mimi nafikiri jukumu hilo litakuwa gumu kulitekeleza. Ni Mwenyezi Mungu tu pekee anayeweza kurefusha au kufupisha umri wa kiumbe. (*maskhara*)

Mheshimiwa Spika, ili kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili kwa manufaa ya Taifa letu. Napendekeza mambo yafuatayo:-

- (a) Serikali ianzishe Taasisi rasmi ya kuratibu uenezaji wa Kiswahili katika Bara la Afrika na nje ya Afrika.
- (b) Taasisi hiyo pamoja na Serikali ziifanye lugha ya Kiswahili iwe moja ya vitega uchumi hasa fedha za kigeni kwa kupeleka nje ya nchi

Walimu wa Kiswahili kama inavyofanya India kwa Wahasibu na Indonesia kwa waendesha meli na Wahandisi wa meli.

- (c) Turuhusu Walimu na wataalam wa Kiswahili wakafundishe nchi za nje ili walete hizo fedha za kigeni hapa nchini.
- (d) Tuanzishe Chuo au Vyuo rasmi vya kufundisha Kiswahili kwa Watanzania na wasio Watanzania.

Lugha za Asili, hizi lugha sasa hivi zinakufa. Kwa hiyo, nashauri Serikali itoe msukumo maalum wa kuendeleza lugha za asili kama inavyofanya Wizira ya Afya kwenye madawa asilia. Utafiti unaotajwa katika Ibara 27 uanze haraka.

Mheshimiwa Spika, katika Sekta ya michezo, napendekeza yafuatayo:-

- (a) Wakati umefika sasa wa Timu ya Taifa ya mpira wa miguu iwe ya kudumu, wachezaji walipwe mishahara na Walimu pia walipwe na Serikali mishahara na marupurupu mazuri.
- (b) Tanzania ifuate mifano ya wenzetu wa Afrika Magharibi ya kuwatoa wachezaji wetu wenyewe vipaji nchi za ng'ambo ili wakajifunze ufundi wa mpira.
- (c) Tuweke mkazo wa michezo mashulenii tujenge vipaji vya michezo mbalimbali angalau terejeshe hadhi ya Tanzania ya miaka ya nyuma ya akina Filbert Bayi, Suleiman Nyambui, Nzae Kyomo na kadhalika. Naiunga mkono hoja hii.

MHE. JUMA SAID OMAR: Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya na hivyo kuweza kufika katika Kikao cha leo cha Bunge. Namwomba Mwenyezi atuzidishie uzima na afya njema.

Mheshimiwa Spika, naomba kukupongeza wewe na Mheshimiwa Naibu Spika pamoja na Wabunge wote kwa mashirikiano ndani na nje ya Ukumbi wa Bunge. Tuendeleze mashirikiano kwa maslahi yetu pamoja na Taifa letu kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, pia nampongeza Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo na Manaibu wake wawili pamoja na Watendaji mbalimbali wa Wizara hii. Wizara hii ina majukumu ya kuongoza, kusimamia na kuratibu shughuli za Habari, Utamaduni na Michezo katika nchi yetu. Hizi ni shughuli muhimu sana kwa Taifa letu. Hivyo, Wizara inalazimika kuwa makini sana katika kuendeleza shughuli hizi ili ziendane na mila na desturi, heshima na mwelekeo wa Taifa hili la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kuna njia nyingi kwa wananchi kupata habari ikiwa ni pamoja na magazeti, redio, luninga na kadhalika. Vyombo hivi vya habari vinaonekana zaidi katika maeneo ya Mijini na kwa kiwango kidogo Vijijini kwa zile sehemu ambazo

umeme unapatikana kwa kutumia luninga. Naiomba Serikali isambaza umeme Vijijini kwa maendeleo ya wananchi likiwemo suala zima la kupata habari.

Mheshimiwa Spika, utamaduni ni moja katika sekta muhimu ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo. Naiomba Wizara iandae mikakati itakayohakikisha kwamba mila, desturi na maadili mema havivunjwi kwa njia yoyote hasa ukizingatia kwamba kuna tamaduni mbalimbali za kigeni ambazo zinaingia katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, michezo ni sekta muhimu sana, kwani mbali na kuitangaza nchi yetu kimataifa lakini pia inasaidia kujenga afya za wananchi. Wizara inapaswa kutoa taaluma na fursa kwa watoto vijana na wazee ili waweze kushiriki katika shughuli za michezo kikamilifu. Hii itasaidia kukuza afya za wazee pamoja na vijana.

Mheshimiwa Spika, suala la mavazi kwa vijana na watoto wetu linaonekana kwenda kinyume na maadili ya nchi yetu, kwani inaonekana jambo la kawaida kwa wanamuziki na waigizaji mbalimbali kuvaan nguo ambazo hazifuniki sehemu zote za siri au zenye kuonyesha miili yao.

MHE. MWANTUMU B. MAHIZA: Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Wizara kuwa na mikakati ya kuboresha michezo sehemu mbalimbali. Mchango wangu katika suala hili ni namna ya kupata viongozi mbalimbali wa Vyama vya Michezo.

Mfano, Chama cha *Netball*, baadhi ya viongozi hawa kujaliwa hata kushika mpira, hawajui sheria wala kanuni zinazoendesha michezo huo. Hivi sasa kiongozi wa aina hii atasaidiaje kuboresha michezo huu? Nathubutu kusema baadhi ya viongozi wengine wanafuata kujitangaza na kusikika badala ya kinua michezo.

Michezo wa *Netball* uliipatia sifa kubwa sana nchi yetu. Sasa nashauri Baraza la Michezo liwe makini sana katika kuteua viongozi wa Vyama mbalimbali ikiwemo *Netball*. Nashauri kuwa michezo huu ambao huchezwa zaidi na wanawake, ni vyema ukasaidiwa kurudisha heshimima ya nchi yetu. Naomba tushirikiane kuufufua michezo huu na tuhakikishe unapatiwa viongozi wenye sifa zinazostahili ikiwa ni pamoja na kuzifahamu sheria, kanuni na uzoefu katika michezo ambao mtu anatakiwa kuongoza.

Wizara au Chama kiandae Semina na mafunzo ya michezo mbalimbali kwa wachezaji kuanzia ngazi za Shule za Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu. Naomba katika *field*, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundji na Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo tulijadili suala hili kwa kina ili tuibue vipaji kutokana kwa watoto wetu. Tusipoteze muda, tuanze sasa tuache, urasimu. Niko tayari kutoa ushirikiano.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa malengo na mikakati yote. Ahsante sana.

MHE. BAHATI ALI ABEID: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kumpongeza, Mheshimiwa Waziri na wataalamu wake kwa hotuba nzuri sana na yenye mwelekeo wa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, habari ni moja ya sekta ya huduma za jamii nchini, kwa hiyo, wananchi wanaposoa magazeti huwa wanaamini yaliyoandikwa humo yote ni ya kweli. Kwa hiyo, waandishi wetu wanapoandika mambo yasio na ukweli kwenye magazeti, ni kupotosha Watanzania walio wengi kwa jambo hilo, kwani ukizingatia Waandishi wa Habari wana nafasi kubwa ya kuelimisha jamii kupitia vyombo wao.

Kwa hiyo, naiomba Serikali iweke sheria ambayo itambana Mwandishi wa Habari ambaye ataupotosha ukweli juu ya Serikali au sekta yejote ile iliyopo chini ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, taarifa na picha za ngono zinazoandikwa kwenye magazeti ya udaku, siyo nzuri kwa jamii. Ninaomba Serikali kwa kupitia Wizara hii, iweze kupitia Waandishi hawa wafanyabiashara wanaojali maslahi yao tu, ili waweze kwenda sambamba na matakwa ya wananchi wa Tanzania ambao hawataki maadili yaendelee kuporomoka.

Mheshimiwa Spika, wasanii ambao wanajiita kizazi kipyga, ni wengi katika nchi yetu na kila msanii hupenda aonekane kwenye televisheni zetu hata kama usanii wake haufahamiki kwenye utunzi wake, anafundisha nini na Serikali imekaa kimyaa!

Mheshimiwa Spika, hivi kile kitengo kinachoweza kuangalia hawa wasanii wetu na nyimbo zao, kimefutwa au hakipo? Kama kipo, basi tujitahidi kurusha zile nyimbo ambazo zinaendana na mila na desturi zetu, kwani wasanii wa kizazi kipyga wameibuka na nyimbo za mapenzi ambazo imekuwa sasa haitoshi kuimba tu, mpaka hivi sasa wasanii wana igiza juu ya mapenzi yao na vivazi wanavyovaa haviendani na mila na desturi hasa baadhi ya wanawake vivazi vyao haviridhishi. Je, kupita kwako Serikali inasemaje juu ya hili?

Mheshimiwa Spika, ninaipongeza Serikali kwa kuleta kocha wa kimataifa, tegemeo letu ni mafanikio ya mpira wa miguu kuinuka na nchi yetu iweze kucheza kwenye ngazi ya kimataifa. Naunga mkono hoja mia kwa mia. Ahsante.

MHE. WILLIAM M. NGELEJA: Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii awali ya yote kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, Manaibu wake pamoja na Watendaji wa Wizara hii kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spika, kuna mambo machache napenda kuchangia katika hotuba hii. Jambo la kwanza ambalo napenda kulijadili ni kuhusu uthibiti wa picha za ngono kwenye maduka au *centre zinazoshughulika* na biashara za *internet (Internet Cafes)*.

Pamoja na kwamba kumekuwepo na mgawanyo wa mitazamo katika jambo hili, kwa maana ya kwamba upande mmoja unadhani kwamba jambo hili haliwezi kudhibitiwa kwa vile linatokana na utandawazi, huku upande mwengine ukiona kwamba udhibiti unawezekana, mimi naamini kwamba udhibiti wa picha chafu (ngono) kwenye *internet cafés* inawezekana kabisa endapo Serikali kupitia Wizara hii itaamua kwa dhati

kushughulikia jambo hilo kwa kushirikiana na wadau wa habari na mawasiliano wakiwemo wanaoendesha *internet cafes*.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali iitishe Semina ya wataalam wa mambo ya mitandao/*computers* waendesha *internet cafes* na kadhalika kwa kila Mkoa hili kuelimishana namna ya kudhibiti picha hizi chafu ambazo zinachangia sana kumomonyoa maadili na utamaduni wa nchi yetu. Nasisitiza tena kwamba, udhibiti wa picha chafu kwenye *internet cafes* unawezekana kabisa kwa kuweka *blocking websites*.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ninalopenda kulijadili ni kurekebisha sheria inayohusu usimamizi wa michezo kwa kuzingatia sheria na kanuni za *FIFA* ili Serikali iweze kudhibiti migogoro kwenye Vilabu vya Michezo nchini.

MHE. MWANAWETU SAID ZARAFI: Mheshimiwa Spika, ninayomaombi kwa Serikali hasa Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na TAMESEMI la kuidhinisha Halmashauri za Wilaya na Mikoa kuweka mafungu kwa ajili ya utamaduni na michezo. Ninaamini kwamba tamko likitoka kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mkoa na Halmashauri zitaziona sekta hizi ni nyeti kama zilivyo sekta nyingine na kuzipatia ruzuku.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali halisi ya mazingira magumu ya Waandishi wa Habari na Vyombo vya Habari kwa ujumla, naiomba Serikali kuongeza maslahi ya sekta hii, kwani itasaidia Waandishi au sekta nzima kufuata maadili. Nina imani kwamba habari nyingine huzitoa au huzionyesha kwa ajili ya kuvutia wasomaji/watazamaji ili ikuingiza kipato. Hivyo basi, ili kuепusha hayo, maslahi ya Waandishi katika Sekta ya habari kwa ujumla yaboreshwe.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nampongeza Rais wetu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kutimiza ahadi yake ya kutuletea kocha wa Taifa. Pia, naipongeza Serikali kwa kutujengea uwanja wa michezo wa Kimataifa.

MHE. GUIDO G. SIGONDA: Mheshimiwa Spika, nashauri Wizara ilete utaratibu wa wanafunzi wa Shule za Msingi na Sekondari wa kutembeleana kwa lengo la kufanya michezo kwa kushindana. Ili kupunguza gharama za chakula na malazi, wanafunzi wenyeji washauriwe kudumisha ukarimu wa kuwakarimu wenzao wageni kwa kuchaguana.

Utaratibu uliokuwa ukitumika enzi za zamani ilikuwa wanafunzi wa Shule wenyeji walikuwa wakijipanga mstari mmoja ikiwa vilevile wanafunzi wa Shule ya wageni kujipanga mstari upande mwengine. Kisha kila mwanafunzi mgeni alikuwa akimchagua anayemtaka. Kwa hiyo, nashauri Wizara ilekeze kuanzisha Bonanza la Michezo kwa Shule za Msingi kwa kila mwaka hasa wakati wa kiangazi.

Mheshimiwa Spika, nashauri Wizara iendelee kuhamasisha wananchi hasa wazee na watu wazima na jinsia zote na hasa waishio Vijijini umuhimu wa kujiweka utimamu kiafya kwa kushirikiana katika michezo na mazoezi ya viungo

Mheshimiwa Spika, katika nchi yetu kuna Mikoa ambayo kiasili hutoa vijana wenye uwezo wa sanaa ya kimichezo kama vile kukimbia, mieleka na ngoma za asili. Nashauri Wizara itambue Mikoa hiyo kwa lengo la kuihamasisha ili ielekeze nguvu zake kuwatambua vijana wenye vipaji na uwezo ili waendelezwe.

Upande wa utamaduni, kila Mkoa una utamaduni, desturi na maadili yake. Wizara ihamashe kuendeleza tamaduni mzuri mionganoni mwa wananchi kwa lengo la kuzidumisha tamaduni hizo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. BALOZI ABDI H. MSHANGAMA: Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuelekeza kwamba Shule ziwe viota nya kukuza michezo na sanaa. Ili kuweka misingi madhubuti ya utekelezaji wa azma hii: Je, Wizara husika zina mipango gani ya kupeleka miongozo mashulenii, ujenzi wa viwanja, mafunzo ya Walimu wa Michezo, Vifurushi nya Vifaa nya Michezo na kadhalika?

Vile vile, Serikali iko tayari kuelekeza na kuzisaidia Halmashauri zote nchini zijenje angalau kiwanja kimoja kizuri cha michezo kila Wilaya.

Mwisho, naipongeza Wizara kwa hotuba nzuri na naunga mkono hoja.

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Spika, napenda kushukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia kwa maandishi katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kutoa pungezi kwa Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo. Mheshimiwa Mohamed Seif Khatib na Manaibu Waziri, Mheshimiwa Nchimbi na Mheshimiwa Bendera pamoja na Watendaji wote wa Wizara hii waliandaa hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba hii nitachangia kwa kuhitaji ufanuzi au maelezo yafuatayo.

Mheshimiwa Spika, hapo zamani kulikuwa na upatikanaji mzuri sana wa habari mpaka Vijiji kwa kupitia Shirika la Habari Tanzania (SHIHATA).

Mheeshimiwa Spiia, tangu Shirika hili life, Serikali ina mikakati gani ya kuweza kupeleka/kupata taarifa za Vijijini? Ni kwa kiasi gani kumeathiri upatikanaji wa habari kutoka Kijijini tangu SHIHATA life? Je, Serikali haioni ni wakati muafaka wa kuanzisha chombo kama SHIHATA? Naomba jibu.

Mheshimiwa Spika, vile vyombo nya Habari, Redio Tanzania na Televisheni ya Taifa ni kwa ajili ya kuhakikisha Watanzania wote wanapata habari, ukizingatia vyombo hivi vinatumia kodi ya wananchi wa nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, ni kwa nini *TVT* haionekani nchi nzima na Serikali ina mikakati gani ya kuimarisha *Radio Tanzania* ili iweze kusikika katika Wilaya na Mikoa yote ya Tanzania? Ni kitu cha ajabu, ni rahisi kusikiliza redio za nchi nyingine na ni vigumu kuipata *Radio Tanzania*. Naomba Jibu.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua mchango mkubwa wa Waandishi wa Habari katika maendeleo ya nchi yetu, Serikali iko tayari kulaani vitendo vyovyyote vile vinavyomzuia Mwandishi wa Habari kutenda kazi yake?

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mikakati ya kukitengeneza Kiwanja cha *Memorial Moshi*? Uwanja ule umesaulika sasa hivi. Mkao wa Kilimanjaro hatuna uwanja kwa ajili ya mpira kabisa? Hata kama ule haurekebishwi, basi kuna mikakati gani ya kutengeneza uwanja wa kuchezza mpira wa mguu kwa Mji wa Moshi, ukizingatia michezo imepewa kipaumbele kwa sasa hivi?

Mheshimiwa Spika, baada ya maoni haya, nashukuru. Naomba kuwasilisha.

MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwanza, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, Manaibu Mawaziri pamoja na Katibu Mkuu na Ofisi yake kwa kutuletea hotuba nzuri na inayotoa matumaini makubwa katika maendeleo ya michezo, uboreshaji wa Sekta ya Habari na Utamaduni.

Mheshimiwa Spika, kama tulivyosikia katika hotuba, pamoja na faida nyingine, michezo ina faida kubwa ya kurefusha maisha. Kwa sababu hiyo basi, sio vyema michezo ikasisitizwa kwa makundi fulani ya jamii au jinsia fulani pekee, ni vyema basi Wizara ikaangalia uwezekano wa kuhamasisha michezo kwa jamii nzima ya Kitanzania, wazee kwa vijana, watoto kwa wakubwa, wake kwa waume, Mijini na Vijijini.

Mheshimiwa Spika, vile vile, Wizara iweke bayana kwa wananchi kuwa michezo sio mpira pekee, bali iko michezo ya aina nyingi ikiwemo ya kuvuta kamba na kuruka kamba. Hivyo basi, wananchi waelimishwe kuchenza michezo ya aina yoyote ambayo inaweza kuleta faida yoyote itokanayo na michezo hasa ile ya kurefusha maisha. Kwa kifupi ni kwamba, michezo isiwe kwa watoto na vijana au kwa watumishi wa Umma Mijini pekee yake. Michezo iwepo hata kwa wakulima Vijijini kulingana na mazingira yao na vifaa vitakavyoweza kupatikana kwa ajili ya michezo fulani.

Mheshimiwa Spika, nzungumzie michezo kwa walemvu. Napenda kuishauri Wizara iwafikirie walemvu kipekee. Nao pia wangesaidiwa kufundishwa michezo ambayo inawafaa kwa aina tofauti ya walemvu kwani hata wao wanao uwezo, wanapenda burudani, kujenga mahusiano mazuri kijamii na wanahitaji kurefusha maisha. Wapo walemvu wa miguu (wanaotambaa) lakini wanaweza kuchenza vizuri sana muziki. Hivyo walemvu wanaweza.

Mheshimiwa Spika, napenda kuongelea kuhusu ushirikiano wa Wizara na watu binafsi au *NGO's* ambazo zinataka kuanzisha *Sports Academy*. Nachukua nafasi hii

kuiomba Wizara itoe ushirikiano wa hali ya juu na wa kutosha kwa *NGO*'s hizi ambazo zimesajiliwa kama asasi za michezo. Hii ina maana kwamba Wizara ifanye ufuatiliaji wa karibu, ijue maendeleo ya *NGO*'s hizi na changamoto zilizopo na iweze kutoa msaada wa kitaalamu au ushauri wowote utakaohitajika.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba Wizara iwafuatilie watoto wenyе vipaji vyа pekee, iwatambue, iwaendeleze na hata ikibidi kuwasomesha nchi za nje katika fani walizonazo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante.

MHE. CASTOR R. LIGALLAMA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Waziri, Manaibu wake, Katibu Mkuu kwa hotuba nzuri yenye kueleweka. Aidha, napenda kuiunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Bodi ya Ukaguzi wa Filamu (*Film Censorship*): Hivi karibuni pamejitokeza tabia katika jamii yetu (hasa kwenye Miji mikubwa) ya kuonyesha picha za ngono kwa makundi au wananchi hata wenyе umri mdogo wasiolielewa tendo la ngono.

Mheshimiwa spika, naomba Kitengo hiki cha Ukaguzi wa Filamu kiajiri Maafisa Wakaguzi ambaо pamoa na kazi nyingine, watakuwa wanapita kwenye Mitaa, Vitongoji na sehemu za Burudani ili kukagua aina ya filamu na kanda za video zinazoonyesha. Hii itawezesha kubaini kama maadili ya Taifa letu yanafuatiwa na kulindwa kwa kuonyesha picha zisizochafua utamaduni wetu kwa kulinda maadili yetu.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo langu la Kilombero, wananchi wamejitolea kwa nguvu zao kujenga viwanja viwili vyа michezo katika Mji mdogo wa Kidatu na Makao Makuu ya Wilaya ya Ifakara. Kwa viwanja vyote viwili yanahitajika matengenezo madogo madogo ili kuvifanya vianze kazi, kwa kutumika ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kile kiwanja cha Kidatu kinahitaji kama Sh. 5,000,000/= wakati kile cha Ifakara Mjini kinahitaji matengenezo ya Sh. 7,000,000/=.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Wizara iwaunge mkono wananchi hao kwa kuwatafutia kiasi hiki cha fedha kilichobaki, yaani Sh. 12,000,000/=, ikiwezekana hata kwa njia ya mkopo ili watakapoanza kuvitumia malipo yaweze kufanyika.

MHE. HAMZA A. MWENEGOHA: Mheshimiwa Spika, ningependa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri na yenye kuonyesha malengo mazuri.

Mheshimiwa Spika, kwanza ningependa kuzungumzia mpira wa miguu. Kwa mwono wangu, sasa wakati umefika kwa Taifa kuruhusu *Professional Players* wa Mpira wa Miguu. Ni kutokana na wachezaji hawa ndio maana Timu za Taifa huwa na wachezaji bora.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa kufungua Vituo vingi vya kurushia matangazo. Kwa mshangao mkubwa, *TVT* imefungua Vituo 12, lakini Morogoro haimo. Pamoja na hayo, ninaishukuru Wizara kwa kuiruhusu Redio Uhuru kupasha anga ya Morogoro na Dodoma.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sasa Redio na televisheni vimekua kwa namna moja ama nyingine, ni vyema basi *RTD* na *TVT* ikatembelea Morogoro Vijijini ili nasi tusikike na tuonekane kwa vipindi mbalimbali ambayo vitarushwa kitaifa.

Mheshimiwa Spika, wakati sasa umefika kwa Wizara hii kusimamia ujenzi wa viwanja vya michezo, viwe vya kisasa ili kukuza taaluma hii ya michezo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MKIWA A. KIMWANGA: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo Seif Khatib, pamoja na Manaibu Waziri wake, Mheshimiwa Bendera na Mheshimiwa Nchimbi, kwa kazi zote zinazofanywa na Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kutokana na habari, tunaiomba Wizara itoe, uhuru kwa vyombo vya habari ili vyombo hivyo viweze kuwa na Uhuru wa kutoa habari pasipo na Serikali kuweka mkono wake. Kuna baadhi ya habari huwekewa mguu ili zisitoke na ili mradi zinamgusa mtu fulani kwa maslahi fulani.

Tunaiomba Wizara hii ikomeshe tabia hii. Mfano, wakati wa Kampeni ya Mwaka 2005 tulishuhudia bila kificho *TVT* na *Radio Tanzania* ambavyo ni vyombo vya Serikali vikielemea kwenye Chama kimoja na kutotoa habari sawa au muda sawa. Habari ndiyo kiunganishi kati ya wananchi na uongozi, magazeti yote hata yale ya Serikali kuegemea Chama fulani na kutotoa fursa sawa kwa Vyama vyote vya Siasa.

Mheshimiwa Spika, hakuna ubishi katika kushuka kwa utamaduni wa Mtanzania. Utamaduni wa Mtanzania umepotea! Ukiangalia vazi la Taifa halina msisitizo, kwani vazi hili lilizinduliwa lakini sijui lilipotelea wapi? Kwani nchi kukosa vazi la Kitaifa ndiyo maana watoto wetu huiga mavazi toka nchi nyingine.

Mheshimiwa Spika, nashauri Kiswahili kiwe lugha ya Taifa na siyo tunavyofanya sasa hivi. Watoto wetu toka Shule za Chekechea wajue kuwa Kiswahili ni lugha ya Taifa. Maktaba za vitabu vya Kiswahili zifike mpaka Wilayani, pia Wizara ya Elimu iwahamasishe wanafunzi kukipenda Kiswahili na faida zake.

Mheshimiwa Spika, pia, napendekeza kuwe na Siku ya Utamaduni wa Mtanzania ili tuweze kukienzi Kiswahili, ngoma za jadi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya michezo mingi hapa nchini ni sawa na kusema imefilia au imekufa kabisa. Mfano, kurusha tufe, mkuki, kisahani, mbio za magunia,

kuruka chini, kuruka juu, kuogelea, *Tennis* na kadhalika. Kwa kuwa Wizara hii ni mpya, tuna imani kabisa michezo hii ikirudi katika Shule za Msingi, tuna imani michezo itapanda sana.

Mheshimiwa Spika, tunaiomba Wizara itumie uzoefu walionao ili kukuza michezo hiyo na tupate vijana watakaotuletea medali kama alivyoileta Koplo Samson Ramadhani. Pia, zawadi za mara kwa mara kwa washindi hao, basi tutawatia moyo vijana wetu na wataithamini michezo na kuipenda.

Napenda kumshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuthamini sana michezo na kutuletea Kocha toka nje. Ombi langu, naomba tumthamini, tumlinde na tumshauri inapobidi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. FAIDA M. BAKAR: Mheshimiwa Spika, napenda kupongeza matayarisho mazuri ya hotuba hii.

Napenda kuwapongeza Waziri na Manaibu Mawaziri wote wa Wizara hii ya Habari, Utamaduni na Michezo kwa kazi nzuri wanayoifanya kwa mashirikiano makubwa. Kwa hiyo, napenda kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, napenda kuongelea suala la Viwanja vya Michezo. Viwanja vya Michezo vya Watoto hapa katika nchi yetu, niseme havijapewa kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, watoto huwa na vipaji tofauti vya michezo mbalimbali, lakini vipaji hivyo havioneckani kutokana na watoto hawa kubakia nyumbani kwa kukinga viwanja vya michezo. Tujiulize kama hawana viwanja vya michezo wangechezea wapi?

Mheshimiwa Spika, kama tunataka michezo iimarike vizuri, kwanza toka utotonii, watoto wakianza toka wadogo tutakuwa na wanachuo wazuri hapo baadaye.

Mheshimiwa Spika, suala la viwanja vya michezo kwa watoto na watu wazima viendelezwe na viimarishwe.

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia suala la Vijarida vya ajabu. Naviita vya ajabu kwa sababu katika mila zetu za Kiafrika na hata dini karibu zote suala la tendo la ndoa ni la siri (ndani).

Mheshimiwa Spika, uhuru wa Vyombo vya Habari umefika mahali ambapo sasa ni tishio kwa watoto wetu hasa wa umri mdogo katika Shule za Msingi na Sekondari. Vipo vijarida vinavyoanikwa kwa wazi karibu kila Mtaa wapitapo watu wazima na watoto.

Mheshimiwa Spika, nikisoma maneno yanayoandikwa juu ya vijarida hivyo nitaitwa kichaa. Acha picha za akinamama za kupigwa na za kuchorwa zinadhalilisha utu wa mwanamke lakini baya zaidi, watoto wetu.

Mheshimiwa Spika, vijarida hivi ni hatari sana kwa watoto wetu kuliko yale yaliyopo kwenye mitandao ya Tovuti na *internet*.

Mheshimiwa Spika, tuondoleeni vijarida hivi Mitaani na hatujui ni nani ametoa kibali cha uchapishaji na kama hakuna, Wizara na vyombo vyatola ni kwa nini havichukui hatua za kisheria?

Mheshimiwa Spika, wenzetu kule nje ambapo baba, mama na watoto huweza kuogelea pamoja na miili yao nusu uchi, hawathubutu kwani majarida hata haya tunayoyaita ya udaku kama Uwazi, wao huyahifadhi kiasi watoto wapitapo, sio rahisi kusoma vichwa vyake vyatola ni kwa habari. Leo hii tunasema tunapambana na UKIMWI!

Mheshimiwa Spika, kwa kweli kuna haja ya mfumo huu, iwe utoaji wa habari ubadilike.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

SPIKA: Sasa ni wakati wa kuanza kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge na kwa mpangilio ambao nimepewa na Mheshimiwa Waziri Mohammed Seif Khatib, ataanza Mheshimiwa Naibu Waziri Joel Bendera kwa dakika 15 na ndipo atafuatiwa na Mheshimiwa Dr. Emmanuel Nchimbi kwa dakika 15. Baada ya hapo nitamwita Mtoha hoja.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE. JOEL N. BENDER): Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia hoja iliyopo mbele yetu, iliyotolewa na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo. Naomba nianze kwa kusema, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hii ni mara yangu ya kwanza kabisa kupata wasaa kama huu kuchangia hoja ya Wizara hii, naomba kabla ya kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge na mimi niungane na wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa ushindi wake murua alioupata katika uchaguzi uliopita.

Aidha, napenda pia kumpongeza kwa ushindi alioupata kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi kwa kura nyingi sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba pia nimpongeze Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Lowassa, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais na baadaye kuitishwa na Bunge Tukufu kuwa Waziri Mkuu wa Awamu ya Nne. Napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote waliochaguliwa na wale wote waliochaguliwa katika nyadhifa mbalimbali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima, napenda nichukue nafasi hii ya pekee kumshukuru sana Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuniteua kuwa Naibu Waziri katika Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo. Ninamshukuru sana na ninamhakikishia kufanya kazi kwa uadilifu na nitachapa kazi kwa jinsi Mwenyezi Mungu atakavyonijaalia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda nimpongeze Waziri wangu, Mheshimiwa Mohammed Seif Khatib, kwa kutusaidia kazi na kutufunza kazi na tukumbuke kwamba yeye ndio Waziri mzoefu wa siku nyingi toka mwaka 1988 ndani ya Bunge hili. Pia, nimpongeze ndugu yangu Emmanuel Nchimbi, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Mama Kijakazi, Wakurugenzi na Wafanyakazi wote wa Wizara, kwa jinsi wanavyotusaidia kufanya kazi katika Wizara hii. Nawapongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba vile vile niwashukuru kwa dhati kabisa wapigakura na wananchi wote wa Jimbo la Korogwe Mjini kwa imani na upendo mkubwa walionionyesha kwa kunichagua kwa vipindi vitatu mfululizo. Ninawapongeza na Mwenyezi Mungu awabariki, nitawalipa utendaji bora wa kazi kwa juhud zangu zote. Lakini pia, sitatenda haki kama sitamshukuru mke wangu Flora na familia yangu kwa ujumla kwa kenisaidia na kunipa moyo katika harakati za kisiasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani hizo, hasa kwa kuzingatia kwamba sisi tumepewa muda mfupi na tuna mambo mengi, nianze kuchangia hoja za Waheshimiwa Wabunge. Kwanza kabisa, napenda niseme wazi kwamba, michango ilikuwa ni mingi sana ambayo ni ya kina na ambayo imetusaidia sisi katika Wizara yetu kuweza kuwa na mwamko mpya wa jinsi ambavyo tunaendeleza michezo. Nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia. Ni michango mizuri, iliyoja maoni, ushauri, mipango na mikakati ya kuendeleza Sekta ya Michezo katika nchi hii. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, naomba kuwahakikishieni wale wote mliochangia kwamba, kwa kuwa hatutaweza kujibu hapa hoja zote, tutawaandikia kwa maandishi ili kila mtu aweze kupata majibu ambayo nadhani yatamridhisha. Tunashukuru sana maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii ambayo yalikuja kusomwa hapa na Mheshimiwa Haroub Masoud kwa niaba ya Mwenyekiti. Tunawapongeza sana kwa maoni yao na yote ni mazuri. Nataka niwahakikishie kwamba, tutayafanyia kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba pia niseme kwamba, maoni yaliyotolewa na Kambi ya Upinzani na Mheshimiwa Grace Kiwelu, napenda niwapongeze sana kwa sababu yote yamejielekeza katika kutoa ushauri. Nataka niwahakikishie kwamba tutayafanyia kazi kwa nguvu zetu zote. Katika michango iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge, mingi ilikuwa imejigawa katika vifungu.

Nasema hivyo kwa sababu Mheshimiwa Waziri wangu atakuja kutamka majina ya wale ambao wamechangia kwa sababu waliochangia ni zaidi ya Waheshimiwa Wabunge 60. Ni wengi mmo. Wapo walioandika na wale ambao wameongea na michango hiyo imegawanyika katika vipengele vikubwa vifuatavyo: Wengi wamezungumzia michezo

kuhusiana na ubovu wa viwanja, ukarabati na ujenzi wa viwanja katika Wilaya zao, Majimbo yao na Kitaifa.

Waheshimiwa Wabunge, nataka niwahakikishie kabisa kwamba, yote mliyoyazungumza, sisi kama Wizara tutayafanya kazi. Lakini kwa upande wa viwanja, naomba nitoe ushauri au maoni au mapendekezo na mikakati ya kutusaidia kufanikisha. Ujenzi wa viwanja uko katika sehemu nyingi.

Maeneo mengine ni Halmashauri zetu kwa kushirikiana na wananchi kujenga viwanja na maeneo mengine ni viwanja ambavyo sisi kama Serikali tuna mkakati wa kujenga Viwanja vya Kitaifa kama ambavyo tunajenga Uwanja wa Taifa sasa hivi. Tutaendelea kujenga viwanja vingine katika maeneo mengine ili tuwe na Viwanja vya Kimataifa na itusaidie angalau tunapajaribu ku-host Mashindano ya Kimataifa, basi tuweze kufanya hivyo bila matatizo yoyote.

Waheshimiwa Wabunge, ndiyo maana sisi kama Wizara tumetengeneza hiki kitabu kidogo, tutakiboresha zaidi ili kila Mbunge apate vipimo vya viwanja ambavyo ye ye mwenyewe kama Mbunge na wataalam wengine katika maeneo mengine wanaweza wakajenga viwanja katika Vijiji na ndiyo maana tumetoa *pamphlets* hizi ili ziwasaidie.

Waheshimiwa Wabunge, naomba mtazame katika *pigeonholes* zenu mtaona ili mtu asiwe na tatizo la kujua vipimo vya viwanja. Tunaomba Halmashauri nazo kwa kupitia Wizara yetu ya TAMISEMI, kuwe na Bajeti ambayo na sisi tutawasaidia kushauri, kuwe na Bajeti ya kutengeneza viwanja katika maeneo yetu. Hili ninalijibu kijumla kwa sababu ni wengi sana ambao wamelalamikia viwanja katika maeneo yao. Lakini pia, viwanja vingine itabidi sisi wenyewe tusaidie kama Wizara.

Mheshimiwa Spika, kule Wizarani kuna Kitengo Maalum cha Wataalam wa Viwanja (Miundombinu) na kuna Mkurugenzi anayehusika na masuala haya. Tutatoa utaalam kwenye maeneo na ushauri na kila Mbunge ambaye atatuomba tutafika huko ili tuwasaidie.

Mheshimiwa Spika, suala lingine la pili ambalo limechangiwa ni suala linalohusiana na mkakati wa vipaji kwa vijana. Tunapozungumzia michezo, ni vijana. Watu wamezungumza kwamba, tuanze michezo mashulen, tuwe na *academies*. Nataka niseme wazi kabisa kwamba, katika kitabu chetu, ukisoma, tayari tuna mwamko mpya wa kuhakikisha kwamba tunaanza michezo kuanzia ngazi ya umri mdogo na ndiyo maana tunamshukuru Rais wetu kwa kuhimiza michezo mashulen na suala hilo sasa Wizara ya Elimu na Wizara yetu tumelitilia mkazo zaidi ili lifanyike.

Pia, kama mnavyofahamu, Waziri wa Elimu aliishatamka hapa kwamba, kuanzia mwakani tunaanza michezo ya UMISHUMTA na UMISETA. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo ni zuri zaidi, wenzetu wa *TFF* nao, Shirikisho la Chama cha Mpira wa Miguu cha Tanzania, wana *program* nzuri tu ya kuanzisha michezo kuanzia ngazi ya utoto katika umri mbalimbali, *under fourteen, under*

seventeen na under twenty. Hilo nalo wanashughulikia. Kwa hiyo, nalo litafanyika bila matatizo.

Pia, Kampuni ya *Coca Cola* imetusaidia vizuri sana juzi kwamba, wao wametoa Shilingi milioni 300. Kuanzia mwaka huu wa 2006 wanaanza ligi ya vijana wadogo chini ya miaka 17 nchi nzima kuanzia Kijijini mpaka Taifa.

Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge mjiandae kuwa na timu zetu zile *football academies* ama michezo mbalimbali ambayo tutashiriki. Kwa hiyo, hili tunalifanyia kazi. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo limezungumziwa ni mafunzo. Huwezi kuendeleza michezo kama huna mafunzo, kwa maana ya makocha wa kutosha kwa michezo yote.

Nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba, Vyama vyा Michezo vyा Tanzania vyote vina *program* zao wenyewe ndani ya Vyama vyao. Kuna kozi fupi fupi za awali ambazo tunaita *intermediate*, za katì mpaka *diploma* na sisi kama Wizara tuna Chuo cha Malya ambacho tunakiendeleza kwa juhudi zetu zote ili kiweze kutoa makocha na Walimu wa kutosha katika nchi yetu.

Kwa upande wa elimu tuna Chuo cha Butimba ambacho nacho kinatoa Walimu na bado tunaendelea. Pia, tuna Vituo Arusha na Songea vyा kuendeleza michezo.

Mheshimiwa Spika, juzi tumepata bahati, watu wa *International Olympic Committee* nao wanataka watusaidie kujenga Chuo Bagamoyo. Kwa hiyo, tutajikuta tuna Vyuo vingi tu ambavyo vitatusaidia kutoa makocha wetu wenyewe. Kwa hiyo, hilo naomba muelewe kwamba tutalifanyia kazi. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge, naomba nizijibu. Kwa mfano, hoja ambayo imezungumzwa na Mheshimiwa Iddi Azzan kuhusu suala la migogoro katika vilabu vyetu, ameuliza Wizara inachukua hatua gani kukomesha migogoro katika vilabu? Amezungumzia hasa Simba na Yanga na kwamba pesa za Simba na Yanga zimechukuliwa na nani na Wizara inachukua mipango gani?

Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, migogoro tutaitatua kwa kuwa na Katiba nzuri.

Tumetoa maagizo kwa vilabu vyote na Vyama vyote vyा michezo nchini kuhakikisha kwamba wana Katiba ambazo sio za kujenga migogoro, bali za kuondoa migogoro.

Sisi kama Serikali, hatuwezi kuingia jikoni sana na ndiyo maana tunaihuisha Sheria ya Baraza la Michezo iendane na wakati, iwe na meno. Sasa hivi haina meno na ndiyo maana tunaihuisha ili iweze kuwa na meno ya kukabiliana na vilabu ambavyo vinafanya ovyo.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Azzan usiwe na wasiwasi, Serikali italitatu tatizo hili bila matatizo. Fedha za Yanga na Simba za kiwanja zimerudishwa Serikalini. Zile ambazo walipewa nusu zimesharudi.

Mheshimiwa Wabunge, lipo suala lingine ambalo limezungumziwa na Waheshimiwa Wabunge wengi katika maeneo yao. Wamezungumzia suala la wataalam wetu kutembelea maeneo.

Nataka niwahakikishie kwamba, suala hilo pale Wizarani, tumeweka mkakati kwamba Idara yetu ya Michezo na Baraza la Michezo watakuwa wanatembelea katika Mikoa mbalimbali na Wilaya mbalimbali kuweza kuona hali halisi ya maendeleo ya michezo yalivyo katika nchi yetu ili tuweze kuwa na mikakati na mipango mizuri ya kufanikisha suala hilo zima.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la Mheshimiwa Mama Margareth Mkanga, ambalo linagusa wale mavu. Kama mnavyojua, katika nchi yetu hii wale mavu ndiyo wametuletea medali nyingi sana.

Kwa hiyo, tunajitahidi kama Serikali kuhakikisha kwamba suala la wale mavu (*Paralympics*) tunalipa kipaumbele. Tumefanya hivyo na kuna makocha maalum ambao wanakuwa wanafundishwa ili waweze kusaidia wale mavu hawa.

Waheshimiwa Wabunge, kama mnakumbuka walipokwenda Ireland wamerudi na medali 21. Ni kitu ambacho kwa kweli kinafurahisha sana. Nataka nimtoe wasiwasi Mama Margareth kwamba hilo litafanyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nataka nirudie kusema kwamba, michango mingi imegusa maeneo ya watu binafsi na viwanja. Kwa mfano, Muleba hawana viwanja au ni vibovu. Ndugu yangu Ng'itu amezungumzia kabisa kwamba huko Ruangwa hawajawahi hata kuona mpira, wanaomba kocha aende huko.

Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie kwamba maeneo yote ya huko tutafika na kama mnavyojua, Wizara hii ni mpya, Bajeti yake mmeionia, tupeni fedha ili tuweze kutembea maeneo mengi tuone. Lakini sio hilo tu, ili na mwakani Bajeti iongezeke zaidi tuweze kusaidia kwenye masuala ya vifaa.

Mheshimiwa Spika, tukiwa na fedha nyingi, kama Wizara tutaweza kusaidia hata vifaa vyta michezo angalau kila Wilaya kupeleka mpira michache, kupeleka viatu na vitu vingine mashulenii na maeneo mengine, tutajitahidi kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Abbas Mtemvu na Mheshimiwa Iddi Azzan wamezungumza kwamba *coach* amefika. *Coach* huyu amefika, asije akawa *frustrated* na yuko pale juu. Amesema kwamba jamani mumpe ushirikiano isije ikawa kama Pape. *Coach* Pape alikuja, lakini hakupewa ushirikiano.

Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie kwamba kocha huyu kwanza analipwa na Serikali, napenda nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete, kwa kutimiza ahadi yake ya kutuletea kocha. Kocha huyu hatakuwa *frustrated*, tutamsaidia kwa uwezo wetu wote. Yule ambaye atam-*frustrate* tutamchukulia hatua za kisheria. Lengo letu ni kuona tunafanikiwa, tutoke pale tulipo twende juu zaidi. Kama alivyotuahidi ye ye ametupa programu kama Wizara kwamba kwa miaka yake miwili atakayokaa programu yake ametupa na tumeona ni programu nzuri ambayo si kufundisha timu ya Taifa tu, lakini pia kufundisha makocha na timu za vijana. Kwa hiyo, tutapata faida kubwa sana kwake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la michezo ya ridhaa na michezo ya *professional*. Kama mnavyojuu nchi nyingi sasa zimebadilika, tunakwenda *professionally*, lakini sisi Tanzania bado mpaka sasa ni *semi professional*, tunajitahidi vilabu ama vyama ambavyo vina uwezo wa kuwa *professional* kuvisaidia navyo viwezi kufanya vizuri na kuvisaidia ni kuhakikisha kwamba wanapata wafadhili ama wanafanya shughuli kibiashara. Klabu ikiwa kibiashara itabadilika, lazima tubalike, twende na wakati wa sasa. Dunia nzima sasa watu wamebadilika, wanakuwa ni *professional*, kwa hiyo, hili nalo ni suala ambalo linashughulikiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, muda ni mfupi Waheshimiwa Wabunge, wako wengi, Mheshimiwa Waziri, atawataja lakini nimezungumzia haya kwa ujumla. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE. DR. EMMANUEL J. NCHIMBI): Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo. Naomba nianze kwa kuchangia kwa kusema naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naungana na Waziri wangu kuwapongeza Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete, Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, Waziri Mkuu Mheshimiwa Edward Lowassa, Spika, Mheshimiwa Samuel Sitta, Naibu Spika, Mheshimiwa Anne Makinda, Wenyeviti wa Bunge Mheshimiwa Jenista Mhagama na Mheshimiwa Job Ndugai, kwa dhamana kubwa waliyokabidhiwa ya kuongoza Serikali na Bunge letu Tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile nawapongeza Mawaziri, Naibu Mawaziri wenzangu na Wabunge wenzangu kwa kuaminiwa na kuchaguliwa au kuteuliwa kushika nyadhifa zao. Niruhusu pia kumshukuru sana Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuniamini na kunteua kuwa Naibu Waziri, nitajitahidi kumsaidia Waziri wangu kwa juhudhi na uaminifu kutekeleza majukumu ya Wizara yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niwashukuru sana Waziri wetu, Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, ambaye anatulea vizuri mimi na mwenzangu, Katibu Mkuu Kijakazi Mtengwa na watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano mkubwa wanaotupa.

Naomba niwashukuru sana wananchi wote wa Jimbo la uchaguzi Songea Mjini kwa heshima kubwa walijonipa ya kuwatumikia kwa nafasi hii ya Ubunge kwa miaka mitano ijayo. Nitakosa usingizi kama sitawashukuru kwa namna pekee wanawake wa jimbo langu la Songea Mjini kwa kazi kubwa walioifanya kunipatia ushindi. Nawashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba sasa nijielekeze kujibu baadhi ya hoja zilizochangiwa na Waheshimiwa Wabunge, katika hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya hoja chache zilizochangiwa ni pamoja na hizi zifuatazo, Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, alitoa changamoto ya kutaka Serikali ione namna ya kuboresha mfuko wa utamaduni. Tunakubaliana naye moja kwa moja na tayari Serikali imeanza kuchukua hatua zikiwemo hizi nitakazozitaja, kwanza tumekwishatoa semina kwa maafisa utamaduni wa Wilaya zote katika mwaka wa fedha unaoishia. Lakini vile vile matangazo magazetini katika vipindi vya redio na katika mtandao wa tovuti tayari yameanza kutolewa ya kuutangaza Mfuko huu na maofisa wa mfuko husambaza habari sehemu mbalimbali nchini pamoja na vipeperushi. (*Makofi*)

Naomba vile vile nimjibu Mheshimiwa Adam Malima, Mbunge wa Mkuranga, kuhusu mchakato gani unafanyika katika kuratibu mtambuka na nafasi ya Mfuko wa Utamaduni. Mchango wa Mfuko wa Utamaduni kwa mikakati ya mtambuka ni pamoja na kudhamini shughuli mbalimbali za kiutamaduni ambazo zina mafunzo ya fani mbalimbali kwa jamii na kusaidia uanzishwaji wa filamu na makumbusho ndogo ndogo lakini pia kutoa tuze mbalimbali kwa wanajamii mahiri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu Mheshimiwa George Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, yeye pamoja na Mheshimiwa Mwanne Mcemba, Mbunge wa Viti Maalum, wao walitaka kujua ni mambo gani yanafundishwa katika Chuo cha Sanaa cha Bagamoyo. Mambo yanayofundishwa katika Chuo cha Sanaa cha Bagamoyo ni pamoja na ngoma, maigizo, muziki, uchoraji, ufundi wa jukwaa, fasihi, ukuzaji wa sanaa na uongozi.

Lakini pia walipenda kujua mipango ya Serikali katika kuboresha Chuo cha Sanaa cha Bagamoyo. Mipango ya Serikali katika kuboresha Chuo cha Sanaa cha Bagamoyo ni pamoja na kuanzisha mitaala mipyä ambayo imekwishaanza kutumika katika mwaka huu 2006/2007, kusomesha walimu zaidi katika vyuo vikuu, kuhakikisha chuo kimepata ithibati ya Baraza la Taifa la Mafunzo ya Ufundii, ambayo imeshapata tayari, kubadilishana walimu na Chuo cha Stephanga cha Sweden pamoja na kuanza mchakato wa chuo hiki kuwa wakala wa Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, halafu Mheshimiwa Grace Kiwel, Mbunge wa Viti Maalum na Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya, Mbunge wa Viti Maalum, wao walitaka kujua mchakato wa vazi la Taifa umeishia wapi, napenda nilithibitishie Bunge lako kwamba mchakato huo unakwenda vizuri baada ya shughuli ya awali kufanyika mwaka 2004 na

kushuhudiwa na Waheshimiwa Wabunge, sasa hivi waraka uko mbioni kwenda katika Baraza la Mawaziri na muda si mrefu tutapata vazi la Taifa.

Mheshimiwa Spika, mheshimiwa Mwantumu Mahiza, Mbunge wa Viti Maalum pamoja na Mheshimiwa Dr. Batilda Burian, Mbunge wa Viti Maalum, walitoa mchango wa kuishauri Serikali kushirikiana na wanajamii na Wabunge katika kuhakikisha kwamba watu wanavaa mavazi ya heshima. Serikali inakubaliana nao mia kwa mia. Tunatoa changamoto kwa wanajamii Watanzania wote kushirikiana kuhakikisha kwamba tunatoa mavazi ya heshima kwa wananchi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, halafu Mheshimiwa Mwajuma Hassan Khamis na Mheshimiwa Suleiman, waliongelea kuhusu kanuni za maneno mapya ya kiswahili na jinsi ambavyo kuna kutofautiana kati ya BAKITA na BAKIZA. Serikali ilikwisha liona hilo na tayari Baraza la Kiswahili Tanzania na Baraza la Kiswahili Zanzibar, vimeshaanza kufanyakazi kwa pamoja katika kuchambua maneno haya na kufanya maamuzi ya pamoja. Mheshimiwa Manju Salum Msambya pamoja na Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim walitaka Kiswahili kiwe katika Katiba ya nchi yetu ili kipate heshima zaidi. Napenda kulitaarifu Bunge lako kwamba mchakato umeshaanza wa kukirasimisha Kiswahili kitambulike rasmi kisheria kama lugha ya Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, halafu Mheshimiwa Ameir Ali Ameir na Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika walitaka Kiswahili kitumike katika makongamano mbalimbali ili kiweze kukua zaidi. Serikali itaendelea kuwashauri wahusika mbalimbali kufanya hivyo kwa sababu kwa kweli ni wazo la busara katika kukuza Kiswahili. Mheshimiwa Ali Haji Ali na Mheshimiwa Athumanji Janguo, wao walitaka uwepo mradi wa kutumia maneno ya lugha za jadi katika Kiswahili badala ya kuazima maneno kutoka mbali. Upo mradi ambaunajaribu kuliangalia hilo kama litawezekana na kuona, lakini mpaka sasa maneno ya lugha za jadi yanaendelea kutumika katika Kiswahili. Kwa hiyo, kasi tu labda ya kuongeza tutaendelea kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Capt. John Komba, aliongelea hali ya Ofisi ya BAKITA, tunamshukuru kwa changamoto yake, ni kweli hali ya Ofisi ya BAKITA ni mbaya na tayari tumekwishaanza kuchukua hatua na katika makabrasha yenu Waheshimiwa Wabunge, naona tumetenga fedha kwa ajili ya kuanza kutengeneza ofisi maalum kwa ajili ya Baraza la Kiswahili la Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile Mheshimiwa Capt. John Komba, alilaani vikali matumizi ya neno msanii kwa watu wasio na sifa za kuwa wasanii. Serikali inaungana nao kwamba wasanii lazima wawe na sifa kama za Waheshimiwa Wabunge, kama wewe Mheshimiwa Capt. John Komba. Kwa hiyo, tunakuuhakikisha kwamba Serikali itachukua hatua kuhakikisha kwamba neno msanii linapewa heshima lakini na Waheshimiwa Wabunge mkikutana huko wasio na sifa hizo msiwaite wasanii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja kuhusu ukaguzi wa filamu na michezo ya kuigiza Serikali inakubaliana moja kwa moja na Mheshimiwa Grace Kiwelu, kwamba kuna haja ya kusimamia kwa karibu mambo ya filamu, ukaguzi wake na kuhakikisha kwamba

zinazingatia maadili ya Mtanzania. Kwa hiyo, Serikali itasimamia kwa karibu lakini vile vile inaboresha nguvu ya Baraza la Filamu ili liwe na meno ya kuweza kudhibiti mambo hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nirudie tena kusema naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri na hasa kwa kuokoa muda na wakati huo umezijibu hoja zilizohusu sehemu yako. Kwa hiyo, namwita sasa Mheshimiwa Waziri Muhammed Seif Khatib ambaye ndiyo mtoa hoja Waziri wetu wa Habari, Utamaduni na Michezo. Anayo saa moja ya kujibu hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi jioni hii, kuanza kujibu baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge. Kwanza nakushukuru wewe binafsi kwa kunisaidia kuongoza asubuhi na jioni ya leo.

Pia nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, kwa michango yenu wale waliochangia kwa maandishi, waliochangia kwa kuongea na wale waliokaa kimya tu bila kusema chochote nao pia wamechangia hoja hii ya leo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia nashukuru sana Katibu Mkuu wetu mwanamama na watalaan kwa kusaidia kuandaa majibu haya ambayo sasa hivi tunayatoa. Namshukuru sana kwa umuhimu wake huo. Pia nitakuwa mwizi wa fadhila kama sitamshukuru Mheshimiwa Jakaya Kikwete, kwa kunitfea kuwa Waziri katika Wizara hii mpya. Napenda nimhakikishie kwamba nitafanyakazi kwa bidii kwa maarifa na uadilifu ili kura isiwe imepotea bure kwangu mimi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia ningependa nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuniamini mara kwa mara akiondoka hapa kunipa nafasi nikakalie kitie chake pale. Lakini wengine wana vivu wanataka mimi na wewe tugombane wananiambia Waziri Mkuu, mimi siyo Waziri Mkuu, Waziri Mkuu yupo hatugombani mimi na wewe bwana, wewe ni Waziri Mkuu, mimi nashughulikia Serikali Bungeni, lakini siyo Waziri Mkuu. Nashukuru kwa imani yako kwangu Mheshimiwa Waziri Mkuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia ningependa nishukuru sana wapiga kura wa Jimbo langu la Uzini kwa kunipa kura nyingi sana na kwa mujibu wa takwimu za kura ni kwamba mimi naongoza kwa asilimia kubwa kwa Tanzania nzima. Angalieni kwenye Tume ya Uchaguzi mtaona siyo mtu wa kunichezea mimi. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, ningependa pia niwashukuru wachangiaji ambao jumla wote walikuwa ni 70 kati yao wachangiaji 54 wameandika, 13 wameongea jioni hii na watatu wamechangia kwenye hoja ya Waziri Mkuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ni mazuri sana na tumeyachukua na tunaahidi kuyafanya kazi. Maoni pia ya Kambi ya Upinzani ya Waziri

Kivuli dada yangu Mheshimiwa Grace Kiwelu, ni mazuri sana ingawa baadhi yake katia chumvi chumvi hivi namsamehe, lakini mazuri sana. Mengi yake kwa kweli ni ya kuboresha Wizara yetu na namuunga mkono kwa maoni yake mazuri. Nataraja na yeze shilingi yangu hataichukua ya Waziri. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuahidi kwamba tunayafanya kazi yote hayo. Hatuwezi kujibu masuala yote kwa sababu ni mengi sana. Lakini tumejaribu kuyajibu na nashukuru sana Naibu Waziri, Mheshimiwa Joel Bendera, kwa kuanza kujibu masuala kuhusu mambo ya michezo na Mheshimiwa Dr. Emmanuel Nchimbi, amejibu mambo ya utamaduni na mnakubaliana na mimi kwamba kwa kweli hawa vijana ni wachapakazi kweli kweli. Nafikiri nina bahati sana kupata vijana ambao wenye upeo mkubwa na ambao wana nafasi nzuri baadaye. Nawashukuru sana Naibu Mawaziri kwa msaada wenu. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya kuna mengine niyachukue. Sasa naomba nitaje Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia hapa. Naomba sasa niwatambue wale wote ambao wamechangia hapa. Kwanza niwataje wale ambao wamechangia kwa maandishi nao ni Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Bahati Ali Abeid, Mheshimiwa Fatma Othman Ali, Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mheshimiwa Tatu Ntimizi, Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mheshimiwa Abbas Mtemvu, Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba, Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Dr. Batilda Burian, Mheshimiwa Kiumbwa Mbaraka, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa William Ngeleja, Mheshimiwa Mussa Azan Zungu, Mheshimiwa Mwantumu Mahiza, Mheshimiwa Joyce Machimu, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi, Mheshimiwa Mariam Mfaki, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mheshimiwa Eustice Katagira, Mheshimiwa Castor Ligallama Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mheshimiwa Fatma Mikidadi, Mheshimiwa Balozi Abdi Mshangama, Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mheshimiwa Omar Ali Mzee, Mheshimiwa Haji Juma Sereweje, Mheshimiwa Vita Kawawa, Mheshimiwa Haji Ali Haji, Mheshimiwa Manju Msambya, Mheshimiwa Ali Juma Haji Mheshimiwa Mwantumu Mahiza, Mheshimiwa Yono Kevela, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mheshimiwa Sijapata Nkayamba, Mheshimiwa Feteh Saad Mgeni, Mheshimiwa Dunstan Mkapa, Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Margreth Mkanga, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa Anastazia Wambura, Mheshimiwa Adam Malima, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Athuman Janguo, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Idd Azzan, Mheshimiwa Martha Mlata na Mheshimiwa Hadija Salehe Ngozi. (*Makofit*)

Sasa niwataje Waheshimiwa Wabunge ambao walichangia Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Anna Lupembe na Mheshimiwa Gosbert Blandes. (*Makofit*)

Mwisho wale ambao wamechangia leo asubuhi na jioni nao ni Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Waziri Kivuli, Mheshimiwa Ali

Haroon Suleiman, Mheshimiwa Zaynab Vulu, Mheshimiwa Nuru Bafadhili, Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mheshimiwa Thomas Mwang'onda, Mheshimiwa Capt. John Komba, Mheshimiwa Amina Mpakanjia, Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Mheshimiwa Dr. Dr. Omari Nibuka, Mheshimiwa Joel Bendera Naibu Waziri na Mheshimiwa Dr. Emmanuel Nchimbi, Naibu Waziri. Kama wako watu nimewasahau naomba wanisamehe nitawataja baadaye. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa najaribu kujibu hoja za Wabunge, nitaanza hoja ya Waziri Kivuli na nafikiri ni muhimu nitaje mwanzo kabla sijachoka ili nielezee kwa ufasaha zaidi na nieleweke hasa hoja ile ya mradi wa TTVT. Mengi ambayo yamesemwa ni kweli na Serikali hii haipendi kuzusha kama jambo la kweli, inakubali kweli na hiyo ndiyo heshima ya Serikali. Kwa hiyo, naomba niseme kwamba yale ya kweli ni ya ukweli na yaliyotiwa chumvi yametiwa chumvi naomba hayo niyaseme ndio maelekezo ya Serikali yetu kwamba zama za uwazi na ukweli na ari mpya, kasi mpya, nguvu mpya na viwango pia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika swal la kwanza limeulizwa kwamba mkataba haukutayarishwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali wakati ujenzi wa TTVT unajengwa. Nasema ni kweli mkataba haukutayarishwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, lakini mkataba huo uliandaliwa na Ofisi ya Waziri Mkuu na akashirikishwa kwa ushauri wa Mwanasheria Mkuu na pia Mwanasheria Mkuu wa Serikali akakubali. Nasema tena ni kweli mkataba haukutayarishwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu bali ultayarishwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, lakini baadaye Mwanasheria Mkuu akashirikishwa na akaidhiinisha Mkataba ule uwepo kati ya sisi na yule mjenzi wa Kituo cha TTVT mara ya kwanza. (*Makofi*)

Swali la pili, tumeambiwa kwamba mzabuni wa kwanza wa TTVT *Epsilon* hayajakabidhi kazi ambayo ameianza, ni kweli kazi kafanya kuna maeneo hajakabidhi nayo ni Arusha na Mwanza, kwa sababu wakati mjenzi huyu anajenga Serikali iligundua kwa ushauri wa Kamati ya PAC na wengine kwamba alitakiwa ajisajili kwenye Msajili wa Makampuni ya Ujenzi, hakufanya hivyo. Kwa hiyo, alipotakiwa ikabidi aje ajibu Mahakamani na baadaye akaondoka nchini. Kwa hiyo, ni kweli hajakabidhi kazi hii na alipotakiwa hakupatikana bado anatafutwa na vyombo vinavyohusika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la tatu, taratibu zilizotumika kumpata mkandarasi kwamba zilikuwaje, kwamba zabuni haikutangazwa, hapana, zabuni ilitangazwa na wakatokea watu nane, wakashindana, baadaye wawili wakashinda, mwisho akapatikana huyu ambaye ameshinda. Kwa hiyo, hili si la kweli.

Mheshimiwa Spika, swal lingine liliulizwa kwamba kampuni gani ilikuwa mshauri katika awamu ya kwanza ya ujenzi wa mradi wa TTVT. Kampuni ambayo ilikuwa mshauri wa kwanza ilianzishwa ni kampuni ya Thomson Foundation ilikuwa mshauri katika kuandaa uchambuzi yakinifu kwamba wapi ijengwe Televisheni na iwekwe wapi. Huyu Thomson Foundation ilikuwa ndiyo mshauri wa wakati ule. Lakini wakati ule hakukuwa na consultant kwa ajili ya mradi endelevu, hilo nalikubali. Baada ya kugundua

makosa haya tukatafuta mshauri mwengine ambaye anaitwa Tauren, huyu ndiye aliendelea kufuatilia ujenzi wa TTVT ya Serikali. (*Makofî*)

Swali lingine likuwa ni kwamba utaratibu gani ulitumika kumlipa mkandarasi wakati ule, alikuwa akilipwa baada ya kuwasilisha *invoice* zake. Wakati ule kulikuwa hakuna sheria za manunuzi kwa hiyo, tunasema haya ndiyo majibu ambayo nimeyajibu kwa uwazi kabisa na ningependa Waheshimiwa Wabunge waelewe kwamba Serikali hii haipendi kuficha yale ambayo ni ya kweli. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nijaribu kuendelea kujibu baadhi ya hoja za watu wengine hasa hoja hizi za habari ambazo hazikujibiwa na mtu yejote. Katika hoja ya Wapinzani imesema kwamba ziko sheria ya magazeti, kwamba sheria hizi mchakato, sheria zilizopitwa na wakati kwa hiyo, lazima zibadilishwe. Tunakubali kwamba sheria hizi zinapitiwa sasa hivi na sasa hivi kuna Muswada wa Sheria utakuja Bungeni hapa wa habari ambao utapitia na kujaribu kuondoa mapungufu yaliyotokea. Kwa hiyo, nakubali kwamba haya ni ya kweli na kufanya hatua hiyo ikusaidie.

Lingine limeulizwa kwamba magazeti ya Serikali hasa *Daily News* hayachapi hotuba za Wapinzani Bungeni. Kweli hatuchapi, lakini kwa sababu ukiwa na Hotuba ya Rais au Waziri analipia kwa hiyo, kama Mpinzani anataka hotuba yake ichapwe mle analipia tu na hatuna ugomvi nayo. Bei yake si ghali sana ni shilingi laki nane basi ukitoa utachapiwa hotuba yako na rangi na picha na kadhalika ili ufurahi mwenyewe. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, lingine kuhusu upendeleo wa uchonganishwaji rushwa katika baadhi ya vyombo vya habari kwanza kabisa nitaendelea kuhimiza vyombo vya habari kufuata maadili vyombo ambavyo havizingatii maelezo vitachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria kwamba kuna rushwa ndani ya vyombo vya habari. Kwa hiyo, tunaomba wenyewe wasikie vyombo vya habari na sisi tukisikia tutachukua hatua.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maslahi ya waandishi, ambayo yamezungumzwa na Mheshimiwa Zaynab Vulu, kwamba maslahi ya waandishi wa vyombo vya habari hayatolewi na Serikali, yanatolewa na mmiliki wa chombo cha habari. Kwa hiyo, sisi Serikali tutaboresha maslahi ya wafanyakazi wetu, lakini pia wenye vyombo vyao binafsi wanatakiwa waboreshewe maslahi ya wafanyakazi wao. Niliwahi kuzungumza wakati mmoja pale Tanga na Chama cha Waandishi wa Habari, wakalalamika kwamba sisi waandishi wa habari wa kujitegemea maslahi magumu. Nikawaambia undeni chama chenu cha kutetea haki zenu mpaka leo hawakuunda. Kwa hiyo, njia rahisi ni kuunda chama chenucha kutetea haki zenu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, lingine kwamba Serikali itoe tamko kuhusu vyombo vya habari vinavyotoa picha chafu. Hili jambo ambalo nalikubali kwamba ni jambo baya sana. Lakini na hawa waandishi wa habari tunawaambia wasikie na mamlaka ya mawasiliano inakamilisha utaratibu wa kununua mtambo. Serikali ina mpango wa kununua mtambo ambao utaweza ku-*monitor TV* zote na redio za nchi kwa wakati mmoja mwaka huu. Kwa hiyo, itatusaidia kuweza kujua nini kinafanyika katika redio zote. Kwa

hiyo, Serikali ina mpango wa kununua vyombo hivyo ili isaidie kuangalia uendeshaji wa vipindi hivi katika *TV*.

Pia tunazungumza na wamiliki wa *internet* kutafuta mbinu bora za kuzuia kuingiza katika *internet* picha chafu ambazo zinapotosha maadili ya nchi yetu. Lakini naomba pia wazee wetu, watoto wakacheze, wasiende kuangalia picha kila mmoja ana wajibu huo. Kuna mtu mmoja alikuwa mzazi alikuwa kafungua picha zile ambazo si nzuri kasahau kwamba kaacha wazi *TV* akaenda kuoga, akasikia watoto wake wanacheka, akaja mbio na taulo lake, akavua taulo akafunika ile *TV* mambo yakawa mabaya zaidi bora ya *TV* kuliko hiyo. (*Makofi/Kicheko*)

Waheshimiwa Wazee wetu wasaidieni watoto wenu wasiangalie *TV* nyie wenyewe muwe mfano kwenye hivyo, mkisahau *TV* watoto wataangalia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna maelezo kwamba *TV* zetu na redio zinaonyesha sehemu kubwa ya maudhui kutoka nje. Ni makosa kwa mujibu wa taratibu zetu kwamba maudhui ya ndani yasipungue asilimia 60, ni kweli kwamba baadhi ya *TV* na redio zinakuwa kama vile za nchi za nje ambayo ni makosa kabisa. Tunaomba kwamba wamiliki wa vyombo vyta habari wajaribu kuweka maudhui ya ndani ya nchi yetu na ya Afrika, ili kujenga uzalendo, umoja na mshikamano kwa kutumia picha zetu, hodari wa kusifu mambo ya nje. Yeye mwenyewe kasema kwamba amesema mtu anasifia mtu wa nje mwenyewe hajui pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, safari zingine kutoa fursa sawa kwa vyama vyta siasa katika kampeni za uchaguzi. Tumelaumiwa kwamba vyombo vyta habari vinapendelea Chama Tawala wakati wa Uchaguzi si kweli na tumeona wenyewe kwamba kuna vipindi maalum katika *Television*, vyama vina *vote* kabisa, kama wenyewe hawaendi pale. Lakini kwa kweli sheria zipo na Tume ya Uchaguzi ndiyo inayomiliki taratibu wakati wa Uchaguzi kwa hiyo, si kweli kwamba Serikali inatumia vyombo hivyo wakati wa kampeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Amina Mpakanjia, anasema iundwe sheria ya kuwalinda waandishi wa habari, ni kweli kwamba waandishi wa habari lazima walindwe na katika Muswada unaokuja wa sheria, tutajaribu kuweka hilo kujaribu kuwasaidia waandishi wa habari ili walindwe na kazi zao.

Kuhusu vyombo vyta habari vyta *IPP* vinavyoandika suala la *NSSF* na *Quality Group* niseme kwamba sisi Serikali hatuwezi kuingilia ugomvi kati ya Manji na Mengi, ni wao wenyewe na Wabunge msipelekwe huko katika ugomvi ambao sisi hautuhusu. Sisi hatuwezi kuingilia ugomvi ambao si wetu, wenyewe wanajuana. Kila mmoja afanye anavyotaka mwenyewe. Kwa bahati nzuri wako mahakamani sasa hivi. Kwa hiyo, hatuna cha kuzungumza zaidi, lakini nizungumze la pili kuna mtu kazungumzi kuwa vyombo vyta habari vyta *IPP* vinatumia nafasi yake kumpaka matope mwenzake, hilo ni kosa kwa mujibu wa sheria. Huwezi kutumia chombo chako cha habari kwa ajili ya maslahi yako mwenyewe. Labda nisome eneo ambalo sera inasema hivyo. (*Makofi*)

Kwa mfano kifungu 3 (2) cha Sera ya Taifa ya Habari ya utangazaji ya mwaka 2003 inasema hivi: "Chombo cha habari kisitumiwe kwa manufaa binafsi ya mmiliki au mtendaji, bali kitatumiwa kwa maslahi ya umma." Kwa hiyo, natoa wito kwa wenyewe vyombo vyahabari, tafadhari tumieni vyombo vyahabari kwa maslahi ya umma siyo kwa yenu binafsi. (*Makofî*)

Niendelee, kuna wengine wanalamika kwamba magazeti yanachafua majina yao. Kuna Baraza la Habari, mtu ye yote ambaye kachafuliwa jina lake basi anatakiwa apeleke habari, ufanuzi zaidi au ampeleke mtu mahakamani. Sisi tusingependa kuingilia mambo ya watu binafsi. Pia kuna suala la kuanzisha ofisi ya habari Lindi, tunaomba kwa mwaka huu hatuna fedha hizo labda kipindi kijacho. Lingine tuna suala Waziri Kivuli kuhusu vyombo vyahabari Serikali ina ubaguzi wakati wa uchaguzi nimeshasema hilo toka mwanzo kwa hiyo, sitasema tena. (*Makofî*)

Lingine ni kwamba TUT kuendeshwa katika misingi ya biashara, tutaendelea na maandalizi ya kuunda Maktaba za Serikali ili iweze kuendeshwa. Wanaolalamika kwamba waandishi wa habari kwamba Serikali inashindana na vyombo binafsi katika kutafuta biashara za magazeti, redio na *television*, ni kweli kwa sasa hivi. Lakini sheria yetu inatuambia kwamba imepewa muda maalum kwa *TV* ya Serikali ifike wakati iwe inajitegemea yenye we bila kutoa matangazo ya watu wengine. Ikitaka kushindana basi ifungue *channels* zake maalum ya *TV*, redio yake ambayo yake hailipi fedha na Serikali ishindane na watu wengine katika uwanja sawa wa biashara. Hayo ni maelekezo ya Serikali.

Kwa hiyo, kwa sasa hivi itabidi *Television* ya Serikali na redio yake ijitegemee yenye we na ishindane na *TV* za watu binafsi iende zote kwa haki kwa nchi yetu.

Kuna pia maelekezo kwamba usikivu wa Redio Tanzania na TTV bado kwenye baadhi ya maeneo, ni kweli mitambo mingi mibovu, mitambo ya Kigoma, Mwanza, Nachingwea, bado iko chini sana. Lakini baada ya muda mitambo ile itaingiza nguvu kazi yake na hivyo kuonekana kwa sehemu kubwa zaidi. Naomba mtuvumilie.

Mheshimiwa Spika, nafikiri mengi haya nimeyasema, niende katika eneo lingine la Mheshimiwa Abbas Mtemvu. Yeye anasema kwamba kilio cha watoto wa Mzee Morice Nyunyusa juu ya nyimbo za baba yao. Ile inapigwa Tititi!! Tititi!! Tititi!!. Anasema Mzee Nyunyusa alitayarisha ngoma hiyo kabla ya taarifa ya habari, baada ya makubaliano kati yake na RTD miaka 60 iliyopita. Kulikuwa na makubaliano kati ya Mzee huyu na Redio Tanzania wakati ule. Kwa hiyo, akarekodi ngoma yake, akapewa pesa, akaondoka, hana lake tena. Lakini Serikali imempa heshima, imempa tuzo, medali gani sijui katika medali za Serikali. Lakini kweli kwa sasa hivi haki yote kaichukua mwenye we. Kwa hiyo, tusikilazimishe kitu ambacho hakipo katika utaratibu wake. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, niendelee na hoja zangu. Nizungumze mambo ambayo kidogo yamezungumzwa na wenzangu hapa kuhusu hili la usikivu kwanza nisije

nikalisahau. Watu wengi wamezungumzia juu ya usikivu wa Redio Tanzania, inakuwa kama mpiga ramli bwana.

Mheshimiwa Spika, limezungumzwa juu ya usikivu na kwamba maelezo kutoka *TICRA* kwamba aidha, usikivu wa Redio Tanzania na *Television* ya Taifa pamoja na utangazaji binafsi utaimarika baada ya kuanza matumizi ya teknolojia ya *digital*.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni Tanzania iliwakilishwa na Mamlaka ya Mawasiliiano Tanzania kwenye mkutano wa Kimataifa na kupanga masafa yatakayotumika kwa teknolojia ya *digital* kufanyika Geneva mjini Uswisi. Mkutano huo uliamua kuwa kuanzia tarehe 16 Juni 2006 hadi 17 Juni, 2015 itakuwa ni kipindi cha mpito kuendelea kwenye *ku-provide digital*. Watangazaji wote na wawekezaji wote katika Sekta ya Utangazaji hawana budi kuzingatia kipindi hiki hadi mwaka 2015 ni kipindi cha maandalizi ya kutumia teknolojia ya *digital*s. Serikali inawataka wawekezaji wote katika sekta ya Utangazaji waanze kuagiza na kununua mitambo ya *digital* kwa vile watazamaji wote wa *Television* wanatumia *running analogy* Serikali kwa kutumia *TICRA* inaandaa sera ya umilikaji inayosimamia mabadiliko hayo.

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwamba kwa muda kati ya mwaka huu na 2015 ni wakati wa mpito wale wote wenye kutumia *television*, *radio* ya *analogy* sasa wajiandae kwa sababu ikifika wakati huo itafutwa. Kwa hiyo, lazima wajiandae kwa sababu wakati huo itafutwa kwa hiyo lazima wajiandae ili wapate usikivu mzuri na pia watu wengi zaidi wapate masafa kwa sababu ya usikivu, kwa sababu ya sheria mpya.

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kusema kuwa suala la michezo limezungumzwa sana Mheshimiwa Joel Bendera, namshukuru sana. Ningependa na mimi nichukue nafasi hii nimshukuru Rais wetu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa ahadi yake ya kiungwana, amesema ataleta kocha, wako wawili pale na mmoja yuko njiani anakuja, watatu watakuwa. Kwa hiyo, tuliomba mmoja yeye kakupa watatu, Mungu akupe nini.

Lakini nini maana yake, maana yake ni kwamba Serikali sasa hivi imeamua kuwekeza katika michezo. Huwezi kuvuna kama huwekeza, muda wote ukilalamika hatuwekezi. Serikali imeamua sasa hivi iwekeze ili kutekeleza azma yake ya kuinua viwango vya michezo nchini. Jana nilimwambia Kocha wa Brazil, tumeamua kuchukua Kocha Brazil, kwa sababu ndiyo kwenye kiwango cha juu cha mpira duniani na tumechukua kocha huyo kwa sababu yeye kasomea mpira wa miguu, umecheza na umefundisha timu mbalimbali, kwa hiyo, hakuna sababu ya kushindwa sisi hata kidogo.

Naomba nimwunge mkono mwalimu wangu Haruna, kwamba tumpe nafasi kocha basi aonyeshe, tupunguze tabia ya kuwatia doa, mara anafukuzwa. Mpeni nafasi aonyeshe uwezo wake ili tupate mafanikio. La pili, tumejenga kiwanja cha kisasa kabisa pale Dar es Salaam, awamu ya kwanza, tutakuwa na viwanja viwili, mwakani cha tatu. Mungu akupe nini. Tunawekeza mamilioni ya fedha yamejengwa kwa ajili ya kuwekeza michezo hapa nchini kwetu. Lazima tuiunge mkono Serikali katika azma yake njema hii.

Mheshimiwa Spika, tumekubali sisi na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu tuanzishe michepuo ya shule za muziki na *football* na michezo. Hapo ndipo chimbuko na viota vya wachezaji bora sana. Tumeruhusu Serikali kwamba watu binafsi waje nchini, wawekeze katika maeneo hayo ya kufungua hizo *academy* tumeambiwa na Mbunge mmoja kwamba huyo Beckham huyo anatoka kwenye *academy* hakuzuka tu hivi hivi. Kwa hiyo, nafikiri kwamba hili lingine ni kwamba ni kuwekeza. (*Makofit*)

La tatu, nimezungumza na Wizara ya Ulinzi kwamba tushirikiane katika kutafuta vipaji vizuri vya wanajeshi na kuimarisha michezo mbalimbali katika nchi yetu na tumekubaliana nayo pia waanzishe shule ya michepuo kwa ajili ya michezo mbalimbali katika nchi yetu. Tumeamua tuimarishe Chuo cha Michezo cha Malya. Nilikuwepo pale juzi mimi, Mheshimiwa Richard Ndassa, huyo anashangilia. Nilikuwapo pale juzi nikatoa vyeti, kulikuwa na Walimu kutoka Kenya, Uganda wa Chuo Kikuu wanafundisha Malya pale, chuo kizuri sana. Nafikiri ni muhimu sana.

Pia Serikali inakusudia kuagiza walimu wengine mbali ya mpira wa miguu, sita mwaka huu kwa ajili ya michezo mbalimbali. Kwa hiyo, ndugu zangu nasema kwamba hiyo ni jitihada ya Serikali ya kuwekeza katika eneo hili la michezo. Naomba msaada kwenu mtusaidie na tumpe nafasi kocha wetu ili aendeleze michezo. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, tumezungumza pia suala la sanaa ambalo limezungumzwa sana na Mheshimiwa Capt. John Komba kwamba wasanii wako wengi sana mpaka wezi ni wasanii pia. Lakini pia hata sisi wanasiasa unaambiwa msanii huyo bwana. Akipanda jukwaani pale, mtu anatoa hotuba pale anakuambia msanii huyo bwana. Kwa hiyo, nasema tuache kuwaambia watu wasanii, wanasiasa ingawa kila mtu msanii kwa sababu ukiamka asubuhi unachagua nguo gani uvae, tai gani uvae imechi shati lako na koti lako. Msanii huyo kabisa na kioo pale sote hapa hatufanani hapa, kwa sababu kila mmoja anataka avae apendeze. Lakini msanii ni muhimu sana katika maisha yetu. Kwa sababu ni eneo ambalo linaburudisha watu, linawapa burudani watu baada ya kufanya kazi kutwa nzima, linajenga umoja, mshikamano, uzalendo. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, haya ni mambo muhimu katika sanaa. Sasa sanaa yetu ilekezwe huko, iende katika kujenga uzalendo, umoja na mshikamano wa nchi yetu, sanaa pia ni ajira. Mimi nimeona hapa wenzetu hawa *ma-promoter* hawa ingawa wengine hawawapendi. Mtu anatoka Marekani anakuja hapa tumbo wazi, anacheza kutwa nzima pale. Lakini anapata pesa, tumbo wazi kabisa. (*Makofit*)

Lakini anapata pesa msanii yule tena mamilioni ya fedha. Marekani si karibu, mbali sana. Kwa hivyo, sisi Watanzania lazima sasa tuwekeze pia kwenye sanaa, tusiwe walaji wa sanaa ya nje. Hodari sana kusifu Wamarekani, Wanigeria, Wakongo, sisi wenyewe ah! ah! Tubadilike sasa hivi na Sera katika Wizara yetu itakuwa ni mfano wa kwenda kuwekeza pia katika sanaa ili tuwe na wasanii wetu bora zaidi nao wao pia waende nchi za nje, waitwe. (*Makofit*)

Kwa hiyo, tunaendeleza pia kuwa na shule za sanaa katika michezo. Lingine limezungumzwa kuhusu lugha ya Kiswahili. Niseme kwamba lugha yoyote, ndugu

zangu Wabunge ni kama binadamu mwenye uhai, isipokua, itakufa. Usipoitumia inakufa ndiyo tabia ya lugha. Kama vile Kilatini, hakipo sasa hivi. Kwa hivyo, wakati mwengine mimi wanapokosea watu matamshi ya Kiswahili, sihamaki sana kwa sababu tunajitahidi, si wanajitahidi hao? Wewe msahihishe tu usimcheke. Kwa sababu amejitahidi, si lugha yake ya kwanza ile. Msahihishe ili akuze lugha yake na watumiaji wawe wengi zaidi badala ya kumcheka. Kwa hivyo, nasema lugha yoyote duniani kama isipotumiwa, isipokuwa na mabadiliko haitakua, itakufa.

Mheshimiwa Spika, Tanzania tuna bahati lugha yetu inakua kila siku. Leo tuna watumiaji zaidi ya milioni 100 duniani kote. Kwa hivyo, ombi langu ni kwamba tufanye Kiswahili kikue, kiendelee, kichukue maneno mapya ambayo yanabadilishwa kwa mujibu wa mazingira yetu na mfumo wetu hapo itakuwa lugha ya Kiswahili imekomaa sana. Lugha zote hizi duniani zina lugha za kigeni basi, ukienda Uingereza kuna mchanganyiko wa lugha mbalimbali pale. Kwa hiyo, si vibaya Kiswahili kuchukua maneno ya kigeni lakini tu yakubaliane na mazingira ya mfumo wa lugha ya Kiswahili ndiyo muhimu zaidi hapo. (*Makofi*)

Lakini nakubaliana na wazo lingine kwamba muhimu kwanza tupate lugha za Kiafrika, za Tanzania kwanza, kabla ya kwenda Arabuni au Ureno. Ni vema tuangalie hapa Tanzania kwetu lugha zetu hizi hakuna lugha yenyenye maana hii? Kwa hivyo, wananchi lazima tufanye hivyo. Lakini niseme kwamba wale ambao kama ni *ku-declare interest* mimi ni mpenzi sana wa lugha ya Kiswahili. Wale ambao wanabeza Kiswahili naona kwamba ni watu ambao hawana fadhila hata kidogo kwa lugha hii. Kwa sababu Kiswahili ndicho kilichomlea tokea mdogo. Lugha ya kwanza kusikia wengi ni Kiswahili, toka mdogo. Kwa hiyo, kimetulea toka wadogo, wengine tunataka kwenda Peponi kwa kuhubiri lugha ya Kiswahili, au siyo? Kiswahili, Kanisani, Kiswahili, Peponi tunahubiri Kiswahini lakini Kiswahili hukitaki, maana yake nini? Kiswahili kilitumika, ni lugha ya ukombozi wakati wa kudai Uhuru katika nchi yetu *TANU* na *ASP*. Tukaungana nchi yetu tukapata Uhuru. Kiswahili kimetumika pia katika kuandaa wapigania uhuru wa Msumbiji, *South Africa*, wa Angola, kwa Kiswahili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, shulen i tumejifunza kwa Kiswahili na *primary* zote hizi ndiyo msingi wake hapo, kwenye msiba Kiswahili, harusini Kiswahili, sokoni Kiswahili, bandarini Kiswahili. Hebu tufikirie sisi makabila zaidi ya 130 Bungeni hapa kama si Kiswahili tungekuwa hali gani, kama si Kiswahili hapa hatuelewani, kuna Msukuma, kuna Msegeju, ingekuwa hali ngumu hapa. (*Makofi*)

Kwa hiyo, sisi tumefadhiliwa sana na lugha ya Kiswahili. Lazima tuone kwamba huyu mfadhili wetu, tuipende, tuikuze na kueneza na wakati mwengine tunasuasua hapa, nje ya mipaka yetu wanakipenda Kiswahili. Ndiyo maana leo katika Afrika, *AU* Kiswahili ndiyo kinatumika na Bunge la Afrika, Kiswahili kinatumika. Tumeomba *SADC* itumike na Afrika Mashariki inatumika.

Kwa hiyo, hatuna sababu sasa hivi ya kuona woga kwamba Kiswahili, lazima tutumie Kiswahili na mfano tuwe sisi wenyewe hapa. Utaona kule katika sinema katika *TV* vijijini huko, watu wakiwa 30, 40 mzungu mmoja tu, lugha pale Kiingereza kwa

sababu ya nini mzungu mfadhili pale, basi. Mnaadhibiwa kwa sababu mfadhili mzungu tu basi. (*Makofi*)

Lazima tubadilike jamani, leo duniani, hakuna Chuo Kikuu chochote duniani ambacho hakuna Idara ya Kiswahili, hakuna. Duniani kote, China, si Urusi, kila mahala Idara ya Kiswahili ipo. Leo wakubwa wote hawa duniani wana Idhaa ya Kiswahili, *Deutstche Welle, Voice of America, BBC, Mjerumani, China*, nani atabakia, hakuna.

Kwa hivyo, nafikiri ndugu zangu hata Saudi Arabia pia wanatumia Kiswahili pia. Sasa ndugu zangu naseme tuonee fahari lugha yetu na tuone kwamba Kiswahili ndiyo mkombozi wetu. Sasa mstakabali wetu nini. Tumeombwa hapa na mimi nashauri kwamba Bunge likubali kwamba Katiba yetu ndani mle hamna kifungu chochote kinachosema kwamba Kiswahili lugha ya Taifa. Ninaomba Wabunge kwamba wakati umefika mtushauri, mtuhimize, tuingize katika Katiba kwamba Kiswahili itakuwa lugha ya Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hapo ndipo tutakapoona kweli Watanzania tumejikita kweli kweli kama lugha hii ndiyo lugha ya Taifa. Sisemi mimi kwamba Kiingereza kisisomeshwe hata kidogo. Kisomeshwe Kiingereza, sana tena na Kireno na Kifaransa, Kiswahili pia kiwemo lakini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema, kama mpiga ramli. Nimalizie kwa kusema kwamba Mheshimiwa Haroub Said Masoud, ana tabia ya kunichokoza. Asubuhi kaniambia kwamba nimetunga shairi la Paka Shume, kweli kitabu hiki hapa. Fungate la Uhuru, kitabu changu hiki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, amesema kwamba nimetunga kitabu hiki, lakini hakusema kwa nini nikatunga shairi hili.

Mheshimiwa Spika, sasa nataka nimwambie. Shairi linasema kwamba, paka mtaka vya watu itakufika ajali, watampaka machatu nyumbani kwa Bwana Ali, kwako utapata kitu, kwani mwenye mkali, nyumba yake madhubuti, wala haina mushkeri, sakafu kangeliti, ukuta matofali, juu kaezeka bati, kuta pande mbili na milango ulifungwa vitasa na kufuli, babu hushika panga kazi yao ukatili na wengine huwanyonga kungoja kauli. Bwana Ali huyo. Amezungusha senyenge pande zote mbili, zinauma kama nge, zikatoka katika mwili kutakuwa na makenge vya aina mbalimbali. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kweli nilitunga shairi hili, lakini niseme nilitunga kwa nini? Kuna Bwana mmoja kuna paka shume mtu huyo, alikuwa ni meneja wa Bwana Ali, nikaambiwa mkali huyo usijaribu. Lakini bahati mbaya maskini, Bwana Ali kafa, na paka kafa. Naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimeambiwa wengine kuwataja hapa. Ni Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Hemed Mohamed Hemed, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Magdalena Sakaya na Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi. Naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA USALAMA WA RAIA: Mheshimiwa Spika, naafiki. (*Makofi*)

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 96 - Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo

Kifungu 1001 – *Administration and General* 1,569,482,000/=

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *Vote 96, Programu Number 10, Sub-Vote 1001*, Kifungu 250100 Mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninazo hoja mbili za Sera zote kwa Waziri. Wakati akitoa majumuisho hapa alizungumzia suala la TVT. Namshukuru kwa kusema nusu ukweli na nusu si ukweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema mwenyewe kwanza sisi tumetia chumvi. Taarifa tulioitoa sisi hapa ni taarifa ya Bunge lako zima ambalo iliwasilishwa kwenye Bunge na ikapokewa na Bunge na tumechukua taarifa hii *Library* ya Bunge. Kwa hiyo, taarifa hii ni ya Bunge si ya kwetu sisi. Kwa hiyo, haina chumvi. Hilo la kwanza.

Lakini la pili katika taarifa hii ilitakiwa Serikali ichukue hatua. Moja ilikuwa ni kwamba wahusika wawe wamepelekwa *PCB* kuchunguzwa na hatimaye taarifa itolewe. Lakini pili, kuna watu ambao walivunja taratibu na pale aliposema kwamba wakati huo taratibu za *procurement* hazikuwa sahihi taarifa ya *PAC* iliipata kutokana na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali alipochunguza. Kwa hiyo, kulikuwa na taratibu zilikiukwa ndiyo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali akatoa hoja na ndiyo maana *PAC* ikakaa kulichunguza taarifa hiyo na hatimaye ikawasilishwa kwenye Bunge zima la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hiyo siyo taarifa sahihi aliyoisema, ningemwomba Waziri akubali tu alivyosema kwamba kweli yametokea na Serikali itachukua hatua. Nafikiri ingekuwa jambo la busara zaidi kuliko kusema kwamba tumetia chumvi. Kama ingekuwa ndiyo Bunge limetia chumvi na siyo sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni suala la viwanja vya michezo ambavyo vinamilikiwa na CCM. Sote tunakumbuka kwamba kabla ya mfumo wa vyama vingi nchi yetu vyama vya siasa tulivyokuwa navyo yaani wakati wa *ASP* na *TANU* na hatimaye CCM vilikuwa ni vyama dola. Kwa hiyo, Serikali na chama kilikuwa ni kitu kimoja. Mimi mwenyewe nilikuwa ni Kamisaa wa Chama katika Wizara ya Mambo ya

Ndani. Kwa hiyo, ilikuwa ni Chama na Serikali ni kitu kimoja, ndiyo maana Serikali wakati ule hata Bajeti yake ikipangwa ilikuwa tunakwenda kwenye Chama kupata idhini ya Chama. Kwa hiyo, kila mipango ilikuwa inakwenda chamani na kurudi ilikuwa chama na Serikali ilikuwa ni kitu kimoja na ndiyo fedha za viwanja vile vilivyojengwa nyingi zimetoka Serikalini.

Kwa hiyo, halali kusema kwamba ile ni mali ya CCM, ile ni mali ya wananchi wa Tanzania na ilikuwa wakati ule chama ni chama dola chama cha CCM ni chama dola, chama *ASP* kuwa chama dola, chama cha *TANU* kilikuwa ni chama dola. Ndivyo ilivyokuwa na hata ndani ya Katiba mpaka ilivyobadilishwa mwaka 1992. Kwa hiyo, sahihi kusema kwamba zile ni mali za Serikali. Tunaomba Serikali itueleze kwa ufasaha. Sera hii kwa nini isibadilishwe, utaratibu huu wa *ku-own* CCM viwanja hivi visibadilishwe na kurudishwa Serikalini? Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti. (*Makofi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. JUMA J. AKUKWETI): Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatana na Kanuni za Bunge Namba 55(3) inasema: “Halikadhalika Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema, na kuomba mwongozo wa Spika. Kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema katika kikao hicho.”

Sasa nakusudia kuitumia hiyo. Mheshimiwa aliyeongea sasa hivi amezungumzia taarifa ambayo iliwekwa Mezani, sasa naomba mwongozo wako. Mimi sikumbuki kama taarifa hii ilijadiliwa na Bunge hili na kutolewa maamuzi na maamuzi hayo huwa ndiyo ya Bunge. Ila nakumbuka kweli iliwekwa Mezani. Sasa kama taarifa imewekwa Mezani hajajadiliwa na kutolewa uamuzi wa Bunge kuhusu taarifa hiyo, je, bado inakuwa taarifa na Bunge linatakiwa kufuata hiyo kwa sababu tu imewekwa Mezani? Ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mwongozi wa Spika, ni kama ifuatavyo, Taarifa ambayo inatambuliwa ya Bunge ni ile ambayo imepitishwa na Bunge. Taarifa iliyowekwa Mezani na Kamati ni taarifa ya Kamati tu na hailifungi Bunge kwa namna yoyote ila tu kama Bunge lingeridhika sasa na kuiweka katika mkondo katika orodha za shughuli za Bunge ili Wabunge wapige kura na kuamua maudhui yake. (*Makofi*)

MHE. JOHN S. MALECELA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe taarifa kwenye Bunge hili kwamba katika viwanja vilivyojengwa mimi ningependa nitoe mfano wa Dodoma, *Jamhuri Stadium* hakukuwa na senti ya Serikali hata moja na wote waliojitolea kutoa fedha zao, kutoa vyombo vya kujengea na kila kitu walitoa baada ya kuhamasishwa na Chama Cha Mapinduzi au *TANU* wakati ule. (*Makofi*)

Kwa hiyo, kwa mtu sasa hivi kuja kusema kwamba ndiyo yeye alikuwa CCM alikuwa Kamisaa, lakini alikuwa ni mmojawapo chini ya CCM akihamasisha kwamba viwanja hivyo vijengwe na CCM. Kwa hiyo, ni vya CCM. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Tunaendelea tupate ufanuzi wa Mheshimiwa Waziri, kuhusu yote. Ile kwamba taarifa ni ya Kamati bado haizuii kwamba Mheshimiwa Mbunge apate ufanuzi na kuhusu viwanja hivi vya michezo nayo pia tupate ufanuzi.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nafurahi sana Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed kuungama kwamba ripoti ile si yake kaichukua Maktaba na mimi nikijua kwamba ile ripoti si yake ni ya Kamati ya Hesabu za Serikali, nafikiri na ililetwa hapa Bungeni ikawasilishwa bila kujadiliwa. Lakini haizuii mimi kusema yale ninayotaka kusema. (*Makofi*)

Mimi nimesema kwamba taarifa ya Kambi ya Upinzani, nzuri na ina chumvi kidogo. Sikusema hili, yako mengi yamezungumzwa hapa. Kwa hiyo, sikusema hili, nimesema mambo mengine ni ya chumvi, mengine ni ya kweli. Sasa niseme kwamba ni kweli kwamba kulikuwa chini ya Kamati ya Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa, Kamati ndogo ya kuchunguza mradi huu na watu wengi walihojiwa na hata na mimi nilihojiwa kuhusu mradi huu. Mwisho wakaamua kwamba ichukuliwe hatua kwa wale amba wanafikiri kwamba wamehusika na wale kama walihusika kwa rushwa basi ipelekwe kwenye *PCB*. Yamefanyika hayo, yule Mkandarasi mkataba umefutwa na taarifa hii imekwenda kwa Tume ya *PCB* na tayari wamechunguza kumaliza wale wote amba wanahusika hapa nchini, sasa wanashubiri wale amba wako nje ya nchi amba wengi wao wako Nairobi. Kwa hiyo, tusubiri taarifa hiyo baadaye tutapata matokeo yake. (*Makofi*)

Kuhusu viwanja ni kweli kwamba viwanja hivi vimejengwa na wanachama wa Chama cha Mapinduzi na wapenzi wao na mimi naamini Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, alichangia pia, kwa sababu alikuwa CCM wakati ule. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mambo haya ya kuchangia sawa sawa na harusi. Mimi nina harusi yangu naomba Mheshimiwa John Malecela, unichangie, Mheshimiwa Edward Lowassa, nichangie. Mimi mke ni wangu peke yangu, si watu wote. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiit, kwa viwanja hivi, viwanja vina wenyewe, wenyewe ni CCM. (*Makofi*)

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Kwanza Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako. Kwa sababu mimi nilipotoa hoja nilimwuliza Waziri anayehusika na hatimaye Mheshimiwa Juma Akukweti, alitumia Kanuni akainuka kunijibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui Mheshimiwa John Malecela, aliponyanyuka alitumia Kanuni gani, sikupata mwongozo. Nataka mwongozo wako. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, katika Kanuni zetu Mbunge ye yeyote anaruhusiwa kama anayo taarifa ya kutoa iwe katika Kamati au wakati Bunge linaendelea

anaruhusiwa kutoa taarifa bila kutoa kwa maandishi, anaruhusiwa kusimama na kutoa taarifa.

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Nakushukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwongozo huo.

Naomba na mimi basi nitumie kifungu hicho hicho na mimi nitoe taarifa tu kwamba wakati Kamati ilipowasilisha taarifa hii kwa Spika, kwa utaratibu vile vile anayo mamlaka ya kusema je, jambo hili lilijadiliwa, akasema lilishatosha Serikali itachukua hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ndiyo jibu alilotupa Mheshimiwa Spika na kwa utaratibu Spika, anayo miongozo anayoitoa nayo inachukuliwa kwenye *practice* kwamba hiyo miongozo inaweza kufanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ndiyo mwongozo aliotupa Mheshimiwa Spika Msekwa wakati ule kwamba baada ya kuiwasilisha kwenye meza alisema tayari ni taarifa ya Bunge na kwa sababu Kamati ya Bunge iliyofanya kazi hiyo ni Kamati ya Bunge ilifanya kazi kwa niaba ya Bunge, basi hii taarifa inatosha. Hiyo ndio taarifa aliyotupa Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, bado nashikilia kwamba hii taarifa ni taarifa ya Bunge kwa sababu ilifanya kazi na Kamati ya Bunge na gharama za Serikali ilikuwa ni ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unilinde, naomba unilinde.

MWENYEKITI: Endelea, ndio maana mimi nimeketi tu, usiwajali hao wewe endelea.

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Kwa hiyo, kwanza naomba kuweka hilo sawa kwamba hii ni taarifa ya Bunge na ndio maana tumechukua kwenye Maktaba ya Bunge, hatukuchukua mahala pengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni la viwanja, mimi naomba Serikali tukubali pindi sisi tutakapotoa *documents* za kuonyesha kwamba kulikuwa na bajeti ya Serikali iliyojenga viwanja hivi, je, Serikali iko tayari kubadilisha maamuzi yake?

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kwa yote mawili ambayo ameuliza Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, si kazi ya Kamati hii kwa sasa hivi kinachotakiwa hapa ni ufanuzi, alichotoa sasa ilani kwamba sasa wataendelea kufanya utafiti katika wakati muafaka nadhani linawezekurejea hapa Bungeni na litakabiliwa kwa namna ya taratibu zinavyoruhusu. (*Makofi*)

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, *vote 96, sub vote 1001*, kifungu 250100 Mshahara wa Waziri.

Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kukiri mapungufu, ndio mara nimesikia toka nimekuja hapa, hongera sana. Mimi nahitaji ufanuzi katika maeneo mawili, katika mchango wangu wa maandishi Sheria ambazo Tanzania iliridhia ikiwa kama mwanachama wa *SADC* ambazo zinahusiana na mambo ya habari na kuanzia sasa nilizieza sina haja ya *kuzi-mention* kwa sababu naamini Mheshimiwa Waziri amepitia karatasi yangu.

Sasa toka mwaka 2001 hadi sasa hivi 2006, hakuna sheria yoyote ambayo imetungwa nikiimaanisha sheria za Tanzania ili kuweza kuingiza vile vitu ambavyo vilikubaliwa *SADC*. Sasa nilikuwa napenda Mheshimiwa Waziri anielezee kama hayo mabadiliko ya sheria za habari ambazo anasema ziko zinataka kupelekwa cabinet haya mambo pia yalikubalika katika *SADC* nayo yamo ndani.

La pili naliuliza hapa kwa sababu nimepitia vifungu vyote viwili sijaona fungu lake linahusiana na mkakati kabambe wa maendeleo ya michezo *plus* maendeleo ya soka *specifically*, sasa tumeambiwa kuna mkakati kabambe na Mheshimiwa Waziri hapa ametuambia kwamba Serikali imejitolea kumlipa mshahara na ni kocha wetu kutoka Brazil. Sasa mkakati kabambe ni zaidi ya mshahara, ningependa Mheshimiwa Waziri aniambie fungu hilo ambalo limetengwa maalum kwa ajili ya programu ya michzo au programu ya soka kwa mapana yake iko wapi, ambayo sasa tunajua kwamba hili litatusaidia kutufikisha Tanzania katika sehemu fulani, nashukuru sana.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swalí kuhusu *SADC* kwamba tunasema kwamba kuna Muswada unakuja Bungeni kuhusu sheria za habari. Muswada huo zaidi unazungumzia juu ya mambo ya ndani ya nchi yetu na hayo ya *SADC* yakija hapa, ukiwa Mbunge unaweza kutoa maoni yako na Muswada uko tayari pia kurekebishwa, kwa sababu mara nyingi Wabunge wakipewa nafasi kutoa maoni yao na nayakubali na sikatai lolote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili naomba uniruhusu nimwachie Naibu wangu, kwani hao ni wasaidizi wangu aidha, atoe maoni yake kwa niaba yangu. (*Makofî*)

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE: JOEL N. BENDERÀ): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa maelezo kuhusu hoja ya Mheshimiwa Halima Mdee, kama ifuatavyo. Anazungumzia kuhusu suala la mkakati wa maendeleo ya michezo kwamba uonekane kwenye kitabu. Kawaida katika vitabu hivi vya hotuba hatutengenezi, hatuweki mkakati mle, programu zinaandalila na Wizara na ziko kwenye sekta husika. Kwenye idara ya michezo kuna programu ya maendeleo ya michezo katika nchi nzima na kwa michezo na vyama vyote vya michezo, vimeandaa programu zao za muda mfupi, za muda wa kati na muda mrefu na zipo wanazo katika vyama, hatuwezi kuziweka kwenye kitabu cha bajeti itakuwa ni *li-volume* la ajabu na huwa halimo humu.

Lakini kuhusiana na *specific*, swalí lake la *national team*, programu ipo, tunayo programu hapa ambayo kwanza chama chenyewe cha *TFF* wanayo programu ya maendeleo, ni *volume* kubwa tu tusingelileta hapa. Lakini kwa *national team*, tunayo programu ambayo kocha wetu ameshatoa hii ya miaka miwili na naweza nikamtolea *copy* nikampa naye akaona. (*Makofî*)

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, inaonekana Waheshimiwa wawili hawakunielewa swali, Mheshimiwa Joel Bendera, hakuelewa swali langu. Mimi sikusema programu, nimesema fungu, fungu ambalo litaendesha hizo programu zenu mnazozisema. Nimeangalia vitabu sijaona fungu, sasa kama anaweza akanielekeza itakuwa ni vizuri zaidi. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Lakini taabu yake ninyi mnapenda kushika tu mshahara wa Waziri, ukurasa wa 266 ipo *Sports Development*, ni 6004, ndani yake kuna hata *Transfer and Subsidence* ambazo nadhani ndio zinakwenda kwenye michezo milioni 309, sasa ukiwahi tu kwenye mshahara, kila mara nawaasa usiende tu kwenye mshahara, tazame humu na ukienda kitabu cha nne, utakuta mambo mengi tena yanahusu uendelezaji wa michezo, pamoja na ujenzi wa mahosteli sijui, *Sports Development* ukurasa wa 128, *Multi Central Projects* na nyingine anapata msaada wa China pamoja na ujezi wa kiwanja bilioni 35 kwa hiyo sijui kama Waziri mimi nadhani inatosha Mheshimiwa Halima Mdee.

Nawaasa hasa Wabunge wa vijana kama wewe kuchukua hivi vitabu na kuviangalia vizuri tena wewe unaonekana unakipaji kizuri tu, maendeleo yako ya baadaye mazuri, lakini kujiendeleza ni pamoja na maandalizi, wewe ni mwanasheria kama mimi, maandalizi, *preparation*. (*Makofii*)

MHE. MANJU S. MSAMBYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na nina hakika mimi nimeangalia vizuri. Lakini vile vile nimemsikia vizuri Mheshimiwa Waziri alipokuwa anajibu. Nazungumzia kifungu cha 96, programu namba 10, *sub vote 1001* kasma ndogo kabisa ya mshahara wa Waziri, 250100. Ninayo mambo mawili.

La kwanza linatokana na kauli ya Mheshimiwa Waziri alipokuwa anajibu hoja zetu hapa, amekiri kwamba ni makosa vyombo vy ahabari vy kwetu hapa nchini kutumika kama *relay* ya vyombo vy aje. Sasa nilitaka nimuulize Mheshimiwa Waziri, hili amelifahamu lini, kama amelifahamu kwa muda mrefu, ni kwa nini Serikali imeendelea kukaa inaona vyombo vyetu vinatumika kama *relay* na katika kutumika huko vinaharibu mila na utamaduni wetu, kwa *ku-relay* mila na utamaduni wa aje kutumia vyombo vy aje.

La pili, Mheshimiwa Waziri ametuambia na mimi ni mmoja katika watu waliochangia kwa maandishi, ameleeza kwamba na ninanukuu kwa sababu nimeandika, amesoma sheria au kanuni wakati anajibu. Kasema: "Chombo cha habari kisitumike kwa manufaa binafsi, bali kwa manufaa ya umma," lakini vile vile akatuambia suala ambalo wengi tumeuliza, lipo mahakamani, lakini suala hilo hilo ambalo liko mahakamani wenye vyombo hivyo wanaelewa suala hilo liko mahakamani, nalo lina malumbano, kati ya Manji na Mengi, lakini mmoja kwa sababu ana vyombo vy ahabari, anamfunika mwingine kwa kutumia vyombo vyake akiwa anajua kwamba suala liko mahakamani, Serikali inasema nini wakati inatambua kabisa suala liko mahakamani na mtu anatumia chombo chake kuendesha malumbano kwa suala ambalo liko mahakamani na Serikali inajua?

MWENYEKITI: Kwa hili la pili sina hakika kinachoombwa Serikali ifanye nini, kwa sababu kama huyu anayeendesha malumbano kwa kumfunika mwenzie, anavunja sheria, ndio hayo hayo yatakuwa mahakamani sasa, yatapata uamuvi na ataadhibiwa. Sidhani kama inatakiwa Serikali itoe tamko kusimama upande mmoja au mwingine kwa suala ambalo liko mahakamani.

MHE. MANJU S. MSAMBYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pengine ni fafanue.

MWENYEKITI: Hebu fafanua.

MHE. MANJU S. MSAMBYA: Nainachotaka kufafanua ni kwamba kwanza nafafanua kutokana na kauli ya Mheshimiwa Waziri alipokuwa anajibu kwamba tayari suala liko mahakamani na ni kweli halitakiwi kujadiliwa katika chombo kingine chochote na Serikali imekiri hivyo. Serikali inatambua liko mahakamani, kwa nini haichukui hatua kama tulivyochangia ya kuweza kuzuia malumbano haya, kwa sababu hata katika michango yetu tumeeleza na Serikali inafahamu, hata vyombo vya dini vilijaribu kuingia kati hili, hayo malumbano yasimame kwanza mpaka masuala haya yamalizike mahakamani. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mimi nadhani hili hakuna haja ya Serikali kusema chochote, itazidi kuharibu tu, kwa sababu vipi leo Serikali mathalani iyafungie magazeti ya Mengi, ndio baadhi ya hatua inayoweza kuchukua na hata ikikemea tu itakuwa inaingilia kitu ambacho kitaamuliwa na mahakama. Sasa kwa kiasi fulani kama yule anaendelea kuchapisha, anaonekana kama anadharau mahakama, yeze naye atakuja kupata adhabu yake kule kule mahakamani. Mimi nadhani tusubiri, tunaamini mahakama zetu na zitachukua hatua inayofaa, Mheshimiwa Waziri jibu la kwanza lile linahusu vyombo habari kutumika kama rilei ya vyombo vya nje. (*Makofi*)

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ni jibu swali la ndugu yangu Mheshimiwa Manju Msambya, ambaye anataka achukue shilingi yangu, sijui kwa nini. (*Makofi*)

Kuna masuala mawili nimesema, nimesema suala la maudhui kuwa asilimia 60 *content*, hili ndilo la Serikali kwamba si kosa, *ku-relay* nje, inategemea kitu gani kama kuna *breaking news*, ubaya gani kusikiliza *breaking news* au mambo ya elimu, kuna ubaya gani, si tatizo, tatizo ni kwamba ni kiasi gani ya maudhui inaonyeshwa na maudhui ya aina gani. Kwa hivyo, mimi najua kwamba *TV*, ina *relay*, *CCTV*, *ITV* na kadhalika, si jambo la kawaida, si vibaya ndugu zangu kujifunga siye tusione nje, hapana, la msingi nasema waangalie wanarusha kitu gani na wakati gani na madhumuni gani, lakini si makosa ya kuonyesha hivyo muhimu kwamba angalau asilimia 60 iwe ya maudhui ya ndani. (*Makofi*)

MHE. AMINA C. MPAKANJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, *vote 96, program 10* kifungu kidogo 250100, mshahara wa Waziri.

Nilichangia kwa kuzungumza lakini pia nilichangia kwa maandishi, niliomba ufanuzi katika mambo yafuatayo na mimi nitaomba ufanuzi wangu uwe katika taasisi ya utangazaji ambayo inabeba Redio Tanzania Dar es Salaam na *Television* ya Taifa. Kulikuwa na matatizo ya malalamiko kwa baadhi ya wafanyakazi ambao wako chini ya Taasisi hii ya Utangazaji kuhusiana na mishahara, matatizo ya uongozi, pamoja na matatizo ya kiutendaji kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri Mkuu Mheshimiwa Edward Lowassa, aliunda Tume ya kuchunguza malalamiko na alitoa muda wa mwezi mmoja. Muda huo umekwisha kazi naomba ufanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, kama Tume hiyo tayari imekwishakamilisha kazi yake na uchunguzi uliofanywa umegundua nini kati ya yale ambayo yalikuwa yakilalamikiwa? (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufanuzi wa pili ambao ningependa kuupata kupitia Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005/2010, ukurasa wa 142, kwa idhini yako naomba nisome hiki kifungu, vyombo vyahabari: "Kwa kuzingatia mchango mkubwa unaotolewa vyombo vyahabari katika jamii katika kipindi cha mwaka 2005/2010, CCM itazitaka Serikali zichukue hatua zifuatazo; (a) nadhani hainihusu, mimi niko (b), kueneza Redio Tanzania, Dar es Salaam na *Television* ya Taifa (TVT) nchi nzima na kuwa hewani kwa saa 24 kila siku."

Ningependa kupata ufanuzi wako Mheshimiwa Waziri kama matayarisho haya yamekwishaanza na lini yatakuwa yamekamilika rasmi utuambie Redio Tanzania na *Television* ya Taifa ni lini itaanza kwenda hewani kwa saa 24?

Mwisho, napenda kujua TVT kama *Television* ya Taifa, ni kwa nini hairushi matangazo ya moja kwa moja ya soka ya michuano mbalimbali ya Ulaya na badala yake mashindano haya au michuano hiyo inaonekana katika *TV binafsi* na wakati ikiwa inaonekana, yanatokea maandishi ambayo yameandikwa hivi ifuatavyo *CFI in collaboration with National Television present* yaani *CFI* kwa kushirikiana na *Television* ya Taifa, inakuletea pambano kati ya timu fulani na timu fulani, lakini si *Television* ya Taifa ambayo inaonekana katika *television binafsi* na kwa nini basi labda Serikali imekaa kimya wakati ikiwa inaandikwa ni *Television* ya Taifa wakati maonyesho yanaonekana katika kituo binafsi, naomba ufanuzi Mheshimiwa Waziri. (*Makofî*)

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii nitoe ufanuzi sio kujibu.

Kwanza suala la kwanza Waziri Mkuu hajaunda Tume, ametafuta timu ya watendaji ndani ya Serikali yenye, sio ya nje, ya ndani na madhumuni makubwa ilikuwa kwenda kufuatilia juu ya uendeshaji na fedha na kazi yake ikipatikana ni kwa ajili zaidi ya Serikali kujua na kuipanga zaidi. Lakini bado taarifa hiyo mimi sijapata kwenye Kamati hiyo, hilo nalo linashughulikiwa, tupe muda tufuatilie baada ya kutoa taarifa hiyo.

La pili kuhusu muda wa kuwa redio ni kweli Chama cha Mapinduzi kimesema kwamba nia yake kwamba *TV* ya Taifa na Redio inatakiwa iende hewani kwa saa 24 na hii kwa sababu haiwezekani Serikali *TV* yake na Redio ikifika usiku inalala, lakini binafsi wanakesha kucha, haiwezekani, pia si nzuri kwa usalama wetu pia na kadhalika.

Kwa hiyo, tukaamua sasa hivi lazima iende saa 24, lakini ina matayarisho na gharama kubwa sana, kwa hiyo tumeanza *TV*, sasa hivi inakwenda saa 24, nafikiri Mheshimiwa Amina Mpakanjia hana habari, lakini sisi tunaochelewa kulala tunajua mpaka saa nane TTV bado ipo mpaka asubuhi. Redio tumeanza kwa *PRT* saa 24, baadaye tutakwenda kwa nchi nzima kwa redio, lakini ni gharama kubwa lakini tumeanza pole pole, kwa *TV* inakuwa saa 24 na pia *PRT* kwa saa 24.

Kuhusu kuonesha mashindano makubwa ya Kimataifa katika *television*, pia ni gharama kubwa pia, lakini mnafahamu ndugu Wabunge kwamba *TV* ya Serikali ina majukumu mengi ya Kitaifa zaidi, lazima ione ipi muhimu, lakini watu binafsi wengi wao ni biashara zaidi, hatuwezi tukarusha mpira saa 24 na kuacha mambo ya msingi ya maendeleo ya nchi yetu, hata hivyo tumejitahidi baadhi ya wakati kuonesha kama mwenyewe amesema kwamba mashindano haya ya Afrika ya *TFA* inaonyesha, naungana na wale ndio wenzetu ambao tunaungana nao, huwezi kuwa peke yako nchi hii duniani bila kupata mtu wa kukusaidia, hasa mambo ya Kitaifa, tunajitahidi lakini kufahamu kwamba *TV* ya Taifa ni ya Taifa ina majukumu ambayo ni ya Kimataifa lazima ipate nafasi pia ya vipindi vingine, sio mpira na kadhalika. (*Makofifi*)

MHE. AMINA C. MPAKANJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, japokuwa kuna sehemu hajanielewa, naona amejibu tofauti na ambavyo mimi nimeuliza na amesema ile iliyoundwa na Waziri Mkuu ilikuwa si Tume, bali ni watu kutoka Serikalini, sasa sijui hiyo ni kitu gani. (*Makofifi*)

Lakini ningependa kukuuliza Mheshimiwa Waziri kwamba unafahamu kwamba kuna malalamiko ya wafanyakazi chini ya Taasisi hii ya Utangazaji ambayo iko chini ya Wizara yako, iko chini ya Serikali, chini ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, ndio maana nimekuuliza kuhusiana na mishahara, kuhusiana na matatizo ya uongozi, utendaji mzima, kuna malalamiko yanayoendelea pale kwa chini chini. Ninachoweza kukuambia ni kwamba kama ufahamu kuna kama mgomo baridi ambao uko pale *Television* ya Taifa, kwa hiyo basi, ningeomba unipe ufanuzi kama unalifahamu hilo na ni njia zipi ambazo unazichukua sasa hivi katika kulitatua tatizo hilo.

La mwisho, ambalo nimekuuliza nilikwambia kwamba inaonekana kwenye *TV* lakini sio *Television* ya Taifa kwa maana ya TTV, kwenye *TV* maandishi yameandikwa *CFI* kwa kushirikiana na *TV* ya Taifa inakuletea yaani *TV* ya Taifa ya nchini mwetu, lakini inaonekana katika vituo vingine binafsi. Kwa nini *Television* ya Taifa inatumika katika *TV* nytingine? Hayo ndio yalikuwa maswali yangu.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimwambie Mheshimiwa Amina Mpakanjia kuwa ninafahamu, mimi ni Waziri wa Wizara hiyo na nimekuwa na mikutano hiyo na wakati Waziri Mkuu

anaongea nilikuwepo pia, kule Redio Tanzania, kwa hiyo, nafahamu kila kitu nakifahamu kama kulalamika, ni jambo la kawaida malalamiko, kila mmoja analalamika tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la msingi kwamba Waziri Mkuu Mheshimiwa Edward Lowassa, amekwenda, ni kwamba anajali matatizo ya wafanyakazi, ni jambo la kupongezwa kwamba Waziri Mkuu amekwenda mpaka kusikiliza matatizo yao na amesikia na ameunda Kamati kuchunguza ili kuwasaidia matatizo hayo. Kwa hivyo, nawatupe nafasi, baadaye tutawasaidia.(*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la pili silifahamu, Mheshimiwa Amina Mpakanjia, anataka nini sijui, la *CFI* na TTV mimi sijaelewa, labda unisaidie.

MWENYEKITI: Unaweza kufafanua, unachosema kuna ubaya kwa matangazo ya *TV* ya ushirikiano wa baina ya TTV na *CFI* kuonekana kwenye vyombo binafsi, ndio hivyo?

MHE. AMINA C. MPAKANJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi, wanaotangaza ni vituo vingine vya *TV* vya hapa nchini kwetu Tanzania, lakini sio TTV. Ila maandishi yanaonekana kwenye *screen*, yanaonyesha kwamba *CFI* kwa kushirikiana na TTV yaani *Television* ya Taifa ndio inakuleta mpambambano huo au shindano hili, lakini si *Television* ya Taifa inayoonesha, yaani kwa nini inaonekana katika *TV* nyiningine? Sijui kama nimeeleweka.

MWENYEKITI: Mimi nimekuelewa, unachosema ni kwamba wakati unatazama matangazo hayo, mechi inaendelea ni kwamba tangazo linalopita kwenye *ticker tape* yaani ya maelezo ya maneno, linasema unaletewa, unarushiwa haya matangazo na chombo cha Taifa na *CFI*, lakini unapotazama pale unaona *Channel Ten*, ndio hivyo? Sasa ndio unauliza hii ni halali, kwamba matangazo yanaonekana ni ubia baina ya *CFI* na TTV halafu wanaonyesha ni *Channel Ten*. (*Makofi*)

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ndio hivyo sijui kuna ubaya gani ushirikiano huo. Kwa sababu kama mtu hataki atashitaki tu, huwezi kwa *TV* ya mtu kama mwenyewe hataki, atakushitaki tu, ni sheria za habari huwezi ukachukua wewe *TV* yako ukaweka kwa mwenzako bila mwenyewe kukubali utashitakiwa. Kwa hivyo, ni makubaliano au kama hataki mtu anashtaki tu kwamba wewe unahuku kipindi changu mimi sitaki mwenyewe, ni utaratibu wa habari, ninavyojua mimi.

MWENYEKITI: Au vyombo vile viwili vimedhamini hilo na vimepata fedha kwa kuitishia kwa hao wengi. (*Makofi*)

MHE. MUSSA AZAN ZUNGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, *vote 96*, programu 10, *sub vote 1001* mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais wetu alipokula kiapo cha kuongoza nchi hii, wanaapa kwa kuwa muadilifu na kuafuata Katiba ya nchi yetu. Iweje vyombo vya habari,

vimwandike vibaya kuwa Rais wetu hupendelea madhehebu fulani ya dini katika uteuzi wake na mpaka leo Serikali haijakanusha hizi habari na hizi habari si za ukweli wala si sahihi kufika mitaani na wananchi wakapata hisia tofauti. Hata gazeti la Serikali halijakanusha hizi habari, mimi naomba maelezo kuwa Waziri atupatie kwa nini mpaka leo Serikali haijakanusha habari hizi ambazo zinazidi kuendelea katika magazeti hapa nchini. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Lakini Mheshimiwa Mussa Zungu, habari hizi ni *editorial* ama ni maoni ya wananchi, kwa sababu mwananchi ana uhuru wa kusema lolote, kuna mwingine anaweza kuwa anaona Rais anapendelea kitu fulani, ana uhuru wa kusema hivyo.

MHE. MUSSA AZAN ZUNGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni *editorial*, ni makala maalum katika gazeti.

MWENYEKITI: Basi kama *editorial* sijui, lakini mimi nimeona watu wanajiandikia lolote tu, wengine wanamshukuru Rais, wanamsifu wengine wanamlamu, ndivyo binadamu tulivyo na uhuru huu jamani waliutafuta wazee wetu wakina Mzee John Malecela, uhuru ili watu wapumue. Sasa Rais anakuwa kama amewekwa kwenye kioo basi usimguse Rais, mimi nadhani, lakini Serikali labda inalo la kusema.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui kama amekuelewa Mheshimiwa Mussa Zungu, kwamba ni maoni ya Mhariri au makala ya mtu maalum. Kama ni makala, kama ulivyo sema wewe, lakini kama ni maoni ya Mhariri basi ndio sauti ya gazeti lile au radio ile, nafikiri hayo yalikuwa ni makala. Hata hivyo nakubaliana na wewe kwamba Serikali imejibu hoja hiyo na kutoa takwimu za kutosha kwamba si kweli hayo. (*Makofi*)

MHE. IDD MOHAMED AZZAN: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi, niko kwenye *vote 96*, programu 10, *sub vote 1001*, kifungu kidogo 250100 Mshahara wa Waziri.

Katika maelezo yangu niliyoyatoa na yale ambayo niliandika, nilizungumzia suala migogoro kwenye michezo naomba nipate ufanuzi mdogo tu.

Katika maelezo ya Waziri amesema kwamba watatatua migogoro hiyo kwa kutengeneza ama kubadili Katiba hizi kwenye vyama vya michezo na vilabu, nakubaliana naye kwa sababu Katiba zetu, kwenye vyama na vilabu zimepitwa na wakati. Lakini nilikuwa napenda anipe maelezo ya ziada tu, pale ambapo kuna migogoro, nimevizungumza vilabu viwili ambavyo ndio vikubwa hapa nchini, Simba na Yanga, tayari ipo migogoro pale, mtafanyaje muitatue migogoro ile? Halafu tuingie kwenye kubadili Katiba zao, nilikuwa naomba ufanuzi huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine nilikuwa nataka nipate ufanuzi juu ya pesa za Serikali zilizoibowi tarehe 26 Machi, 2006 kulikuwa kuna mechii kubwa tu kati ya Simba na Yanga, mechii ile ilingiza takribani shilingi milioni 98, katika pesa zile yako

makato ambayo yanatakiwa yachukuliwe na Serikali, kama gharama za uwanja, ambayo yalikuwa yanazidi shilingi milioni tisa, lakini siku ile zilitolewa shilingi milioni tatu takriban shilingi milioni 6.9 ziliyeyuka kwa maana zilichukuliwa na wasiohusika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ktika maelezo ya Waziri, amesema kwamba pesa zile zimerudishwa, nilitaka njue, ni muda gani umechukua pesa zile kurudisha, lakini kwa nini yule ambaye hakupaswa kuchukua pesa zile akazichukua? Akakaa nazo mpaka pale mtu mmoja alipofichua siri kwamba kuna hela za Serikali zimechukuliwa na wasiohusika, ndio zikarudishwa na nilisema kwamba katika maelezo yangu, Wizara muangalie watendaji, kama hamkuwa makini na watendaji na ninyi pia mtaangushwa Mheshimiwa Waziri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hili nalo linanitia mashaka, naomba maelezo ya kina, kama ni mtu ameiba pesa ziko sheria katika nchi hii, mtu aliyeiba, sio tu anarudisha pia anatakiwa afikishwe kwenye vyombo vy a sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa napenda nipate maelezo ya ziada tu yatakayoniridhisha kuhusu kocha wetu kutoka Brazil, Maximo, pamoja na kufundisha timu ya Taifa, pia atakuwa na jukumu la kuafundisha walimu amba watazisaidia kufundisha vilabu yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua ni watu gani, ama ni vijana gani watachukuliwa kwa ajili ya kupata mafunzo hayo, kwa sababu kama tunavyosema kwamba wachezaji wa hivi sasa wa timu ya Taifa hawafundishiki, pia tunao makocha wa nchi hii ambao tayari nao hawafundishiki na kila siku kozi zikija, utawakuta ni wale wale tu ndio wanakwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nipate maelezo ya kina kwamba sasa tunaachana na wale, tunachukua vijana wapya kabisa kuanza kuwapa mafunzo ya ukocha.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimruhusu Mheshimiwa Joel Bendera, ajibu swali hili, lakini niseme hivi kabla sijamjibu na kwa kujibu kwamba sisi Wizara yetu mpya tusingependa kujiingiza katika migogoro wa vilabu. Hiyo ni sera yetu, hatuwezi kumpa mtu magoli akashinda au akashindwa si kazi yetu, ni kazi ya vyama vy a michezo.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE. JOEL N. BENDERA): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufanuzi kwa mambo matatu aliyozungumza Mheshimiwa Azzan.

Hili la kwanza ya migogoro nililijibu haraka haraka pale wakati nachangia hoja lakini nataka nimweleze Mheshimiwa Idd Azzan kwamba suala la migogoro ya Simba na Yanga, vilabu vyote vina Katiba zao, ni vilabu vinajitegemea pia ni vilabu ambavyo wana wanachama wao na uongozi wao, ni sawasawa na Serikali, mtu aingilie nyumba ya

mtu na mkewe ndani ya nyumba wanagombana wewe unakwenda kuamua ugonvi ambao huujui chanzo chake. Lazima tufike mahali kwamba vilabu hivi vina Katiba zao, vilabu hivi vina viongozi wao tunategemea ni watu wazima na wanaelewa wanachokifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa mgogoro wa Yanga imejitahidi sana na suala hili liko Mahakamani sasa sisi kama Serikali hatuwezi kuingilia mgogoro ambao uko Mahakamani, utakapomalizika na tumewashauri Yanga wafute kesi kule Mahakamani ili Serikali iwasaidie kukaa nao kama ambavyo Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya, wakati huo akiwa Waziri alikaa nao wakafikia hapo walipo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kusema Serikali iingilie mgogoro kwa kweli ni kitu kigumu sana, tunaomba ndugu zetu wa Yanga na Simba waache migogoro haiwasaidii wazungumzie maendeleo ya mchezo wa mpira nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili la fedha mechili iliyochezwa tarehe 26 Machi, 2006 ni kwamba mchezo ulichezwa, fedha zikapatikana maduhuri ya Serikali ya Wizara yangu mimi ilikuwa ni shilingi 9,225,000 ambazo walikuwa wapate. Fedha hizi ziligawiwa kwanza mwanzoni milioni tatu akapewa Meneja wa Uwanja lakini kwa utaratibu ambao wenyewe walikubaliana Yanga na Simba kwamba hawawezi kuzichukua zile fedha ili wazipeleke kwenye *custody* ya *TFF* ikabidi wazipeleke kwenye *custody* ya *TFF*. Kampuni iliyochaguliwa na Simba na Yanga kusimamia mchezo ule ndiyo ambayo ilichukua zile fedha kwa makosa lakini baada ya Meneja wa Uwanja kuwaandikia barua na *TFF* kuwaandikia barua wazirudishe fedha zile wamezirudisha zote Serikalini, kwa hiyo, hakuna ugomvi, tayari fedha zile ziko Serikalini na hakuna tatizo lingine na wala hakuna wizi wowote uliotokea. (*Makofi*)

Suala la *coach* nataka nimhakikishie Mheshimiwa Idd Azzan kwamba kwanza hata ofisini hajaingia, tuwaachie *TFF* wakae wapange programu, ni nani wanastahili kufundishwa na *coach* Maximo na kariba gani. Sisi tunachofanya kama Wizara tumeshamkabidhi *coach TFF* tutakuwa karibu na jicho letu kuona maendeleo yanavyofanyika lakini na sisi tutatoa ushauri kwamba ma - *coach* wale ambao hawajapata mafunzo yoyote watafundishwa na *coach* huyu tutaanza na shule za msingi, sekondari, Vyuo, Vilabu vyote na wengine wale ambao wamepata utaalamu huo ili *coach* huyu tumtumie vizuri. Tutahakikisha hatutatumia nafasi hiyo vibaya. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, ngoja na mimi niongeze yangu huwa inasaidia.

Kwanza kuhusu *coach* nimetaarifiwa wakati wa *break* ya mchana kwamba tusitamke kama tunavyotamka kiingereza *maximum*, hili jina lina lafudhi ya Kilatini, Kireno kwa hiyo, ile x ni ya kimya kinachotoka pale ni Masimo siyo Maximo.

Sasa tumzooe hivyo maana yake itakuwa inamkera mwisho hata atashindwa kufundisha vizuri, kama jina linakosewa kila siku, kwa hiyo, ni Masimo siyo Maximo. (*Makofi*)

Kuhusu migogoro hii ya Simba na Yanga Mheshimiwa Idd Azzan, sisi tulioishi katika mambo haya Dar es Salaam kwanza kwa taarifa yenu Waheshimiwa Wabunge mimi nilitunga Katiba ya Simba mwaka 1973. (*Makofi*)

Tatizo pale ni ulaji tu hakuna la zaidi na mimi nadhani kadri Serikali ya Awamu ya Nne inavyoongeza fedha za uvezeshaji na kadhalika, watu wataacha kugombania hii mipesa ya milangoni kwenye mipira watahamia sasa kwenye kuangalia mpira tutapata watu wanaojali mpira, hivi vikundi vinavyogombania pesa pale kwenye Yanga na Simba ndiyo matatizo makubwa. (*Kicheko/Makofi*)

Lakini Mheshimiwa Idd Azzan, labda wewe unafahamu tofauti, mimi naelewa hivyo na nilikuwa katika kamati hizi. Tayari eeh, basi tunaendelea. (*Makofi/Kicheko*)

MHE. ADAM K. MALIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru. *Vote 96, program 10 Administration Sub-Vote 1001 Administration and General 250100 Mshahara wa Waziri.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kusema haya baada ya wenzangu kunitangulia kwa sababu kimsingi mimi nilikuwa naomba kuuliza kuhusu utekelezaji huu wa Sera ya Habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, habari kimsingi ni huduma ya jamii pamoja na kwamba kwa Tanzania hapa tumeruhusu kwamba watu binafsi wawe na umiliki wa vyombo vy ya Habari, Magazeti na kadhalika. Lakini kuna kitu ambacho ni *ownership* ya Serikali na *society* peke yake ambayo ni *enabling environment*, jamii yetu inaweka mazingira mazuri ya hawa wamiliki kufanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala langu lilikuwa kwamba katika nchi zote ambazo zinakuwa na mfumo wa namna hii panakuwa na chombo maalum cha kuratibu cha *supervision* na *regulation* ya habari zote kwa ujumla kujua habari zifi zinifikia viwango fulani ambavyo vinastahili wao kupewa leseni ya kuendelea kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo na ninashukuru kupata nafasi hii kwa sababu siku nydingi hili jambo limenikera. Nimewahi kushuhudia mimi Rais wa Jamhuri ya Muungano ana habari nzito kwenye taarifa ya habari ya saa mbili anapewa dakika moja na nusu, Waziri Mkuu anataka kuzungumzia njaa anapewa dakika moja na nusu, watoto wa *primary* wanakuja kutoka Zanzibar kutembelea kiwanda cha *Coca Cola* wanapewa dakika kumi. Mmiliki wa *TV* anakwenda kuongea na watoto wa *Madrasa Msasani* kwa ajili ya kugombana na Sheikh mmoja anapewa dakika kumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii haitokei nchi nydingine, ni lazima pawe na *priority* ya *information* ambayo inatoka *especially* kwenye *news* kwa sababu pale mtu yeoyote ambaye tunakupa leseni, kwanza kabisa hiyo leseni inatoka kwa mamlaka ya Bunge lako hili, sasa tunapokupa leseni hiyo tunataka ujue kwamba tunakupa nafasi ya kufanya huduma ya jamii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa swalı langu lilikuwa moja, nimetazama humu ndani ya hotuba ya Waziri nimeshindwa kufahamu lakini inawezekana kwa sababu mambo yalikuwa mengi labda atanisaidia, je, kuna chombo haswa ambacho kisheria kimepewa dhamana ya kufanya *regulation, supervision* na kudhibiti viwango vyatangazaji na maandishi (*written print*) as well kwenye magazeti?

Lakini lingine ni kwamba kama chombo hiki au nafasi hii ipo je, kuna pesa ambazo zimetengwa katika hizi ambazo tunaidhinisha hapa ili kuwawezesha ama kitengo hiki ama idara hii ama Taasisi hii kufanya kazi hii kwa manufaa ya jamii ya Watanzania kwa ujumla?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Adam Kigoma Malima, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri wakati najibu hoja hapa nimezungumzia juu Kifungu Namba 2.22 cha Sera ya Taifa ya Habari, Utangazaji ya mwaka 2003 nikanukuu kwamba chombo cha habari kisitumiwe kwa manufaa binafsi ya mmiliki au mtendaji bali kitatumiwa kwa maslahi ya umma. Hayo ni maelekezo ya Sera yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, najibu hoja kwamba chombo cha habari kisitumike kwa manufaa binafsi ya mmiliki au mtendaji kwa hiyo anayefanya hivyo anakwenda kinyume na Sera ya Habari ya nchini mwetu.

Pia kuna chombo kinaitwa *TCRA* ambacho ndiyo kina dhamana ya ku-regulate mambo yote hayo kama kutoa leseni, kuwaadhibu watu na kadhalika. Kwa hiyo, naomba kutoa wito kwa wamiliki wa vyombo vyahabari wafuate sera hii na waache tabia ya kujitangaza wenyewe badala ya kutangaza mambo ya umma na mambo ya Taifa la nchi yetu. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Lakini sehemu moja Mheshimiwa Waziri hujajibu ni mpangilio katika kipaumbele cha habari, kaongea Rais au Waziri Mkuu lakini watoto wametembelea *Coca Cola* ile dakika kumi Rais au Waziri Mkuu dakika moja. Naona hiyo hujaigusia. (*Makofi*)

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, vyombo vyahabari kuna kitu kinaitwa Sera zao na Mhariri, yule Mhariri ndiye anaamuni ipi iwe *lead story* siku ile ndiyo maana wakati mwingine katika magazeti yetu unaona kwamba siku moja kila gazeti na namna yake au *TV at hot* kwa hiyo, inategemea yule Mhariri wa siku ile habari gani anataka iongozwe na kwa muda gani. Lakini lazima wote hawa wakifuata sera hii watajua kwamba kitu gani kipewe kipaumbele. (*Makofi*)

MHE. ADAM K. MALIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimeridhika na majibu ya Waziri lakini bado naendelea kusisitiza kwamba Waziri anakubaliana na mimi kwamba kuna kazi ya *TICRA* ambayo haitekelezwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hili lipo katika nchi zote ukiangalia Uingereza na kadhalika siku ambayo Rais anatoa habari nzito *TV* na Magazeti zote zinakuwa na *headline news* kwa sababu *that is national news*. Sasa badala yake Rais anatoa habari nzito zinatokea kwenye magazeti au chombo kimoja, lakini huyu mwingine anatoa habari ambazo ni za kwake yeye mwenyewe binafsi. Sasa tunasema kwa sababu Sheria ipo na *TCRA* ipo, mimi namwomba tu Waziri kwamba anihakikishie kwamba atawaelekeza *TCRA* kwamba watekeleze kazi yao yenye manufaa kwetu sisi wote siyo kwa wao wamiliki peke yao. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Nadhani umeelewaka, Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu karibu.

WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Linalelewaka lakini kama ulitaka niseme nitasema.

MWENYEKITI: Nilidhani umesimama kwa ufanuzi.

WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kufafanua tu kwamba kwa Sheria *TICRA* ni Shirika lililo chini ya Wizara ya Miundombinu na Sheria hairuhusu Waziri kulielekeza shirika hilo kwa maana hii inayozungumzwa hapa, lakini naweza mimi kama Waziri wa Sekta hiyo kukieleza chombo hicho kuzingatие *concerns* za Wabunge ambazo zinalezwu hapa kwamba waliangalie kama kuna mahali wanapoweza kulishughulikia kwa maana hii inayozungumzwa kwamba kuna watu na watu katika mambo ya habari basi walishughulikie. Mimi nitaweza kuwaomba walishughulikie *without prejudice* kwa sababu wana uhuru huo. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Nadhani Waheshimiwa kikubwa hapa ni kuiomba Serikali kwamba kwa kuwa kuna Sera ya Habari hata *TCRA* chini ya miundombinu basi wazingatie Sera ya Habari kwa sababu ni sera ya Serikali.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu 1002 - *Finance and Accounts* 267, 401,000/=

Kifungu 1003 - *Policy and Planning* 210,442,500/=

(*Vifungu viliyyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu 6001 - *Culture and National Languages* 1,541,829,100/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sameer Ismail Lotto, haya ufanuzi.

MHE. SAMEER ISMAIL LOTTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi nitakuwepo katika *Vote 96, Program 60, Sub-Vote 6001 Culture and ...*

MWENYEKITI: Tumeshapita.

MHE. SAMEER ISMAIL LOTTO: Ndiyo hiyo tulipo.

MWENYEKITI: Hapana, tuko 6004 siyo? Ah! Bado tuko 6001? Samahani endelea.

MHE. SAMEER ISMAIL LOTTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, *Program 60, Sub-Vote 6001, Culture and National Languages.* Hapa ningependa kusaidiwa kuhusu maadili na lugha kama inavyofafanua kifungu chenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu imekuwa kidogo dhaifu katika kufuatilia katika kusisitiza suala la maadili na maadili yanazidi kumomonyoka na kwa kweli watoto wetu, wazee wetu, akinamama pia hawazingatii maadili, siku hizi huwezi kuwakemea watoto wa jirani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inazungumzia vipi juu ya suala hili katika kurekebisha maadili kama nguo fupi, wanakuja wazungu wanaoga uchi kwenye fukwe zetu, je, Serikali ina mkakati gani katika kuhakikisha kwamba haya mambo yanadhibitiwa ili tusije tukapotoka na watoto wetu wakawa wanaiga huko?

Vile vile la pili nataka kuzungumzia kuhusu picha chafu zinazotoka kwenye *TV* na kwenye *internet*. Je, Serikali ina uwezo wa kuweza kudhibiti vitu hivi au lah!

La tatu ni habari zinazotoka kwenye magazeti yetu ambayo yanatoka mchana mara nydingi magazeti kwa mfano ya Dar Leo na Magazeti ya udaku huwa yanatoa taarifa za kutudanganya na mimi nilishawahi kulizungumzia hili wakati niko kwenye Kamati yetu ya Huduma za Jamii na hapa niko na Mwenyekiti wangu ananisogezasogezza kwenye hili ni kwamba tunapewa taarifa kwamba kuna dawa za kuongeza nguvu za kiume na kadhalika ambazo taarifa hizi si za kweli. Lakini huko bado zinaendelea kutangazwa hivyo hivyo, mimi sijazajaribu lakini. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba matangazo haya aidha, kwenye magazeti au kwenye *TV* au Mabango yanachukuliwa hatua? Ahsante. (*Kicheko*)

MWENYEKITI: Kwanza pole sana Mheshimiwa Sameer Lotto, kama umeliwa kwenye hayo matangazo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Waziri ufanuzi tafadhali.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu maswali yake matatu kama ifuatavyo:-

Suala la magazeti nasema wenyе magazeti wengine wanafanya biashara ya kuuza magazeti yao tu na si vema kufuata kila ambalo gazeti linaandika. Kama kuna dawa, bora uende hospitali ukapime na kisha utapewa dawa inayohusika, usifuate dawa za magazetini. (*Makofi*)

Sisi hatuwezi kupiga marufuku kila kitu kwa sababu kwao ni biashara lakini nasema kama mtu kaathirika na dawa hizo basi unakwenda kuwashtaki gazeti hilo kwamba wamenipa dawa haikunifaa kama nilivytaka mwenyewe.

Kuhusu *TV* na *Internet* tumesema hapa kwamba kule kwenye *TCRA* kuna kitengo cha Maudhui yaani *Content Committee* wao ndiyo wenyе dhamana ya kudhibiti filamu na maudhui ambayo ni machafu kwa ajili ya televisheni na wana haki ya kuwaadhibu watu kama hao kwa hiyo nasema *TCRA* ina dhamana hiyo chini ya Kamati ya *Content* ambayo mimi nasimamia jambo hilo na nimesema hapa kwamba *TCRA* pia wanaangalia uwerekano wa namna ya kuzuia hizi pitch zisionekane katika *Internet* au mitandao yetu na wanafanya kazi hiyo kusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maadili nasema hili jambo si la Serikali, kila mtu ana nafasi hiyo, kila mmoja ajitahidi kuhakikisha kwamba watoto wake, jamaa zake, wake zake na pia waume zake wavae vizuri kwani Serikali haiwezi kutoa amri kwamba kila mmoja kuanzia leo mvae nguo ndefu haiwezekani, mambo ya kizamani hayo. Tunaomba tusaidiwe na wazazi kila mmoja achukue jukumu lake. (*Makofi*)

(*Kifungu Kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote*)

Kifungu 6004 - *Sport Development* 941,369,600/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba.

MHE. KABUZI F. RWILOMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nipate ufanuzi. *Vote 96, Program 60 Sub- Vote 6004.*

Napenda kufahamu kwenye kifungu kizima hicho. Wakati nachangia kwa maandishi nilikuwa nimepitia vifungu hivi nikaangalia kwamba hapa kwenye *Sports Development* ndiyo mahali ambapo utendaji mkuu ulipo, ndipo mahali ambapo michezo yote inatakiwa ipate fedha kwa ajili nchi nzima. Nategemea kwamba Serikali itaweza kuhamasisha michezo kuanzia Wilaya, Mikoa hadi Taifa kuweza kuweka kwa nguvu ili tuweze kupata wachezaji bora na nilisema kwamba nafikiri kufikia 2010 tutaweza kuonekana kwenye *World Cup* badala ya kuangalia wenzetu.

Je, hapa Mheshimiwa Waziri Kifungu hiki hakina fedha ingawa ilionekana kwamba kifungu 280500 ndiyo fedha itakayotumika lakini siyo kazi yake, hiyo napenda kufahamu watatoa wapi fedha ya kuweza kuendesha programu zote hizi za michezo ambazo wamesema watazitekeleza na michezo itakuwa juu, mimi nakuwa na wasiwasi kwa sababu ninaangalia watashirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, lakini

hata Wizara ya Elimu sikuona kifungu kikubwa kilichowekwa kwa ajili ya michezo na nimeangalia hata katika kitabu cha pili hakuna kitu hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, utekelezaji hata huyu *coach* tuliyempata watamfanyaje mimi bado nashangaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Joel Bendera anisaidie.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE. JOEL N. BENDER): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba kama ifuatavyo:-

Ni kweli alichozungumza kwamba kifungu kile cha *Sports Development* fedha ni chache ambazo zimetolewa na kama unavyofahamu Wizara yetu bado ni changa ndiyo tunaanza kutetea mafungu, tunategemea kwamba katika bajeti ijayo na baada ya kuishawishi Serikali kweli kweli kwamba suala la michezo sasa ndiyo limepamba moto, tunategemea tutaongezewa fedha. Lakini kwa wakatu huu tumetengewa shilingi milioni 90 kwa ajili ya maendeleo ya michezo na masuala mengine katika wilaya na sehemu nyingine.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba, bado hajaridhika.

MHE. KABUZI F. RWILOMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniruhusu niweze kutoa ushauri, sikusudii kutoa fedha kwa sababu anaanza.

Lakini kifungu hiki kama hakitapewa fedha ikiwezekana kutoka sehemu nyingine kwenye vifungu ambapo naona kuna shilingi bilioni saba kwa mfano kwenye kifungu hiki kingine na sehemu nyingine hatutafanya kitu chochote maana Serikali haitasaidia Mkoa wala hivyo vyuo na haitasaidia Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi naomba waende wakaangalie upya hili, waangalie watafanyaje kwa sababu yote walijotueleza bila kuwezesha kifungu hiki hakuna kitakachofanyika. Ahsante.

MWENYEKITI: Hapo ni pa kuanzia tu, unajua michezo ilishuka mno, mafanikio nayo huwa yanavutia fedha, nina hakika hoja yao itapata nguvu kama wataanza na mwanzo mzuri na kuletwa kwa ma-*coach* ni mwanzo mzuri.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu 7003 - *Information and Printing Information Service*... ... 8,420,062,800/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kifungu 6001 - *Culture and National Language* 2,930,000,000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kifungu 6004 - *Sport Development* 36,412,064,000/=

MHE. OMAR S. KWAANGW': Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. *Vote ni hiyo hiyo 96, Sub-Vote 6004, Sports Development.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kifungu hiki mradi mkubwa unaoonekana ni mmoja ni huo mradi wa *National Sports Complex* na tukitaka kuendeleza michezo ili tuweze kutoka hapo tulipo kwa kweli kuna haja ya kuwa na mipango hasa ya maendeleo. Uzoefu unaonyesha kwamba Wizara hii huwa haipewi sana fedha za maendeleo kwa upande wa kujenga viwanja na ndiyo maana Chama cha Mapinduzi kimejenga viwanja katika mikoa yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia hoja yangu kwa maandishi nilitoa mfano kwamba tuna vipaji vingi sana katika nchi hii na nikatoa mfano wa Manyara kwamba mkoa wa Manyara vipaji vingi sana vyta wanariadha amba wameiletea sifa nchi hii kwa kweli wengi wanatoka mkoa wa Manyara, lakini ule Mkoa amba ni mpya kwa kweli hauna Stadium ya aina yoyote lakini ndiko sifa kubwa inakotoka ya wanariadha kuipatia nchi hii sifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ufanuzi ni kwamba je, kuna mipango ya kibajeti kwa miaka inayokuja? Mwaka huu mradi unaoonekana ni huo mmoja kwamba sasa Serikali na yenye kujenga viwanja vyta michezo walau kusema hata katika ngazi ya Mkoa. Kama itaanza na mkoa wa Manyara nitashukuru kama ufanuzi huo utatoka kwa sababu eneo lipo limetengwa na wanariadha wazuri kabisa ndiyo wanatoka Manyara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe mwenyewe ulikuwa shahidi na Waziri Mkuu wakati mnawapongeza wale vijana amba kwa kweli tuliwapongeza hapa Bungeni mmoja anatoka mkoa wa Manyara. (*Makofii*)

Kwa hiyo, nilitaka tu ufanuzi kuona je, kuna mipango huko mbele ya safari? Tunaanza vizuri, tuna mradi mkubwa mmoja. Nilitaka tu ufanuzi kiasi. Ahsante.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE. JOEL N. BENDER): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Omar Kwaangw', kwamba ni kweli amechangia kwa maandishi na nataka pia nimpongeze kwa sababu wanariadha wote amba wamevunja rekodi hasa ya mbio

ndefu katika nchi yetu wametoka Babati, nampongeza sana wengi wametoka huko. (*Makofi*)

Lakini nimwambie ukweli kwamba sasa hivi kama unavyojuwa uwanja amba tunaujenga wa *Taifa Complex Stadium* unatugharimu shilingi bilioni 64, ni mradi mkubwa kweli na ni fedha nyingi. Serikali imeanza na huo mmoja ninaamini kabisa kwa jinsi Serikali ya awamu ya nne ilivyo tunaweza tukasonga mbele kutafuta uwezekano wa kujenga viwanja vingine.

Lakini kubwa ambalo naomba niwaombe Waheshimiwa Wabunge wote kwamba ni vizuri Halmashauri zetu za Wilaya zikaanza kujenga viwanja ili juhudhi hizo zionekane na Serikali ipange nayo inaweza kusaidia lakini kubwa ni wao wenye kwanza waanze hasa Mkoa wa Manyara kwa sababu ni mpya wawe na mkakati wa ujenzi wa uwanja linawezekana. Kama mikoa mingine imeshafanya ninaamini kabisa hata mkoa wa Manyara hasa ninavyomwelewa Mheshimiwa Omar Kwaang', tunaweza tukafanya kitu pale. (*Makofi*)

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu 7003 - *Information Services* 662,000,000/=

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

(*Bunge lilirudia*)

T A A R I F A

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, kabla sijasoma nataka nitoe maelezo hapa kwamba wakati ninamruhusu Mheshimiwa Joel Bendera, si kuwa siwezi kujibu, hapana nilikuwa nampa nafasi naye pia aseme tu. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako Tukufu likikaa kama Kamati ya Matumizi na kupitisha kifungu kwa kifungu Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2006/2007 ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo na kupitisha bila mabadiliko yoyote.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Makadirio hayo sasa yakubaliwe, kwa heshima na taadhima naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Spika, naafiki. (*Makofi*)

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kwa Mwaka
2006/2007 yalipitishwa na Bunge)*

*(Saa 01.00 usiku Bunge lilahirishwa mpaka siku ya Alhamisi
Tarehe 3 Agosti, 2006 saa tatu asubuhi)*